# UHAKIKI WA METHALI ZA KIJINSIA KATIKA JAMII YA WANYANKOLE: MTAZAMO WA KIPRAGMATIKI

**NA**

**ANNENSIA ARINAITWE**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SAYANSI NA SANAA ZA KIJAMII, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2023**

# IKIRARI

**Ikirari ya Mtahiniwa**

Hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa bila kibali cha mwandishi au Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: ______________________________________Tarehe:___________________

**Annensia Arinaitwe**

**SASS/DPHIL/KIS/01/19**

**Ikirari ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini na ridhaa yetu kama washauri na wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:______________________________________Tarehe:___________________

**Dkt. Magdaline Wafula**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi.

ELDORET- KENYA

Sahihi:______________________________________Tarehe:___________________

**Prof. Mosol Kandagor**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi

ELDORET- KENYA.

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wanangu wapendwa Denise Wanjiku pamoja na Jeremiah Mutiso kwa uvumilivu wao kwa kipindi hiki chote cha kuandika tasnifu hii. Ninatambua kuwa walikosa haki za mama kama watoto kila mara nilipokuwa ninasoma na kuandika tasnifu hii. Kwa pamoja, mmenipa tumaini na nguvu za kuiona siku nyingine katika daraja lingine la masomo maishani mwangu. Nawapenda sana na Mungu awalinde na awabariki.

**SHUKURANI**

Natoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote walionisaidia kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha kazi hii. Awali, nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi ambao wengi wao wamewahi kunifundisha tangu nilipojiunga na chuo hiki mnamo mwaka wa 2011. Nawashukuru wahadhiri wote walionipa mafunzo katika kiwango cha uzamili na baadhi yao ambao wameendelea kunifunza hadi kiwango cha uzamifu. Nitawataja wahadhiri hawa japo kwa uchache; ni Prof. Nathan Ogechi, Prof. Mark Kandagor, Prof. Samuel Obuchi, Prof. Issa Mwamzandi, Prof. Robert Oduori na Dkt. Magdaline Wafula. Wote hawa walijitolea kwa kila hali kuona ya kwamba sijarudi mikono mitupu nchini Uganda. Kweli walimu wangu mlikuwa ufunuo wa kheri maishani mwangu, hasa hasa pale nilipoona hapakuwa na uwezekano, mlinipa moyo na kuniwezesha kuona mwanga zaidi. Nawashukuru na kuwatakia kila la heri maishani. Pia, siwezi kuwasahau wahadhiri wangu wengine ambao ingawa hawakunifunza darasani, lakini bado walikuwa nguzo kuu katika kunipa mawaidha na kunitia moyo wa kuendeleza masomo na kufanya utafiti huu bora. Hao ni pamoja na Dkt. Allan Opijah, John Munyua na marehemu Davies Mukuria.

Kwa namna ya pekee, siwezi kuwasahau wasimamizi wangu Dkt. Magdaline Wafula na Prof. Mark Kandagor. Kwa hakika walijitolea kunishauri na kunielekeza katika kufanikisha utafiti wangu, na, licha ya majukumu mengi waliyokuwa nayo chuoni. Mawaidha ya wakwasi hawa wawili yalinisaidia sana kuiboresha kazi yangu hadi kufikia umbo hili. Mola awabariki.

Siwezi kuwasahau wazamifu wenzangu ambao tuliweza kushikana mkono katika hali zote wakati wa masomo yetu. Hawa ni Viktor Kyomuhendo, Beatrice Bii na Baya Mercy. Shukrani za ziada ziwaendee Dkt. Gilbert Gumoshabe, Dkt. Peripetua

Arinaitwe, Dkt. Boaz Mutungi na Bw. Nelson Nsereko ambao walitumia muda wao mwingi na kunielewesha kuhusu masuala fulani muhimu yaliyohusiana na jamii ya Wanyankole na methali za kijinsia.

Nisingependa kusahau kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Makerere ambacho kilinipa likizo ya masomo ya muda huu wote na hata kunilipia karo zote za kozi hii. Kwa kweli nashukuru sana.

Aidha, michango hii yote imekuja baada ya mapenzi na usaidizi wa familia. Awali ya yote, nashukuru sana mjomba wangu Bart Katureebe pamoja na mama yangu Bi. Bernadet Katureebe kwa usaidizi wao na mawaidha yao ambayo yalifanikisha masomo yangu. Pili, siwezi kuwasahau mama zangu Bi. Maria Wafula, Bi. Cecelia Lwanga na Bi. Godliver Ikol. Tatu, ni wajomba zangu Bw. Tumusiime Robert na Bw. Rutaremwa John. Mwisho, nawashukuru ndugu wafuatao kutokana na mazingira ya udugu na upendo walinionesha: Ronald, Sarah, Cordelia, Barnard, Simon, Silver, Joseph, Dan, David, Fiona, Sheila na Happiness.

# IKISIRI

Jamii ya Wanyankole imekuwa ikitumia methali kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kutambua uwezekano wa kuendeleza dhulma za kijinsia kupitia methali hizi. Kiini ni kuwa jamii ya Wanyankole kitamaduni inaegemea mfumo wa kuumeni unaoendeleza ubabe-dume. Utafiti huu ulilenga kuhakiki methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kipragmatiki. Malengo mahususi ya utafiti ni mosi: Kupambanua methali za kijinsia kwenye nyanja maalum katika jamii ya Wanyankole. Pili, kuchanganua maana mahsusi ya methali za kijinsia katika jamii ya jadi na ya kisasa miongoni mwa Wanyankole. Tatu, kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya jadi na ya kisasa miongoni mwa Wanyankole. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Nadharia ya Udenguzi. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilibainisha namna ujinsia unavyojitokeza katika methali za Kinyankole nayo Nadharia ya Udenguzi ilituongoza kuhakiki maana na matumizi ya methali za kijinsia kimuktadha katika jamii ya Wanyankole. Data ya utafiti ilikusanywa nyanjani kutokana na makundi mawili ya Wanyankole. Kundi la kwanza ni la wazee wa miaka 50-80 ambao wana ujuzi wa muda mrefu kuhusu methali za kijinsia na utamaduni wa Wanyankole. Kundi la pili ni la vijana wa miaka 25-45 linalowakilisha jamii ya kisasa yenye mtazamo wa kisasa kuhusu methali za kijinsia za Wanyankole. Sampuli ya kimaksudi ndiyo ilitumika katika kukusanya data ambapo methali 42 za kijinsia zilikusanywa. Methali hizo 42 zilitafsiriwa na kuainishwa katika nyanja mbalimbali za jamii ya Wanyankole. Methali hizo zilihakikiwa kiudenguzi na kipragmatiki kutegemea matumizi kimuktadha. Matokeo ya utafiti huu ni kama ifuatavyo: Kwanza, kuna methali hasi ambazo zinaendeleza ubaguzi na dhuluma za kijinsia. Pili, kuna methali za kijinsia chanya ambazo lazima zihifadhiwe na Wanyankole kwa manufaa ya kizazi kijacho. Tatu, kuna methali za kijinsia ambazo zinafaa kudenguliwa na kufasiriwa upya ili ziambatane na uhalisia wa jamii ya kisasa ya Wanyankole. Utafiti huu unaonyesha wazi namna miktadha tofauti inaweza kuathiri maana na matumizi ya methali za kijinsia. Kwa msingi huu, utafiti huu ni muhimu kwa vile unachangia pakubwa katika kuimarisha uelewa wa methali za kijinsia miongoni mwa Wanyankole. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunaweza kuhitimisha kuwa ijapokuwa methali ni semi zinazopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ni muhimu kila kizazi kizifasiri semi hizi upya ndipo ziwe na uamilifu katika jamii inayobadilika kila uchao. Napendekeza tafiti za usoni zichunguze methali za kijinsia katika jamii nyinginezo za Kiafrika ili kubainisha namna maana na matumizi ya methali katika jamii hizo yameathirika na mpito wa wakati.

# ABSTRACT

The Nyankole community has been propagating gender bias in their usage of proverbs from generation to generation because the Nyankole are basically a patriarchal community. This study is a critique of gender proverbs in the Nyankole community from a pragmatic perspective. The research objectives were firstly, to identify the gender proverbs in the Nyankole community in specific contexts. Secondly, to analyze the various meanings captured in the gender proverbs from the traditional and modern Nyankole communities. Thirdly, to assess the relevance of specific gender proverbs in the traditional and modern Nyankole communities. This study was guided by African Feminism theory and Deconstruction theory. African Feminism theory was instrumental in revealing how gender is captured in the Nyankole proverbs while Deconstruction theory was useful in validating the gender proverbs in terms of their meaning and usage in the traditional and modern Nyankole communities. 42 proverbs were purposively sampled and collected from two categories of the Nyankole community. The first one constitutes of men and women aged between 50 and 80 years who are conversant with the traditional Nyankole culture. The second group constitutes of men and women aged between 25 and 45 years representing the modern Nyankole community. The collected data was categorised in various Nyankole social contexts and analysed. The meaning and application of the gender proverbs were then critically analyzed from a pragmatic point of view. The study findings are as follows: Some gender proverbs enhance gender discrimination especially against women and hence should not be propagated in the progressive Nyankole community. Secondly, gender proverbs that enhance good morals in the Nyankole community should be retained for posterity. Thirdly, gender proverbs that are overtaken by time should be deconstructed and given new meanings in line with the socio-economic and political needs of the modern Nyankole community. From the study findings it can be concluded that although gender proverbs are an integral part of a community's heritage, they ought to be interpreted from a pragmatic perspective as they are handed down from one generation to the other. This is because, as a social construct, gender proverbs are bound to acquire varied meanings with the passage of time and the context in which they are constructed and deconstructed. Future studies could focus on the analysis of proverbs or other genres in African oral literature in various aspects other than gender to assess the impact of rapid socio-economic and political changes on the African cultural heritage.

# YALIYOMO

IKIRARI ..................................................ii
TABARUKU .................................................. iii
SHUKURANI..................................................iv
IKISIRI ..................................................vi
ABSTRACT ..................................................vii
YALIYOMO .................................................. viii
UFAFANUZI WA ISTILAHI ..................................................xii
**SURA YA KWANZA ..................................................1**
**MISINGI YA UTAFITI ..................................................1**
1.0 Utangulizi ..................................................1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti..................................................1
1.1.1 Asili ya jamii ya Wanyankole ..................................................15
1.1.2 Ndoa na familia katika jamii ya Wanyankole ..................................................19
1.1.3 Nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii ya Wanyankole ............20
1.2 Suala la Utafiti..................................................22
1.3 Malengo ya Utafiti..................................................23
1.4 Maswali ya Utafiti ..................................................23
1.5 Sababu ya Kuchagua Mada ..................................................24
1.6 Upeo wa Utafiti ..................................................25
1.7 Umuhimu wa Utafiti..................................................27
1.8 Hitimisho ..................................................29
**SURA YA PILI ..................................................30**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA ............................30**
2.0 Utangulizi ..................................................30
2.1 Mapitio ya Maandishi..................................................30
2.2 Dhana ya Lugha na Jinsia..................................................30
2.3 Hadhi ya Mwanamke na Mwanamume katika Jamii..........................................40
2.4 Msingi wa Kinadharia ..................................................56
2.4.1 Nadharia ya Ufeministi ..................................................56
2.4.2 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ..................................................58
2.4.2.1 Mihimili ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika ....................................59
2.4.3 Nadharia ya Udenguzi..................................................62

2.4.3.1 Mihimili ya Nadharia ya Udenguzi........................................................67
2.5 Hitimisho .......................................................................................................71
**SURA YA TATU .........................................................................................73**
**MBINU ZA UTAFITI ..................................................................................73**
3.0 Utangulizi .....................................................................................................73
3.1 Muundo wa Utafiti.........................................................................................73
3.2 Eneo la Utafiti................................................................................................74
3.3 Wango............................................................................................................75
3.4 Sampuli na Usampulishaji ............................................................................75
3.4.1 Sampuli ya Kimaksudi ................................................................................75
3.5 Ukusanyaji Data ............................................................................................76
3.6 Vifaa vya Utafiti ...........................................................................................77
3.7 Uchanganuzi wa Data....................................................................................78
3.8 Hitimisho .......................................................................................................79
**SURA YA NNE ............................................................................................80**
**MATUMIZI YA METHALI ZA KIJINSIA KATIKA NYANJA MBALIMBALI MIONGONI MWA WANYANKOLE ........................................80**
4.0 Utangulizi .....................................................................................................80
4.1 Ujinsia kwenye Malezi na Maadili ................................................................80
4.2 Matumizi ya Ndoa na Kazi Kijinsia ..............................................................83
4.3 Matumizi ya Methali za Kijinsia katika Uwanja wa Uongozi.......................85
4.4 Methali za Kijinsia katika Uwanja wa Utamaduni ........................................87
4.5 Ujinsia kwenye Masuala ya Uchumi .............................................................91
4.6 Hitimisho .......................................................................................................93
**SURA YA TANO .........................................................................................94**
**UHAKIKI WA KIPRAGMATIKI KATIKA METHALI ZA KIJINSIA KATIKA JAMII YA WANYANKOLE.........................................................................94**
5.0 Utangulizi .....................................................................................................94
5.1 Methali za Kijinsia, Kimalezi na Kimaadili ..................................................94
5.1.1 Methali za kijinsia ya kike, kimalezi na kimaadili.......................................95
5.1.2 Methali za kijinsia ya kiume kimalezi na kimaadili....................................109
5.2 Maana na Matumizi ya Methali za Kijinsia Kikazi .....................................115
5.2.1 Methali za jinsia ya kiume kikazi...............................................................116
5.2.2 Methali za jinsia ya kike kikazi..................................................................123

5.3 Maana ya Methali za Kijinsia Kiuongozi ..... 127
5.3.1 Methali za jinsia ya kiume kiuongozi ..... 127
5.3.2 Methali za jinsia ya kike kiuongozi ..... 132
5.4 Maana na Matumizi ya Methali za Kijinsia Kitamaduni ..... 133
5.4.1 Methali za jinsia ya kike kitamaduni ..... 133
5.4.2 Methali za jinsia ya kiume kitamaduni ..... 139
5.5 Maana ya Methali za Kijinsia Kiuchumi ..... 142
5.5.1 Methali za jinsia ya kiume kiuchumi ..... 143
5.5.2 Methali za jinsia ya kike kiuchumi ..... 145
5.6 Hitimisho ..... 148
**SURA YA SITA ..... 149**
**UAMILIFU WA METHALI ZA KIJINSIA MIONGONI MWA JAMII YA KISASA YA WANYANKOLE ..... 149**
6.0 Utangulizi ..... 149
6.1 Methali za Kijinsia za Kuhifadhiwa ..... 149
6.2 Methali za Kinjisia za Kudenguliwa ..... 156
6.3 Methali za Kinjisia za Kutupiliwa Mbali ..... 178
6.4 Hitimisho ..... 189
**SURA YA SABA ..... 191**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 191**
7.0 Utangulizi ..... 191
7.1 Muhtasari wa Tasnifu ..... 191
7.2 Matokeo ya Utafiti ..... 193
7.2.1 Matokeo kuhusu kupambanua methali za kijinsia ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii ..... 193
7.2.2 Matokeo kuhusu uhakiki wa maana na matumizi mbalimbali ya methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole ..... 194
7.2.3 Matokeo kuhusu tathmini ya uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole ..... 195
7.3 Mchango wa Utafiti ..... 195
7.4 Hitimisho ..... 197
7.5 Mapendekezo ya Utafiti ..... 198
MAREJELEO ..... 200
VIAMBATISHO ..... 207

Kiambatisho 1: Mwanamke katika Methali za Kijinsia ..........................................207
Kiambatisho 2: Mwanamume katika methali za Kijinsia .......................................209
Kiambatisho 3: Maswali ya Mahojiano Kwa Wasailiwa Kumi na Wawili (12)....211

# UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Jinsia:** Ni ufafanuzi wa baolojia yetu namna inavyofafanuliwa katika jamii zetu mfano kuwa mwanamume au mwanamke.

**Methali:** Ni usemi wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kuelimisha na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.

**Pragmatiki:** Ni hali ya kuchanganua lugha kwa kuzingatia maana, matumizi na muktadha dhahiri wa matini katika awamu tofauti.

**Uchanganuzi:** Ni kuhakiki kwa kazi kwa kutenganisha vitu vilivyoshikamana.

**Wanyankole:** Ni watu wanaozungumza lugha ya Kinyankole kutoka Magharibi mwa Uganda wenye asili ya Kibantu.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii kimsingi inahusu masuala yafuatayo ya utafiti: Uwazi wa usuli wa suala la utafiti; asili ya jamii ya Wanyankole; ndoa na familia katika jamii ya Wanyankole; nafasi ya mwanamume na pia mwanamke katika jamii ya Wanyankole. Aidha, haya yalifuatiwa na suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na sababu za kuchagua mada. Mipaka ya utafiti huu imefafanuliwa katika sehemu ya upeo wa utafiti na hatimaye umuhimu wa utafiti.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Wamitila (2008) anafasili fasihi kuwa ni sanaa inayotumia lugha na ambayo hujishughulisha na binadamu pamoja na maisha yake na huathiri, hugusa au huacha athari fulani na hupatikana katika umbo ambalo linatambuliwa na jamii fulani. Aidha, Nandwa na Bukenya (1992) wanasisitiza hoja hii kuwa, kazi ya fasihi haitokei katika ombwe tupu bali huchota maudhui yake kwa mfano, elimu, uchumi, siasa na utamaduni katika jamii husika, kwa hivyo fasihi ni kioo cha jamii. Aidha, kimsingi dhima za fasihi ni kurithisha utamaduni wa jamii husika pamoja na kukuza lugha. Kwa msingi huu, fasihi hurithisha mila na desturi za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi inaweza kuwa andishi au simulizi.

Fasihi andishi huhifadhiwa kimaandishi ilihali fasihi simulizi huhifadhiwa ubongoni. Fasihi simulizi ni utanzu pendwa na wa kijadi mno ambao jamii nyingi za Kiafrika zimekuwa zikiutumia kwa njia ya kupokezana kupitia mdomo kwa kuelimisha na kuburudisha wanajamii. Kwa sasa, jamii nyingi zinajaribu kukusanya na kuhifadhi

fasihi simulizi katika vitabu na kanda za kunasia sauti. Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii zinazotumia njia hizi za kuhifadhi fasihi simulizi.

Fasihi simulizi imegawanyika katika tanzu kadhaa zikiwemo methali, vitendawilli, misemo, visaasili, nyimbo, hadithi, mafumbo, ngano na ushairi. Aidha, ni kutokana na tanzu hizi nyingi, mtafiti aliteua kuangazia methali kama kipera kimojawapo muhimu cha fasihi simulizi katika utafiti huu. Methali ni aina za semi ambazo zimekuwa zikitumika katika shughuli mbalimbali katika kama vile katika masuala ya uchumi, siasa, elimu, ndoa, utamaduni na dini. Jamii nyingi zimetumia methali katika shughuli hizi kama nyenzo ya kuelimisha, kuonya na kuburudisha wanajamii. Maelezo haya yanathibitishwa na Senkoro (1987) anayedai kuwa maendeleo pamoja na vipindi na mifumo mbalimbali ambayo jamii fulani hupitia, huelezwa katika kazi mbalimbali za kifasihi. Kama mojawapo ya jamii za Kiafrika, jamii ya Wanyankole ina shehena kubwa ya methali ambazo zimekuwa zimekuwa zikitumika na kupitishwa kutoka akizazi kimoja hadi kingine. Methali ni sehemu ya lugha na hutumika kuyatafakari, kuyapima maisha na kufunzia jumuiya. Kama vipera vingine vya fasihi, methali huchipuka na kupata uhai wake katika jamii inayokua na kubadilika kiwakati.

Hata hivyo, jamii ya Wanyankole, imekuwa ikitumia methali katika shughuli mbalimbali kutoka kizazi kimoja hadi kingine bila kutambua uwezekano wa ujinsia kujitokeza na athari yake kwa wanajamii. Hii ni kwa sababu jamii ya Wanyankole imejengeka katika mfumo wa kuumeni ambao huendeleza ubabe-dume. Methali za kijinsia zimetamalaki katika nyanja tofautitofauti ndani ya jamii hii zikiwemo nyanja za uchumi, siasa, ndoa, dini, elimu na utamaduni. Uchunguzi wa kina wa methali hizi za kijinsia unabainisha kuwa maana na matumizi ya methali hizi yanaambatana na muktadha ambamo zilitungwa na kutumika na kizazi cha jadi. Hii inamaanisha kuwa

kuna uwezekano mkubwa kuwa maana na matumizi ya methali hizi yamebadilika hasa tukizingatia muktadha mpana wa jamii ya kisasa. Hii ni kwa sababu jamii ya Wanyankole kama jamii zingine za Kiafrika imepitia mabadiliko makubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ni bayana kuwa mahusiano ya kijinsia pia yameathiriwa na mabadiliko ambayo yameikumba jamii ya Wanyankole. Ni kwa msingi huu ndipo tunachukulia kuwa uchunguzi wa methali za kijinsia za Kinyankole unaweza kudhihirisha namna fasihi kama zao la jamii yafaa iakisi uhalisia wa jamii na pia kuwa nyenzo ya kuizindua jamii kuhusiana na mabadiliko yanayotokea katika jamii husika.

Kwa msingi huu, inahalisi kuchunguza upya maana na matumizi ya methali hizi za kijinsia kiulinganishi kwa kuzingatia jamii ya Wanyankole ya jadi iliyokuwa chemichemi ya kuchipuka kwa methali za kijinsia na jamii ya kisasa ya Wanyankole katika karne ya 21. Kwa kuegemea mkabala wa kipragmatiki, utafiti huu unahoji athari ya mabadiliko ya jamii ya Wanyankole kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa na kidini katika ufasiri wa maana na matumizi ya methali za kijinsia miongoni mwa Wanyankole wenye tajiriba tofauti wanaoishi na kutagusana katika nchi ya Uganda.

Baadhi ya methali huenda zimepitwa na wakati hasa kwa kuzingatia shinikizo la usawa wa kijinsia katika jamii za kisasa. Kwa mfano, methali hii inathibitisha ipo haja ya kuzitazama upya methali hizi; *"Obworo obuterwa mukasho"* tafsiri yake "Umaskini huletwa na mama wa kambo." Katika utamaduni wa Wanyankole, mama wa kambo alionekana adui katika boma, kwani alichukuliwa kuwa katili na mwenye nia ya kupora mali ya mwanamume. Kwa hivyo, mama wa kambo alikuwa anaonywa kutokuolewa na nia hiyo. Mtazamo huo ulielekezwa tu kwa jinsia ya kike ilhali jinsia ya kiume haikuhusishwa katika mtazamo huo. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, jinsia zote zimejiendeleza kimaisha kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii. Hivyo basi, si

lazima mama wa kambo apore mali ya mumewe kwani sheria ya kisasa ina mikakati ya urithi wa mali ya familia. Isitoshe, mwanamke wa kisasa ana haki ya kuchuma na kumiliki mali tofauti na ilivyokuwa hapo kale. Kutokana na madai haya, imebidi methali hii kudenguliwa, kwa sababu muktadha wake umeathirika kimaana na kimatumizi na kulazimisha idenguliwa ili kueleweka katika  ya jamii hizi tofauti za Wanyankole.

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii za wafugaji wa ng'ombe. Ni kutokana na mazoea ya ufugaji huu, tunapata baadhi ya methali zilizotungwa kutokana na jinsia tofauti ambazo zilimsifia mwanamke tofauti na mwanamume. Kwa mfano, usafi wa mwanamke ulilinganishwa na maziwa ya ng'ombe, kumaanisha jamii ilimtarajia kuwa safi kuliko mwanamume katika kazi zake tofauti ndani ya jamii. Mfano wa methali inayosawiri namna mwanamke anavyopaswa kuwa safi ni ile ya, "*Omukazi aba amate"* tafsiri yake "Mwanamke huwa maziwa." Ilhali mwanamume alipewa sifa za wanyama wakali mfano simba, chui na ndovu kuonyesha ushujaa na uongozi wake. Hili limeonyesha kuwa, jamii ya Wanyankole iliweza kutumia methali zake kutokana na amali za jamii katika miktadha tofauti ndani ya jamii. Kwa msingi huu, methali hizi hazina budi kudenguliwa ili maana zake zieleweke katika jamii ya kisasa na ile ya kijadi ya Wanyankole.

Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano, na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa (TUKI, 2004). Ni muhimu kuchunguza amali zinazopitishwa kama mirathi kwani ni bayana kuwa hadhi ya mwanamke inatokana na jinsi alivyotambulishwa katika utamaduni uliosheni taasubi ya kiume. Utafiti huu ulikusudia kumwangalia mwanamume na mwanamke alivyotambuliwa katika mitazamo ya

wanajamii inayopitishwa katika methali za kijinsia za Wanyankole. Huku kukiwa na ukweli kuhusu kile ambacho jamii hufumbia, ni dhahiri kabisa kwamba methali hubeba maana zaidi kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa. Kwa hivyo basi, Nadharia ya Udenguzi ilituwezesha kuzichanganua methali za kijinsia za Wanyankole katika miktadha mbalimbali kama vile siasa, elimu, ndoa, utamaduni, na uchumi.

Madumulla (1981), anaeleza kuwa methali ni usemi mfupi unaoelezea uzoefu wa masuala mbalimbali ya kimaisha, na fikra za jamii kuhusu ukweli wa dunia kwa kutumia maneno machache ya kisitiari. Katika fasili hiyo, *uzoefu wa masuala ya maisha na fikra kuhusu ukweli wa dunia* ni uti wa mgongo wa methali. Hii ni kwa sababu methali huundwa baada ya jamii kushuhudia matokeo ya vitendo fulani kuwa ni mazuri au mabaya kulingana na upeo wa kifikra wa jamii inayohusika.

Vilevile, ni muhimu kusisitiza kuwa methali zilitegemea mazingira kwa sababu watu wa jamii fulani hutunga na kutumia methali kulingana na kile walichokiamini, walichokiona na walichokielewa. Jamii ya Wanyankole ilikuwa ni ya ufugaji kama jukumu kuu la kuendeleza maisha yake. Walipata maziwa, nyama na ngozi ya ng'ombe kutokana na wanyama hao. Ni kutokana na baadhi ya shughuli hizi ndipo jamii iliweza kutunga baadhi ya methali zinazomrejelea mwanamke tofauti na mwanamume kwa kuonyesha umaarifa, uzoefu, busara na kile walichokiona kuwa ndio ukweli. Kwa mfano methali; "*Obuzaale bwente gaba amabeere"* ikitafsiriwa kama "Umuhimu wa mwanamke ni matiti yake ambayo hunyonyesha watoto wa mwanamume." Kwa msingi wa methali hii, ng'ombe alichukuliwa kuwa mnyama mwenye thamani kutokana na manufaa yake ya maziwa. Kwa hiyo, ikiwa ng'ombe alikuwa hana matiti hayo bila shaka hangethaminiwa. Kwa hivyo, mwanamke analinganishwa na ng'ombe. Hata

hivyo, methali hii iliathirika kimuktadha na kimaana na kubidi kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Okpewho (1992) anaeleza kwa upana zaidi nafasi ya methali katika mazungumzo ya kawaida. Anasema "Methali ni ghala la busara za jamii na zina kina cha falsafa kwa kuwa zinatokana na uzingatiaji mkubwa kuhusu tabia za mwanadamu na uzoefu wake katika mazingira anamoishi." (uk). Kulingana na maoni yake, wanajamii wanaposhiriki katika shughuli za jamii, hupata ujasiri wa kuimarisha uwezo wa kufikiria, kuwasiliana na hata kutatua matatizo yanayowakumba katika maisha yao. Baadhi ya methali za Wanyankole zilihimiza tabia maalum kijinsia. Mfano methali iliyowahusu wasichana kuwa na tabia nzuri ni; "*Omwana wo'mwishiki atsimba amaju yaba nayihura"* tafsiri yake "Ni heshima mtoto wa kike kupakua chakula akiwa amepiga magoti." Katika jinsia ya kiume; "*Omwojo arya nishe"* ikitafsiriwa kama "Mtoto wa kiume anastahili kula na babake." Maadili haya yamekuwa yanaenziwa katika jamii ya Wanyankole tangu jadi hadi leo. Hata hivyo, jamii ya kisasa ina mtazamo tofauti kuhusu wanawake kupiga magoti. Inaona kuwa ni utamaduni ambao umepitwa na wakati. Wanyankole wa kisasa wanapendekeza jinsia zote zichukuliwe kuwa sawa pasi na kubaguliwa. Hii inamaanisha kwamba, kila uchao maana na matumizi ya methali hizi yanabadilika kimuktadha na hivyo kuhitaji kudenguliwa.

Alex (1980) anasema kuwa methali ni semi fupi zenye maana fiche zinazokubalika na kutumiwa kufafanua ukweli na hekima ya jamii. Kutokana na maelezo haya, tunatambua kuwa jamii ya Wanyankole ilikuwa na methali kama hizi ambazo zilisaidia kuelimisha kuhusu utu bora. Kwa mfano *"Omukazi tanyarira Ikara"* tasfiri yake ikiwa "Mwanamke hastahili kukojela kaa." Neno "Kaa" lina maana fiche inayorejelea mwanamume. Kwanza kabisa kaa kwa maana ya figa lina jukumu kubwa la kutekeleza

nyumbani kwani ni muhimu katika shughuli za upishi wa vyakula. Kwa hiyo kulikojelea inamaanisha vyakula havitaweza kupikwa. Hii ni kumaanisha mwanamke hakustahili kumdharau mumewe au kumtendea maovu kwa sababu alikuwa nguzo kubwa nyumbani. Tofauti na mwanamume, mwanamke alistahili kujua daima ni mumewe ambaye alikuwa anamlinda na kumwajibikia siku zote. Aidha, ni kutokana na hali hii ndipo tunaona jamii ya kisasa inapinga methali hii na kupendelea ifasiriwa upya. Hii ni kwa sababu jinsia zote zimepewa fursa sawa kushiriki katika shughuli za kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi, kielimu, kitamaduni na kisiasa.

Maganga (2000) anaeleza kwamba, "Methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalumu lakini kwa namna ya fumbo. Usemi huu mara nyingi hukusudiwa kumuonya na kumuongoza mwanadamu…." Kwa mfano, katika jamii ya Wanyankole, baadhi ya methali zenye usemi mzito zilizotumiwa kuwaonya na kuwaongoza wanajamii ni pamoja na, *"Omuhuuru tagaya gabo"* tafsiri yake "Mwanamume ambaye hajaoa hastahili kudharau chakula." Katika utamaduni wa Wanyankole, mwanamume alikuwa anafaa kufanya kazi kwa bidii ili apate mahari ya kumwoa mke. Ikiwa alizembea katika kazi, basi alilazimika kula chochote alichopewa. Aidha, katika jamii ya kisasa, methali hii ingali na ufaafu kwa sababu jamii ingali inamtazamia mwanamume kufanya kazi kwa nguvu ili kuwajibikia familia yake. Kwa hivyo basi, ili kubainisha uzito wa methali hii, ni lazima ihakikiwe ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Wamitila (2001) anathibitisha umuhimu wa kipera hiki cha methali kwa kueleza kuwa methali hutoa mafunzo kwa wanajamii hali kadhalika kurekebisha tabia mbaya miongoni mwa wanajamii. Hali hii inajitokeza wazi katika jamii ya Wanyankole ambapo methali za kijinsia zilitumika kama nyenzo ya kuelekeza mahusiano ya kijinsia

na hasa tabia za watoto wa kike na wa kiume. Kwa mfano methali: "*Kubwira omwishikye ataha omwishe"* tafsiri yake "Ifikapo usiku sharti mtoto wa kike aingie nyumbani mwa baba yake". Katika jamii ya Wanyankole ni mtoto wa kike ambaye alikuwa anastahili kufika nyumbani mapema kama ishara ya maadili mazuri tofauti na mtoto wa kiume. Hii ni kwa sababu jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni. Mwanamke alichukuliwa kuwa dhaifu kwa vile hakuwa na nguvu ya kujikinga iwapo angevamiwa kule nje wakati wa usiku. Isitoshe mwanamke kuwa nje usiku ilikuwa ni ishara ya ukahaba. Hali hii ilikuwa tofauti na mtoto wa kiume ambaye aliruhusiwa kuingia nyumbani wakati wowote kwa madai kuwa mwanaume alikuwa na nguvu na uwezo wa kujilinda. Hata hivyo katika jamii ya kisasa, methali hii imeathirika kimatumizi kwa vile jinsia zote katika karne ya 21 zinashiriki katika masuala ya ulinzi usiku na mchana kama askari. Kwa hiyo, methali hii haina budi kudenguliwa ili maana na matumizi yake yaafikiane na muktadha wa kisasa.

Kulingana na mawazo ya Joon (1992), methali ni maneno ya kale yanayotumika kama vilinganishi. Ni maneno yenye maana iliyofichika ambayo baada ya kuyasikia humfanya mtu kufikiri huku akijiuliza aliyemwambia alikusudia nini? Methali husaidia katika kushauri, kufundisha na kuonya wanajamii. Aidha, hii ina maana kwamba, maana za methali zina mchomo wa moyo baada ya mtu kuambiwa methali fulani. Mchomo huu wa moyo ukizingatiwa kwa undani una kazi kubwa katika kukuza na kuendeleza maadili. Methali zinapotolewa kwa wanajamii, wanatarajiwa kuyafikiria yaliyomo kwa undani ili kutenda kama walivyotahadharishwa ili kujiepusha na jambo lolote baya.

Kutokana na maelezo haya, jamii ya Wanyankole imekuwa ikitumia methali kama kipengele mojawapo muhimu katika kuelimisha jamii yake kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano methali, "*Omukazi wokubanza aba nka nyoko"* ikitafsiriwa kama, "Mwanamke wa kwanza huwa kama mama na anastahili kuheshimiwa na mumewe hata akiwa amepata mke wa pili." Mwanamke wa kwanza alistahili kupewa heshima kwa vile alikuwa amesaidiana na mume wake kupata mali ya familia. Ni kwa msingi huu ndipo mtafiti aliamua kuchunguza methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki na kiundenguzi kubainisha ukamilifu wake.

Wakishadidia dhima muhimu inayotekelezwa na kipera cha methali, Akivaga na Odaga (1982) wanasema kuwa methali ni kusanyiko la kauli zinazozungumzia maisha ya watu. Baadhi ya methali hizi zimezuka kutokana na hali ngumu ya maisha ya binadamu. Aidha, methali huonyesha kile watu wanapenda na kile wanachukia. Kwa hivyo methali huonyesha msimamo wa watu na falsafa yao kuhusu maisha na mazingira yao. Kwa msingi huu, tunaweza kusema kuwa methali huakisi tajiriba na mwonoulimwengu wa jamii husika. Ni kutokana na maelezo haya ndipo tunadai kuwa maana na matumizi ya methali zikiwemo methali za kijinsia za Kinyankole lazima yazingatie muktadha ambamo methali hizo zimechipuka. Lazima tujiulize je, ni hali gani iliyosababisha kuibuka kwa methali maalum? Je, ni ujumbe gani uliofumbatwa katika maneno yaliyotumika katika utunzi wa methali husika? Uzingatifu wa maswali haya ndio umetuchochea kuchunguza methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki na kiudenguzi.

Mathalan methali ya Kinyankole "*Ebitsya by'embuzi tibyanga muguha*" ikitafsiriwa kama "Shingo la mbuzi haliwezi kukata kamba" lazima ifasiriwe kwa kuzingatia muktadha ambamo ilichipuka na pia mafumbo yaliyomo. Katika jamii ya jadi ya

Wanyankole, methali hii ilikuwa inatumiwa na wazee kuwakumbusha wanawake kuwa, ni lazima wamheshimu mwanamume ambaye alitambuliwa kuwa kiongozi kule nyumbani. Kwa mujibu wa methali hii, tunaona nafasi ya mwanamke na mwanamume katika ndoa. Katika kusisitiza mahusiano ya kijinsia miongoni mwa Wanyankole, tunaona matumizi ya mbuzi; mnyama aliyefugwa na aghalabu alifungwa kamba shingoni ishara kwamba hakuwa na uhuru juu ya maisha yake. Aidha, hali hii ilitokana na ubabe-dume ambao ulikuwa unaendelezwa na jamii ya Wanyankole inayoegemea mfumo wa kuumeni.

Kutokana na maelezo hayo, ni wazi kuwa baadhi ya methali za kijinsia huenda zisiwe na uamilifu katika jamii ya kisasa ya Wanyankole ambayo imeshuhudia mabadiliko mengi ambayo yameathiri mtazamo wa wanajamii kuhusiana na masuala mbalimbali yakiwemo mahusiano ya kindoa. Ni dhahiri kuwa wanaume na wanawake Wanyankole wamepitia mfumo wa kisasa wa elimu na wengi ni waumini wa dini ya Kikristo ambayo inahimiza upendo na usawa miongoni mwa wanandoa. Kwa hivyo, methali za kijinsia zenye mwelekeo hasi huenda zikatupiliwa mbali au kudenguliwa ili ziafikiane na uhalisi wa jamii ya kisasa.

Meider (1985) anarejelea zaidi utendakazi wa methali kwa kusema kuwa methali huwa na mchomo fulani kwa sababu baada ya mtu kuambiwa methali fulani, huathirika moyoni na huweza kutafakari kwa undani ujumbe uliofumbatwa na methali husika. Kwa njia hii, methali hutekeleza jukumu kubwa la kukuza na kuendeleza maadili ya wanajamii. Wanajamii hutarajiwa kufumbua maana iliyofumbatwa katika methali maalum kwa kutenda kama walivyoonywa, kutahadharishwa au kuwahamasishwa. Kuongezea ni kwamba, methali hizi ni tungo zilizoakisi ukweli wa maisha ya dunia katika jamii fulani na huchukuliwa na jamii kama semi zenye mshindilio mkubwa wa

maarifa ya kawaida, uzoefu busara na ukweli. Katika jamii ya Wanyankole tunapata methali zifuatazo zenye busara; '*Okukunda akuha ente otayenda kuofa akuha omukazi*' tafsiri yake, "Akupendaye hukupa ng'ombe na yule ambaye hakutakii kifo hukupa mke." Jamii ya Wanyankole ilienzi ndoa kama njia moja ya kuleta udugu na vilevile kuenzi wanyama wao ambao walikuwa ng'ombe. Aidha, methali hii ilikuwa inamkumbusha mwanamume kufanya kazi kwa bidii ili apate ng'ombe wa kutoa mahari ili apewe mke. Vilevile katika jamii ya kisasa, wanaume wanastahili kufanya kazi kwa bidii, ili wapate mahari ya kuoa ingawa wakati mwingine wanawake wanawasaidia. Kwa msingi huu, methali hii iliathirika kimuktadha na kimaana na kulazimika kudenguliwa.

Katika kusisitiza mawazo haya, methali kama vile "*Omukazi aba awamisho genyina"* tafsiri yake "Mwanamke anastahili kuwa na macho ya kuvutia na kupendeza kama ndama wa ng'ombe" inapaswa kudenguliwa. Katika jamii ya Wanyankole, ng'ombe ni mnyama aliyeenziwa zaidi na kwa hivyo jamii ilipendelea mwanamke kupewa sifa kama hizo ambazo zilikuwa tofauti na za mwanamume. Aidha, kutokana na hali hii, tunaona mwanamke anafananishwa na ndama ambaye alikuwa anapendeza na kuvutia. Ndama huyu mara nyingi, huwa anavutia kutokana na macho, upole, ukarimu, ujana wake na rangi yake. Kwa hivyo, mwanamke mzuri alistahili kuwa na sifa kama hizo ndipo mumewe ampende zaidi. Isitoshe, mwanamke alitazamiwa kuwa kifaa cha kumfurahisha mumewe kingono mbali na shughuli nyingine muhimu ndani ya ndoa. Hii ndiyo sababu tunaona analinganishwa na ndama ambaye ni mpole na ambaye anafaa kumfurahisha mmiliki wake pasi na kuteta.

Katika kufasiri maana ya methali hii lazima tuzingatie muktadha halisi wa jamii ya Wanyankole hasa wa jadi. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, methali hii huenda ikachukuliwa kuwa imepitwa na wakati. Mahusiano ya kijinsia ni tofauti hali kadhalika

vigezo vya mwanamke mzuri au mwanamume mzuri katika jamii vimebadilika. Kwa hivyo iwapo methali hii lazima itumike katika jamii ya kisasa ya Wanyankole lazima idenguliwe kimaana.

Methali ni aina mojawapo ya fasihi simulizi pendwa iliyojulikana kwa matumizi ya lugha ya mkato yenye mafunzo mahususi. Lugha ya mkato yenye madhumuni ya kuelimisha jamii hutumika sana na wakongwe kwa minajili ya kuwaelemisha wanajamii ambao wana jukumu la kufahamu historia na utamaduni wao. Kuhusu jambo hili, Alster (1993) anasema:

> Ni jambo la kawaida sana kwa wazee kutumia methali katika maongezi yao baina yao na hata wanapowasiliana na watu wengine. Aghalabu kuishi kwingi kwa wazee ni hazina kubwa na tajriba ya maisha marefu yenye michango ya dhana zinazobeba aina nyingi za fasihi mkiwemo methali. Kwa hivyo, hakuna mshangao kuona wazee wakitumia methali mara kwa mara zaidi kuliko watu wengine.

Kwa hivyo, kulingana na maelezo hayo, wazee katika jamii walikuwa na mazoea ya kutumia methali katika mazungumzo yao. Methali zilikuwa ni sehemu muhimu ya mawasiliano yao na yaliakisi ukwasi wa maarifa na hekima waliyodunduliza kutokana na siku nyingi walizoishi duniani. Huu ndio msingi wa wazee na hasa wanaume kuheshimiwa katika jamii. Hali hii inabainika katika methali ifuatyo: "*Ahunyineeka atari ebichere bitembe enju*" tafsiri yake "Penye mwanamume hapana vyura wanaopanda nyumba." Methali hii ilienziwa sana na wanaume katika jamii ya Wanyankole. Hii ni kwa sababu jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengwa kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendeshwa kwa ubabe-dume. Huu ndio msingi wa kuwalinganisha wanawake na vyura ambao hawakutarajiwa kuezeka nyumba. Miongoni mwa Wanyankole, mwanamume ndiye aliaminiwa kushikilia wadhifa wa kuwa kiongozi. Ndiye alitarajiwa kutoa mwelekeo katika takriban masuala yote kule nyumbani na katika jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, methali hii ilikuwa inaonyesha umuhimu wa mwanamume katika jamii akilinganishwa na mwanamke. Hata hivyo,

katika jamii ya kisasa, methali hii imepata kuathirika kipragamatiki kwa sababu jinsia zote zina uwezo wa kushikilia hatamu za uongozi. Kuna baadhi ya familia ambapo mama ndiye kiongozi kwa vile pengine baba ameaga dunia au ametelekeza majukumu yake. Amepewa fursa sawa katika nyanja tofauti ndani ya jamii. Kwa kweli siku hizi kazi ambazo zinafanywa na mwanamume zinaweza kufanywa na mwanamke pia. Hali hii imesababisha methali kudenguliwa ili kuafikiana na Wanyankole wenye tajiriba tofauti maishani.

Manufaa ya matumizi ya methali katika lugha hayawezi kutiliwa mkazo zaidi ya inavyostahili, kama Alexander (1985) alivyodai: *"Methali ni chombo kinachotumika na jamii kusafirisha maadili yake ya mwongozo kwa njia ya onyo, tahadhari, tashtiti, mawaidha, wasia, utafiti, kutia moyo na dhima nyingi katika mazingira hayo. Hii ni kazi mojawapo inayobatiza methali sifa ya chombo cha kusafirishia falsafa katika jamii."* Aidha, ni kutokana na madai haya, tunatambua kuwa jamii ya Wanyankole ilikuwa imegawanya majukumu yake kijinsia, na isitoshe ni kupitia methali hizi wanajamii waliongozwa katika utekelezaji wa majukumu yao, na kuonywa dhidi ya kutelekeza majukumu hayo katika jamii nzima. Kwa mfano katika methali hii; *"Orugyendo rwita abashaija okuzara kwita abakazi"* tafsiri yake, "Safari huwaua wanaume, ilhali kuzaa huwaua wanawake." Methali hii imeonyesha kuwa, mwanamume alikuwa na jukumu la kuwajibikia familia yake kwa kutembea safari ndefu kutafuta riziki, ilhali mwanamke alikuwa na jukumu la kuzaa na kulea watoto. Aidha, ni kutokana na majukumu haya tofauti, tunaona jamii inaonywa na kuelemishwa kuhusu umuhimu wa kufanya kazi na athari zinazojitokeza kutokana na kazi hizo tofauti. Kwa hivyo kutokana na muktadha wa kisasa, ingawa mwanamke angali na jukumu kuu la kuzaa na kulea, jamii ya kisasa imewahusisha wazazi wote katika malezi ya watoto kwa sababu ulezi ni jukumu nyeti na ambalo linahitaji jinsia zote mbili

tofauti na mtazamo wa jadi. Ni kwa msingi huu ambapo methali hii imepata kuathirika na kubidi kufasiriwa upya kipragmatiki ili kuafikiana na jamii ya kisasa ya Wanyankole inayobadilika kila uchao.

Zakaria (1989), katika kitabu chake cha methali za Kiswahili anasisitiza kuwa methali ni muhimu kwa vile hutumika kuwaelimisha watu wawe na utu na uvumilivu kwa wanajamii wenzao. Hii inamaanisha kuwa iwapo kuna methali ambazo zinaweza kuendeleza dhuluma dhidi ya baadhi ya wanajamii hazina budi kutupiliwa mbali. Kwa mfano katika jamii ya Wanyankole tunapata methali kama vile, *"Omwishikyi katwala ajumisha omugongo gwona"* ikitafsiriwa kama "Msichana akibebeshwa mimba husababisha wasichana wote kutukanwa kijijini." Kutokana na hali hii, msichana katika jamii ya Wanyankole hakuruhusiwa kupata mimba kabla ya ndoa. Hili lilikuwa jambo la aibu, ambalo lilimpelekea kuuliwa tofauti na mvulana ambaye alifukuzwa katika ukoo wao. Aidha, kutokana na utofauti katika kuadhibu jinsia hizi mbili, ni wazi kwamba methali hii iliendeleza dhuluma dhidi ya mtoto wa kike ilhali mtoto wa kiume ambaye bila shaka alihusika katika kumtunga mimba msichana haadhibiwi. Ni kutokana na mawazo ya Zakaria (keshatajwa) ndipo utafiti huu unasistiza kuwa methali hasa za kijinsia zinafaa kufasiriwa upya kipragmatiki ili kudengua maana na matumizi hasi kwa baadhi ya wanajamii.

Isitoshe methali kama kipengele cha lugha ya kimapokeo ya jamii, ilikuwa na maana mbalimbali katika matumizi yake katika jamii (Mtesigwa, 1989). Hali hii ilitokana na sababu kuwa methali ni misemo ya hekima na busara iliyobuniwa na kutumiwa kimapokezi katika mawasiliano ya jamii. Kutokana na dhima yake ya kale katika jamii, methali ziliweza kutumiwa na kurithishwa kimasimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hivyo, matumizi ya methali hizi yalikuwa na maana fulani katika jamii, mbali na kuwa kiungo au kitoweo muhimu cha lugha ambacho hutumiwa katika

kuyatafakari na kuyapima maisha huku zikifichua falsafa na hekima ya jamii katika muktadha wa utamaduni maalumu.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Ndalu na Kingei (1999) ambao wanafafanua methali kama usemi wenye fumbo lenye falsafa nzito, lenye utata na mguso wa jamii ambao ni msemo wenye ukale uliorithishwa kwa njia ya masimulizi kutoka kizazi hadi kizazi. Kutokana na fasiri ya wataalam hawa, ni wazi kuwa methali ni semi ambazo hufumbata maana ambayo ni tata kuifasiri kikamilifu. Hii inamaanisha kuwa methali moja inaweza ikafasiriwa kuleta maana anuai hasa katika miktadha tofauti ya kijamii.

Kutokana na maelezo ya Mtesigwa (1989) pamoja na Ndalu na King'ei (1999) ni wazi kuwa ijapokuwa methali ni sehemu ya turathi ya jamii iliyopokezwa kizazi baada ya kizazi, ni muhimu kutambua kuwa methali hizi zilisheni falsafa na maarifa ambayo yanahusishwa na muktadha na utamaduni maalum. Hii inamaanisha kuwa baadhi ya maarifa na utamaduni ulioafiki jamii katika kipindi fulani huenda yasiafiki wanajamii katika mazingira tofauti kihistoria na hata kijiografia. Hali hii ndiyo hupekelekea kuibuka kwa methali mpya au kudenguliwa kwa baadhi ya methali za kimapokeo ili zikidhi mahitaji ya jamii ya kisasa. Huu ndio msingi wa kuchunguza methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki na kidenguzi katika utafiti huu.

### 1.1.1 Asili ya jamii ya Wanyankole

Mungonya (1961) anaeleza kuwa Wanyankole walitokana na watu wawili; Bairu na Bahima na ambao ndio wazazi wa jamii ijulikanayo leo kama Wanyankole. Akina Bairu ni kizazi kilichojulikana kutokana na umaarufu wake wa kulima wimbi. Hiki ni chakula chao cha kawaida kilichotambulika kama "Oburo." Katika jamii ya Wanyankole, makundi haya mawili yalikuwa na hadhi tofauti. Kwanza kabisa, Bairu walikuwa wanatoka katika daraja la chini la jamii na walikuwa watumishi wa Bahima.

Bahima nao walikuwa wanatoka katika daraja la kifalme na ndio sababu walikuwa wanafanya kazi za kifahari kiuchumi kama ufugaji wa ng'ombe. Bahima wanatambulika kutokana na ng'ombe wao wa pembe ndefu. Katika jamii ya Wanyankole, ng'ombe ndio wanyama ambao wanaenziwa sana kutokana na manufaa yao kama vile maziwa, mafuta ya ng'ombe, nyama na ngozi. Ng'ombe walitumiwa kulipa mahari na kutoa kafara katika sherehe maalum za kidini, kitamaduni na za kisiasa. Ng'ombe wa Kinyankole wenye pembe ndefu walithaminiwa sana kwa sababu walistahimili ukame na magonjwa. Aidha, ng'ombe hawa walienziwa kwa kutoa idadi kubwa ya maziwa, rangi nyeupe na urefu wa pembe zao. Methali nyingi za kijinsia zilitungwa kutokana na ng'ombe hawa, kuthibitisha umuhimu wa ng'ombe katika jamii ya Wanyankole. Kwa mfano methali, "*Omukazi aba amate nka engente ayerinda ebitokozi"* ikitafsiriwa kama "Mwanamke ni kama maziwa ya ng'ombe, yafaa kuwa safi na mwenye tabia nzuri." Methali, *"Omukazi oyera amaino nka angete n'otari wawe"* tafsiri yake "Mwanamke ambaye ana meno meupe kama ng'ombe si wako." Methali hizi zilidhihirisha ubaguzi wa kijinsia kwani zinaelekea kusisitiza tabia nzuri kwa mwanamke pekee. Kutokana na mabadiliko mengi ndani ya jamii, methali za aina hii zinafaa zidenguliwe ili ziendane na matarajio ya jamii ya kisasa inayohimiza usawa wa kijinsia.

Kwa mujibu wa Morris (1950), mfumo wa ukoo katika jamii ya Wanyankole uliashiria ubaguzi wa jinsia. Morris anasema kuwa kitu mojawapo kilichounganisha Wanyankole wa kundi la Bairu na lile la Bahima ni nguzo ya kiutawala ya jamii ya Ankole kuegemea mfumo wa kuumeni. Mkuu wa familia na hivyo ukoo mzima wa Ankole alikuwa ni mwanamume. Wanyankole wote walitokana na mojawapo ya koo zifuatazo: Bahindi, Baititi, Bagahe, Basyaba na Bashambo. Ni kutokana na mfumo wa kuumeni katika jamii ya Wanyankole ndipo mwanamume akawa na hadhi ya juu katika takriban nyanja

zote za jamii ya Wanyankole akilinganishwa na mwanamke. Kwa hivyo takriban methali zote zilizotungwa zilizungukia mfumo wa kuumeni. Huenda waliozitunga walikuwa ni wanaume na kwa hivyo walihakikisha zinadumisha ubabe-dume. Kwa mfano methali kama vile *"Akashaija keyombekyi toketa kana"* tafsiri yake "Mwanamume ambaye amajijengea nyumba huwezi kumwita mtoto." Katika jamii ya Wanyankole, mwanamume hakustahili kudharauliwa hata kama alikuwa mdogo kimaumbile bali asifiwe kwa matendo yake.

Mfumo wa kuumeni katika jamii ya Wanyankole ulioendeleza ubabe-dume unaakisiwa pia katika methali ifuatayo: *"Omukazi oine Iba tarya nkonko"* ikitasfiriwa kama "Mwanamke aliye na mume hastahili kula nyama ya kuku." Katika jamii ya Wanyankole, ni wanaume ambao walistahili kula vyakula vizuri kwa madai kuwa walikuwa wanafanya kazi nzito zilizohitaji nguvu. Kwa hivyo mwanamke alinyimwa haki ya kupata lishe bora kwa madai kuwa hakuhitaji nguvu nyingi katika kazi zake ambazo hazikuthaminiwa sana zikilinganishwa na zile zilizotekelezwa na mwanamume. Kwa hivyo methali za aina hii zilikuwa zinaendeleza ubaguzi wa kijinsia katika masuala ya lishe bora katika jamii ya jadi ya Kinyankole.

Ujinsia pia ulijitokeza katika uwanja wa sheria na mahakama katika mwa jamii ya Wanyankole. Wanyankole walikuwa na sheria za kiasili ambazo zilitumika katika kuadhibu wahalifu. Adhabu iliyotolewa ilitegemea kosa na jinsia ya mhalifu. Kwa mfano kijana aliyemkosea babake, aliadhibiwa hadharani kwa njia ya aibu sana na pia aliamrishwa kumbeba babake mgongoni huku akizunguka ikulu siku nzima. Baba alikuwa na uhuru wa kumkojelea mwanawe kama ishara ya kufedhehesha kutokana na tabia yake mbaya. Kwa upande mwingine, mvulana aliyembembesha msichana mimba alipewa adhabu ya kufukuzwa katika ufalme huo maishani ilhali msichana aliuawa kwa

kuzamishwa ndani ya maji. Hapa tunaona kuwa msichana aliadhibiwa vikali kuliko mvulana. Hali hii inajitokeza katika baadhi ya methali za Kinyankole. Kwa mfano methali *"Omwana womwishikye katarwa ajumisa omugongo gwona"* tasfiri yake "Msichana akibebeshwa mimba husababisha wasichana wote kijijini kutukanwa," *"Omwana amanyirwa ahari ishe"* tafsiri yake "Mtoto hujulikana kutokana na baba yake." Katika jamii ya Wanyankole, ilikuwa ni jukumu la baba kumfunza mtoto wake wa kiume maadili mazuri ili kuepukana na hali hii ya aibu ya kufukuzwa katika ufalme wake. Kwa hivyo, jinsia zote zilikuwa zinaelimishwa kupitia methali ili kuepukana na adhabu kali. Kutokana na utofauti huu katika methali za kijinsia ndiposa kunakuwa na haja ya kuzihakiki ili kutathmini uamilifu wake katika jamii endelevu ya Kinyankole.

Ni dhahiri kuwa fasihi simulizi na hasa kipera cha methali kimechangia pakubwa katika kutekeleza shughuli za kila siku za jamii ya Wanyankole. Kuna wataalam ambao wamejitolea mhanga kuhifadhi historia na utamaduni wa Wanyankole. Maandishi ya George Nathan Patrick, H. F. Morris mnamo (1914-1890) na Mugonya (1961) yalikuwa msingi wa taarifa kuhusu chimbuko la jamii ya Wanyankole. Mugonya (keshatajwa) anaeleza kwamba utamaduni ni nguzo muhimu katika kila jamii. Hii ina maana kwamba, jamii bila utamaduni ni kama ganda tupu lisilo na thamani, ubunifu, heshima, lengo, maarifa, umoja, mshikamano na uwezo wa kujivunia miongoni mwa jamii zingine.

Jamii ambayo haidumishi utamaduni wake kwa kuurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine, haina budi kuzoroteka, kuoza, kugawanyika na mwishowe kutokomea. Ni kwa sababu hii, jamii ya Wanyankole na jamii zingine za Afrika zinahofia kwamba tamaduni zao zitatokomea hivi karibuni au baadaye ikiwa hakutakuwapo na majadiliano na nguvu za pamoja za kuokoa yale ambayo bado hayajapotea kwa vizazi

vya baadaye. Huu ndio msingi wa jitihada za Cisternino (1987) anayejaribu kukusanya baadhi ya methali za Wanyankole na kuzihifadhi kimaandishi kwa ajili ya kizazi kilichopo na kile kijacho. Kwa hivyo utafiti huu unawania kuzihakiki methali za kijinsia za Kinyankole kiundenguzi ili kuzihifadhi na kuziimarisha kipragmatiki.

### 1.1.2 Ndoa na familia katika jamii ya Wanyankole

Katika jamii ya Wanyankole msichana alipofikisha umri wa miaka minane au tisa, aliandaliwa kuolewa. Hakuruhusiwa kutembeatembea ovyo na hata chakula alichopewa kilikuwa tofauti na kile cha mvulana. Kwa mfano, alipewa nyama ya ng'ombe, uji wa wimbi na alilazimishwa kunywa maziwa kwa wingi. Miongoni mwa Wanyankole, unene uliandamana na urembo wa mwanamke. Msichana alipaswa kuwa mrembo na kupendeza zaidi kuliko mvulana. Aidha, mawaidha aliyopewa mtoto wa kike kabla ya ndoa, yalikuwa tofauti na yale ya mvulana. Kwa mfano, msichana alifunzwa namna ya kumtunza mumewe kwa kumpikia, kufanya tendo la ndoa kitandani, kudumisha usafi nyumbani na kutambua kuwa sehemu yake kuu ni jikoni. Kwa upande mwingine, mvulana alifunzwa namna ya kulinda boma lake, kuwajibikia mkewe na watoto, kuwinda, kuwa hakimu mzuri na mwishowe kuwa mjenzi hodari. Methali zifuatazo zilidhihirisha ujinsia huo "*Omwana omwe tamara nyina obugumba,*" ikitafsiriwa kama "Mtoto mmoja hamalizi mama yake ugumba." Katika jamii ya Wanyankole, mwanamke alistahili kuzaa watoto wengi kama ishara ya kuwa na kizazi kizuri. Pia, jamii ilikuwa na rasilimali nyingi ambayo ilikidhi mahitaji ya watoto wengi. Kwa hivyo, ilikuwa ni mwiko kwa mwanamke kuzaa mtoto mmoja tu.

Methali "*Eshaija ibiri tiritekwa mu nju emwe*" tafsiri yake "Wanaume wawili hawawezi kuishi kwenye nyumba moja." Jamii ya Wanyankole ilikuwa inaruhusu mwanamume mmoja kuwaoa wake wengi katika boma moja lakini si mwanamke

kuolewa na zaidi ya mume mmoja. Vilevile ilikuwa rahisi wanawake kuishi katika nyumba moja, tofauti na jinsia ya kiume ambayo haingethubutu. Ingawa jamii ya jadi ilikuwa inatumia methali hizi kufundisha majukumu ya watoto kijinsia, mabadiliko katika jamii ya Wanyankole yanachochea udenguzi ufanyike katika methali hizi katika muktadha wa kisasa. Kuna mabadiliko mengi ambayo yametokea katika jamii kwenye uwanja kama vile wa uchumi, siasa, elimu na utamaduni. Hali hii imesababisha muktadha wa methali mbalimbali za kijinsia kuathirika kimaana na kubidi kudenguliwa.

Kuhusu suala la ndoa, ilikuwa ni kazi ya baba na ukoo kumtafutia mvulana mke kutoka katika familia yenye historia nzuri. Jambo hili halikuwa linaruhusiwa kufanywa kwa jamii ya msichana. Wakati wa kuolewa, msichana alitarajiwa kuwa bikira tofauti na mvulana. Vilevile, jamii ilimtarajia mwanamke kumzaa mtoto wa kiume ambaye alikuwa mrithi. Kushindwa kumzaa mrithi, ilikuwa sababu mojawapo ya mwanamume kuoa mwanamke mwingine au kumtaliki mke wake wa awali. Kwa sasa, hali imebadilika katika majukumu ya kijinsia kwa sababu ya mabadiliko katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa hivyo basi, methali zinazohusu majukumu ya kijinsia, lazima zidenguliwe kipragmatiki ndipo ziafikiane na hali halisi ya jamii ya Wanyankole ya karne ya 21.

### 1.1.3 Nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii ya Wanyankole

Kulingana na Tumusiime (1982), Mwanamume miongoni mwa Wanyankole ndiye mwenye mamlaka yote. Alimiliki kila kitu wakiwemo wake zake. Isitoshe, wanaume walikuwa wanaruhusiwa kuoa wanawake wengi ili wapate watoto wengi. Kati ya watoto hawa wengi, mtoto wa kiume alithaminiwa kuliko wa kike. Hali hii inajitokeza katika methali, "*Ozara mwojo tacwa ruganda*" ikitafsiwa kuwa "Anayemzaa mtoto wa

kiume hakomeshi ukoo, bali huuendeleza tofauti na yule anayemzaa mtoto wa kike.” Kirindi (2008) anaongezea kwa kusema, katika jamii ya Wanyankole kukosa mtoto wa kiume ilikuwa ni wazi kabisa mwanaume kumuoa mke wa pili bila wasiwasi yoyote. Kwa hiyo, ndoa iliyokosa mtoto wa kiume iliwabidi kumchukua mtoto wa ndugu ya Bwana kuwasaidia kufuga ng’ombe na mwishowe kurithi mali ya familia hiyo. Suala la mrithi kuwa mtoto wa kiume katika jamii ya kisasa halina mashiko sana, kwa sababu jamii ya kisasa inachukulia mtoto ni mtoto; awe ni wa kike au wa kiume. Kwa vile jinsia zote zina fursa ya kwenda shule, watoto wa kike wanaruhusiwa kurithi mali ya wazazi sawa na wa kiume. Wazazi wa kisasa wamebadili msimamo kuwa, mtoto wa kike ni wa manufaa zaidi ukiweka suala la kuendeleza ukoo kando, watoto wa kike wanaonekana kuwajibikia familia zao kuliko wa kiume. Kwa msingi huu, methali hii haina budi kudenguliwa kuafiki jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Mwanamume alikuwa ana majukumu ya kawaida, ikiwemo kufanya kazi zote ambazo ni ngumu kama kujenga nyumba, kubeba vitu vizito, kuwinda, kulinda usalama wa boma lake, na hata kuhudhuria mikutano ya mahakamani kwa niaba ya mkewe ambaye hakuruhusiwa kuhudhuria. Jambo hili lilikuwa linamfanya mwanamke kubaki nyuma kimaendeleo. Mwanamke alitarajiwa kufanya kazi ambazo zilichukuliwa kuwa nyepesi lakini kwa mtazamo wa jamii ya kisasa zinachukuliwa kuwa nzito na zenye thamani kubwa. Majukumu haya yanajitokeza katika methali kama vile: *“Akaremire Omushaija tokazingira engata*” tafsiri yake “Kilichomshinda mwanamume huwezi kukitengeneza”, *“Omwana obushumba abuteerwa Ishe”* tafsiri yake “Umaskini wa mtoto hutokana na baba yake.” Methali hizi ziliweka msimamo wa kijadi bayana kuwa, mwanamume ndiye kiongozi na mwenye nguvu kuliko mwanamke. Hata hivyo, katika karne hii ya 21 wanawake wamepewa fursa sawa na wanaume kufanya kazi katika nyanja mbalimbali ndani ya jamii. Mabadiliko haya katika majukumu ya wanawake na

wanaume katika jamii ndiyo yamechochea utafiti huu kuchunguza maana na matumizi ya methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole.

Ujinsia pia ulijitokeza katika vyakula ambavyo wanawake na wanaume waliruhusiwa kula kitamaduni. Kwa mfano, miongoni mwa Wanyankole, mwanamume ndiye alistahili kula nyama ya mbuzi na wala sio mwanamke. Iliaminika kuwa wanawake wakila wangemea pembe na ndevu. Kizazi cha kisasa kinapinga methali hii kwa madai kuwa, jinsia zote zinafanya kazi sawa na zinastahili lishe bora. Aidha, kuna uwezekano ilikuwa ni tamaa na ubabe-dume ndio ulichochea jamii kuwanyima wanawake vyakula vilivyothaminiwa zaidi. Methali hii inatueleza zaidi, "*Omukazi tarya mbuzi*" ikitafsiriwa kama "Mwanamke hastahili kula nyama ya mbuzi." Methali hii inaenda kinyume na mapendekezo ya lishe bora hasa kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha. Kwa hivyo, methali za sampuli hii lazima zidenguliwe ili ziafikiane na uhalisi wa jamii ya Wanyankole wa kisasa.

### 1.2 Suala la Utafiti

Katika jamii ya Wanyankole ni muhimu kutambua kwamba, methali ni mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi vinavyoenziwa sana. Hii inatokana na ukweli kwamba kimapisi, methali zilitumika kutoa elimu, uhamasisho na burudani miongoni mwa mambo mengine muhimu katika jamii hii. Hata hivyo, kama ilivyo katika jamii nyingi ulimwenguni, jamii ya Wanyankole imepitia mabadiliko ya kitamaduni, kiuchumi, kielimu, kidini, kisiasa na kijamii kutokana na utandawazi. Hali hii imeathiri asasi za kijamii kama vile: mfumo wa jamii, lugha, utamaduni, fasihi ikiwemo. Kwa hivyo, pana haja ya kutathimini athari ya mabadiliko haya katika asasi hizi hasa katika fasihi simulizi. Methali za Wanyankole katika Karne ya 21 zimeshuhudia tafiti chache mno licha ya kipera hiki cha fasihi simulizi kuwa na dhima kubwa katika maendeleo ya jamii

ya Wanyankole. Dhima hizi zinaafiki malengo yake ya kitamaduni, kielimu, kiuchumi, kisiasa na kijamii kama jinsi inavyopendekezwa katika malengo ya kudumu ya kiulimwengu.

Kipera cha methali kimesheheni mila na utamaduni wa jamii ya Wanyankole katika miktadha mahsusi ambamo zilitungwa na kutumika. Methali hizi zimeendelea kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi pasi na kuzingatia mabadiliko ambayo yametokea katika jamii hii. Tafiti za awali zimejikita katika usawiri wa mwanamke peke yake katika methali za Wanyankole na kuupuuza ukweli kuwa methali za Wanyankole zinahusu jinsia zote mbili na uamilifu wake hauna budi kufumbata mabadiliko ya kiutandawazi kwa manufaa ya jamii katika kipindi cha sasa na cha siku za usoni. Ni kwa misingi hii ndipo utafiti huu unachanganua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwa mkabala wa kipragmatiki ili kutathimini jinsi mabadiliko haya yanaathiri usawiri wa jinsia katika methali hizi na ufasiri wa methali hizi kimaana na kimatumizi katika miktadha tofauti ndani ya jamii ya Wanyankole.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

i. Kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii.
ii. Kuchanganua maana na matumizi mbalimbali ya methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole.
iii. Kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Je, ni methali zipi za kijinsia zinajitokeza katika nyanja maalum katika jamii ya Wanyankole?

ii. Ni maana na matumizi yapi yanayojitokeza katika methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole?

iii. Methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zina uamilifu gani?

### 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada

Jamii ya Wanyankole imekuwa ikitumia fasihi simulizi ambayo imekuwa ikirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa upokezi wa mdomo kwa muda mrefu hadi leo. Ingawa jamii hii imekuwa ikitumia kipengele hiki kwa muda mrefu, hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu methali za kijinsia zinavyojitokeza katika miktadha tofauti ndani ya jamii hii.

Methali kama kipengele mojawapo cha fasihi simulizi kilienziwa zaidi kuliko vipengele vingine na kina babu kwa sababu kilitumiwa kila siku katika kuelimisha, kuburudisha na kuonya wanajamii kuliko kipengele kingine chochote. Ingawa jamii hii imekuwa ikitumia methali kwa ujumla, haijathubutu kuchunguza namna methali hizi za kijinsia zinavyoweza kuwaathiri wanajamii hawa kijinsia. Sababu nyingine ya kuchunguza methali hizi katika jamii ya Wanyankole, ni kwamba jamii hii imekuwa na miundo na utamaduni ambao umekuwa unaendeleza ubabe-dume katika nyanja tofauti ndani ya jamii. Hili lilifanyika kwa kugawa majukumu kijinsia na katika mgao huu ujinsia ulijitokeza kwa njia moja au nyingine.

Mathalan methali nyingi zilionyesha kwamba wanawake walipewa kazi nyingi na hasi ikilinganisha na zile zilizofanywa na wanaume ambazo zilikuwa za hadhi ya juu. Inaonekana kazi walizozifanya wanaume zilikuwa za kifahari na za kiuongozi zaidi. Kwa hivyo, katika kuchunguza methali hizi za kijinsia, kipengele cha udenguzi kinaenda kutumiwa kwa Mtazamo wa Kipragmatiki ili kuweza kutambua, iwapo methali hizi bado zina mashiko katika jamii ya Wanyankole wa kale na wale wa jamii

ya kisasa. Kufanikisha hili, methali hizi zimeweza kuhusishwa katika miktadha tofauti ndani ya jamii hii kama vile kindoa, kisiasa, kielimu, kiuchumi, na kitamaduni. Kwa hivyo, mtafiti alitaka kuchunguza zaidi namna jamii hii iliyo na imani, mila, desturi na utamaduni wake, inavyozungumzia suala la ujinsia kupitia methali za Wanyankole.

### 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti ulihusu uhakiki wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwa mtazamo wa Kipragmatiki. Wanyankole ni kundi la watu wanaopatikana Magharibi nchini Uganda Wilayani Bushenyi. Vilevile, lugha inayozungumzwa na jamii hii ni Runyankole. Katika wilaya hii, mtafiti alihusisha watafitiwa kumi na wawili kutoka katika makundi maalum. Mtafiti alihusisha wanaume na wanawake. Alihusisha wazee sita wenye umri kati ya miaka 50- 80 kutoka eneo la vijijini Wilayani Bushenyi ambapo mazingira ni yale yaliyokuwa na mashiko thabiti ya fasihi simulizi na eneo asili la jamii ya Wanyankole. Vilevile, watafitiwa wanawake na wanaume sita wenye umri kati ya miaka 25-45 walihusishwa katika utafiti huu. Watafitiwa hawa ni wale wanaopatikana katika mazingira ya kisasa ya mjini lakini wenye asili ya Kinyankole na wenye mtazamo tofauti kuhusu suala la methali za kijinsia. Sababu za kuteua makundi haya mawili ni kwamba, watafitiwa katika kundi la kwanza wenye umri kati ya miaka 50-80 walizaliwa wakati ambapo fasihi simulizi ilikuwa imeshika mizizi katika jamii hii. Kwa hivyo, bila shaka maoni yao ya kijadi yalimfaa mtafiti kulijibu suala la utafiti. Kutokana na dai hili, mtafiti aliweza kutumia lengo la kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, aliweza kutambua namna methali hizi za kijinsia zilivyojitokeza tofauti kimaana katika jamii hizi mbili za Wanyankole.

Kundi la pili lenye watafitiwa wenye umri kati ya miaka 25-45 lilipatikana katika mazingira ya mjini. Kundi hili lilimsaidia mtafiti kutambua utofauti uliopo kati ya jamii ya kisasa ya Wanyankole na ile ya kijadi. Lilimsaidia mtafiti kulinganisha mitazamo yao tofauti kuhusu kipengele hiki cha methali za kijinsia kutokana na jamii hii inayokua kila uchao kwa Mtazamo wa Kipragmatiki. Utofauti huu ulisaidia kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa miongoni mwa Wanyankole. Kwa hivyo, michango ya watafitiwa hawa wote katika makundi haya tofauti ilikuwa ya manufaa zaidi katika kulijibu suala la utafiti. Mtafiti aliteua Wilaya ya Bushenyi Magharibi mwa Uganda kama mahali mahususi pa kufanyia utafiti kwa sababu sehemu hiyo kulipatikana wazungumzaji wa Kinyankole na ndiyo makao yao asilia. Hili liliwezesha mtafiti kupata data kamili kuhusu methali za kijinsia kuliko sehemu nyingine yoyote. Eneo la mjini lilikuwa la manufaa katika kumpatia mtafiti data kwa sababu ni sehemu mojawapo ambapo kizazi cha kisasa kimepata kuzaliwa na kulelewa tofauti na mazingira ya kijijini. Kutokana na utofauti huu wa kimazingira kama vile kielimu, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni, mtafiti aliweza kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii.

Kwa ujumla, mtafiti alihusisha watafitiwa kumi na wawili na methali arobaini na mbili. Sababu ya kuteua watafitiwa kumi na wawili ni kwamba, hii ndiyo idadi ambayo mtafiti alitambua kuwa na uzoefu wa methali hizi kutokana na mazingira wanamoishi na waliweza kujibu suala la utafiti. Isitoshe, ilikuwa ni idadi ambayo mtafiti alionelea ingemfaa kwa sababu makundi yote mawili yalikuwa yamegawika kijinsia. Kutokana na mgawanyo huu, mtafiti alipata maoni tofauti ambayo yalisaidia kupata data ya utafiti. Hata hivyo, malengo ya utafiti yalichangia uteuzi wa watafitiwa kumi na wawili waliotumiwa pamoja na methali arobaini na mbili za kijinsia ambazo hazikuhitaji idadi kubwa ya wasailiwa kuzishughulikia. Hata hivyo, ni methali arobaini na mbili ndizo

mtafiti alitumia, kwa sababu ziliweza kubeba ujumbe mahususi ambao ulihitajika katika kujibu suala la utafiti.

### 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa wa manufaa katika kupanua uelewa wa methali katika utamaduni wa jamii ya Wanyankole. Hii ni kwa sababu, methali hizi za kijinsia zimechangia pakubwa katika kuhakiki methali hizi kwa kutumia kipengele cha udenguzi kwa Mtazamo wa Kipragmatiki.  Methali hizi zimewekwa katika makundi mawili ya kimajukumu; yaani zile zinazomhusu mwanamke na zile zinazomhusu mwanamume katika miktadha tofauti ndani ya jamii ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, tumetambua namna methali hizi zinavyoweza kujitokeza kijinsia katika miktadha tofauti ndani ya jamii na kuathiri maana na matumizi ya methali hizi baada ya kudenguliwa.

Utafiti huu pia utafaidi na kuchangia katika uwanja wa fasihi, kwa sababu kipengele cha fasihi simulizi ndicho kigezo kikuu katika utafiti huu. Pia, kitasaidia kuweka wazi namna kipera chake cha methali kinavyoweza kusaidia jamii hii kuelewa namna ujinsia unavyoweza kujitokeza ndani ya jamii, kutokana na majukumu tofauti. Vilevile, kitawezesha kuhimiza ufasiri mbadala wa methali ili kukirutubisha kipengele hiki cha fasihi simulizi kwa kuchochea vipengele vingine vya fasihi simulizi. Vipengele vinavyoweza kuchochewa ni kama vile vitendawili, nyimbo, misemo, ngano, mafumbo na ushairi ili viweze kutumiwa katika kushughulikia suala la ujinsia ndani ya jamii zao. Hili litakuwa ni jambo la busara katika kuchunguza miktadha ipi ya kijamii inayoathiri usawiri wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole na jamii nyinginezo kwa kutumia vipera vingine vya fasihi. Aidha, utafiti huu utabainisha uamilifu wa methali

za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa ya Wanyankole ambayo ni miongoni mwa jamii nyingine za Kiafrika.

Kundi jingine ambalo litafaidika kutokana na utafiti huu ni walimu wa somo la fasihi ya Kiswahili. Kundi hili hasa ni la wale ambao wanataka kujiendeleza katika fasihi kwa kuchunguza namna fasihi inavyoweza kutoa michango mikubwa katika kutumia vipengele vyake kama vile fasihi simulizi. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni zile za Ufeministi wa Kiafrika na Udenguzi kwa sababu zinaenda kuchangia katika uelewa wa walimu na wanafunzi katika kutambua mchango wa nadharia hizi katika utekelezaji wa kazi yake. Pia, walimu na wanafunzi wataelewa namna nadharia hizi zilivyo na mchango mkubwa katika fasihi na si isimu peke yake.

Huku sifa muhimu za mikabala ya nadharia hizi zikiwekwa wazi katika utekelezaji wa kazi yake, nadharia hizi zitasaidia kutatua suala la kuimarisha mahusiano ya kijinsia katika jamii ya Wanyankole na hivyo kupunguza migongano ya kijamii. Hii ni kwa sababu Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imesaidia kuweka wazi vipengele ambavyo vinapatikana ndani ya jamii na vinavyosababisha migongano kama vile utabaka, utamaduni, uchumi, elimu, siasa, ndoa na historia ambavyo vimechangia katika kumdunisha mwanamke. Kwa upande mwingine, Nadharia ya Udenguzi imesaidia katika kubomoa maana mbalimbali za methali za kijinsia na kusaidia kuelimisha wanajamii kuwa, kuna uwezekano wa jinsia zote kushirikiana katika maendeleo ya jamii kutokana na miktadha tofauti inayopatikana ndani ya jamii bila migongano.

Utafiti huu ulihusu uhakiki wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwa mtazamo wa Kipragmatiki. Kwa hivyo, utafiti huu utasaidia kuondoa mtazamo hasi wa kale kuhusu majukumu tofauti ya jinsia, kwa kuonyesha na kuelimisha jamii kwamba katika karne hii inabidi wanaume na wanawake washirikiane katika kutekeleza

majukumu yao nyumbani. Hali hii itaepusha kubaguana kama ilivyokuwa ikifanyika katika enzi za kina babu zetu. Kwa muda mrefu, waandishi na wataalamu wengi wameshikilia msimamo kuwa methali hizi ziachwe namna zilivyo kwani zilionyesha nafasi ya kila jinsia katika jamii, jambo ambalo tumeonyesha kwamba sivyo. Mazingira ambamo methali hizi zimeibuka na kutumiwa yamebadilika kutokana na mabadiliko ya utamaduni, uchumi, siasa, elimu na ndoa. Kwa hivyo, kuna haja ya kuzitupilia mbali, au kuzifasiri upya methali hizi kutokana na ulimwengu wa utandawazi unaokua kila uchao. Hata hivyo, bado kungali baadhi ya methali ambazo zinaenziwa na jamii zote mbili na kupendekezwa zihifadhiwe kwa manufaa ya kizazi kijacho.

**1.8 Hitimisho**

Sura hii imeweka bayana usuli wa mada ya utafiti, pale ambapo tumetambua jamii ya Wanyankole kitamaduni ilikuwa inatunga methali kutokana na jinsia na wala si kwa uwezo wa mtu. Pia, uchumi wao ulikuwa umefungamana na ufugaji wa ng’ombe. Vilevile, katika suala la utafiti, tumetambua mwamko mpya ndani ya jamii hii kama vile wa; kiuchumi, kisiasa, kielimu, kidini, kindoa na kitamaduni ambao umechangia pakubwa katika kuleta mabadiliko ndani ya jamii hii. Aidha, katika sura hii tumebainisha umuhimu wa utafiti katika jamii ya Wanyankole na jamii zingine kwa jumla ikiwemo wasomi na walimu. Utafiti umeonyesha mtazamo mpya kuhusu jamii ya Wanyankole, ambapo mwanamume au mwanamke anaweza kusoma kazi hii na kubadili mtazamo wake kuhusu suala la ujinsia. Hili limetokana na dunia kuwa kijiji kidogo ambacho kimechangia pakubwa katika kuleta mabadiliko ndani ya jamii ya Wanyankole. Kwa hivyo, utafiti huu umeleta picha mpya katika jamii ya Wanyankole, kwa kuangazia zaidi kwa nini methali hizi zilihitaji kudenguliwa kwa Mtazamo wa Kipragmatiki katika jamii hizi mbili za Wanyankole. Sura inayofuata inashughulikia mapitio ya maandishi yanayohusu mada ya utafiti na kiunzi cha nadharia

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tuliangazia masuala ya msingi ya utafiti huu. Sura hii imezungumzia yale tuliyoyadurusu kuhusiana na mada ya utafiti pamoja na nadharia zilizotuongoza katika utafiti huu zikiwa ni Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na ile ya Udenguzi. Aidha, tumeeleza yale yaliyokwisha kuandikwa juu ya mada kwa kubainisha namna hoja zilivyojitokeza, kutathimini jinsi hoja hizi zinavyoafikiana na utafiti wetu na kisha kupambanua tofauti ya kazi zao na kazi yetu. Maandiko haya yamegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni: Dhana ya lugha na jinsia, maandiko kuhusu hadhi ya mwanamke na mwanamume ikiwemo kigezo kikuu cha methali za kijinsia. Mwishowe, tuliangazia nadharia za utafiti zilizofanikisha utafiti huu. Mapitio ya maandishi hayo yamekuwa ya manufaa kwa sababu yalisaidia kuimarisha hoja za utafiti na vilevile kuonyesha pengo lililoachwa, hivyo kuzua tatizo la utafiti huu.

## 2.1 Mapitio ya Maandishi

Sura hii imehakiki maandishi mbalimbali yaliyohusiana na malengo ya utafiti huu. Maandiko haya yamegawanywa katika sehemu kuu mbili: yaliyoandikwa kuhusu lugha na jinsia na yaliyoandikwa kuhusu hadhi ya mwanamke na mwanamume ikiwemo kigezo kikuu cha methali za kijinsia. Kwa hivyo, tumefafanua dhana ya lugha na jinsia na pia kuangazia maandishi mbalimbali yanayohusu methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole na kwa ujumla katika jamii nyinginezo ulimwenguni.

## 2.2 Dhana ya Lugha na Jinsia

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii nyingi ulimwenguni ambazo zinatumia methali kama njia mojawapo ya mawasiliano. Aghalabu, lugha inavyotumiwa katika

jamii huakisi ujinsia unaojitokeza katika maongezi ya kila siku katika miktadha tofauti. Jamii ya Wanyankole imekuwa ikizitumia methali katika shughuli mbalimbali tangu jadi hadi leo. Kwa hakika, methali ni kipengele mojawapo cha lugha ambacho huwasilisha mahusiano ya kijamii yakiwemo yale ya kijinsia.

Kabla ya kupambanua uhusiano uliopo baina ya lugha na jinsia, ni muhimu kupambanua dhana za 'lugha' na 'jinsia'. Kulingana na TUKI (1990) lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni sawa ama utamaduni ambao unafanana. Naye Mgullu (1999), anasisitiza kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu ambazo zimekubaliwa kutumiwa na watu wa taifa au kundi fulani kwa lengo la kuwasiliana vyema. Nao Mohammed (2000) na Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanadai kuwa jinsia ni kigezo cha maumbile ambapo kibaolojia inadhihirisha iwapo mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume pamoja na majukumu yanayohusishwa na maumbile hayo. Mawazo haya yanaungwa mkono na Edward (1985) anayedai kuwa jinsia ni ufafanuzi wa matokeo ya kijamii yanayosababishwa na hali ya kuwa mwanamke au mwanamume kutokana na kazi wanazozifanya.

Katika jamii ya Wanyankole, ujinsia unatokana na majukumu au kazi maalum ambazo hutengewa wanawake na wanaume katika jamii. Hoja hii inathibishwa na Tusiime (1982) ambaye anapambanua tofauti baina ya wanawake na wanaume ifuatavyo: wanaume huchukuliwa kuwa viongozi ilhali wanawake huwategemea wanaume, wanaume ni wenye nguvu ilhali wanawake ni dhaifu; wanaume ni jasiri ilhali wanawake ni waoga; wanaume ni wenye akili timamu na wanawake ni wenye mihemko na mwisho mwanamume ni mshari na mwanamke ni mpole.

Ijapokuwa sifa anazozirejelea ni zile ambazo kitamaduni zimehusishwa na wanaume na wanawake katika jamii ya Wanyankoe, ukweli ni kuwa hali imebadilika kadiri jamii

ya Wanyankole imeendelea kijamii, kisiasa na kiuchumi. Graddol na Swann (1989) pia wanasisitiza kuwa tofauti za kijinsia hutokana na mazingira wanamokulia wanadamu. Siku hizi baadhi ya watu hujishughulisha na kazi mbambali ili kukidhi mahitaji yao kiasi cha kuvunja mipaka ya kitamaduni kuhusu ugavi wa majukumu kijinsia.

Ukweli ni kwamba namna jamii inafasiri 'jinsia' itaathiri lugha inayotumiwa katika miktadha mbalimbali ndani ya jamii, kwani lugha huwasilisha masuala na mahusiano ya kijinsia. Kwa hivyo, methali ambazo hujengwa kwa lugha nazo zaweza kudhihirisha mahusiano ya kijinsia katika jamii-lugha ya Kinyankole.

Lugha pia huhusishwa na masuala ya kijinsia; yaani uhusiano kati ya wanawake na wanaume na pia huchangia katika kuendeleza tofauti kati ya jinsia hizi mbili. Haya yanadhihirishwa na Reik (1945) anayedai kuwa kuna maongezi ya wanaume na ya wanawake.  Reik anasisitiza kuwa lugha ya wanaume mara nyingi huwa ni ya wazi na isiyokuwa na haya. Anatetea hoja yake kwa kutoa mfano kwamba, ni nadra kwa mwanamke kusema "hapa pananuka" iwapo atapita mahala ambapo mbwa amefia. Badala yake, huenda akasema "Hapa pana harufu mbaya." Hali hii pia inajitokeza katika jamii ya Wanyankole. Kwa kawaida, wanawake Wakinyankole hutumia tafsida kupunguza ukali katika kuzungumzia masuala nyeti kama vile sehemu za siri. Hata hivyo, kwa wanaume, maneno ya siri husemwa hadharani hali ambayo huchukuliwa kuwa kawaida.

Wanaume wa Kinyankole hadharani hurejelea wanawake wachafu ifuatavyo; *"Nonuka etuutu"* tafsiri yake "Unanuka jasho." Hali ni tofauti ikiwa ni mwanamume ndiye anayenuka jasho, mwanamke atamwambia kwa heshima na upole, "*Iroko onabe wariha*" tafsiri yake "Nenda ukaoge umechoka," *"Otwijukye"* tasfiri yake "Utukumbuke" badala ya mwanamke kumwomba mumewe mahitaji ya nyumbani

akiwa anaondoka atamkumbusha kwa upole mumewe kwa kutumia maneno hayo. Tofauti na mwanamume ambaye angemwambia mkewe "*Orete ebintu byomuka"* ikitafsiriwa kama "leta vitu vya nyumbani," *"kyinga ekyinwa kyawe wayomba"* tafsiri yake ikiwa "Funga domo lako unapiga kelele. Maneno haya husemwa na mwanamume akiwa anagombana na mkewe ilihali mwanamke humwambia "*Nakushaba gamba mpola"* ikitafsiriwa kama "Tafadhali naomba uzungumze kwa sauti ya chini." Kwa hivyo, ni dhahiri kabisa kwamba lugha ya wanaume ina ukali kuliko ya wanawake. Kwa mantiki hii, lugha inayotumika katika methali kwenye mazungumzo au maandishi inaweza kutambulisha jinsia ya msomaji au mwandishi wa matini husika. Kwa mfano, tunapochungaza methali, "*Ozara omwojo tacwa ruganda"* tafsiri yake "Anayemzaa mtoto wa kiume hakomeshi ukoo." Neno '*tacwa*' linamaanisha kutoweza kukatika. Neno hili liliashiria ukali katika jinsia ya kike tofauti na ile ya kiume. Kiini ni kwamba jamii ilimwona mwanamke kuwa sababu kuu ya kukomesha ukoo tofauti na mwanamume. Jambo hili ni tofauti katika jamii ya kisasa ambapo imebainika kwamba kiafya kila jinsia inaweza kushindwa kuzaa.

Katika kusisitiza hoja hii, methali kama vile, *"Ozara omwana omwe tahwa bugumba"* tafsiri yake "Anayemzaa mtoto mmoja haishi ugumba." Neno "*Obugumba"* lilizua hisia kali na za aibu kwa sababu mtu kukosa kuzaa ilikuwa ni jambo baya sana. Ingawa neno 'obugumba' lilizua hisia kali, wanaume hawakuona ubaya kulihusisha na mwanamke ambaye alikuwa amebahatika angalau kumpata mtoto mmoja. Isitoshe, kutokana na maarifa ya kisayansi, ugumba huweza kutokana na maumbile ya mwanamke au mwanamume. Kwa hivyo si haki kumalaumu mwanamke wanandoa wanapokosa kupata kizazi. Kutokana na mfano huu, mtafiti aliona kuwa methali hizi zilipaswa kudenguliwa kwa sababu maana na matumizi yake yalikuwa yameathirika kutokana na mitazamo tofauti ya Wanyankole wa jadi na wale wa kisasa.

Dhana ya ‘jinsia’ kwa mujibu wa Iribemwangi na Mukhwana (2011) ni kigezo cha maumbile ambapo kibayolojia kinadhihirisha ikiwa mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume, na hali hii haibadiliki kamwe. Madai haya ya utofauti wa jinsia yamechangia pakubwa katika majukumu tofauti yanayofanyika ndani ya jamii ya Wanyankole. Majukumu haya yanaenda pamoja na lugha ambayo kila jinsia inatumia katika kutekeleza kazi. Kwa mfano, katika jamii ya Wanyankole mwanamume ndiye msema yote. Jamii inamtarajia awe anatoa amri katika kila sekta ya jamii ndipo atambuliwe kuwa mwenye boma. Kwa mfano, katika methali *“Omushaija aba byoona*” tafsiri yake “Mwanamume ndiye kila kitu”, na mwanamke alistahili kunyenyekea kwa kila hali katika majukumu yake ndani ya boma. Kwa hivyo, matumizi ya kirai ‘mmaliza yote’inaashiria ukali kwa kuonyesha nguvu alizonazo mwanamume akilinganishwa na mwanamke. Aidha, lugha ambayo imetumika, imeonyesha ukali na nafasi ya mwanamume katika jamii.

Ngugi (1975) anasisitiza kuwa lugha hutumiwa kuendeleza taasubi ya kuwadunisha wanawake. Anasema lugha ni chombo kinachotumiwa kutoa taswira hasi za mwanamke katika jamii. Ndungo (1985) ameangalia suala la mwanamke katika nyakati mbalimbali za kihistoria kulingana na mabadiliko katika mazingira yake. Picha ya mwanamke inayojitokeza ni ya kiumbe duni ambacho kimeshurutishwa na mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume. Ni kutokana na ukweli kuwa lugha husheheni ujinsia ndiposa tunachunguza methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki.

Aidha, Evans (2010) ametafiti kwa kina kuhusu unyanyasaji wa kiusemi katika ndoa huko Marekani ya Kaskazini. Anabainisha kategoria kadhaa za unyanyasaji wa kiusemi ambazo ni kuficha hisia, mawazo au habari yoyote; upinzani wazi dhidi ya hoja;

unyanyasaji wa kimzaha; kukata kauli na kupotosha; kushauriana katika ndoa; kutoa hukumu; vitisho; matumizi ya lakabu; kujifanya kusahau; kuamrisha pamoja na kudhihirisha hasira. Kategoria hizi kwa ujumla zinalenga kumdhulumu, kumfanya awe na wasiwasi na mwishowe kumweka chini mwathiriwa, huku mnyanyasaji akihisi ushindi na kuendeleza mamlaka yake. Hali hii ilijitokeza mno katika methali za kijinsia za Wanyankole pale ambapo mwanamke alitazamiwa kuwa kiumbe duni katika hali zote za jamii, huku mwanamume akipewa sifa zote za hadhi ya juu. Kwa mfano katika usemi wa kila siku tunapata methali hii; "*Omusyo tigurara na nyama"* ikitafsiriwa kama "Kisu hakilali na nyama". Tunapochunguza kwa undani methali hii, tunatambua mwanamume ndiye kisu ilihali mwanamke ni nyama. Kumaanisha mwanamume alikuwa mtu mkali, kiongozi na mwenye kuogopwa siku zote tofauti na mwanamke aliyekuwa hana uwezo wa kufanya chochote ila kumhudumia mwanamume daima kwa kulinganishwa na nyama. Aidha, ni kutokana na usemi kama huu, tunaona ujinsia unavyojitokeza katika methali za Wanyankole na kusababishwa kufasiriwa upya katika jamii ya Wanyankole.

Utafiti wa Kramer (1974b) uliohusu maneno mwiko, hasa yale yaliyo na herufi nne au tano, mathalan, "kuma" na "tako" kadhalika unaonyesha kuwa wanaume wavulana wa kiume ndio wanaopenda kutumia maneno haya. Vilevile, katika jamii ya Wanyankole, maneno ya mwiko husemwa na wanaume hadharani bila haya, tofauti na wanawake ambao huogopa kutamka maneno hayo. Aidha, ni lazima wanawake watafute msamiati unaotoa ukali wa maana ya neno hilo waziwazi; kukosa kufanya hivyo, watakuwa wameenda kinyume na utamaduni. Mawazo haya yanaungwa mkono na baadhi ya methali za Wanyankole, ambazo zina mashiko na maneno ya mwiko ambayo wanaume au wavulana hutumia hadharani bila kuogopa. Kwa mfano, "*Efakazi tegaya mboro"* ikitafsiriwa kama "Mjane hadharau mboro", neno hili 'mboro' linaibua hisia kali na pia

methali hii inamdhalilisha mwanamke. Ni bayana mjane hakuwa na hiari kujichagulia mwanamume. Jamii ilimpatia mwanamume yeyote kwa sababu hakuwa na usemi juu ya mwili wake. Hii inamaanisha kuwa mtunzi wa methali hii ni mwanamume. Mwanamke angetumia neno angalau 'uume' kuficha ukali wa neno 'mbolo'. Huu ndio msingi mmojawapo wa kuchanganua methali za kijinsia za Kinyankole ili kudengua maana hasi katika baadhi ya methai hizi.

Kulingana na Litosseliti (2008), maneno *uana* na *jinsia* mara nyingi hutumiwa kama visawe. Wananadharia wa lugha na jinsia, wamegundua uana kama dhana ya saikolojia na utamaduni. Hurejelea kazi wapewayo wanajamii, kwa msingi wa hali yao kibayolojia zenye tamaduni tofauti. Lugha isemwayo na mwanamke ni tofauti na ile inayosemwa na mwanamume. Mambo mengi yanayohusishwa na hotuba za wanawake, huwa ni tofauti kijinsia na mara nyingi humpatia mwanamke nafasi hasi katika jamii nyingi. Aidha, kuna madai kwamba ingawa wanaume wanazungumza sana kuwazidi wanawake, wanawake wana uwezo wa kuzungumza vizuri sana wakiwa wanazingatia stadi za lugha kuliko wanaume. Ninakubaliana na mawazo haya kwa mfano kuhusu suala la siasa katika jamii ya Wanyankole, ambapo wanaume huzungumza sana kuliko wanawake. Vilevile, kwa upande wa wanawake, wao hupanga maneno kitaratibu kujizuia kuongea sana kwani ni kinyume na utamaduni. Hata hivyo, mwanamke hujaribu iwezekanavyo, kutumia lugha sanifu jambo ambalo wanaume wengi huwa hawalizingatii wanapokuwa wanazungumza. Hali hii inatokana na utamaduni kumhusu mwanamke kuwa mwenye maneno machache. Ilikuwa ni ishara mbaya mwanamke kuzungumza kupita kiasi. Kwa mfano, katika methali hii, "*Omukazi mubi omumanyira ahangamba*" ikitafsiriwa kuwa "Mwanamke mbaya hutambuliwa kutokana na maongezi yake."

Aidha, kutokana na mawazo haya, imejitokeza wazi kuwa mwanamke katika jamii ya Wanyankole hakuwa huru kugombea nyadhifa ambazo zilihitaji mtu kuzungumza sana, kwa madai ilikuwa ishara ya utovu wa nidhamu. Hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kumzuia mwanamke kujieleza vilivyo. Ubaguzi wa aina hii umetupiliwa mbali katika jamii ya Wanyankole ya kisasa kwa kuzipatia jinsia zote fursa sawa za kielimu, kisiasa, kindoa, kidini, kiuchumi na kitamaduni. Wanawake wana fursa ya kupata elimu ya kisasa na kugombea baadhi ya nafasi ambazo zinahitaji kuzungumza sana kama vile za kisiasa. Lubuuka (2010), anadai kuwa methali zinapotumiwa katika maongezi ya kawaida, huendeleza ubaguzi wa kijinsia hasa dhidi ya mwanamke.

Methali nyingi katika jamii ya Wanyankole kama zilivyokusanywa na Lubuuka (2010), zilimdunisha mwanamke na kumbagua kitamaduni. Mfano wa methali za aina hii ni "*Abakazi nendere tizihwa murutokye"* tafsiri yake "Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani"; "*Omukazi ne'ibega"* tafsiri yake "Mwanamke ni bega." Methali kama hizi ziliendeleza ujinsia kwa kuonyesha jinsi mwanamke alivyobaguliwa katika lugha ya maongezi ya kila siku kiasi cha kumlinganisha na majani ya migomba. Katika kurejelea methali hizi ambazo Luubuka alitumia kumsawiri mwanamke, ni wazi kabisa zilimsawiri mwanamke wa Kinyankole kama kiumbe cha thamani ya chini katika jamii. Kwa mfano, tunapochunguza methali hii; "*Abakazi nendere tizihwa murutokye" tafsiri yake* "Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani," neno 'nendere' tafsiri yake "Majani ya migomba" lina ukali sana, kwa sababu majani haya huwa mengi sana shambani. Hii inamaanisha kuwa japo idadi ya wanawake ni kubwa, thamani yao ni ndogo ikilinganishwa na ile ya wanaume.

Mugo (1982) anathibitisha kudunishwa kwa mwanamke katika masuala ya ndoa anaposema: "Mwanamume alipendelea kuoa mke mchanga katika uzee wake ili yule

mwenye “damu moto” ya ujana amhudumie na kumsisimua mzee. Katika kufanya hivi, mzee yule anakuwa anasisimka kila wakati na kuchangamka, na hivyo kuonekana mchanga kila uchao.” Hii ni kuonyesha kuwa wanawake walichukuliwa kuwa viumbe vya kuwastarehesha wanaume. Japo ‘damu’ ni kitu cha thamani katika maisha ya wanadamu, mwanamke hathaminiwi zaidi ya kumfurahisha mwanamume kitandani.

Kutokana na usawiri huu, jamii ya kisasa imepinga vikali methali hii, na kusisitiza vikwazo vyote ambavyo vilikuwa vimewekwa dhidi ya mwanamke wa kijadi vivunjwe. Katika kufanikisha hili, jinsia zote zimepewa fursa sawa katika kugombea nyadhifa sawa ndani ya jamii. Jambo hili limemfanya mwanamke kujiendeleza pasipo kumtegemea mwanamume kama ilivyokuwa kijadi. Kwa hivyo, ufaafu wa methali hizi katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole utapatikana zinapodenguliwa kimaana na kimatumizi.

Holmes (1992) anaeleza sababu za wanawake kutumia lugha sanifu kuliko wanaume. Kwanza Holmes anadai kuwa wanawake huwa na ufahamu wa hadhi za kijamii wakilinganishwa na wanaume. Hii ni kwa sababu wanawake hutarajiwa kuwa na “tabia nzuri” kuliko wanaume. Aidha, wanawake ndio hupewa wadhifa wa kurekebisha tabia za watoto katika jamii nyingi. Kutokana na wadhifa huu, jamii hutarajia wanawake wazungumze kwa njia mwafaka huku wakitumia lugha sanifu hasa wanapoipokeza kwa kizazi kipya. Aidha, wanawake wanapaswa wawe wanyenyekevu na wasiwachokoze mabwana zao. Kwa hivyo, wanawake hutarajiwa wazungumze kwa upole tena kwa makini. Angalau upole huo hudhihirika kupitia matumizi ya fani za lugha sanifu. Kwa upande mwingine, Klein (1971) anadai kuwa lugha ya wanaume haina upole wowote ikilinganishwa na ile ya wanawake. Hali hii hujitokeza wakati wa kutoa hotuba hadharani.

Akishadidia tofauti baina ya Lugha ya wanaume na wanawake, Fisher (1958) anaeleza kuwa shida wanazokabliana nazo wanaume katika harakati za kutafuta riziki kwa familia zao hujitokeza katika lugha yao. Kwa hivyo, lugha isiyo na upole ni kitambulisho cha kuwa mwanamume katika jamii. Licha ya maelezo ya Fisher (1958) na Trudgil (1972) anadhihirisha kuwa tangu wanawake wameshurutishwa kutumia lugha ya unyenyekevu kudhihirisha hadhi ya chini katika jamii wakilinganishwa na wanaume.

Ni bayana kuwa katika jamii za mfumo wa kuumeni, mahusiano ya kijinsia huweza kudhihirika katika lugha za jamii hizo. Hali hii inadhihirika katika jamii ya Wanyankole na hasa katika kipera cha methali. Miongoni mwa Wanyankole, mwanamke hutarajiwa kuwa na lugha sanifu na tabia nzuri kuliko mwanamume kwa vile alikuwa na jukumu la kuadilisha watoto. Kwa msingi huu, kuna methali kadhaa zilizotumiwa kukuza maadili ya jamii kama vile: "*Omwana omusiru no wanyina owobwengye no wiishe*" tafsiri yake "Mtoto mjinga ni wa mama na mwerevu ni wa baba." Methali hii inamaanisha kuwa siku zote ujinga ulihusishwa na mama mzazi na wala si baba ya mtoto. Methali hii inaelekea kumdunisha mwanamke na pia kumuondolea mwanamume jukumu la malezi kwa watoto. Kwa msingi huu, maana hasi katika methali hii ndiyo msingi wa kudenguliwa, ili maana na matumizi yazo yaendane na mahitaji ya leo ya Wanyankole.

Wataalam wengi wakiwemo Lakoff (1975) na Bernard akirejelewa na Hass (1974) wanathibitisha kuwa mahusiano baina ya wanawake na wanaume katika jamii nyingi hudhihirika katika lugha wanayotumia katika mazungumzo yao. Mathalan Hass anadai kuwa katika majadiliano ya runinga, wanawake waliekea kukatwa kauli mara nyingi

zaidi na wanaume. Hii inamaanisha kuwa wanawake walipaswa kuwasikiliza wanaume wanapoongea na wala si kinyume chake.

Hali hii inajitokeza wazi katika jamii ya Wanyankole hasa kwa vile kitamaduni mwanamke alikuwa anatarajiwa kuwa mpole na mnyenyekevu mbele ya mwanamume. Kwa msingi huu, kuna methali ambazo zilitungwa kudumisha hali hii. Kwa mfano methali: "*Omukazi omumanyira ahamigambire"* ikitafsiriwa kama "Mwanamke hutambulika kutokana na usemi wake" inamaanisha kuwa mwanamke anapaswa kuwa mwangalifu katika mazungumzo yake ili asije akachukuliwa kuwa na tabia mbaya. Methali nyingine ni: "*Ofubire ayesiimirana ish*e" ikitafsiriwa kama "Mtoto mjinga huringia mali ya baba yake." Katika jamii ya Wanyankole, baba alikuwa na jukumu kubwa la kumfunza mtoto wake wa kiume kufanya kazi kwa bidii ili kujirundikia mali yake kibinafsi kabla hajapewa urithi. Asipofanya hivyo, mtoto atakuwa mvivu na kutgemea tu kurithi mali ya baba yake.

Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa kuna uhusiano baina ya lugha na jinsia. Lugha ni chombo muhimu katika kupambanua jinsia na mahusiano ya kijinsia katika jamii. Wanaume na wanawake wanatofautina katika matumizi ya lugha hali ambayo inaakisiwa katika methali za kijinsia miongoni mwa Wanyankole. Zaidi ya hayo, methali ni kipera mojawapo katika fasihi simulizi ambacho kilitumiwa na jamii kuelimisha wanajamii kuhusu hadhi na majukumu ya wanajamii kijinsia.

### 2.3 Hadhi ya Mwanamke na Mwanamume katika Jamii

Tumusiime (1982), anaeleza kuwa mwanamke kutokana na utamaduni wa Wanyankole ni mwenye kumtegemea mwanamume. Hawezi kujisimamia, ni mwenye kujali sana, anajali hasa kwa kutunza familia, watoto na vitu vyake. Hufanya kazi zake za kibinafsi zisizo za umma. Ni mwoga, mrembo sana, mpole na mwenye kuongea machache.

Mawazo ya Tumsiime yanaafikiana na yale ya Uchendu (2005) anayedai kuwa ubabe katika vijana wa kiume unahusishwa na umbo la mwili, kisaikolojia na kibayolojia. Anasisitiza kuwa wavulana wanapendelea kuwa na sauti nzito, nywele fupi, malaika mwilini na mavazi yanayokubaliwa na jamii. Aidha, wanaelekea kupendelea masuala ya vita.

Kando na sifa hizi ambazo jamii ya Wanyankole humpatia mwanamume na mwanamke, Greville (1982) ana mtazamo tofauti kuhusu sifa za kijinsia zinazomsawiri mwanamke na mwanamume katika jamii mbalimbali ulimwenguni. Anadai kwamba mwanamke bado hajaweza kupewa sifa zinazobainisha hadhi yake katika jamii kikamilifu. Licha ya mwanamke kujitolea kufanya kazi za umma, kuwa kiongozi na kazi nyinginezo, bado hadhi yake haijathibitika. Madai haya yanatiliwa mkazo na Beavoir (1952) akieleza uhusiano wa mwanamume na mwanamke. Anadai kuwa majukumu tofauti ndani ya jamii ndiyo huleta unyanyasaji ambao unatokana na mfumo wa kijamii. Anaeleza zaidi kuwa ulimwengu huu una baadhi ya sehemu ambazo zinadhibitiwa na mifumo ya kijamii ambayo huwakweza wanaume na kuwatweza wanawake. Aidha, ni wanawake wachache tu ambao wana imani inayofungamana na misingi ya kisiasa na ambao wamechukua hatua ya kujiunga na kuunda vyama vinavyowasaidia kutetea haki zao.

Kutokana na mawazo ya wataalam hawa, ni wazi kuwa kuna haja ya kubadilisha taswira na hadhi ya mwanamke katika jamii ya kisasa. Kwa mujibu wa Ndulute (1987), utafiti uliofanywa Marekani kuhusu majukumu ya kijinsia ulionyesha kuwa hii leo, wanawake zaidi wanajitokeza kufanya kazi za kuajiriwa na zile zilizodhaniwa kuwa za wanaume, ikilinganishwa na awali. Utafiti huo uligundua kuwa mnamo mwaka wa 1965, kati ya wanafunzi ishirini na watano waliojiunga na chuo cha sharia, mmoja tu

ndiye alikuwa wa kike. Mwaka wa 1979, wakawa wanawake watatu kwa kila wanafunzi ishirini na watano. Kijumla ilionekana kuwa idadi ya wanawake wanaopata shahada za uzamifu inaongezeka kadiri miaka inavyoendelea. Mwanamke wa kisasa anapendelea kuwa na majukumu sawa na ya mwanamume.

Katika jamii nyingi za jadi barani Afrika, mwanamke alitelekezwa katika hadhi ya chini. Haya yanathibitishwa na Maitaria (2019) anayeeleza kwamba utamaduni wa Kiafrika unamjengea mwanamke mazingira na majukumu ya kujituma na kushughulikia mambo ya "ndani ya nyumba au kwenye boma," na kumtegemea mume kwa mambo ya hapo nje ya nyumba/boma. Hata hivyo, Momanyi (1998) anakashifu hali hii kwa madai kuwa kuwabakisha wanawake katika hizo sehemu za 'nyuma' na 'ndani' ya nyumba kunawapumbaza na kuwanyima fursa ya kukabiliana na maisha halisi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Maitaria (2019) anasisitiza kuwa kuwaweka wanawake 'nyuma' ni njia nyingine ya kuwatenga, kuwadhalilisha na kuwadhulumu kwani wanabaki 'nyuma' kimawazo na kimatendo, huku mwanamume akipewa nafasi mbele, yenye mamlaka na uamuzi kuhusu uendeshaji wa mambo ya familia na jamii. Kelly (2003) na Mosha (2013) wanashadidia hoja wakisema kwamba kwa kuwa wanawake hawashiriki katika shughuli muhimu kama raia kamili katika jamii, hawawezi kujiendeleza, na hivyo wanabaki kundi duni linalodhalilishwa na kunyanyaswa kwa urahisi.

Ni dhahiri kuwa hali ya wanawake kwa mfano ya kutojihusisha na siasa na kazi nyingine za umma, imechochewa sana na misingi ya kijamii na tamaduni za Wanyankole ambazo zimefungamana na methali za kijinsia. Kwa mfano methali, *"Obushaija buruga omu bwerere"* tafsiri yake "Uume huanzia utotoni", *"Emigambire niyo migirire*" tafsiri yake "Usemi ndio utendaji kwa mwanamume." Methali hizi

ziliwafanya wanawake kuona uongozi kuwa jambo gumu, kwani mwanamume alikuzwa kutambua kuwa yeye ni shujaa, jambo ambalo lilikuwa gumu kubadilishwa.

Hali hii inajitokeza pia katika jamii ya Waswahili kupitia methali ifuatayo: *"Mume ni mume, hata awe gumegume ana sifa ya mtume,"* Katika jamii ya Waswahili, mwanamume alitambuliwa kuwa mwenye uwezo mkubwa na utukufu, hata akiwa mnyonge, masikini au mlemavu. Methali hii inatiwa nguvu zaidi na beti mbili zifuatazo za Utendi wa Mwanakupona zinazodhihirisha nafasi ya mwanamume katika jamii ya Waswahili.

25. Siku ufufuliwao
Nadhari ni ya mumeo
Tauliza atakao
Ndilo takalotendewa

26. Kipenda wende peponi
Utakwenda dalhini
Kimena wende motoni
Hana budi utatiwa. (Utendi wa Mwanakupona)

Ijapokuwa Utendi wa Mwanakupona ni kazi ya ubunifu, kwa kiasi kikubwa inaakisi hali halisi katika jamii ya Waswahili enzi hizo. Mwanamume alikuwa ametambuliwa kuwa na uwezo wa kuamua iwapo mkewe ataingia jahanamu, paradiso na uamuzi wake utaheshimiwa. Hapa ni wazi kuwa jamii ya Waswahili huongozwa na mfumo wa taasubi ya kiume. Hali hii si tofauti na ile inayopatikana katika jamii ya Wanyankole, ambayo ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa ubabe-dume. Kwa mfano katika methali hii, *"Akashaija kache okagayira seri yomjera*" ikitafsiriwa kama "Mwanamume mdogo humdharawi ukiwa ng'ambo ya mto." Kumaanisha usidharau mtu ukiwa unamwonea mbali na kabla hujashikamana naye kwa mkono kwa kuwa katika jamii ya Wanyankole, kila mwanamume alikuwa na nguvu na uwezo kando na maumbile yake ya kimwili.

Kwa hivyo, lilikuwa ni jukumu la mwanamume kudhihirisha kwamba alikuwa na nguvu za kuwajibikia familia yake. Kwa upande wake, mwanamke alitarajiwa kumheshimu mwanamume yeyote yule kwani kitamaduni mfumo wa kuumeni ulimpa hadhi ya juu zaidi ya mwanamke. Ni kwa msingi huu ndipo Beuvoir (1949) anadai kuwa utamaduni umechangia pakubwa katika kumnyima mwanamke nafasi ya kujiendeleza vilivyo katika masuala ya kijamii akilinganishwa na mwanamume. Imani potovu kuwa kuna kazi maalum hazina mashiko kimantiki. Kwa hivyo methali za kijinsia zinazoendeleza fikira hizi hazina budi kudenguliwa ili maana zake zieleweke katika jamii ya Wanyankole inayobadilika kila uchao.

Maelezo haya yanatiliwa mkazo na Jeniffer (1975) na Humm (2022) wanaosisitiza kwamba utambuzi wa kiutamaduni wa mke na mume mnamo miaka (1980) uliwafanya wanawake kukataa kuwa katika kikundi cha wafuasi na kuanza kusema kuwa wana sauti tofauti, namna tofauti ya mapenzi na familia ikilinganishwa na mwanamume. Kwa hivyo, wataalam hawa wanamwona mwanamke kama aliye na uwezo mkubwa punde anapopewa nafasi katika jamii yoyote ile. Maoni haya yametuchochea upya kuchunguza methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Mathalan, methali, "*Omukazi enyejweka biri aine Iba"* ikitafsiriwa kama "Mwanamke ambaye amevaa vizuri ni lazima ana mume." Methali hii inapochunguzwa tunaona ni moja kati ya zile ambazo zinahimiza wanawake kubaki na fikra za kizamani kwamba pasipo mwanamume, mwanamke hawezi kuvaa vizuri. Pia, kutokana na mabadiliko ya ulimwengu kuhusu utamaduni, uchumi, dini, siasa na elimu, methali kama hizi hazina budi kubadilishwa ili kumpatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika nyanja tofauti ndani ya jamii. Ili kufanikisha hili, imebidi kipengele cha udenguzi kitumike katika kuhakiki methali hii kimaana na kimatumizi. Kwa hivyo, suala la jinsia lingali na msingi mkubwa katika methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole.

Kulingana na White (1987), wanawake na wanaume walikuwa wakiishi katika hali sawa kwa muda mrefu katika enzi za ujamaa. Mgawanyiko wa kijinsia ulizuka wanaume walipoanza kutawala mahusiano yote ya jamii kama wababe baada ya kuona kazi za wanaume za uwindaji na uchinjaji kuwa za faida zaidi kuliko za wanawake kama vile kupika na kazi zingine za nyumbani. Hali hii ilisababisha utofauti kati ya mwanamke na mwanamume kiuchumi, kielimu, kisiasa na kitamaduni. Huu ndio msingi wa mwanamume katika jamii ya Wanyankole kupewa hadhi ya kuwa kiongozi, kufanya kazi za umma, mwenye usemi usiopingwa, mwenye kujitegemea, mwenye nguvu, na mwenye kufanya kazi kwa bidii ili kuilisha familia yake tofauti na kazi za mwanamke.

Ni bayana kuwa, sifa na majukumu hayo yametokana na maamuzi ya wanaume ambao walijipa mamlaka juu ya jinsia ya kike na wala si majaaliwa kimaumbile. Aidha, ingawa mwanamume alipewa sifa hizo zote za ushujaa kuliko mwanamke, hizo sifa kwa kiasi fulani ni tofauti na kile ambacho kinapatikana katika jamii ya Wanyankole ya kisasa. Kwa mfano, kuna wanaume ambao ni wapole na hawana nguvu. Hawa kwa jinsi walivyoashiriwa, ni wafuasi wa wanawake na tena hawawezi kujitegemea. Kwa hivyo, suala kuhusu ujinsia na hadhi ya mwanamke na mwanamume katika jamii ni suala ambalo linahitaji kutazamwa upya. Hii ni kwa sababu kiuchumi, kielimu, kitamaduni na kisiasa ulimwengu umebadilika na kulazimisha utamaduni wa jamii nyingi kubadilika ikiwemo ya Wanyankole. Kwa msingi huu, baadhi ya methali ambazo zinafaa kuchunguzwa kiusasa ni, "*Omushaija kwakura ahindura eibara ry'engwe*" tafsiri yake "mwanamume anapokuwa mtu mzima hubadili doa kama chui." Tamaa ya kujirundikia mali na mamlaka ilisababisha wanaume kutunga methali kama hizi ili kuwanyima wanawake fursa ya kujiendeleza katika jamii. Vilevile, katika kuendeleza ubabe-dume, walianza kutunga methali za kujilinganisha na sifa za

wanyama wakali kama vile chui. Lengo lilikuwa kumsawiri mwanamume kama kiumbe chenye uwezo mkubwa zaidi ya mwanamke. Kwa hiyo, ni kutokana na mawazo hayo, mtafiti alilazimika kutumia kipengele cha udenguzi kuhakiki methali hii kimaana na kimuktadha katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

Katika kusisitiza hoja hii, Coates (2004) anasema kuwa tofauti za jinsia yaani ubwana wa mwanamume na unyonge wa mwanamke zinaanzia siku zao za utotoni. Anasema kuwa wakiwa nyumbani watoto hawa hufunzwa na mwanamume kitofauti. Wasichana huwa wanabaki na mama zao huku wakifunzwa misamiati inayohusiana na upole, unadhifu na upishi. Kwao wavulana huwa wanabaki na baba zao wakifunzwa misamiati inayohusiana na ujenzi, maendeleo na uongozi. Pia, lugha ya kawaida inayotumiwa katika jamii husababisha ubaguzi huu wa kijinsia. Katika jamii ya Waigbo wa Nigeria kuna methali ambazo humlinganisha mwanamke na mnyama na nyingine humlinganisha na miti. Kwa mfano methali zifuatazo: *A woman, a dog and a walnut tree, the more you beat them the better they be* **(**Whiting, 1987) *ikitafsiriwa,* **'**Mwanamke, mbwa na mti wa mnazi jinsi unavyowapiga ndivyo wanavyokuwa wazuri.' Methali kama hii inapatikana katika jamii ya Wanyankole ambayo ni: '*Abakazi n'ndeere tizihwa murutookye'* ikitafsiriwa, 'Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani' (Lubuuka, 2010). Methali kama hizi huwafanya wanajamii kumwangalia mwanamke kama kitu duni katika jamii. Vilevile, mwanamke hukaa akijua kwamba hiyo ndiyo hali yake katika jamii.

Geoff (2007), anadai kuwa methali hutumiwa kama mbinu ya kusawiri upole katika mazungumzo. Kupitia katika methali, wanajamii huheshimu mawazo na amali za jamii. Methali wakati mwingine hutumiwa kuficha ukali wa mambo wakati wa kuwasiliana. Methali inakuwa mbinu ya kuficha uso hasa mzungumzaji anapokusudia

kutamka maneno makali. Kupitia kwa methali, wanajamii huhimizwa kuheshimu mawazo na amali za jamii. Kwa hivyo, methali ni nyenzo mwafaka katika kutosheleza matarajio ya jamii kwa wanawake kutii kanuni za jamii kuhusu nafasi yao kijamii. Madai haya yanachochea utafiti huu kuchunguza namna methali hizi za kijinsia zinavyoweza kufasiriwa kwa kudenguliwa ili jinsia zote zijumuike katika maendeleo ya jamii.

Katika jamii ya Wanyankole, kuna methali zinazowahimiza wanawake wawe wanyenyekevu kuliko wanaume. Mfano, *"Nyineeka kwa kuteera ereisho, oyereebesa aha rubaju"* tafsiri yake "Mwanamume anapokukodelea macho tazama kando". Mwanamke hakustahili kumtazama mumewe machoni kwa sababu ilikuwa ni ishara ya kumdharau. "*Eifubo ryongyerera obushaija"* tafsiri yake "Mwanamume anayejiheshimu huchukuliwa kuwa kiongozi. Japo mwanamke alitarajiwa kumnyenyekea mwanamume katika jamii ya kitamaduni, mambo mengi yapata kubadilika katika jamii ya kisasa na kusababisha methali kama hizi kupingwa. Hili limetokana na mwamko mpya wa kuzipa jinsia zote fursa sawa katika uendelezaji wa jamii, tofauti na mtazamo wa zamani. Huu ndio msingi wa utafiti huu kuhakiki methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki.

Wanjiku na Akinyi (1993), katika utafiti wao wanabaini kuwa jamii nyingi za Kiafrika humnasibisha mwanamke na maovu katika jamii. Nafasi za uongozi na za kiuchumi hudhibitiwa na mwanamume. Mwanamke hashirikishwi katika uongozi wa jamii nyingi za Kiafrika. Wataalam hawa wanapendekeza kuwapo na vyama vya kijinsia katika jamii. Wanawake kwa wanaume wanafaa kushirikiana katika kupiga vita ubabedume katika jamii. Wanaeleza kuwa maumbile hayawezi kubadilishwa, lakini mfumo unaweza kubadilishwa kwa sababu ni tokeo la jamii la mazoea na desturi.

Mawazo yao yaliuchochea utafiti huu kwa kutathimini methali hizi za kijinsia kiudenguzi na kipragmatiki katika jamii ya Wanyankole. Kwa mfano, katika methali hii "*Omukazi ku'aikarirwa tayimuka*" tafsiri yake "Mwanamke anapoangushwa chini hawezi kuamka tena." Methali kama hii inafaa kudenguliwa kwa sababu katika jamii ya kisasa, kuna baadhi ya wanawake ambao kimaumbile wana nguvu kuliko wanaume na wamejiendeleza kimaisha. Kwa hivyo, dhana ya 'nguvu' ya mwanamume au ya mwanamke inastahili kuchunguzwa kimuktadha kwa kuzingatia mabadiliko ambayo yametokea katika jamii ya Wanyankole. Kwa msingi huu, ilibidi kudengua methali hii ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole kwa Mtazamo wa Kipragmatiki.

Wataalam mbalimbali (Eagly, 2009; Urlich na Cosell, 2009; Eisenchlas, 2013), wanaeleza kuwa majukumu ya kijinsia yanarejelea tabia na shughuli ambazo wanawake na wanaume wanatarajiwa kutekeleza au kufanya kulingana na jinsi au hali yao kibayolojia huku wakizingatia imani za jamii maalum. Kulingana na maelezo haya, majukumu ya kijinsia katika jamii hudhibiti tabia na mienendo ya wanawake na wanaume kwa kutofautisha hadhi na shughuli zao maalumu. Mathalan, majukumu ya wanaume yanadhihirisha mamlaka na uwezo mkubwa ilhali majukumu ya wanawake yanawaonesha kama binadamu wa hadhi ya chini ambao hawafai kupewa haki na heshima sawa na wanaume katika jamii (Joro, 2016). Kwa mfano katika methali hii, *"Omushaija ku afa naagyenda amaguru tigamugaya"* Ikitafsiriwa kama "Mwanamume akifa katika mwendo, miguu humsifu." Kimajukumu katika jamii ya Wanyankole, mwanamume alistahili kusafiri miendo mirefu ili kuwajibikia familia yake. Kwa hiyo alipokufa akiwa katika majukumu ya kiume alisifiwa sana kutokana na ushujaa wake, tofauti na mwanamke aliyekuwa na majukumu duni. Ni kwa msingi huu, Joro (keshatajwa) anasema, majukumu ya wanawake kwa ujumla yanajikita katika

kuwatii, kuwahudumia na kuwategemea wanaume. Kwa upande mwingine, wanaume wanajitokeza kama vichwa vya familia, wasimamizi wa kipato cha familia ambao wanamiliki kila kitu nyumbani. Pia, Joro anabainisha kwamba wanawake wanapoonekana kutotii au kupinga taratibu za majukumu ya kijinsia, uhasama na mivutano inayozusha unyanyasaji baina ya wanawake na wanaume hutokea. Aidha, ni kutokana na hali kama hizi, tunaona baadhi ya methali za Wanyankole za kijadi zinastahili kufasiriwa upya ili kubeba uzito unaokubalika katika jamii ya kisasa inayokua kila uchao.

Katika jamii nyingi za Kiafrika, mwanamke ana majukumu mengi kuliko mwanamume. Kwa kusisitiza hoja hii, Denoon (1971) anasema mwanamke Mnyankole alikuwa na jukumu la kutunza mumewe, watoto wenyewe, kupika, kutengeneza chumba cha mumewe kwa namna ambayo ilikuwa tofauti ili kiwe kinavutia atapokuwa anafanya ngono na kudumisha usafi nyumbani. Aidha, alikuwa ana jukumu la kulima na kupanda vyakula vya kutosha kwa familia nzima kama vile mtama, wimbi, mahindi, muhogo na maharagwe. Kwa hivyo swala la hadhi ya mwanamke kumnyenyekea mwanamume na kutazamwa kuwa kiumbe duni limekuwepo tangu jadi. Kwa hiyo ni muhimu kuchunguza namna gani methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinaweza kutumika kulingana na mpito wa wakati zinapopokezwa kizazi hadi kizazi.

Mawazo ya Lakoff (1975) ni msingi muhimu katika kutathmini ufaafu wa methali za kijinsia za Kinyankole hasa katika miktadha ya jadi na ya kisasa. Kwa vile methali ni semi zinazobeba hekima, ukweli na tajriba na ushauri kuhusu maisha na zinazorithishwa kutoka kizazi hadi kizazi, je, ukweli na tajriba zinazopitishwa zinabadilika kutoka kizazi hadi kizazi au la? Jibu ni kuwa zinabadilika. Uwezo wa mwanamke unaelezwa vizuri na Eleanor (1884-1962) anayesema “mwanamke ni kama

kijifuko cha majani chai, hauwezi ukatambua nguvu zake hadi pale utakapomweka kwenye maji moto.” Kutokana na kauli hii, ingawa mwanamke ana nguvu fulani kule kuonwa kwake kama kiumbe dhaifu kumefanya nguvu zake kutotambulika. Hata hivyo, iwapo mwanamke atapewa nafasi, ataonyesha nguvu hizo. Hali hii inajitokeza katika methali, “*Ahu abashaija batari abakazi bacwe emanja*” tafsiri yake “Penye wanaume hawapo wanawake hutoa hukumu.” Katika jamii ya Wanyankole, ni wanaume pekee walioruhusiwa kutoa hukumu. Kupitia kwa methali hii, wanaume wanaonywa kuepuka kuzembea katika jukumu lao la hukumu, kwani wanawake nao wana uwezo wa kulifanya.

Katika jamii nyingi ulimwenguni, wanawake wengi wamethibitisha uwezo wao katika masuala ya uongozi. Leo hii kuna baadhi ya nchi kama vile Ethiopia, ambako wadhifa wa urais unashikiliwa na mwanamke. Nchini Uganda kuna wanawake kama vile, Jesca Alupo makamu wa rais, Annet Among mkuu wa bunge la Uganda, na Rebecca Kadaga mkuu wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hao ni baadhi ya wachache tu ambao wametajwa. Nchini Kenya, Martha Koome ndiye anashikilia wadhifa wa Jaji Mkuu. Aidha, nchini Tanzania tunaye Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni mwanamke pia. Kutokana na mawazo haya, ni muhimu methali hii ya kijinsia kudenguliwa ili maana na matumizi yake yaendane na hali halisi ya jamii ya Wanyankole. Aidha, ikumbukwe kila kizazi kina tajriba zake na kwa hiyo lazima tajriba hizo zizingatiwe katika ufasiri na matumizi ya methali kama usemi wa kimapokeo. Ni muhimu methali zipokezwe kizazi kipya kiudenguzi na kiuamilifu.

Enock (2014), akielezea usawiri wa mwanamke katika methali za Kiafrika, anatoa methali kutoka sehemu mbalimbali za Afrika na kuzifafanua. Ananukuu methali moja kutoka nchini Ghana inavyosema, “Mwanamke ni ua la bustani na mume wake ni ua

linalomzunguka." Msemo huu unaelekea kumsawiri mwanamke kama mali inayomilikiwa na mwanamume. Kwa kuongezea, Enock (keshatajwa) anasema kuwa, Wanyarwanda wanawasawiri wanawake kwa kuwatazama kuanzia kifuani palipo maziwa yao. "*Omukazi nasinga amashereka ge"* tafsiri yake "Mwanamke ni zaidi ya maziwa yake, hata mbuzi ana matiti mawili". Methali yenyewe ilionyesha mwelekeo hasi wa mwanamke kwa kulinganisha urembo wake na mbuzi. Mwanamke huyo ni sawa na mbuzi ambaye pia ameumbiwa chuchu mbili kama mwanamke. Mfano mwingine unatoka katika jamii ya Baganda unaosema kwamba *"Omukazi leka eyo, leeta embwa*" tafsiri yake "Ni heri kuishi na mbwa kuliko mwanamke." Methali hizi ziliweka wazi nafasi ya mwanamke katika jamii hizi tofauti. Mwanamke hakuheshimiwa hata kidogo, jambo ambalo lilimdumaza kimaendeleo. Urembo wake na maadili vilikuwa ni vipengele muhimu ambavyo alistahili kuwa navyo tofauti na mwanamume. Jamii ya kisasa inapinga methali hizi zinazomdhalilisha mwanamke. Wanamapinduzi wanapendekeza fursa sawa kwa wanaume na wanawake ili washiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii kiuchumi, kitamaduni na kisiasa.

Finnegan (1970) anathibitisha kwamba methali ni kigezo cha lugha nzito na yenye hekima na nguvu inayohusu mbinu mbalimbali za usemaji wenye mvuto. Anasisitiza kuwa methali ni maneno ya busara na hutolewa kwa vijana kuwaonya maishani mwao. Hata hivyo, methali husheheni ujinsia kwa njia moja au nyingine katika jamii ya Wanyankole. Hii ni kwa sababu, methali hizi zililenga kumsaidia mtoto wa kike hasa katika masuala ya ndoa tofauti na yule wa kiume. Methali, "*Akaremire Omushaija tokazingira engata"* tafsiri yake "Kinachomshinda mwanamume hakiwezi mwanamke." Methali hii ilionyesha hadhi ya mwanamke kuwa ya chini ukilinganisha na ile ya mwanamume. Aidha, mwanamke alionyeshwa hakuwa na nguvu na uwezo kama mwanamume katika jambo lolote ndani ya jamii. Jamii ya kisasa inapinga desturi

zinazomdunisha mwanamke. Wapinzani hawa wanadai katika jamii ya kisasa, wanaume wengi wameshindwa kufanya kazi na wanawake wamejitokeza kufanya kazi walizotengewa na jamii. Kwa msingi huu, methali sharti idenguliwe ili maana na matumizi yake yaafikiane na jamii halisi ya Wanyankole.

Vilevile, Millet (1969), anaeleza kuwa malezi ndiyo chanzo cha hali dhalilishi na duni ya mwanamke katika jamii. Kwa kuwa mtoto wa kiume analelewa kwa namna ya kumdhihirishia sifa za kiume; kujikidhia ‘haja’ za kiume, atainuka kuiendeleza taasubi ya kiume. Katika jamii ya Wanyankole, methali zinachangia pakubwa katika kuipa jamii mwelekeo kuhusu hadhi na ugawaji wa majukumu kijinsia. Kwa hivyo, mtafiti alilitilia maanani suala la malezi ili kutambua ujinsia katika methali za Wanyankole akilinganisha jamii ya kijadi na ile ya kisasa. Mawazo ya Millet yamefaa utafiti huu, kwa sababu imetambulika kuwa ujinsia katika jamii ya Wanyankole umetokana na malezi ya wanajamii.  Hivyo basi, kubadili mtazamo huu kuhusu jinsia hizi, ni bora methali ambazo ni nyenzo kuu za kuiadilisha jamii zichanganuliwe na kufasiriwa kipragmatiki ndipo zipokezwe kutoka kizazi hadi kizazi.

Fasihi kama zao la jamii, huweza kuakisi uhalisi fulani katika jamii. Kwa mfano, Chomba (2005), alifanya utafiti kuhusu sura ya mwanamke kwa kutazama methali katika muktadha wa jamii za Kiafrika zinazoshikilia kwamba kiongozi wa familia ni mwanamume. Kwa mfano, katika methali za Kikuyu “*Wa kahii ti wa kairitu”* tafsiri yake “Mtoto wa kiume si sawa na wa kike”; *“Mundu wa muka umwe ni tuhu wa kanyenje”* tafsiri yake “Mwanamume wa bibi mmoja ni dubwasha.” Vivyo hivyo katika jamii ya Wanyankole, kuna baadhi ya methali za kijinsia ambazo zinaonyesha mwanamume ndiye kiongozi katika kila jambo kama vile “*Obushaija bukye buhwerana*” tafsiri yake “Wanaume wembamba husadiana ili kutekeleza jambo.” Hili

liliashiria ni bora wanaume wasiokuwa na nguvu za kutosha, kusaidiana pasipo kumwita mwanamke. Iliaminika kuwa, kumwita mwanamke wangekuwa wanashusha hadhi yao kama wanaume. Hali hii ni kinyume katika jamii ya kisasa; jinsia zote zinafanya kazi sawa na kushirikiana katika maendeleo ya jamii. Kwa hivyo, japo methali ni semi za kimapokeo, kuna haja ya kuzichunguza upya zinapotumika katika mazingira tofauti na yale ambamo zilitungwa na mababu zetu. Huu ndio msingi wa kuchanganua methali za kijinsia za Kinyankole kiudenguzi na kipragmatiki.

Jamii ya Baganda nchini Uganda pia ina shehena kubwa ya methali za kijinsia. Mfano wa methali zilizotumiwa ni kama vile *"Akato kato kekaba kakazi kalungi kufumbirwa"* tafsiri yake "Rika dogodogo ndilo zuri la kuolewa." Katika kabila la Baganda, msichana alipofikisha umri wa miaka 12 au 13 alikuwa tayari kuozwa. Aidha, miongoni mwa Waganda ilikuwa kawaida mwanamume kumrithi mwanamke na hata kumlazimisha msichana kuolewa na mume wa dada yake. Hata hivyo, mambo yamebadilika sana katika jamii za kisasa na wasichana wengi hawakubali ndoa za kulazimisha.

Kuzuka kwa maradhi mengi, UKIMWI ukiwemo, kumechangia utamaduni huu kukomeshwa na serikali na mashirika mengine ulimwenguni kama vile ya WHO (World Health Organisation), TASO (The Aids Support Oranisation), AIC (Aids Information Centre), UBHCT (Home-based HIV Counseling and Testing), TACAIDS (Tanzania Commission for Aids), na AMREF (African Medical and Research Foundation); tukiyataja japo kwa uchache. Desturi hii ya kurithi mwanamke ilikuwapo pia miongoni mwa Wanyankole. Ugumba au ukosefu wa mtoto katika ndoa, ulichukuliwa kuwa kosa la mwanamke na wala si la mwanamume. Kwa hivyo, mwanamume alikuwa na hiari ya kumwoa dadake mkewe kufidia mahari yake. Jamii

ya kisasa inapinga msimamo huu wa kitamaduni kwa kupendekeza jinsia zote kutafuta matibabu katika hospitali za kisasa kusuluhisha ugumba na utasa katika ndoa.

Maltz na Borker (1982) wanaunga mkono suala la udenguzi wa methali za kijinsia. Wanadai, "Ubaguzi wa kijinsia si wa kimaumbile bali umejengwa kiutamaduni na mwishowe umemnyima mwanamke haki za kupata elimu nzuri, kazi nzuri na furaha katika jamii. Wanasisitiza kuwa, amali za jamii ndizo zinamtengea mwanamke majukumu yanayombagua kijinsia." Kwa hivyo, methali kama sehemu ya utamaduni ni nyenzo kuu ya kuendeleza ubaguzi wa kijinsia kihadhi na kimajukumu. Kwa mfano, Wakikuyu wana methali isemayo "*Wa kahii si wa kairitu*" tafsiri yake "Mtoto wa kiume si sawa na wa kike." Katika jamii ya Wanyankole, kuna methali isemayo "*Ebibero ebikikiire omwojo bikikiire agajwire*" ikitafsiriwa kama "Mapaja ambayo yamembeba mtoto wa kiume ni yale yaliyokamilika." Kutokana na methali hizi, ni wazi kuwa watoto wa kiume walienziwa kuliko watoto wa kike. Mwanamke aliyeshindwa kumzaa mtoto wa kiume alitalakiwa au alilazimika kuletewa mke mwenza. Methali nyingi katika jamii ya Wanyankole kama zilivyokusanywa na Lubuuka (2010), zilimdunisha mwanamke na kumbagua kiutamaduni. Kwa mfano methali, "*Abakazi nendere tizihwa murutokye"* ikitafsiriwa kama "Wanawake ni majani ya migomba hayamaliziki shambani." Methali kama hii iliendeleza ujinsia kwa kuonyesha jinsi mwanamke alivyobaguliwa kiasi cha kumlinganisha na majani ya migomba. Katika jamii ya Wakikuyu, kuna mifano ya methali zinazomsawiri mwanamke kama kitu duni na hata maneno anayoyasema yanatazamwa kuwa si ya kweli. Kwa mfano methali, *"Cia atumia ciitikagio ciarara"* ikitafsiriwa kuwa "Yaliyosemwa na wanawake si ya kuaminika." *"Mundu muka na iguru itimenyagirwo*" ikitafsiriwa kuwa "Mwanamke ni kama hali ya anga, hatabiriki." Kwa msingi huu, siyo tu katika jamii ya Wanyankole

ambako ujinsia unajitokeza katika methali, bali pia hata katika jamii nyingine ulimwenguni.

Kutokana na mifano yote ya methali ambayo imetolewa, ni dhahiri kwamba ni jamii ambayo imechangia pakubwa katika kumdunisha mwanamke ikitumia mifumo ya kijamii, kisiasa na kitamaduni. Kwa vile mifumo hii haijatwama bali inabadilika kadiri jamii inavyobadilika, kuna haja ya kutathmini baadhi ya vipengele vya kitamaduni kama vile fasihi ili kuvikarabati ndipo viendane na mahitaji ya jamii ya kisasa. Huu ndio mtazamo ambao umechochea uchunguzi wa methali za kijinsia za Kinyankole kipragmatiki.

Hata hivyo, dhihaka dhidi ya mwanamke pia inajitokeza katika baadhi ya methali za Wanyankole kwa mfano, *"Omukazi enshambani tagira simbo"* ikifasiriwa kama "Mwanamke kahaba ni bure kabisa hana heshima." Methali kama hizi zimechangia pakubwa kumdunisha mwanamke na kumwinua mwanamume kijamii. Aidha, methali hizi zinambagua mwanamke katika masuala ya uaminifu katika ndoa ilhali tendo la ngono nje au ndani ya ndoa linahusisha mwanamke na mwanamume. Swali la kujiuliza, ni kwa nini mwanamume anayeshiriki tendo la ngono nje ya ndoa asikashifiwe pia? Ni kwa nini kusiwepo na methali kama hizi kumrejelea mwanamume mkware? Ni kutokana na maswali kama haya ndipo kunazuka haja ya kuzichunguza upya methali za kijinsia ili ziafikiane na maslahi ya jamii ya kisasa.

Friedan (1963), anabainisha chuki yake kubwa dhidi ya nafasi ya mwanamke nyumbani na anawahamasisha wanawake kujikomboa kutoka kwenye tundu la nyumba zao za familia na kusisitiza kuwa nyumbani si mahala mwafaka kwa wanawake. Kutokana na utafiti huu tunagundua kuwa mwanadamu hawezi kuficha ukweli wa kupambana na fikra na maumbile yake asili katika kipindi kirefu.

Kutokana na maoni haya, kuna mfano wa methali katika jamii ya Wanyankole, ambayo inamkweza mtoto wa kike. Methali; *"Omwana tagurwa igana"* ikifasiriwa kama "Ng'ombe mia moja hawawezi kumnunua mtoto wangu". Methali hii inaonyesha wazi kuwa mtoto wa kike ana thamani kubwa na hawezi kulinganishwa na vitu anavyomiliki mwanadamu.

Kipury (1983), anadai kuwa tabia za watu hujengeka kwenye misingi ya utamaduni wao. Kwa hivyo, mila na miiko ya jamii huzingatiwa katika kutambua mienendo na tabia hizo. Ni bayana kuwa methali za kijinsia zimejengeka katika misingi ya mila na utamaduni wa jamii ya Wanyankole. Hivyo basi, mabadiliko katika mila na utamaduni wa jamii ya Wanyankole, yataakisiwa katika maana na matumizi ya methali za kijinsia. Kwa msingi huu, uchanganuzi wa methali za kijinsia za Wanyankole kiudenguzi utachangia katika kubadilisha mahusiano ya kijinsia miongoni mwa Wanyankole na jamii nyinginezo za Kiafrika.

## 2.4 Msingi wa Kinadharia

Katika utafiti huu tumeongozwa na nadharia mbili ambazo ni Ufeministi wa Kiafrika na ya Udenguzi. Utafiti wetu ni wa kifasihi na hivyo tumeongozwa na nadharia za kifasihi kulingana na uamilifu wake katika utafiti wetu. Tuanze na nadharia ya Ufeministi.

### 2.4.1 Nadharia ya Ufeministi

Uteuzi wa nadharia inayofaa unategemea mada ya tafiti, malengo na suala la utafiti. Ni bora kuelewa kuwa, kila nadharia huwa na ubora wake na udhaifu wake na hivyo hakuna nadharia sahihi bila mapungufu kwa asilimia mia. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili. Mtafiti alitumia Nadharia ya Ufeministi hasa Ufeministi wa Kiafrika ili kuhakiki methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole

kwa Mtazamo wa Kipragmatiki. Ufeministi wa Kiafrika umesaidia kulifikia lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii.

Ufeministi ni dhana inayotoka kwenye neno la kilatini 'femina' linalomaanisha mwanamke. Dhana hii inarejelea uwakilishaji wa kazi za mwanamke kufuatana na imani ya usawa wa kijinsia. Imejikita sana katika mwamko wa wanawake unaolenga kupigania na kukomesha udhalimu dhidi yao na kufichua matatizo wanayoyapitia katika jamii. Wataalamu mbalimbali wanaeleza dhana ya Nadharia ya Ufeministi ifuatavyo:

Njogu na Wafula (2007), wanaeleza kuwa Nadharia ya Ufeministi ni nadharia inayoyaangalia na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii inayotawaliwa na wanaume. Matatizo ya wanawake yanahusiana na kusababishwa na jinsia. Hii ina maana, shida nyingi zinazowakumba wanawake zimejengeka kwenye msingi wa jinsia yao. Kutokana na matatizo ya jinsia, mwanamke amewekwa katika kitengo maalum cha jamii. Nadharia inayohusu masuala ya wanawake, inajaribu kufichua matatizo yanayowapata wanawake kama tabaka la kiuchumi na pia kama wanawake.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), Ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai kujieleza katika jamii mbali na wanaume wanaokubali jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopingana na mfumo dume. Aidha, Nadharia ya Ufeministi imegawanyika katika matapo mbalimbali kwa kutegemea vigezo tofauti. Wafula na Njogu (wameshatajwa) wanabainisha matapo hayo ya ufeministi. Katika tapo la ufeministi wa kiitikadi, kuna mikabala mitatu inayozingatiwa yaani ufeministi huru, ufeministi wa kijamaa na ufeministi wa kimapinduzi.

Eagleton (1991) na Murfin (1991) wanaainisha ufeministi wa kimaeneo kwa kuugawia katika matapo manne ambayo ni Ufeministi wa Kifaransa, Ufeministi wa Kingereza, Ufeministi wa Kimerekani na Ufeministi wa Kiafrika. Steady (1981), anasema Ufeministi wa Kiafrika unajikita katika misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayotegemeana na kukamilishana, yenye usambamba na usawa katika kuiendeleza jamii. Anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika huweka pamoja masuala ya jinsia, ubaguzi na utabaka na mielekeo tofauti ya kitamaduni ili kuibua ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe duni. Aidha, tapo hili huchunguza masuala ya hali za kitamaduni, na kijamii zinazomnyima mwanamke haki zake katika jamii na kumdunisha.

Msimamo huu wa Steady kuhusu suala la utamaduni kumlemaza mwanamke, unajitokeza katika jamii ya Wanyankole. Hili limetokana na jamii hii kujengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume. Utamaduni unapewa kipaumbele katika ndoa. Kutokana na msisitizo huu, methali nyingi zilizotungwa zilikuwa zinampatia mwanamume hadhi ya juu kuliko mwanamke. Kwa mfano, katika methali hii, *“Omushaija ni byoona”* tafsiri yake “Mwanamume ndiye kila kitu”. Hii inamaanisha mwanamume ndiye msema yote, mfanya yote na hakimu wa mwisho kuhusu kila jambo ndani ya jamii. Kwa hiyo, mtafiti aliegemea tapo la ufeministi wa kimaeneo akizamia kwenye Ufeministi wa Kiafrika ili kutathmini jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika tamaduni za Kiafrika hasa katika jamii ya Wanyankole kwa kuangazia methali za kijinsia.

### 2.4.2 Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika

Mtafiti ametumia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kama tapo la nadharia ya ufeministi. Mtafiti ametumia tapo hili kwa sababu katika utafiti wake, amechunguza

namna methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinavyotumiwa kimuktadha katika shughuli tofauti ndani ya jamii. Ufeministi wa Kiafrika ulimwongoza mtafiti kuchunguza namna utamaduni unavyomlemaza mwanamke katika jamii ya Wanyankole. Steady (1981), anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika unajikita katika misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayotegemeana na kukamilishana, yenye usambamba na usawa katika kuiendeleza jamii. Aidha, anaeleza kuwa Ufeministi wa Kiafrika huweka pamoja masuala ya kijinsia, ubaguzi, utabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuibua Ufeministi unaomwangalia mwanamke kama kiumbe lakini sio kiumbe kijinsia. Kwa hiyo, ni nadharia inayofaa kuchunguza hali za kitamaduni na kijamii zinazomnyanyasa na kumnyima haki mwanamke katika jamii. Mawazo haya ya Steady ni ya manufaa sana katika utafiti huu, kwa sababu tangu jadi jamii ya Wanyankole imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa ubabe-dume. Jambo hili limesababisha methali za Kinyankole kutungwa katika msingi wa ujinsia. Hili lilichangiwa pamoja na utamaduni ambao ulikuwa umemtengea mwanamke kazi tofauti na zile za mwanamume. Kwa hivyo, nadharia hii imesaidia kuweka wazi namna ujinsia ulivyojitokeza katika methali za Kinyankole na hasa namna zinavyochangia kumdunisha mwanamke.

### 2.4.2.1 Mihimili ya nadharia ya ufeministi wa Kiafrika

i. Ufeministi wa Kiafrika huchunguza hali za mwanamke katika jamii zilizokuwa na harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza hali mbalimbali zilizomdunisha mwanamke katika jamii ya kijadi ya Wanyankole, kwa kulinganisha na ile ya jamii ya kisasa ambayo imepata mwamko mpya wa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini. Methali hizi zilichunguzwa kijinsia na kwa undani, ili kuona namna nyanja hizi zilivyochangia kuweka hali mbalimbali

zilizosababisha mwanamke kudunishwa. Kwa hivyo, lengo ni kuona ikiwa mwanamke amepewa uhuru wake katika nyanja hizi tofauti au bado utamaduni umeendelea kumtweza katika maendeleo ya jamii.

ii. Ufeministi wa Kiafrika huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa na utawala na ushujaa wa wanawake. Mhimili huu ulisaidia kuonyesha namna historia kuihusu jamii ya Wanyankole ilivyokuwa imejengeka kwenye mfumo wa kuumeni kitamaduni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume. Aidha, tumetambua utamaduni ulikuwa umefungamana na miundo ya jamii na kumkandamiza mwanamke katika hali zote. Kwa hivyo, lengo lilikuwa kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, tuliona namna jamii ya kisasa inavyobadili historia hiyo kupitia methali za kijinsia kwa kumpatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika jamii kupitia uchumi, siasa, elimu, ndoa, dini na utamaduni tofauti na mtazamo wa kijadi.

iii. Mhimili wa tatu hunuia kuzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Mhimili huu ulisaidia kuonyesha mabadiliko ambayo yamejitokeza kati ya jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kidini na kitamaduni. Mwamko huu mpya umewezesha jinsia zote kupata nafasi sawa, katika nyadhifa mbalimbali ndani ya jamii moja jambo ambalo lilikuwa kinyume wakati wa kijadi. Kutokana na mhimili huu, lengo la tatu la kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa

Wanyankole lilitimizwa. Hili limesaidia kuonyesha ikiwa mwanamke amepata uhuru wake katika jamii ya kisasa au bado anaendelea kutwezwa kijadi.

Maelezo kuhusu ufeministi yameweka wazi kuwa mwanamke ni kiumbe kama mwanamume. Kwa hivyo, anahitaji kushirikishwa katika maendeleo ya jamii kwani ulimwengu umebadilika na kulazimu jinsia zote kushirikiana kiuchumi, kisiasa, kielimu na kitamaduni. Hata hivyo, kuweza kuafikiana na hili, ni lazima baadhi ya methali za kijinsia zidenguliwe ili zieleweke kimuktadha na kimaana katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Ingawa nadharia hii ilitumiwa, bado kungali na upungufu wa kiasi fulani ambao ulimsukuma mtafiti kutumia nadharia ya pili ambayo ni ya Udenguzi. Katika kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, imetusaidia kuona namna methali za kijinsia zilivyoathirika kimaana na kimatumizi katika miktadha tofauti, iliyopatikana ndani ya jamii na namna ilivyosababisha migongano kama vile; utabaka, elimu, uchumi, siasa, utamaduni na historia ambavyo vimechangia katika kumdunisha mwanamke.

Kwa upande mwingine, nadharia ya pili ambayo ni ya Udenguzi imesaidia katika kubomoa maana mbalimbali za methali za kijinsia na kusaidia kuelimisha wanajamii kuwa, kuna uwezekano wa jinsia zote kushirikiana katika maendeleo ya jamii kutokana na miktadha tofauti inayopatikana ndani ya jamii bila migongano. Mabadiliko haya katika majukumu ya wanawake na wanaume katika jamii, ndiyo yamechochea utafiti huu kuchunguza maana na matumizi ya methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwa mtazamo wa kipragmatiki.

Kwa hivyo nadharia hizi zimeonyesha kuwa, fasihi ni utanzu hai ambao ni kioo cha jamii na ambacho hukua kila uchao. Kwa msingi huu itakuwa ni kosa kubwa,

kutochunguza upya methali hizi za kijinsia ndani ya jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole katika karne hii ya 21.

Kutokana na hali hii, methali zilizotungwa zilikuwa zinazungukia katika suala la ujinsia kimaana, kimatumizi na kimuktadha. Lakini kutokana na mabadiliko mengi ambayo yamejitokeza ndani ya jamii hii, methali hizi zimeathirika kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa na kitamaduni na hivyo kulazimu zichunguzwe upya tena ili kuweza kuafikiana na jamii inayokua kila uchao kwa Mtazamo wa Kipragmatiki. Ni kwa msingi huu, nadharia ya pili ilibidi kutumiwa ili kudengua methali hizi kwa kuzifasiri upya, ili zikubalike katika jamii ya Wanyankole inayokuwa kila uchao. Aidha, kwa kutumia nadharia hizi mbili, mtafiti aligundua fasihi haijatwama kwa kukubali mabadiliko yanayojitokeza katika vipera tofauti vya fasihi, methali zikiwemo.

### 2.4.3 Nadharia ya Udenguzi

Udenguzi ni nadharia iliyoasisiwa na Mfaransa Derrida (1981). Alianza kutumia neno ‘deconstruction’ alipokuwa akijadili athari za kuelewa lugha kama maandishi bali si usemi (Derrida, 1981). Anaeleza kuwa mtazamo ambao umekubalika kuhusu ulimwengu na lugha ukichunguzwa kwa kuangazia matumizi ya ishara tunazozifahamu, taswira itakayojitokeza ni tofauti na ile tunayoifahamu. Kulingana na Derrida, kile ambacho kimejulikana kutokana na mazoea, hakifahamiki kwa sababu ya kuzoeleka tu. Kitu hicho kikiwekwa katika mchakato wa kujifahamu, itabainika kuwa maelezo kukihusu ni potofu. Ili kufahamu matini, Derrida (1981) anasema:

> Kusoma kwa makini kwa matini huleta vinyume ambavyo havina mwisho. Hata hivyo, msomaji hatakiwi kukoma bali anapaswa kuendelea kusoma na kung’amua vinyume vingi kadri ya uwezo wake. Aidha, kile kinachorejelewa huwa ni ishara ambayo aghalabu huendelea kubadilika na kuwa kitu kingine, yaani kinachorejelewa pia hurejelea kitu kingine na azimio la udenguzi ni kuiainisha matini kwa njia ya kisanaa ili kuonyesha kile ambacho hakifahamiki (Tafsiri Yangu).

Kwa hivyo, Nadharia ya Udenguzi huzama katika ufafanuzi wa matini na kuyatazama kwa jicho la ndani kwa kuyadengua na kuyabomoa. Nadharia hii inadai kuwa uelewaji wa ndani wa matini unaweza kutupa mwanga kamili kuhusu jamii husika. Mawazo haya ya Derrida yamekuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu, kwani methali za kijinsia zinapotazamwa moja kwa moja zinakuwa na maana tofauti zinapoendelea kuchunguzwa kwa makini na kwa undani. Ijapokuwa methali hizi zilikuwa zinatumiwa katika shughuli za kila siku, kuna ujumbe fiche ambao akina babu walikuwa wanauwasilisha kwa wanajamii ambao ulihitaji umakini ili kuuelewa.

Isitoshe, kutokana na mabadiliko ya ulimwengu kitamaduni, kiuchumi, kielimu, kindoa na kidini, methali kama semi za kimapokeo zinahitaji kuchunguzwa zaidi kimaana katika jamii ya kisasa. Mtazamo wa mambo upya, umebidi methali hizi kudenguliwa kimaana na kimatumizi katika miktadha ya jamii ikiwemo uchumi, utamaduni, maadili na malezi, dini, siasa na elimu. Kwa mfano tunaporejelea methali hii; "*Omwana mubi ajumisa nyina"* tafsiri yake "Mtoto mbaya husababisha mamake kutukanwa." Methali hii inapotazamwa katika muktadha wa kale, maana na matumizi yake yanakuwa tofauti katika jamii ya kisasa. Katika jamii ya kale, mwanamke ndiye alitarajiwa kuzaa na kulea watoto wala si mwanamume. Lakini katika jamii ya sasa, mambo yamebadilika na kulazimisha jinsia zote kuwajibikia watoto. Kwa msingi huu, ili methali iendane na hali halisi katika ulimwengu wa kisasa, imebidi idenguliwe kimaana na kimatumizi.

Mawazo ya Derrida yanaungwa mkono na Mwamzandi (2013) anayebainisha kuwa mbinu kuu na muhimu inayotumiwa na Wanaudenguzi ni ukinzani wa jozi za maneno. Mwamzandi anatueleza kuwa tasnifu ya Derrida kuhusu jozi hizo ni kuwa jamii za Kimagharibi zimejenga upendeleo wa wazi pale neno moja katika jozi husika daima linapowakilisha utukufu au kile kinachopaniwa kufikiwa kama kitu adili huku dhana

ya pili ya jozi hiyohiyo ikiangaliwa kama ghushi, isiyo safi na ya daraja la chini. Kwa hivyo, kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi katika kuhakiki methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwa Mtazamo wa Kipragmatiki, tumebainisha jozi hizi za methali za kijinsia na kuzifafanua ili kuweza kupata maana na matumizi ya methali hizi katika miktadha tofauti ya jamii ya kijadi na ile ya kisasa.

Carter (2006) anatambua kuwa watu hupania tu kuweka mipaka kati ya vitu vya kufikirika na Udenguzi kwa upande mwingine hutuelekeza tuangalie kwa makini ukinzani unaojitokeza ndani ya matini. Kwa maoni ya Carter, tunaweza kuwa tulisoma kazi fulani na tukajiwekea mipaka na imani kuhusu kazi hiyo bila kufikiria zaidi nje ya mipaka ya kazi hiyo. Hata hivyo, kulingana naye, tunaweza kupata maana tofauti ya matini yenyewe na kwa hivyo tukabomoa mipaka na imani tuliyokuwa nayo kuhusiana na kazi husika. Hoja hii ni muhimu sana katika utafiti huu, kwa sababu jamii ya kale ilijiwekea mipaka kuhusu methali hizi za kijinsia kwa sababu zilitokana na utamaduni, siasa, uchumi, ndoa, elimu na dini ya jamii hii ya Wanyankole ya wakati huo. Kutokana na uelewa wao wa mambo katika muktadha wa jamii yao, wanapinga ufasiri wa jamii ya kisasa kuhusu baadhi ya methali hizi za kijinsia. Wao wana imani kwamba methali hizi zimesheheni maana iliyokusudiwa na methali hizo zinafaa zihifadhiwe zilivyo. Kwa kukubali kudenguliwa, basi maana na matumizi yaliyokusudiwa yatapotea pia. Hali hii ya kujiwekea mipaka, imefanya jamii ya kisasa kutupilia mbali baadhi ya methali hizi na zingine kudenguliwa kwa madai, ulimwengu umebadilika na kubidi zidenguliwe kuafikiana na jamii ya kisasa.

Kwa hiyo, kutokana na mitazamo hii tofauti, ilimlazimu mtafiti kutumia kipengele cha udenguzi kwa mtazamo wa Kipragmatiki ili maana na matumizi ya methali hizi, iweze kujitokeza waziwazi kwa jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Mfano mmojawapo

wa methali ambayo jamii ya kijadi imejiwekea mipaka, huku jamii ya kisasa ikitaka idenguliwe ni *"Kiburwa e'nte kiburwa omukazi*" tafsiri yake "Akosaye ng'ombe hukosa mke." Methali hii ilipochunguzwa kimuktadha katika jamii ya Wanyankole wa kijadi, ilionyesha umuhimu wa kila mwanamume kufanya kazi kwa bidii ili kupata ng'ombe wa kutoa mahari. Vilevile, katika muktadha wa leo, mwanamume angali anahimizwa kufanya kazi kwa bidii ili kupata mke na kuwajibikia familia yake, japo si lazima mtu kuwa na ng'ombe ndipo apate mwanamke. Kwa msingi huu, methali hii imeonyesha ufaafu wake katika jamii zote mbili, ingawa miktadha ni tofauti lakini maana ni sawa.

Schmitz (2007), anaeleza kuwa ni kutokana na maneno kwenye matini ambapo tunaweza kufanya udenguzi ili kupata ukweli wa maana iliyokusudiwa. Ubomozi huu wa kazi hufanyika ili kuweza kupata dhana mpya kabisa kwa wasomaji wa kazi husika. Kwa mfano katika methali hii, "*Omwana wobwengye ahangura ebyeishe"* ikifasiriwa kama "Mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake." Kutokana na methali hii, kuna uwezekano mtoto mwerevu kurithi mali ya baba yake, lakini pia ni vizuri kutambua vigezo ambavyo ni vya urithi ambavyo jamii ilipendelea kuhusu mrithi. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa kuibua dhana mpya kutokana na uelewa wa methali hii. Vivyo hivyo katika kuchunguza methali hii, kuna uwezekano wa mtoto kurithi mali ya mama yake. Hii ni kwa sababu ya usawa ambao jinsia zote zimepewa ndani ya jamii kiuchumi, kisiasa, kielimu, kidini, kindoa na kitamaduni unawezesha jinsia yoyote kurithisha mtoto. Kutokana na usawa huu, tunaona methali hii inafaa kudenguliwa kimaana na kimuktadha ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Miller (1976), anaufafanua udenguzi kuwa ni juhudi ya kufikia nguvu na uwezo wa matini kama chombo kinachoweza kujifafanua. Miller anaeleza kuwa matini ni kazi

ambayo inaweza kujieleza na kujifafanua kwa mapana. Kwa mfano, methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinaposomwa tena, mawazo mapya ambayo hayakuibuliwa awali yanaweza kuchipuka kwa kuelekezwa na Nadharia ya Udenguzi. Mawazo ya Miller yanaenda sambamba na methali za Wanyankole, kwa sababu methali hizi za kijinsia zinaposomwa au kusemwa unaona kweli kuna uwezekano wa maana nyingine kupatikana tofauti na ilivyokusudiwa na watunzi wake wa awali. Aidha, nguvu katika matini ambazo Miller anazungumzia, zimeonekana katika mawazo tofauti katika jamii ya Wanyankole wa kale na wale wa kisasa. Kwa mfano methali; *"Mkasho taba nyoko"* tafsiri yake "Mama wa kambo si mama yako mzazi" inaonyesha namna methali ilivyoweza kujifafanua kwa upana zaidi tofauti na namna jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole zilivyokusudia. Methali hii inapochunguzwa kwa undani, maana zaidi ya moja inaweza kupatikana kwa kutegemea muktadha na matumizi. Kitamaduni, tunatambua kina babu walikuwa wanamwonya mama wa kambo awe mama mzuri kwa watoto aliowakuta hapo bomani. Pili, walikuwa wanamkumbusha mwanamke awe na maadili ili kuimarisha ndoa yake isije ikavunjika. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, methali hiyo ingali inatumiwa kwa kumrejelea mama wa kambo kuwa mbaya. Kwa hivyo, Miller hakukosea aliposema kwamba, matini yoyote ile ina uwezo wa kujifafanua kwa upana. Vilevile, katika kupata ufaafu wa methali hii, ni lazima kipengele cha udenguzi kitumiwe kuhakiki maana na matumizi ya methali hii katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Kwa jumla, udenguzi unachunguza lugha kama chombo cha mawasiliano chenye utata na uwezo wa kujifafanua, hasa katika maandishi. Ni uchambuzi unaoweka wazi ukinzani wa fasihi na matini nyingine zisizo za kifasihi. Nadharia ya Udenguzi inapinga mgao mkali wa hali mbili au zaidi zinazokinzana na kuonyesha uwezekano wa hali kama hizo kuwa pamoja na kuchangiana kimaana. Aidha, ni vizuri kuelewa kuwa

vipengele hivi vitatu yaani upragmatiki, udenguzi na Ufeministi wa Kiafrika vina mshikamano wa nguvu katika kulijibu suala la utafiti. Ni vizuri kuelewa kuwa methali hizi zimejitokeza kwa msingi wa muktadha wa ujinsia, ambao umehitaji Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika kuweka usawa wa kijinsia katika methali hizi zinazopatikana ndani ya jamii.

Pili, ili kufanikisha hili, ni lazima methali hizi zitazamwe kipragmatiki pale ambapo maana na matumizi ya methali hizi yanaangaziwa katika miktadha tofauti ndani ya jamii. Mwisho, methali hizi zilihitaji kudenguliwa zaidi, ili maana faafu kuzihusu ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na matumizi yake katika miktadha tofauti. Kwa hivyo, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na ya Udenguzi zilitumika kwa pamoja ili kuyafikia malengo ya utafiti huu.

Kutokana na mawazo haya, tunapata mihimili mitano inayoongoza Nadharia ya Udenguzi kama ifuatavyo;

#### 2.4.3.1 Mihimili ya Nadharia ya Udenguzi

i. Mhimili wa kwanza unatokana na mawazo ya Derrida (1981) ambaye anaeleza kuwa, udenguzi au ‘ubomozi’unahusishwa na usomaji wa kila neno katika matini kwa jicho pekuzi. Huu ni usomaji upya na utazamaji wa kila neno katika matini kwa jicho pekuzi. Usomaji huu umependelewa sana na wadenguzi wanaodai kuwa aghalabu matini za fasihi huzungumzia mambo yasiyodhamiriwa. Hii ni mianya inayostahili kufuatiliwa na msomaji ili aweze kuidengua kikamilifu matini husika. Madhumuni ya nadharia hii ni kujenga maana kwa njia ya kubomoa maana na kujenga mvuto wa kisanaa. Mtu anaweza kujenga maana hata katika mwanya mtupu. Mawazo ya Derrida kuhusu kujenga maana kwa njia ya kubomoa maana yalikuwa na mchango

mkubwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, methali nyingi za Wanyankole zimetungwa hapo zamani na maana zinazorejelewa pia zimetokana na amali za jamii hiyo asilia. Aidha, jinsi ambavyo wakati unazidi kusonga mbele, ndivyo mabadiliko ya vipengele kama vile uchumi, elimu, siasa, ndoa na utamaduni vinavyopata kubadilika na kulazimisha baadhi ya methali za Wanyankole kubadilika pia kimaana na kimatumizi. Kwa msingi huu, mhimili huu ulisaidia kutimiza lengo la pili ambalo ni kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole. Katika kufanya hivi, tumetambua ikiwa maana za methali hizi zimepata kubadilika katika jamii ya kisasa au zingali zinaendeshwa kwa msingi wa kijadi kimaana, kimatumizi na kimuktadha.

ii. Katika mhimili wa pili, Rorty (1996), anabainisha kuwa udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza, huonekana kama ni usaliti, lakini utokeaji wa ukiushi si ajali bali hukusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Maelezo haya ya Rorty yanatupa picha halisi ya mabadiliko yanayoweza kutokea katika uundaji wa matini. Kwa mfano, uundaji wa methali hizi za kijinsia mwanzoni ulikuwa unaendana na vipengele vya utamaduni wa kijadi kama vile; kiuchumi, kisiasa, kielimu, kidini na kindoa katika jamii hii ya Wanyankole. Lakini kutokana na yale yanayojitokeza ndani ya jamii na ulimwengu kwa ujumla, kizazi cha kisasa cha vijana na wasomi kinaonelea methali hizi zinahitaji kufasiriwa upya kimaana au kimatumizi katika muktadha wa leo. Mfumo wa kuumeni ndio uliokuwa unatumiwa kutunga methali hizi na kwa hivyo kuendeleza ubabe-dume. Mfumo huu unakosa mashiko katika jamii ambayo inawania kuwa na usawa wa kijinsia katika takriban nyanja zote za maisha. Kwa hivyo, mhimili huu

ulisaidia kulifikia lengo la pili na tatu la utafiti huu. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza iwapo methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinahitaji kudumishwa kimaana na kimatumizi au kudenguliwa kuendana na mabadiiko katika nyanja mbalimbali za jamii.

iii. Katika mhimili wa tatu, Mohamed (2006) anasema, msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana. Kwa maoni yetu, Nadharia ya Udenguzi ilikuwa ya manufaa kwa sababu iliweza kuyasoma matini upya na kuzirejelea maana zilizokusudiwa na watunzi wa methali hizo. Mhimili huu ulituongoza katika utafiti wetu. Mtaalamu Mohamed amechangia kimawazo katika uchunguzi wa methali hizi za kijinsia. Ni vizuri kutambua, methali hizi za Wanyankole zimejengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume. Hii ni kumaanisha katika uundaji wa methali hizi, mwanamke alipewa hadhi ya chini ukimlinganisha na mwanamume. Kwa hivyo, methali zilizotungwa zilikuwa za ujinsia. Pia, kutokana na mazingira ambamo methali hizi zilitungwa, kuna uwezekano jamii ya kisasa kupoteza maana kamili iliyokusudiwa na kina babu kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii wa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa na kidini na kitamaduni. Aidha, hili linatokana na muktadha na maana tofauti iliyokusudiwa katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Kwa hiyo, lengo ni kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Hili lilisaidia kuonyesha ikiwa, methali hizi za kijinsia zingali na ufaafu katika jamii ya kisasa na ile ya kijadi ya Wanyankole. Kwa msingi huu, ili kuepukana na kupoteza maana iliyokusudiwa katika methali hizi, ni bora udenguzi utumike ili ufaafu wa methali hizi ueleweke katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

iv. Mhimili huu wa nne unashikilia kwamba, udenguzi hushughulikia maneno yanayokinzana na wakati huohuo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya. Kupitia uchanganuzi makini wa lugha ya matini, wanaudenguzi hudhihirisha ukinzani na utepetevu wa matini hizo. Hili ndilo linalowafanya wanaudenguzi kudai kuwa, matini hujiumbua na kujibomoa yenyewe na wala siyo wao wanaudenguzi wanaofanya hivyo. Kadhalika, kufikia lengo hili, methali hizi za kijinsia zimesomwa na kudenguliwa kutokana na jamii ya kisasa ya Wanyankole kwa kuchunguza maana na matumizi ya methali hizi katika miktadha tofauti. Tunapotazama methali za Wanyankole, tunapata kutambua kuwa kuna baadhi ya methali unapozisoma unaona zilikuwa zinamdunisha mwanamke. Wakati huohuo, unatambua mwanamke alikuwa amechangamkia hali yake na hakuona ugumu wowote kuhusu maisha. Hili ni jambo ambalo mhimili huu unaonyesha maneno yanayokinzana na wakati huohuo kubainisha itikadi kuu inayojitokeza na inayostahili kusailiwa upya. Kwa msingi huu, lengo ni kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, tunaweza kubaini ikiwa kimaana methali hizi zingali na ukinzani wa kumdunisha mwanamke na kumfanya kufurahia hali yake, au mwamko mpya ndani ya jamii umebadilisha mtazamo huu katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Aidha, katika kutambua hili, imebidi methali hizi kudenguliwa ili zieleweke kimaana na kimatumizi katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

v. Mhimili wa mwisho unashikilia kwamba, udenguzi ni uhakiki unaokita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Katika utafiti wetu tulizingatia lugha na

matini. Tulipasua matini mbalimbali katika vipengele vyake vyote ili kuweka wazi kilichofichika kuhusiana na yaliyoandikwa kuhusu methali za kijinsia za Wanyankole. Ili kufanikisha hili, kuna baadhi ya methali za kijinsia, zilizotumiwa kuonyesha namna zinavyoweza kujitosheleza kimaana na kimatumizi katika miktadha tofauti ndani ya jamii ikiwemo; siasa, dini, ndoa, utamaduni na elimu. Kwa hivyo, lengo lilikuwa ni kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii. Kwa kufanya hivi, tumetambua ni kwa namna gani methali hizi za kijinsia zinavyoweza kujitosheleza na kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha husika. Kwa msingi huu, ilibidi methali hizi kudenguliwa ili zieleweke kimuktadha na kimaana katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii imehakiki mapitio ya maandishi ya wataalamu mbalimbali na misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti huu zikiwa ni Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Udenguzi. Aidha, nadharia hizi zimeangazia mawazo ya wataalamu mbalimbali. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilisaidia kuonyesha namna ujinsia unavyojitokeza katika methali za Wanyankole. Nadharia ya Udenguzi ilitumika kuhakiki, na kutoa maana zaidi kuhusu methali hizi za kijinsia. Pia, mapitio ya maandishi yameweka wazi, mchango wa waandishi kutoka ulimwenguni kote kuhusu namna methali hizi zilivyotumiwa katika jamii tofauti, ikiwemo ya Wanyankole kwa kuonesha namna jinsia tofauti zinavyojitokeza katika kutekeleza majukumu yao. Vilevile, mapitio ya maandishi yameonyesha pengo la utafiti kuhusu uchanganuzi wa methali kijinsia kwa mkabala wa udenguzi na kipragmatiki. Hali hii inatokana na utambuzi kuwa methali kama kipengele chochote cha fasihi huchipuka na kutumika katika mazingira maalum ya jamii husika. Kwa hivyo mabadiliko ya jamii ya Wanyankole katika nyanja

mbalimbali za kijamii lazima yameathiri maana na matumizi ya methali zinazohusiana na masuala ya jinsia. Huu ndio msingi wa mtafiti kutaka kuona namna maana na matumizi ya methali za kijinsia za Kinyankole yanaendana na mabadiliko ya jamii hii kiwakati. Sura inayofuata inashughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika uhakiki wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole: Mtazamo wa Kipragmatiki.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tulihakiki maandishi kuhusu mada ya utafiti na kufafanua nadharia zilizotumika katika utafiti huu. Sura hii inaeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchanganua data. Inaeleza kuhusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli, vifaa vya kukusanya data; kompyuta, kinasa sauti, orodha ya mwongozo ya maswali, ukusanyaji wa data na hatimaye uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia muundo wa utaratibu wa kithamano. Muundo huu ulisaidia katika kutekeleza hatua za usampulishaji, ukusanyaji na uchanganuzi wa data ambazo si lazima zijitokeze katika vigezo tofauti kama yalivyo katika utafiti wa kitakwimu. Katika matumizi ya utafiti wa kithamano, mtafiti anaweza kuanza utafiti wake na kigezo kimoja. Pindi data zinapokusanywa, mtafiti huanza kwa kutafuta ruwaza na maudhui katika kutengeneza vipengele. Haya yakiibuka, uchanganuzi wa kimsingi wa kiwakati huendelezwa. Maudhui haya yaliweza kujitokeza katika utafiti wa kithamano pale ambapo tuligawanya data kutokana na makundi matatu ya methali za kijinsia. Mgawanyo huu ulizingatia methali zilizopendekezwa kudenguliwa, zile zilizopendekezwa kuhifadhiwa katika jamii zote mbili za Wanyankole, na mwishowe zile zilizopendekezwa kuondolewa kabisa katika jamii ya kisasa. Utafiti wa kithamano hupendelea matumizi ya sampuli ndogondogo ambazo zina uwezekano, ili zisomwe kwa makini (Rwegoshora, 2006).

### 3.2 Eneo la Utafiti

Babbie (1992), anaeleza kuwa eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti unafanyika au unakusudiwa kufanyika. Kwa hiyo, eneo ni mahali ambapo mtafiti anatembelea kwa nia ya kukusanya data inayofaa kufanikisha malengo na maswali ya utafiti. Kwa msingi huu, mtafiti alijikita nyanjani kwa sababu data iliyotarajiwa kufanikisha utafiti huu ilipatikana nyanjani. Nia mojawapo ya kwenda nyanjani ni kwamba, mtafiti aliweza kukutana na wahojiwa wake ana kwa ana na kwa urahisi ili kupata data ya utafiti aliyotarajia. Mtafiti alisafiri hadi Wilayani Bushenyi Magharibi mwa Uganda. Sababu kuu ya kufanyia utafiti huko ni kwamba ndilo eneo asilia la Wanyankole na lugha inayozungumzwa ni Runyankole. Kwa hivyo, hili lilikuwa eneo mahususi kwa mtafiti kwa sababu angeweza kupata methali hizi za kijinsia kwa urahisi kuliko eneo lingine lolote.

Mtafiti aliwahoji wasailiwa kumi na wawili katika utafiti wake. Katika kundi la wazee aliwateua wanawake watatu na wanaume watatu wenye umri kati ya miaka (50-80) kutoka eneo la kijijini pale ambapo mazingira ni yale yenye mashiko thabiti ya fasihi simulizi na eneo asilia la jamii ya Wanyankole. Kundi la pili lilikuwa la vijana watatu wakike na watatu wakiume wenye umri kati ya miaka (25-45) walipatikana katika mazingira ya kisasa lakini wenye asili ya jamii ya Wanyankole. Vijana hawa ni wale wenye msimamo tofauti kuhusu methali za kijinsia katika karne ya 21. Sababu kuu ya kuteua makundi haya mawili tofauti ni kumwezesha mtafiti kupata maoni tofauti kuhusu methali hizi za kijinsia katika jamii hizi mbili za kijadi na zile za kisasa. Sababu kuu ya kuteua watafitiwa kumi na wawili, ni kwamba mtafiti aliamini kutokana na malengo ya utafiti angeweza kupata majibu sahihi kuhusu suala lake la utafiti. Hili liliwezesha kupata data kuhusu methali za kijinsia Arobaini na mbili ambazo zilikuwa zimeteuliwa.

### 3.3 Wango

Katika utafiti huu, jumla ya wahojiwa ilikuwa kumi na wawili, yaani vijana wa kike watatu na wa kiume watatu wenye umri kati ya miaka 25-45, na pia wazee sita; watatu wakiwa wanawake na watatu wanaume wenye umri kati ya miaka 50-80. Aidha, sababu kuu ya wahojiwa hawa kuwa tofauti kiumri ni kuwa, watafitiwa katika kundi la kwanza ambalo ni miaka 25-45, wana mtazamo tofauti kuhusu methali hizi za kijinsia kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii wa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kidini, kitamaduni na kindoa tofauti na namna kundi la pili la wenye umri wa 50-80 linavyoona mambo kitofauti kwa mtazamo wa kijadi. Jumla ya methali 42 zilikusanywa na kuhakikiwa kwa kutumia kipengele cha udenguzi kwa Mtazamo wa Kipragmatiki.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia sampuli ya methali 42 kutoka jamii ya Wanyankole wanaopatikana Magharibi mwa Uganda katika Wilaya ya Bushenyi. Mbinu ya sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuteua jamii ya Wanyankole kwa ajili ya kufikia malengo ya utafiti. Isitoshe, methali 42 zilizochanganuliwa ziliteuliwa kwa kutumia mbinu hiyohiyo ya kimaksudi.

#### 3.4.1 Sampuli ya Kimaksudi

Sampuli ya kimaksudi ni aina ya sampuli ambayo hutoa nafasi kwa watafitiwa lengwa tu, ili waweze kupata fursa ya kujumuishwa katika sampuli ya utafiti (Babbie, 1999). Kama ilivyokwisha bainishwa, mtafiti alikusanya data kwa kutumia mbinu ya mahojiano. Kwa hiyo, sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kukusanya data katika methali za kijinsia 42 za Wanyankole zilizobeba ujumbe kutoka jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Hii inamaanisha, methali zote za kijinsia zilizoainishwa zilijadiliwa kwa kina, kisha kuhakikiwa kwa kutumia kipengele cha udenguzi. Ili kurahisisha

uchambuzi wa data, methali hizi ziligawanywa katika makundi makuu mawili, yaani kundi la methali za kijinsia lililohusu wanaume na lile lililohusu wanawake.

### 3.5 Ukusanyaji Data

Data zilizomo kwenye tasnifu hii zilikusanywa kupitia njia ya nyanjani na maktabani. Hii ina maana kwamba, data ya msingi ilikuwa ya nyanjani na ya ziada ilikuwa ya maktabani. Katika kupata data ya msingi, mtafiti alizuru eneo la watafitiwa lengwa na kuwahoji ana kwa ana kuhusu methali hizi za kijinsia ambazo zimekuwapo tangu jadi hadi sasa. Kutokana na kuwahoji watafitiwa hawa, iligunduliwa kwamba walikuwa wamesahau baadhi ya methali jambo ambalo lilimfanya mtafiti kuzuru maktaba ya Chuo Kikuu cha Makerere ili kupata methali zingine. Maktaba ya Chuo Kikuu cha Makerere ilikuwa ya manufaa kwa sababu, mtafiti aliweza kupata vitabu ambavyo vilizungumzia methali za kijadi za Wanyankole. Kwa kiasi kikubwa, data hizi zilimsaidia mtafiti kuelewa na kufafanua suala la utafiti, malengo, na upeo wa utafiti huu. Pia, mtafiti aliweza kuwashirikisha wasailiwa kueleza namna methali hizi zilivyopata kubadilika katika jamii hii, tofauti na namna ilivyokusudiwa na kina babu kimaana, kimatumizi na kimkutadha ndani ya jamii. Kutokana na mahojiano haya, mtafiti alipata data za kutosha na vilevile kutambua kuwa kuna baadhi ya methali za kijinsia ambazo zilikuwa zimesahaulika kimaana katika jamii ya kisasa kwa madai kwamba zilikuwa zimepitwa na wakati. Kutokana na hali ya kusahau, mtafiti alitamani kufahamu ni kwa sababu gani methali hizi zilihitaji kudenguliwa ili kuafikiana na jamii hii ambayo inakua kila uchao, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kindoa, kielimu na kidini kwa Mtazamo wa Kipragmatiki.

### 3.6 Vifaa vya Utafiti

Kifaa kilichotumika katika utafiti huu ni kompyuta. Kifaa hiki kilisaidia kupata taarifa ya kutimiza malengo ya utafiti. Kifaa hiki kilitumika kurekodi na kuhifadhi taarifa zilizokusanywa nyanjani na kisha kuzisikiliza tena wakati wa jioni baada ya kutoka nyanjani na kuzinakili kwenye kompyuta. Kompyuta ndicho kifaa kilichotumika katika mahojiano yetu ya ana kwa ana. Kifaa hiki kilitufaa zaidi, kwa sababu kilituwezesha kuhifadhi betri kwa muda mrefu. Kando na hilo, wahojiwa pia waliweza kusikika vizuri wakiongea pamoja na kunasa picha zao. Kwa kufanya hivi, mtafiti aliweza kutambua ni mhojiwa yupi alikuwa anasema ukweli kutokana na usemi wake pamoja na viziada lugha vyake. Kutokana na ishara hizo, mtafiti aliweza kuona msisitizo ulikuwa unaegemezwa mno katika jinsia ipi ndani ya jamii ya Wanyankole. Aidha, kompyuta ilisaidia kuchapa kazi ya utafiti, kuhifadhi data na kutafuta machapisho na maandiko mbalimbali ambayo yalihusu utafiti huu hasa yale yaliyopatikana katika tovuti na yaliyokusanywa kutoka kwa wahojiwa.

Vifaa hivi viliwezesha kurudia kusikiliza data iliyokusanya wakati wa ziada ili kuendelea kuchambua methali hizi vilivyo. Kwa msingi huu, vifaa hivi vilikuwa vya umuhimu kwa sababu viliwezesha kuhakiki methali za kijinsia za Wanyankole. Vilisaidia kwa Mtazamo wa Kipragmatiki katika miktadha tofauti ndani ya jamii ikiwemo siasa, uchumi, dini, elimu, malezi na maadili, ndoa na utamaduni katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Aidha, mtafiti aliweza kusikiliza, kurekodi na kuhifadhi methali hizi kwenye kompyuta jambo ambalo liliwezesha methali hizi kuchanganuliwa kwa urahisi.

Kifaa cha mwisho kilichotufaa katika utafiti huu, ni orodha ya maswali ambayo ilikuwa imeandaliwa kutokana na methali za kijinsia zilizopatikana ndani ya jamii ya

Wanyankole. Maswali haya yalitumika kama mwongozo katika mahojiano, na pia kuzuia wasailiwa kupotoka kutokana na suala kuu la utafiti na mwishowe kuokoa muda. Ni kutokana na maswali haya, mtafiti alipata data ya msingi kuhusu utafiti huu.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data uliongozwa na maswali na malengo ya utafiti, ili kuonyesha namna methali za kijinsia zinavyoweza kuhakikiwa kiudenguzi kwa Mtazamo wa Kipragmatiki katika jamii hii. Hii ilisaidia kudhihirisha namna maana na matumizi ya methali hizi zinavyoweza kujitokeza katika miktadha tofauti ndani ya jamii kama vile kindoa, kidini, kielimu, kimalezi na kimaadili, kindoa, kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Data ilikusanywa kutokana na methali za kijinsia arobaini na mbili. Kisha data hiyo ilihakikiwa kwa kuzingatia Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Udenguzi. Nadharia hizi zilikuwa za manufaa katika uchanganuzi wa data. Kwanza kabisa, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imesaidia kuweka wazi vipengele ambavyo vinapatikana ndani ya jamii na vinavyosababisha migongano kama vile utabaka, utamaduni, uchumi, elimu, siasa, ndoa na historia ambavyo vimechangia katika kumdunisha mwanamke.

Kadhalika, Nadharia ya Udenguzi imesaidia katika kubomoa maana mbalimbali za methali za kijinsia na kusaidia kuelimisha wanajamii kuwa, kuna uwezekano wa jinsia zote kushirikiana katika maendeleo ya jamii kutokana na miktadha tofauti inayopatikana ndani ya jamii bila migongano kwa mtazamo wa Kipragmatiki. Uchanganuzi huu ulijikita katika methali zilizoainishwa, moja baada ya nyingine kwa kuongozwa na malengo ya utafiti. Methali hizi zilikusanywa kwanza na kutafsiriwa katika Kiswahili, kwani zilikuwa katika Kinyankole kisha kuwekwa katika makundi mawili. Baada ya hapo, mtafiti aliweka methali hizo katika makundi tofauti ya kijinsia.

Kisha mtafiti aliainisha methali hizi kutokana na nyanja mahususi ndani ya jamii kama vile uchumi, siasa, elimu, utamaduni, ndoa na dini. Mtafiti aliendelea kuainisha methali hizi kwa kuzingatia zile zilizoegemea katika upande wa jinsia ya kike na ile ya kiume akizihakiki kimaana. Hatimaye, aliainisha methali hizi kutokana na ufaafu wake ndani ya jamii ya kisasa, kwa kuziainisha katika makundi matatu. Kundi la kwanza, ni methali zilizopendekezwa kundenguliwa ili ziafikiane na jamii ya kisasa. Pili, ni methali zilizopendekezwa kuhifadhiwa kutokana na uamilifu wake katika jamii zote mbili za Wanyankole. Na mwisho, ni kundi la methali ambazo zilipendekezwa kuondolewa kabisa katika jamii ya kisasa, kwa sababu zilikuwa zimepitwa na wakati.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura hii tumefafanua mbinu za utafiti zikiwemo muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli, vifaa vya kukusanya data, ukusanyaji wa data na hatimaye uchanganuzi wa data ya utafiti huu. Methali mahususi za kijinsia za jamii ya Wanyankole zilizochunguzwa katika utafiti huu ni 42. Sura inayofuata inahakiki matumizi ya methali za kijinsia kimuktadha miongoni mwa jamii ya Wanyankole.

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA METHALI ZA KIJINSIA KATIKA NYANJA MBALIMBALI MIONGONI MWA WANYANKOLE

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tulibainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Katika sura hii, mtafiti amehakiki data kwa mujibu wa lengo la kwanza ambalo ni kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii. Katika kufanya hivi, tumetambua ni methali zipi za kijinsia zilizopatikana ndani ya miktadha hii tofauti katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Katika jamii ya Wanyankole, majukumu yaligawanywa katika maeneo mbalimbali kama vile uchumi, siasa, utamaduni, elimu, ndoa na dini kutegemea jinsia husika. Ugawanyaji wa majukumu ulitokana na msingi kuwa, jamii hii ilikuwa imejengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume jambo lililosababisha kazi kugawanywa kijinsia kama inavyofafanuliwa hapa chini.

## 4.1 Ujinsia kwenye Malezi na Maadili

Katika jamii ya Wanyankole majukumu yaligawanywa kutolingana na jinsia. Kwa hivyo, kutokana na ugawanyaji huu wa kazi, mwanamke alipewa jukumu la malezi na maadili kutokana na maumbile yake ya kuweza kuzaa na kulea watoto tofauti na mwanamume. Kwa msingi huu, suala la malezi na maadili lilihusishwa zaidi na jinsia ya kike na hii ndiyo sababu tunapata methali za kijinsia zinazohusu malezi na maadili. Hali hii ya kumpatia mwanamke jukumu hili, imetusaidia kuelewa historia ya jamii ya Wanyankole, ambayo ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa ubabe-dume. Hali hii imemkweza mwanamke katika maendeleo ya jamii, kwa madai kimaumbile alistahili kuwa na jukumu hili.  Historia na utamaduni vilishikana na kumtenga mwanamke kutohusika na majukumu nyeti ya jamii. Lakini kwa upande mwingine, jukumu hili

lilifaa kuwa la mwanamke, kwa sababu mara nyingi alikuwa na kazi za nyumbani tofauti na mwanamume aliyekuwa na kazi za nje kama vile kuwinda, kujenga, hakimu na kulinda usalama wa nyumbani.

Mnenuka (2001) anasisitiza hoja hii kwa kuchunguza nafasi na hadhi ya mwanamke katika jamii kama inavyojadiliwa katika nyimbo za Bongo Fleva za Dege, Samaki na Bata zilizoimbwa na Offside Trick na Vocha iliyoimbwa na Hassan Kumbi na Ashlay. Anaeleza kuwa, uhusiano wa kingono baina ya mwanamke na mwanamume, sambamba na hadhi na nafasi zao katika uhusiano huo umetokana na malezi ya kijamii. Katika jamii mwanamke anapaswa kuwa mtulivu, ilihali mwanamume anapaswa kuwa mtendaji mkuu na mwenye kutoa sehemu kubwa ya uamuzi katika masuala mengi. Hivyo taswira ya mwanamke, inayopatikana katika misemo na nyimbo za kazi nyingi za kifasihi zinaonesha udogo wa mwanamke kama ulivyo katika jamii nyingi. Kwa mfano katika nyimbo teule za bongo flava, taswira ya mwanamke inayoonekana ni chombo cha starehe cha mwanamume hasa kingono na thamani yake kushuka mara tu anapomaliza kukutana na mwanamume kimwili na kuwa kiumbe asiyefaa katika jamii. Maelezo ya Mnenuka yanaenda sambamba na yale ya jamii ya Wanyankole. Kwanza kabisa mwanamke alichukuliwa kama kifaa cha kumfurahisha mwanamume kingono, kuzaa na kulea watoto tu. Mwanamke hakutazamiwa kuwa wa manufaa yoyote ndani ya jamii. Kwa msingi huu, hakuna jinsi mwanamke angeepuka jukumu hili kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

**Mf 1**

**Kinyankole**: *Omwana mubi ajumisa nyina.*
**Kiswahili:** Mtoto mbaya husababisha mama yake kutukanwa.

**Mf 2**

**Kinyankole:** *Enaku yotagambire nyoko tetuba.*
**Kiswahili:** Shida ambayo hujamwambia mama yako haipungui.

**Mf 3**

**Kiswahili**: *Omukazi tayechwa kizire.*
**Kinyankole:** Mwanamke hajikati kizazi.

**Mf 4**

**Kinyankole:** *Eziwaterwa nyoko tizaba nkoni.*
**Kiswahili:** Viboko ambavyo umepigwa na mama yako si viboko.

**Mf 5**

**Kinyankole:** *Omukazi taba mugyenyi.*
**Kiswahili:** Mwanamke hawi mgeni.

**Mf 6**

**Kinyankole:** *Omwana oine mukaishe tahwa bunaku.*
**Kiswahili:** Mtoto ambaye yuko na mama wa kambo haishiwi huzuni.

**Mf 7**

**Kinyankole:** *Omukazi otamanyire ekimutungire eyiba ajikwasa omukono gumwe.*
**Kiswahili:** Mwanamke asiyejua thamani ya mumewe hushika uume wake kwa mkono mmoja.

**Mf 8**

**Kinyankole***: Omukazi ayomba azibira omutabani kuragwa.*
**Kiswahili:** Mwanamke mgomvi husababisha mtoto wake wa kiume kutorithishwa.

**Mf 9**

**Kinyankole**: *Enkoni eteire mukabaro ku'ogireba ogirenzya orugo.*
**Kiswahili**: Fimbo iliyotumiwa kupiga mke mwenza, ukiipata unaitupa nje ya zizi.

**Mf 10**

**Kinyankole**: *Omukazi mubi tumwihaho Omwana.*
**Kiswahili**: Mwanamke mbaya huzai naye.

**Mf 11**

**Kinyankole:** *Omukazi murungi niwe abyamisiriza Iba.*
**Kiswahili:** Mwanamke mzuri ndiye humbembeleza mumewe kulala.

**Mf 12**

**Kinyankole:** *Abashaija tibabagaya.*
**Kiswahili:** Wanaume hawadharauliwi.

**Mf 13**

**Kinyankole:** *Ibega tiringana na omutwe.*
**Kiswahili:** Bega halilingani na kichwa.

**Mf 14**

**Kinyankole:** *Nyineeka kuagamba Omukazi tamugarukamu.*
**Kiswahili:** Mwenye nyumba akiongea mwanamke hamjibu.

**Mf 15**

**Kinyankole**: *Taaha omwasho teba rwango.*
**Kiswahili:** Kwenda nyumbani kwa baba yako si chuki.

Methali hizi zimeweka bayana kuwa, mwanamke alikuwa nguzo katika suala la malezi na maadili katika jamii ya Wanyankole kuliko mwanamume. Jambo hili limejitokeza waziwazi kutokana na nyanja mbalimbali zilizoainishwa katika kundi hili.

## 4.2 Matumizi ya Ndoa na Kazi Kijinsia

Muktadha wa pili umehusika na suala la kazi katika ndoa. Katika jamii ya Wanyankole, suala la kufanya kazi ndani ya ndoa lilikuwa ni kipaumbele na la kijinsia. Aidha, kila mtu alikuwa ameteuliwa jukumu lake pasipo kugawana. Ni kwa sababu hii tunaona mwanamke aliyekuwa mvivu, hakuweza kuolewa kwa madai kuwa alikuwa anaenda kumfilisisha mumewe kimaendeleo. Isitoshe, jinsia zote zilibidi kufanya kazi kwa nguvu, huku mwanamume akijitokeza kuwa kiongozi katika kila jambo ndani ya jamii kwani utamaduni ulikuwa umempatia uwezo huo. Mtaalam Coates (1993) anatilia mkazo sababu zinazowafanya wanaume kuchukuliwa kuwa na sifa tofauti na wanawake. Anasema, tofauti za jinsia yaani ubwana wa mwanamume na utumwa wa mwanamke zinaanza siku zao za utotoni. Madai haya yanaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza hali mbalimbali za mwanamke katika jamii zao ambazo ndizo chanzo cha unyanyasaji. Hali hizi za kumdunisha mwanamke zilizotokana na baadhi ya sifa alizopewa kama vile kiumbe dhaifu, mwoga, mpole, mkarimu, mvumilivu, mwenye upendo na mshauri kuliko mwanamume. Kwa hivyo,

mwanamke alistahili kazi nyepesi ambazo hazikuhitaji 'nguvu'. Hali hizi za kumnyima uhuru wa kujihusisha katika baadhi ya majukumu ya jamii ilimtweza mwanamke kimaendeleo.

Beavoir (1949), anasisitiza hoja hii kwa kusema, utiifu si miongoni mwa majukumu ya mwanamke. Anadai kuwa ingawa kila mwanamke nchini Ufaransa ana uhuru wa kujiamulia mambo, uhuru huo ni wa kidhahania tu kwa sababu haumbatani na uhuru wa kiuchumi. Hali hii inatokana na kuwa mwanamke anayemtegemea mumewe, hawezi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo kwa sababu mila na desturi hazimruhusu. Hali inabainika hasa katika mataifa mengi barani Afrika. Maelezo haya yanaafikiana na hali ilivyo katika methali za kijinsia za Wanyankole ambapo kazi zilizotengewa mwanamke zilikuwa duni ukilinganisha na zile za mwanamume katika jamii. Aidha, ilikuwa kwamba, hata mwanamke angekuwa na uwezo wa kufanya kazi fulani hakuruhusiwa kwa madai kuwa utamaduni haukumruhusu. Zifuatazo ni baadhi ya methali zilizomtweza mwanamke:

**Mf 16**

**Kinyankole:** *Emirimo mingi ekazibira Bigyemano okutobora omukazi.*
**Kiswahili:** Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutoboa ubikira wa mwanamke.

**Mf 17**

**Kinyankole***: Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire.*
**Kiswahili:** Mtoto ambaye yuko na baba yake huepuka majonzi ambayo yangemuua.

**Mf 18**

**Kinyankole:** *Omwana bamutinira obushaija bweishe.*
**Kiswahili:** Mtoto huogopwa kutokana na uume wa baba yake.

**Mf 19**

**Kinyankole:** *Meeme mememe tezaza mwojo.*
**Kiswahili:** Kubembeleza hakuishi kuzaa mtoto wa kiume.

**Mf 20**

**Kinyankole**: *Eka efire nyineeka ayetondera abaana.*
**Kiswahili:** Boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto wake msamaha.

**Mf 21**

**Kinyankole:** *Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro.*
**Kiswahili:** Boma ambalo linaelekea kuharibika mwenye boma huamka na kuanza kula kiporo.

**Mf 22**

**Kinyankole:** *Omwana oine ishe tayekorara enku.*
**Kiswahili:** Mtoto ambaye ana baba yake hastahili kubeba kuni.

**Mf 23**

**Kinyankole:** *Obwenda kusimwa omukazi akasa oburo ahaekire Iba.*
**Kiswahili:** Mwanamke kupenda kushukuriwa alisaga wimbi akimbeba mumewe mgongoni.

**Mf 24**

**Kinyankole:** *Omukazi ne myenda, Omushaija nemirimo.*
**Kiswahili:** Mwanamke ni nguo mwanamume ni kazi.

**Mf 25**

**Kinyankole:** *Omukazi ahinga hamwe na Iba taba mugara.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye analima na mumewe si mvivu.

**Mf 26**

**Kinyankole:** *Nyineeka atutuka narya obuhoro.*
**Kiswahili:** Mwenye boma anakula kiporo akitoka jasho.

Kundi hili limedhihirisha umuhimu wa mwanamume katika kufanya kazi kuliko mwanamke. Aidha, mwanamke alikuwa anasawiriwa dhaifu kutokana na aina ya kazi alizopewa ndani ya jamii. Hali hii ilitokana na mfumo wa kuumeni uliokuwa unatawala jamii ya Wanyankole.

### 4.3 Matumizi ya Methali za Kijinsia katika Uwanja wa Uongozi

Katika muktadha wa tatu, tunaona suala kuhusu ndoa na uongozi. Katika jamii ya Wanyankole, ni mwanamume ambaye alikuwa kiongozi katika kila jambo ndani ya familia huku mwanamke akiwa vilevile, mwanamke alichukuliwa kuwa kiumbe dhaifu, asiyeweza kulinda usalama wa familia au kuongoza kitu chochote. Hali hii ya

kumdunisha mwanamke na kumpatia mwanamume ushujaa imetokana na mfumo wa kuumeni uliotamalaki katika jamii ya Wanyankole. Huu ndio utamaduni ambao wanaufeministi wa Kiafrika wanashikilia unapaswa kutupiliwa mbali iwapo tunataka kumkomboa mwanamke na kumpa fursa ya kushiriki katika maendeleo ya jamii kikamilifu. Kitamaduni mwanamke alihusishwa na sifa kama vile mwoga, mpole, mkarimu, mvumilivu na mwenye maneno machache. Kwa msingi huu, hangeweza kutegemewa kuiongoza jamii ya Wanyankole.

Akidhihirisha athari hasi ya mfumo wa kuumeni katika jamii nyingi za Kiafrika, Mwita (2005) anasema kuwa, kutokana na mfumo wa kuumeni uliokithiri katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana iliyojaa dhuluma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke daima ni mtegemezi. Hali zote za maisha yake hutegemea uamuzi wa mwanamume. Mwita anahitimisha kuwa ni sifa kwa mwanamke wa Kikuria na wa Kiafrika kwa ujumla kuzoea kujiamulia mambo pasi na kupata ushauri wa mwanamume. Kwa hivyo, usawiri huu wa mwanamke ulimnyima fursa kushika hatamu za uongozi katika asasi mbalimbali ndani ya jamii ya Wanyankole. Methali zifuatazo zinaonyesha nafasi ya mwanamume katika jamii ya Wanyankole:

**Mf 27**

**Kinyankole:** *Omushaija tahinduka omubigambo ahinduka aha kitandi honka.*
**Kiswahili:** Mwanaumme hageuki kwenye usemi ila hugeuka kitandani tu.

**Mf 28**

**Kinyankole**: *Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja.*
**Kiswahili:** Mahali ambapo hakuna wanaumme, wanawake ndio hutoa hukumu.

**Mf 29**

**Kinyankole:** *Omukazi akanyampira obwato bya ishezaara ati munda yamawe tuzira emitahe.*
**Kiswahili:** Mwanamke alijambia mtumbwi wa baba mkwe kisha akasema kwetu ni mwiko kunywa pombe.

**Mf 30**

**Kinyankole:** *Omukazi aba orubaju rwomushaija.*
**Kiswahili:** Mwanamke huwa ubavu wa mwanamume.

Kutokana na methali hizi nne, ni wazi kuwa mwanamke hakuchukuliwa kuwa na uwezo wa kutoa hukumu katika jamii. Ni mwanamume tu ndiye aliyeachiwa jukumu hili. Jambo hili lilitokana na ubabe-dume ambao ulikuwa unaendelezwa ndani ya jamii hii. Aidha, Bamghose (2016) na Larsen (2016) wanaonyesha kuwa kiini cha mamlaka ya kiume ni mfumo- dume ambao unampendelea zaidi mwanamume. Hadhi hiyo ya kitabaka inampa mume mamlaka ya kudhibiti uamuzi na utendaji wa mambo mbalimbali katika mahusiano ya ndoa kijinsia. Aidha, mamlaka kwa kawaida yanaendelezwa kwa kutumia njia mbili kuu. Njia ya kwanza ni kutumia nguvu kwa kulazimisha walio chini kutii mamlaka ya walio juu. Njia ya pili ni kuwashawishi kwa namna moja au nyingine walio chini ili waweze kutii na kuheshimu mamlaka ya tabaka tawala. Aidha, kutokana na njia hizi mbili, jamii ya Wanyankole ilikuwa inatumia njia ya kwanza ya utabaka yaani ya kutawala na kunyanyasa, kwa mfano katika methali kama vile, *"Omushaija kuagaba omukazi tamugarukamu."* Tafsiri kama "Mwanamume akiongea mwanamke hastahili kumjibu". Kwa hivyo, hii ilikuwa njia mojawapo iliyomfanya mwanamke kunyamaza na kujitenga na masuala muhimu ndani ya jamii. Ni kwa msingi huu, methali kama hii inafaa ifasiriwe upya ili itumike katika jamii ya kisasa ya Wanyankole ambayo inakua kila uchao kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kielimu.

### 4.4 Methali za Kijinsia katika Uwanja wa Utamaduni

Muktadha huu umeweka wazi kuwa, utamaduni ulikuwa ni kipengele mojawapo muhimu katika ndoa ndani ya jamii ya Wanyankole. Ni kutokana na muktadha huu ndipo tunapogundua namna utamaduni ulivyokuwa unamtweza mwanamke kwa kiasi

kikubwa kuliko mwanamume. Hii ilitokana na utamaduni ambao ulikuwa umefungamana na ubabe-dume, ambao ulimwona mwanamke kuwa kiumbe duni katika kila hali ya maisha. Momanyi (2000) anaonyesha namna mwanamke anasawiriwa kama kifaa cha kumstarehesha mwanamume na huchukuliwa kama pambo au kiumbe asiyeaminika.

Katika jamii ya Wanyankole, mwanamke alidunishwa kutokana na utamaduni wa kulipiwa mahari. Mwanamume alipolipa mahari yake kwa kutoa ng'ombe kwa wazazi wake, ilikuwa ni kama kibali cha mwanamke kuteseka na kunyanyaswa kwa kufanyishwa kazi nyingi na familia ya mumewe. Maelezo haya yanaungwa mkono Dery (2015) ambaye anasema, "Katika utamaduni wa Kiafrika, ulipaji wa mahari ni desturi ambayo inaidhinisha na kuhalalisha mahusiano ya ndoa". Mahari inalipwa kama shukran au zawadi na ni amana kwa wazazi na ukoo mzima wa yule ambaye anaolewa (Maitaria, 2019). Hata hivyo, Kaye na wenzake (2005b) na Muthengeki, Kule na Neemah (2012) wanaeleza kwamba mahari ni mojawapo ya mambo yanayochangia udhalilishaji na unyanyasaji wa wanawake katika mahusiano ya ndoa. Mathalan, mume aliyelipa mahari anathibitisha mamlaka kwa kuhisi kwamba alilipia mke huyo, na hilo linamnyima mke haki na usawa.

Oguli (2004) anaielezea mahari kama mkataba unaohusisha malipo ya pesa, wanyama au vitu vingine kwa familia ya bi-harusi. Oguli anabainisha kwamba mkataba huo ni kama muamala wa kimabadilishano ambapo bwana arusi anatoa mali hiyo ili kumpokea bi-harusi na uwezo wake wote, hususan nguvukazi na uwezo wa kuzaa watoto. Wanaufeministi wa Kiafrika wanakiri kuwa mahari kwa mwanamke ni mojawapo ya vyanzao vya mateso ya mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika. Kwa hivyo, tamaduni za jamii za Kiafrika ndizo zilizomfanya mwanamke kutohusishwa

katika baadhi ya kazi kwa madai kuwa ni za wanaume. Kwa hivyo, utamaduni haukumpatia mwanamke fursa ya kuonyesha uwezo wake kuhusu masuala nyeti ya jamii, jambo ambalo lilimfanya kubaki nyuma kimaendeleo. Methali za kijinsia zifuatazo zimejaribu kuweka bayana namna mwanamke alivyodhulumiwa na utamaduni wa jamii.

**Mf 31**

**Kinyankole:** *Omukazi oine Iba tarya nkoko.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye ana mume hali nyama ya kuku.

**Mf 32**

**Kinyankole:** *Omufukazi tagaya mboro.*
**Kiswahili:** Mjane hadharau mboro.

**Mf 33**

**Kinyankole:** *Omukazi oraite eka asiga yacuriza.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye ataharibu boma lake hupiga mbinja.

**Mf 34**

**Kinyankole:** *Abana bahwa omumukazi tibahwa mumushaija.*
**Kiswahili:** Watoto huisha ndani ya mwanamke lakini si kwa mwanamume.

**Mf 35**

**Kinyankole:** *Ozara Omwojo tacwa ruganda.*
**Kiswahili:** Anayezaa mtoto wa kiume hakomeshi ukoo.

**Mf 36**

**Kinyankole:** *Omukazi akaferwa Iba ati zambona.*
**Kiswahili:** Mwanamke alifiwa mumewe akasema zimenikuta.

**Mf 37**

**Kinyankole.** *Empitsi ekagira eti, kumbugana omushaija ashendekyerize ondijo nteraa mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheeka nkaba.*

**Kiswahili:** Fisi alisema kwamba akimkuta mwanamume akimsindikiza mwanamume mwenzake hujificha lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu.

**Mf 38**

**Kinyankole:** *Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki.*
**Kiswahili:** Ukoo ambao utaharibika huwazaa wasichana.

Kutokana na methali hizi, ni wazi kuwa mwanamke alidhibitiwa sana kitabia na pia kulikuwa na miiko mingi iliyomzuia kujiendeleza kimaisha ndani ya jamii ukilinganisha na mwanamume. Madai haya yanatiliwa mkazo na methali ya Wakikuyu isemayo, "*Gutiti njamba ya mwera ummwe*" ikitafsiriwa kama, "Hakuna jimbi wa mtamba mmoja." Methali hii ina maana kuwa mwanamume asioe mke mmoja. Utamaduni wa jamii ya Agikuyu uliwakubalia wanaume kuoa wake wengi mradi tu yule mume awe na uwezo wa kuwakimu. Wanawake walichukuliwa kama "mali" hivi kwamba mume mwenye wake wengi aliheshimiwa katika jamii na kuonekana kuwa mwenye mali nyingi.

Madai haya si tofauti na yale yanayopatikana katika jamii ya Wanyankole. Kwa mfano katika methali hii, *"Omushaija aba owashwera abakazi binji"* ikitafsiriwa, "Mwanamume ni yule ambaye amewaoa wake wengi." Kutokana na methali hii, tunatambua mwanaume alisifika kutokana na wake ndani ya jamii ya Wanyankole. Wanaufeministi wa Kiafrika wanapinga utamaduni unaomnyima mwanamke hadhi ya utu na badala yake kuchukuliwa kama sehemu ya mali ya mwanamume. Huu ndio msingi wa harakati zao za kuchunguza historia za tamaduni zilizomdunisha mwanamke na kuona namna wanavyoweza kumzindua katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Suala la mwanamke kutazamwa kama mali si geni katika jamii ya Wanyankole. Jamii ya Wanyankole ilienzi watoto wa kiume kuliko wa kike, watoto wa kike walitazamiwa kuwa njia moja ya kuleta mali nyumbani kwao na hawakuwa na umuhimu mwingine wowote. Hali hii inathibitishwa na methali isemayo: *"Abana bahwa omumukazi tibahwa mumushaija"* ikitafsiriwa kuwa "Watoto humwisha ndani ya mwanamke

lakini si mwanamume". Methali hii ilikuwa mfano mzuri wa kuthibitisha kwa nini wanaume walistahili kuwaoa wake wengi. Iliaminiwa kuwa mwanamke alifaa azae watoto wengi na iwapo hakufanya hivyo, mwanamume alikuwa huru kuoa mke mwingine.

Hapa tunaona kuwa hisia na afya ya mwanamke haitiliwi maanani na jamii ya jadi iliyoegemea mfumo wa kuumeni. Mwanamke alichukuliwa kama mtambo wa kumzalia mwanamume watoto. Wanaufeministi wa Kiafrika wanapinga hali hii kwa madai kuwa haki za mwanamke kama binadamu mwenye uwezo wa kufanya maamuzi apate watoto wangapi inakiukwa. Aidha, katika jamii ya Wanyankole inatambua kuwa wakati mwingine tatizo la kutokuwa na kizazi huenda likatokana na maumbile ya mwanamume na wala si mwanamke peke yake. Kwa msingi huu, methali zinazoelekea kuendeleza dhuluma dhidi ya jinsia ya kike kuhusiana na masuala ya ndoa zinapingwa vikali na Wanaufeministi wa Kiafrika.

### 4.5 Ujinsia kwenye Masuala ya Uchumi

Jamii ya Wanyankole katika muktadha wa jadi iliendeleza uchumi wake katika ufugaji wa ng'ombe na ukulima wa vyakula vichache vya nyumbani kama vile wimbi, mtama, mihogo, viazi vitamu na nafaka. Aidha, jamii hii ilikuwa na jinsi ya kuendeleza uchumi wake. Kazi hizi zilifanyika kijinsia, kwani wanawake walikuwa wakulima, ilhali wanaume walikuwa wafugaji. Jamii ya Wanyankole ilimwona mwanamke kuwa kiumbe dhaifu, asiyestahili kupatiwa majukumu magumu kama ya ufugaji. Hili lilitokana na kipato kikubwa ambacho kilitokana na uuzaji wa mifugo tofauti na ukulima. Utofauti huu kiuchumi, ulimfanya mwanamke kubaki nyuma kimaendeleo kwani hakuhusishwa na biashara nyeti za jamii. Jamii ilishikilia kwamba, mwanamke hakuweza kufikiria sawa na mwanamume katika nyanja hii. Kutokana na mitazamo hii

tofauti ya ugawanaji kazi, tunaona Wanaufeministi wa Kiafrika wanasaidia kuchunguza hali tofauti mwanamke alimofanyia kazi tofauti na ile ya mwanamume katika jamii za Kiafrika. Ni kutokana na hali tofauti za ubaguzi zilizosheheni ndani ya jamii, na kuendelezwa kwa ubabe-dume ndizo zilizomnyima mwanamke uwezo wa kujikomboa na kujenga jamii mpya sawa na mwanamume. Hili linajidhihirisha kupitia mifano ya methali zifuatazo.

**Mf 39**

**Kinyankole:** *Kiburwa ente kiburwa Omukazi.*
**Kiswahili:** Akosaye ng'ombe humkosa mke.

**Mf 40**

**Kinyankole:** *Okukunda akuha ente otayenda kuofa akuha Omukazi.*
**Kiswahili**: Akupendaye hukupa ng'ombe asiyetaka ufe hukupa mke.

**Mf 41**

**Kinyankole**: *Omukazi enyerisa biri aine enfuka.*
**Kiswahili**: Mwanamke anayejilisha ana jembe.

**Mf 42**

**Kinyankole:** *Omukazi mubi akwita hona.*
**Kiswahili:** Mwanamke mbaya hukudhoofisha kwa kila hali.

**Mf 43**

**Kinyankole:** *Omwana wobwengye nahungura ebyaishe.*
**Kiswahili:** Mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake.

Kutokana na methali hizi, tumetambua mwanamume alipewa kipaumbele katika suala la uchumi tofauti na mwanamke. Dai kuu lilikuwa ni kwamba mwanamke alikuwa hana uwezo kiakili kuzifanya shughuli hizo kama mwanamume. Kutokana na fikra kama hii, mwanamke aliachwa nyuma kimaendeleo. Engels (1975), anatoa mwanga zaidi kuhusu chanzo cha ubinafsi kuhusu ugawanaji wa mali ndani ya jamii. Anasema kuwa hapo mwanzo, mwanamume na mwanamke walithaminiwa sawa katika jamii. Jamii ziliishi maisha ya ujima. Mfumo wa utawala wa ubabe-dume ulianza pale jamii zilipoanza kubadilika kwa kugundua kuwa kazi za waume za kuwinda na ufugaji

zilikuwa na faida kubwa zikilinganishwa na kazi za nyumbani za wanawake. Mwanamume alipoendelea kupata mali zaidi, wazo la mali ya kibinafsi lilizuka. Hapa ndipo shughuli zote za mwanamume zikaonekana kuwa muhimu kuliko za mwanamke. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa mwanamke kuanza kumtegemea mwanamume kiuchumi. Usawa wa mwanamume na mwanamke ukafikia kikomo.

### 4.6 Hitimisho

Sura hii imeweka wazi kwamba, ni kutokana na majukumu mbalimbali yaliyotengewa wanajamii katika miktadha tofautitofauti katika jamii ya Wanyankole ndiposa tunapata ujinsia kimajukumu unaothibitishwa na methali za kijinsia. Imedhihirika kuwa majukumu haya yalikuwa yamejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa kupitia ubabe-dume. Kutokana na madai haya tunapata kiini cha nafasi duni aliyotengewa mwanamke licha ya kuchukuliwa kuwa ni hali iliyokubaliwa na kufurahiwa na wanajamii. Ni kutokana na hali hii ndipo utafiti huu unapendekeza uhakiki wa methali za kijinsia kiudenguzi ili kuamua ni zipi zihifadhiwe na zipi zidenguliwe ili ziende sambamba na matakwa ya jamii ya Wanyankole inayobadilika kila uchao. Sura inayofuata imehakiki methali za kijinsia kimaana na kimatumizi katika jamii ya Wanyankole.

# SURA YA TANO

# UHAKIKI WA KIPRAGMATIKI KATIKA METHALI ZA KIJINSIA KATIKA JAMII YA WANYANKOLE

## 5.0 Utangulizi

Katika sura ya nne, tulifafanua namna methali za kijinsia za Wanyankole zilivyojitokeza katika nyanja maalum ndani ya jamii. Katika sura hii tunaangazia lengo la pili ambalo ni uhakiki wa kipramatiki katika methali za kijinsia katika jamii ya jadi na ile ya kisasa miongoni mwa Wanyankole. Inafahamika kwamba jamii ya Wanyankole imekuwa ikitumia methali za kijinsia katika nyanja mbalimbali kama vile uchumi, utamaduni, elimu, siasa, ndoa na dini, na kuwasilisha maana tofauti ndani ya jamii. Katika sura hii, tumechunguza namna methali hizi zinavyoweza kuathirika kimaana kutokana na mabadiliko ambayo yametokea katika nyanja hizi tofauti hasa katika karne hii ya 21. Ili kufanikisha lengo hili, methali hizi zimegawanywa katika Nyanja tano kuu ambazo nazo zimegawanywa katika miktadha mahsusi ili kuonyesha jinsi methali hizi zilivyoathirika kijinsia. Kwa msingi huu, tumeweza kuonyesha namna muktadha wa matumizi unaathiri maana ya methali maalum na hivyo kupendekeza mkabala wa kiudenguzi ili kupambanua maana ya methali za kijinsia katika jamii ya jadi na ile ya kisasa miongoni mwa Wanyankole.

## 5.1 Methali za Kijinsia, Kimalezi na Kimaadili

Jamii ya Wanyankole kama mojawapo ya jamii nyingi za Kiafrika, ilichukulia kipengele cha malezi na maadili kuwa ngao kuu katika kuendeleza familia na jamii kwa jumla. Kutokana na mgao wa kazi ndani ya jamii kijinsia, ilijitokeza kwamba mwanamke alikuwa ni nguzo kuu katika kuzaa na kulea watoto huku malezi yakiendana na maadili ya jamii pamoja na utamaduni wake tofauti na jinsia ya kiume. Mawazo haya yanathibitishwa na Maingi (2005) ambaye anaonyesha namna

mwanamke amewekwa pembeni kwa kutoshirikishwa katika maamuzi muhimu ya kijamii ilhali anasifiwa kwa mchango wake wa kuwalea watoto nyumbani.

Joro (2016) anashadidia utawala huo dhalimu akieleza kwamba mamlaka katika familia huandamana na mabavu ya mume, na mke hutarajiwa kutii mamlaka. Kwa mfano katika jamii ya Wanyankole, mwanamke alistahili kuomba ruhusa kwenda kwao na alipochelewa kurudi alikemewa na mumewe na kupigwa viboko. Hali hii ni bayana kwamba, mwanamke hakuweza kujihusisha na masuala nyeti ya kijamii ijapokuwa uzuri wake ulitokana na malezi yake mazuri katika jamii. Katika sehemu ifuatayo tunajadili methali zilizomhusu mwanamke kutokana na suala la malezi na maadili.

### 5.1.1 Methali za kijinsia ya kike, kimalezi na kimaadili

Kundi hili la kwanza limejadili mifano ya methali ambayo ilihusu malezi na maadili ya mwanamke tofauti na mwanamume katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Ilijitokeza kwamba, mwanamke alikuwa angali na jukumu hili la ulezi kuliko mwanamume hata katika jamii ya kisasa kwa kutegemea muktadha na maana ya methali. Katika kufanikisha hili, ililazimu kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole katika nyanja maalum ndani ya jamii. Ni kutokana na nyanja hizi ndipo mwanamke anapoonekana kuathirika kimuktadha na kimaana kutokana na majukumu aliyopewa kama inavyojidhihirisha:

**Mf 44**

**Kinyankole:** *Omwana mubi ajumisa nyina*
**Kiswahili:** Mtoto mbaya husababisha mama yake kutukanwa

Kijadi, methali hii ilitumika kusisitiza jukumu la mama katika malezi na maadili ya watoto. Jamii ilikuwa imemtengea mwanamke kazi hii huku mwanamume akitelekezwa. Hii ni kwa sababu iliaminiwa mwanamke ndiye alishinda nyumbani na

watoto wakati mwanamume akijishughulisha na mambo muhimu zaidi kule nje. Aidha, katika jamii ya kisasa, mambo ni tofauti, mwanamke wa kisasa amepata mwamko mpya katika kugombea nafasi sawa na mwanamume kielimu, kiuchumi, kidini, kitamaduni, kisiasa na kindoa. Hivyo basi, jinsia zote zimelazimika kufanya kazi ya kulea watoto.

Kutokana na mwamko huu mpya, Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitokeza na kuchunguza historia ya wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa ni chanzo cha kuwanyanyasa. Pia, wamejitokeza kuchunguza mwamko mpya katika jamii ya kisasa ambayo imempatia mwanamke usawa ndani ya jamii. Ni kutokana na historia hii ambayo imetusaidia kuelewa jamii ya Wanyankole, ambayo imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni ambao ulichangia katika kumtweza mwanamke na kumnyima nafasi ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii. Huu ndio mfumo wa kitamaduni ambao Wanaufeministi wa Kiafrika wanaupinga na kupendekeza mabadiliko ili jinsia zote ziwajibike katika malezi na maadili ya watoto.

Mwamko huu mpya unashadidiwa na Jeniffer (1975) ambaye anasema kuwa ingawa mwanamke amejitolea kufanya kazi za umma kama vile kuwa kiongozi, hadi sasa hadhi ya mwanamke haina msimamo dhabiti. Anaendelea kusema kuwa, utambuzi wa kiutamaduni wa mke na mume mnamo miaka (1980) wanawake walikataa kuwa kikundi cha wafuasi na ndipo kuanza kusema wana sauti tofauti, kazi tofauti, namna tofauti ya mapenzi na familia kulingana na mwanaume kama ilivyoendelezwa na Humm (1989) na hapo, tofauti za kijinsia zikaendelea. Kutokana na kauli za wataalam hawa, ni wazi kwamba mwanamke amesawiriwa kwa namna iliyo tofauti na ile ya jamii ya Wanyankole. Wao walimwona mwanamke kama mwenye uwezo na hivyo wanapinga utamaduni ambao ulimnyima fursa ya kuweza kujiendeleza. Madai haya yanaungwa mkono, na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao hunuia kumzindua

mwanamke kutokana na udunishaji wa utamaduni. Methali zifuatazo zinashadididia uwezo wa mwanamke.

**Mf 45**

**Kinyankole:** *Enaku yotangambire nyoko tetuba.*
**Kiswahili:** Shida ambayo hujamwambia mama yako haipungui.

Kimuktadha wa kijadi, mama alichukuliwa kuwa jinsia tofauti na baba kutokana na sifa alizopewa ndani ya jamii kama vile upole, ukarimu, unyenyekevu, ushauri, usikivu na usamehevu. Kwa hivyo, kutokana na sifa hizi, alitarajiwa kuwa suluhisho kwa shida ambazo watoto walikumbana nazo nyumbani na nje ya boma. Hii ilimaanisha kwamba, mama alikuwa na muda wa kutosha kuwaelewa watoto tofauti na mwanamume. Hata hivyo, ni vizuri kutambua kuwa wakina baba walikuwa hawahusiki moja kwa moja katika malezi ya watoto, ijapokuwa walikuwa watoto. Kwa mfano, kina baba walipata muda na watoto wa kiume namna ya kuwa viongozi hodari na warithi wazuri. Kwa msingi huu, ni vizuri kutambua kila jinsia iliwajibikia watoto licha ya kuwa kwa kiwango kikubwa ilikuwa ni mama. Ni kutokana na hali hii katika jamii ya kisasa, ushirikiano huu umesisitizwa sana kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii. Hii ni kwa sababu, jinsia zote zimepata usawa katika nyanja zote ndani ya jamii. Hoja hii inaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika, ambao huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa na harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya. Hii inatubainishia hali ngumu tofauti ambazo mwanamke alikuwa anapitia ndani ya jamii zilizosababisha kuonewa na kupewa jukumu kama hili.

Kwa msingi huu, Wanaufeministi wa Kiafrika wamejaribu iwezekanavyo, kumpatia mwanamke uwezo wa kujikomboa na kujenga jamii mpya kwa kumpatia fursa sawa na mwanamume katika jamii ya kisasa.

Wanaudenguzi wanawaunga mkono Wanaufeministi wa Kiafrika kuhusu jukumu la ulezi na maadili. Wao kama wanaudenguzi wanasema, udenguzi ni uhakiki unaojikita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Kwa mfano, katika muktadha wa kijadi, mwanamke alipewa sifa nzuri za kuwa mama mlezi kuliko mwanamume kutokana na uzoefu wake wa kulea watoto. Vivyo hivyo katika jamii ya kisasa, mwanamke angali anarejelewa kwa sifa hizo ingawa kuna ushirikiano kati ya mwanamke na mwanamume tofauti na ilivyokuwa katika enzi za jadi.

Kwa msingi huu, wanaudenguzi wanasema methali inaweza kujitosheleza na kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Kwa mfano, katika muktadha wa kijadi, mama alistahili kuwa mlezi mkuu wa watoto, ilihali katika jamii ya kisasa mama angali na jukumu hili lakini wanasaidiana na baba tofauti na mtazamo wa kijadi. Katika kusisitiza ufaafu wa mama katika malezi ya watoto kumliko baba, Meider (1950), anasema "Mama alikuwa mwalimu wangu mkuu, mwalimu wa huruma, upendo na kutoogopa. Ikiwa upendo ni mtamu kama ua, basi mamangu ni hilo ua tamu la upendo." Ni wazi kuwa mama ndiye hukaa na watoto kwa muda mwingi, kwa hivyo ndiye alipewa jukumu la malezi kwa watoto hasa katika muktadha wa jadi. Hali hii inajitokeza katika mifano ifuatayo:

**Mf 46**

**Kinyankole:** *Omukazi tayechwa kizire*.
**Kiswahili:** Mwanamke hajikati kizazi.

Katika muktadha wa kijadi, ilikuwa ni kazi ya mama kuzaa na kuwalea watoto. Kutokana na huruma yake, hakuweza kumpiga mtoto hadi kumfukuza nyumbani, tofauti na mwanamume ambaye alikuwa na mamlaka ya kufanya hivyo. Kitamaduni, mwanamke alitazamiwa kuwa mwenye huruma na mwenye kuendeleza maadili kuliko baba. Aidha, baba pia alikuwa mwenye huruma, ijapokuwa hakuweza kulinganishwa

na mama kimaumbile. Hili lilitokana na ukaribu ambao mama alikuwa nao kumhusu mtoto. Kwa hivyo, ikiwa mama alikuwa anampiga mtoto, hakuweza kumuumiza au kumfukuza nyumbani. Hii ilitokana na sababu kuwa, utamaduni haukumruhusu, na pili alikuwa na huruma ya mama mzazi. Katika jamii ya kisasa, wazazi wote wanastahili kuwajibikia watoto wao kwa kila hali bila kuachia jinsia moja. Usawa huu katika malezi na maadili unaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika, ambao huchunguza hali ngumu ambazo mwanamke alipitia kuwalea watoto tofauti na mwanamume. Ni kutokana na hali hizi, wanaufeministi wamejitokeza na kuweka mikakati ya kuleta usawa katika nyadhifa tofauti za jamii. Kwa kufanya hivi, muktadha wa methali hii umeathiri maana na kulazimu udenguzi ufanyike ili methali ieleweke katika jamii ya kijadi na kisasa ya Wanyankole.

**Mf 47**

**Kinyankole:** *Eziwaterwa nyoko tizaba nkoni.*
**Kiswahili:** Viboko ambavyo umepigwa na mama yako si viboko.

Katika muktadha wa kijadi,, viboko vya mama vilikuwa haviwezi kumuua mtoto. Kupiga mtoto ilikuwa ni njia mojawapo ya kumkumbusha kuwa alikuwa ameenda kinyume na matarajio ya familia. Katika jamii ya kijadi, mama alitazamiwa kuwa mwenye kueneza maadili kwa watoto tofauti na kina baba. Jukumu hili ambalo mama alipewa hakuweza kulitimiza pasipo na kumpiga mtoto. Hata hivyo, si sahihi kusema kuwa kina baba walikuwa hawawapigi watoto, la hasha. Jamii ilichukulia kuwa baba aliwajibika mara tu mama alipoona kuwa mtoto ameshindwa kubadili kabisa. Hii ilimaanisha kuwa, mwanamume alikuwa na uwezo kuliko mwanamke kuhusu mambo ya malezi na maadili, kwani alikuwa hakimu wa mwisho nyumbani. Aidha, katika jamii ya kisasa, mama angali anapewa kipaumbele katika malezi ya watoto. Hata hivyo, jinsia zote zimeweza kujiendeleza kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kidini na kitamaduni. Tofauti na jamii ya kijadi, jinsia zote zinashirikiana sasa katika kuwalea

watoto kwa pamoja. Hii ina maana kwamba, baba si hakimu wa mwisho tena kama utamaduni ulivyokuwa unamchukulia. Mawazo haya tofauti yanaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, ambayo hunuia kumzindua mwanamke katika nyanja tofauti ndani ya jamii tofauti na kijadi. Hali hii imemwezesha mwanamke kuwa na usemi ndani ya jamii, jambo ambalo limemwezesha kushirikiana na mwanamume bila kubaguana. Kwa hivyo, imebidi kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia, katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Kwa kufanya hivi, umuhimu wa mama katika methali hii umeeleweka kimaana katika miktadha hii miwili tofauti katika jamii ya kisasa na ile kijadi ya Wanyankole.

**Mf 48**

**Kinyankole:** *Omukazi taba mugyeni.*
**Kiswahili:** Mwanamke hawi mgeni.

Mwanamke katika muktadha wa kijadi alikumbushwa yeye hawi mgeni daima. Hili lilieleweka katika jamii ya Wanyankole, kwa sababu tangu utotoni mwanamke alikuwa amefunzwa kazi tofauti na zile za mwanamume na hakuona shida yoyote kuzifanya ugenini. Kitamaduni, mwanamke alikuzwa kutozembea kazini kwani hangeweza kupata mwanamume wa kumuoa. Kwa hiyo, kutokana na tishio hilo, hakuwa na budi kufanya kazi zake bila kulalamika. Aidha, mwanamume pia alikuwa na kazi zake maalum ambazo alistahili kuzitimiza. Kwa msingi huu, utamaduni ulikuwa unamwonya mwanamke zaidi kuliko mwanamume dhidi ya uvivu. Katika jamii ya kisasa, jinsia zote zimepewa fursa sawa ya kujiendeleza kimaisha pasipo tishio la kukosa kuolewa. Kutokana na kushirikiana, jamii imepata mwamko mpya wa kimaendeleo kama vile kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kidini na kitamaduni na kulazimu jinsia zote kufanya kazi kwa pamoja bila kubaguana. Kutokana na mabadiliko haya, Wanaufeministi wa Kiafrika wamesaidia kuchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa na harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya. Kwa kufanya

hivi, mwanamke amekombolewa kutokana na hali duni za kijadi na kupewa uhuru wake wa kujikomboa na kujenga jamii mpya.

Greville (1982), anasisitiza haja ya mwanamke kujitoa katika hali hii kwa kusema kuwa, kila utamaduni una namna unavyomsawiri mwanamke, lakini kwake alikuwa na sifa za kuweza kuendeleza jamii. Mawazo ya Greville yanaungwa mkono na Gazeti moja nchi Yemen (2015) liitwalo *Yemen Time*. Katika gazeti hilo, Mohammed Nasher anasema kuwa mwanamke si lazima afanye kazi nyumbani tu, pia anaweza kufanya kazi nje ya nyumba. Vilevile anasema kuwa mwanamke anaweza kuongoza nchi. Kwa hiyo mtalaam huyo, anaona mwanamke kama aliye na uwezo mkubwa punde anapopewa nafasi katika jamii tofauti na namna methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole zinavyomsawiri mwanamke. Kwa msingi huu, kuna methali hii inayoonyesha umuhimu wa jinsia zote kushirikiana katika jamii ya kisasa ya Wanyankole. Hii inamaanisha kuwa kuna haja ya kuzidengua baadhi ya methali za kijinsia ili ziambatane na mahitaji ya jamii ya jadi na ile ya kisasa miongoni mwa Wanyankole. Baadhi ya methali hizo ni kama zifuatazo:

**Mf 49**

**Kinyankole:** *Omwana oine mukaishe tahwa bunaku.*
**Kiswahili:** Mtoto aliye na mama wa kambo haishiwi huzuni.

Katika muktadha wa jadi, tunapata picha kuwa, mama wa kambo hakuwa mzazi mzuri kwa watoto ambao alikuwa amewakuta ndani ya nyumba hiyo. Jambo hili liliwafanya watoto hao kuishi kwa huzuni. Hii ilimaanisha kuwa, katika jamii ya Wanyankole, mwanamke alipoolewa alikumbushwa methali hii ili aendeleze malezi na maadili mazuri kwa watoto hawa. Ikiwa mwanamke alienda kinyume na methali hii, ilikuwa ishara kuwa malezi yake kwao yalikuwa mabaya. Aidha, jamii ya Wanyankole ilikuwa inapenda umoja katika ndoa, ingawa wanaume waliruhusiwa kuoa zaidi ya mwanamke

mmoja. Vilevile, kutokana na jamii ya kisasa ambayo imepata mwamko mpya, mama wa kambo ameweza kujiendeleza kimaisha na hata kuwa bora kuliko mama mzazi katika malezi. Kwa hivyo basi, si sahihi kusema mama wa kambo ni mbaya, kwani kuna baadhi yao ambao ni wazuri. Kuna uwezekano ubaya wa mama wa kambo ulitokana na hali duni iliyopatikana. Kwa mfano hali kama ukosekanaji wa usawa katika ugawanyaji wa mali, wake wengi bomani, kazi nyingi, na pia kulea watoto wengi ndani ya boma. Haya yote yanaweza kuwa yalichangia mama huyu kuwa mbaya. Ni kutokana na hali hizi duni, Wanaufeministi wa Kiafrika wamesaidia kuchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa chanzo cha kunyanyaswa na kisha kumsaidia kupata uhuru wake kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii ya kisasa. Hali hii imemwezesha kushirikiana na mwanamume ili kubadili mtazamo hasi wa kijadi. Ni kwa msingi huu, methali hii ilibidi kudenguliwa ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Kwa kufanya hivi, mwanamke amepata fursa sawa na mwanamume na kujikomboa. Aidha, kutokana na msingi huu, mama wa kambo katika jamii ya kisasa anasawiriwa kwa njia chanya kuliko ilivyokuwa hapo awali.

**Mf 50**

> **Kinyankole:** *Omukazi otamanyire ekimutungire eyiba ajikwasa omukono gumwe.*
> **Kiswahili:** Mwanamke asiyejua thamani ya mumewe hushika uume wake kwa mkono mmoja.

Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, mwanamke alifaa kumtii mumewe kwa kila hali kwa sababu ni yeye aliyekuwa anamwajibikia kwa kila jambo. Hii ina maana kwamba, kukosa kumheshimu ilikuwa ni ishara ya kukosa maadili. Kwa hivyo, mwanamke alikuwa anaonywa atambue nafasi muhimu ya mumewe ndani ya familia na katika jamii nzima. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa hali ya kumdunisha mwanamke miongoni

mwa Wanyankole inatokana na suala la kulipiwa mahari. Katika jamii ya Wanyankole, ilikuwa ni jambo muhimu mwanamke kutolewa mahari ya ng'ombe kama ishara ya kuwashukuru wazazi wa msichana. Hata hivyo, kwa mwanamke, mahari ilikuwa chanzo cha kuteseka na kunyanyaswa kwake katika jamii hii. Mwanamume alihisi kuwa alikuwa amemnunua na kwa hivyo mwanamke alifanyishwa kazi nyingi na wala hakuruhusiwa kuwatembelea wazazi wake kwa urahisi. Oguli (2004) anathibitisha hoja hii kwa madai kuwa kuwa katika baadhi ya jamii za Kiafrika, mahari inaangaliwa kama mabadilishano ya nguvu kazi za mke. Aidha, Kaye, Mirembe, Ekstron, Bantebya na Johansson (2005b) wanasema kuwa mahari ilimpa mume mamlaka ya kumdhibiti na kumtumikisha mke wake.

Msimamo huu wa jamii ndio unapigwa vita na Ufeministi wa Kiafrika kwa kuhakiki hali za mwanamke katika jamii zilizokuwa chanzo cha kudunishwa na kupendekeza namna mwanamke anaweza kujikomboa na kujenga jamii mpya. Wanaufeministi wanasistiza kuwa ni kunyimwa haki za usemi kuhusu masuala nyeti ya jamii ndiko kulichangia katika udunishaji wa mwanamke. Hali hii ni tofauti na muktadha wa jamii ya kisasa, ambao umeanza kuona mambo tofauti kutokana na ubadilikaji wa uchumi, siasa, elimu, utamaduni, dini na ndoa. Katika jamii nyingi za kisasa, tunaona mwanamke na mwanamume wanashirikiana katika nyadhifa tofauti ndani ya jamii.

Kwa kweli mwanamke kushiriki katika masuala mbalimbali katika jamii ya kisasa kumemwezesha mwanamke kufanya kazi kwa bidii na kujenga jamii mpya na pia kupata ukombozi wake. Margaret (1845) anasisistiza kuwa iwapo tunataka kuimarisha maendeleo ya jamii, kila mwanajamii lazima apewe nafasi ya kuchangia kadiri ya uwezo wake bila kudhibitiwa kwa misingi ya jinsia yake au hali yoyote ile inayowekwa na jamii. Maoni haya yalimchochea mtafiti kuchunguza namna majukumu yanagawanywa kijinsia katika jamii ya Wanyankole. Kutokana na hali hii ilitambulika

kwamba, wanaume walipewa kazi za kihadhi kama vile za ushujaa na uongozi huku wanawake wakifanya kazi za hadhi ya chini kama vile kupika, kufurahisha mwanamume kingono, kuzaa na kulea. Kwa msingi huu, muktadha wa methali hii umeathirika na kufanya maana ya methali kubadilika na kumtazama mwanamke wa kisasa kuwa na uwezo sawa na mwanamume katika jamii moja kimaendeleo.

Kwa msingi huu, methali katika Mf 50 inaweza kupoteza maana katika jamii ya kisasa, ikiwa msomaji hataweza kuisoma kwa makini. Mohammed (2006) anasisitiza kuwa, msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana. Kwa mfano katika methali hii, tunapata maana ya moja kwa moja kuwa mwanamke alistahili kumheshimu mumewe, kwa sababu alikuwa anamwajibikia. Kwa hivyo, ingawa jamii ya kisasa imeweza kupiga hatua na kupewa usawa, ni lazima mwanamume aendelee kuheshimiwa kwa sababu ndiye kiongozi wa familia.

Ingawa katika jamii ya jadi mwanamume aliheshimiwa kutokana na maumbile yake akilinganishwa na mwanamke, sifa hii pekee haina mashiko katika jamii za kisasa. Katika jamii ya kisasa, mwanamume anaheshimiwa zaidi kwa kuiwajibikia familia yake. Baadhi ya wanaume katika jamii ya kisasa wanaelekea kuyatelekeza majukumu yao kwa wake zao hali ambayo inawaondolea madaraka haya. Kwa msingi huu, methali hii iliweka wazi kuwa jinsia zote katika jamii ya kisasa lazima zishirikiane kufanya kazi na hivyo kustahili kupewa heshima.

**Mf 51**

> **Kinyankole:** *Omukazi ayomba azibira omutabani kuragwa.*
> **Kiswahili:** Mwanamke mgomvi husababisha mtoto wake wa kiume kutorithishwa.

Katika muktadha wa jamii ya Wanyankole wa kijadi, mtoto alirithishwa kutokana na malezi aliyopewa na mama yake. Hii ilimaanisha kwamba, mama alitazamiwa kuwa kipaumbele katika kudumisha malezi na maadili mazuri kwa mtoto huyu ndiposa

arithishwe. Kwa mfano, ilichukuliwa kitamaduni kuwa, mwanamke akiwa mgomvi bila shaka mtoto wake naye angekuwa vivyo hivyo. Vilevile, mtoto huyo hangekuwa kiongozi mzuri na kwa hivyo baba angelazimika kutafuta mrithi mwingine. Kwa hivyo, mama alilazimika kuwa mfano mzuri hata ikiwa alikuwa anapitia hali ngumu. Giddens (2004) anasisitiza kuwa ubaguzi wa kijinsia si wa kimaumbile bali umejengwa kiutamaduni na mwishowe umemnyima mwanamke haki kama za mwanaume za kupata elimu nzuri, kazi nzuri na furaha katika jamii. Kwa hivyo amali za jamii ndizo zinazomtengea mwanamke majukumu yanayombagua kijinsia.

Kwa hivyo, kutokana na mabadiliko mengi ambayo yametokea katika jamii ya Wanyankole, maana na matumizi ya methali katika Mf 51 yameathirika. Hii ni kwa sababu mwanamke wa kisasa amepewa fursa sawa na mwanamume. Hali hii imemwezesha kurundikia watoto wake mali pasipo kumtegemea mwanamume. Uwezo huu ndio Wanaufeministi wa Kiafrika wanauunga mkono, kwa kumsaidia mwanamke kupata utawala na ushujaa wake katika karne hii ya 21. Kwa kufanya hivi, miktadha hii miwili imeweza kuathiri maana ya methali hii na kuilazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Rorty (1996), anabainisha kuwa udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi utokeapo kwa mara ya kwanza, huonekana kama ni usaliti, lakini utokeaji wa ukiushi si ajali, bali hukusudia ujumbe uliokusudiwa. Mawazo haya yanaendana na mfano wa methali hii, *"Omukazi ayomba azibira omutabani kuragwa"* tafsiri yake "Mwanamke mgomvi husababisha mtoto wake wa kiume kukosa kurithishwa." Moja kwa moja, methali hii imeonyesha ukali kwa kumwonya mwanamke kuhusu maadili yake tofauti na mwanamume. Methali hii inaposomwa kwa mara ya kwanza, inaonyesha kuwa mwanamke alikuwa anasalitiwa na jamii. Lakini ukiichunguza zaidi utabaini si usaliti. Jamii ya kijadi ilimtarajia mama kuwa mnyenyekevu, mkarimu, mwenye huruma,

mwenye kupenda na mpole. Kwa hivyo, sifa hii ya ugomvi jamii haikumtarajia kuwa nayo. Lakini hata hivyo katika jamii ya kisasa, mwanamke mgomvi hakubaliki kumaanisha kuwa methali hii ingali na mashiko katika jamii hizi mbili. Kwa hivyo, mawazo ya Rorty yalikuwa tofauti na wanaufeministi, kwa sababu hakuna usaliti katika methali hii isipokuwa ni ukweli kuhusu maadili ya mwanamke. Kwa msingi huu, inakuwa ujenzi bora wa jamii jinsia zote zinapoheshimiana katika maendeleo ya jamii. Hivyo basi, methali hii ilibidi kudenguliwa ili kueleweka katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole; yaani ile ya kijadi na kisasa.

**Mf 52**

> **Kinyankole:** *Enkoni eteire mukabaro ku'ogibona ogirenzya orugo*.
> **Kiswahili:** Fimbo iliyotumiwa kumpiga mke mwenza, ukiipata unaitupa nje ya zizi.

Kutokuwa na maadili ilikuwa ni sababu moja ya mwanamke kupigwa na mumewe katika jamii ya Wanyankole ya kijadi. Kwa hivyo, mwanamke alistahili kuwa amelelewa vizuri na kufunzwa maadili kutoka kwa wazazi wake. Kwa hivyo, alipoolewa na kuanza tabia mbaya kama vile, uvivu, kugombana, uchafu, mdomo kaya na kukosa kuwajibikia watoto wake, alipigwa na mumewe. Kwa sababu hii, mke mwenza alikuwa anaonywa kuwa angepigwa kama mwenzake ikiwa alikosa maadili. Kutokana na kuogopa kupigwa, aliamua kutupa fimbo hiyo nje ya zizi. Mwanamke kupigwa kulitokana na utamaduni ambao wanaufeministi wanapinga kwa kuchunguza historia ya wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa chanzo cha kunyanyaswa kwa mwanamke. Mara nyingi unyanyasaji huu, ulitokana na dai kuwa mwanamume alikuwa ametoa mahari na kwa hivyo mwanamke alikuwa kifaa tu cha kupigwa, kwa sababu utamaduni haukumruhusu kurudi kwao.

Dai hili potovu linawekwa wazi na Mary (1969). Akirejelea kabila la Nso kule Cameroon anasema kuwa mahari nyingi za Kiafrika ni chanzo cha wanawake kuteseka.

Katika kabila hilo, mwanamke hakuruhusiwa kuomba talaka hata ikiwa alikuwa ananyanyaswa na mumewe kwa vile alikuwa amelipiwa mahari.

Tunaona hali hii haikuwa tofauti na ile iliyopatikana ndani ya jamii ya Wanyankole. Ni ukweli kabisa baada ya mwanamke kutolewa mahari, hakuruhusiwa kurudi kwao isipokuwa alipomwomba ruhusa mumewe na kuambiwa siku ambazo angefaa kurudi kwake. Ni hali duni kama hizi ndizo zinapingwa na Wanaufeministi wakidai usawa wa kijinsia ndani ya jamii. Wanaufeministi wa Kiafrika wanashikilia kuwa wanawake waliteseka kutokana na historia za ufungwa wa utamaduni zilizoendelezwa na ubabe-dume ndani ya jamii. Kwa hivyo wanahimiza wanawake kugombea tena utawala na ushujaa wao kutokana na mwamko huu mpya ndani ya jamii. Hali hii imesababisha jinsia zote kuheshimiana na kuleta maendeleo ndani ya jamii. Kutokana na utofauti huu wa mambo, methali hii imeathirika kimaana na kimuktadha na kuilazimu idenguliwe ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 53**

**Kinyankole:** *Omukazi mubi tumwihaho Omwana.*
**Kiswahili:** Mwanamke mbaya huzai naye.

Imejitokeza wazi kuwa, jamii ya Wanyankole jadi ilikuwa na umakini mwingi kuhusu suala la ndoa. Kimuktadha, ilibidi wazazi kuwatafutia watoto wao wake, kwa madai kwamba walitambua familia ambazo zilikuwa na historia nzuri katika jamii. Kwa kufanya hili, walikuwa wanaepukana na historia mbaya ya maadili kama vile uchawi, ugomvi, ugumba, wizi, wivu na uchafu. Hii ni kwa sababu waliamini mwanamke kama huyo alipoolewa ndani ya boma, alikuwa kisirani na kwa hivyo hata watoto wake vilevile wangekuwa kama yeye tofauti na mwanamume. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, mabadiliko yamewezesha jinsia zote kujichagulia mchumba pasipo kuhusisha wazazi. Jambo hili limewezesha jinsia zote kujuana vizuri, ili kuzuia historia mbaya

ndani ya ndoa zao. Wanaufeministi wa Kiafrika wanaunga mkono uhuru huu, kwa kumwinua mwanamke ili kupata ukombozi wake. Lakini hata hivyo, ingawa wamepewa uhuru huu, suala la familia lingali jukumu la wazazi kufuatilia kuhakikisha wanafanya sherehe za utamaduni. Ni kutokana na hali hii, tunaona utamaduni wa kulipa mahari bado unazingatiwa kuhusu suala la ndoa. Kwa msingi huu, methali hii iliathirika kimaana, kimatumizi na kimuktadha na kuilazimu kudenguliwa ili kueleweka katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 54**

**Kinyankole**: *Omukazi murungi niwe anyamisiriza Iba.*
**Kiswahili**: Mwanamke mzuri ndiye humbembeleza mumewe kulala.

Katika jamii ya Wanyankole kimuktadha, mwanamke mzuri ni yule aliyekuwa amefunzwa namna ya kumtumkia mumewe katika kila jambo. Kwa mfano, kuweza kupika chakula kitamu, kuzaa watoto wazuri na kuwalea, kulima na kumfurahisha mumewe kingono. Kutokana na uwajibikaji wa mwanamume katika familia yake, mwanamke alijitahidi kumbembeleza mumewe. Kwa hivyo, mwanamke alikuwa mtumwa ndani ya nyumba yake tofauti na mwanamume kimajukumu.

Kwa mujibu wa Bamgbose (2006) mume anapewa 'idhini' au haki fulani kutokana na kulipa mahari, ambapo 'anaruhusiwa' kumfanya chochote mke wake. Anaendelea kusema kusema, " Mwanamke aliyelipiwa mahari na mume wake kwa namna ya kununua lazima atachukuliwa na kutumiwa kama mtumwa, yaani bila kuheshimwa kama binadamu aliye sawa na mume wake katika mahusiano yao (Kaye na wenzake, 2005b; Dery, 2015). Hivyo, mahari inakuwa kiini cha udhalilishaji na unyanyasaji wa mke huyo ambapo mume atahakikisha mke anatumiwa kama mtumwa kadri inavyowezekana, kwa ajili ya kufidia mahari aliyotoa. Maoni haya yalikuwa kweli kabisa katika jamii ya Wanyankole, kwa sababu mwanamke alikuwa amedunishwa

kiasi cha kumbembeleza mumewe kulala na kufanya kazi zote nyumbani kwa madai kuwa alikuwa amelipiwa mahari.

Kwa upande mwingine, hadhi aliyopewa mwanamume, ilikuwa tofauti na ile ya mwanamke kwani alitambulika kama shujaa katika ndoa: Neno hilo linafafanuliwa katika TUKI (2004), kwamba shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari. Kwa hivyo, wanaume wamerejelewa kama mashujaa, hali inayowapa hadhi ya juu sana wanaume wote kwa jumla. Katika muktadha wa kisasa, jamii ingali inashikilia methali hii kuwa ya muhimu katika ujenzi wa familia na jamii kwa ujumla. Ingawa jamii imepata mabadiliko mengi, bado mwanamke kwa kiasi kikubwa anafaa kumjali mumewe na wote kushirikiana. Kwa msingi huu, jinsia zote zimepewa uhuru katika jamii ya kisasa kujiendeleza kimaisha tofauti na mtazamo wa kijadi. Huu ndio ukombozi ambao wanaufeministi wanaukubali katika kumpatia mwanamke ushujaa wake aliokuwa ameupoteza hapo awali. Kwa msingi huu, methali hii ililazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

### 5.1.2 Methali za kijinsia ya kiume kimalezi na kimaadili

Kimuktadha katika jamii ya Wanyankole, kila jinsia ilikuwa na namna ilivyoendeleza maisha yake kuhusu malezi na maadili ndani ya jamii hii. Katika kundi hili, tumeainisha baadhi ya methali ambazo zilitumiwa na wanaume katika majukumu yao ya kila siku. Kimuktadha katika jamii ya Wanyankole, wanaume walikuwa hawahusishwi kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza malezi na maadili ya nyumbani. Hali hii ilitokana na kuwa wakina mama ndio waliokuwa wanashinda na watoto. Ni kutokana na madai haya tunaona Wanaufeministi wa Kiafrika wakijitokeza na kuchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa ni chanzo cha kumdunisha mwanamke kutokana na maumbile yake. Hii inamaanisha kwamba, ni kutokana na historia za utamaduni ndizo zilizomfanya mwanamume kutohusishwa kwa

kiasi kikubwa kwa madai kuwa ni kazi ya mwanamke. Ni kupitia historia ya utamaduni huu, tunaona wanaufeministi wanajitokeza na kujaribu kuibadili kwa kumpatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika jamii. Fursa hizi ni kama vile kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kitamaduni na kidini ili kuwapo usawa katika kuendeleza ushirikiano. Ubadilikaji huu wa mambo katika miktadha hii miwili, umeweza kuathiri maana na matumizi ya methali hizi na kusababisha kudenguliwa kama inavyojidhihirisha:

**Mf 55**

**Kinyankole:** *Abashaija tibabagaya*.
**Kiswahili:** Wanaume hawadharauliwi.

Methali hii imeonyesha wanaume katika jamii ya Wanyankole kijadi hawakufaa kudharauliwa na wanawake, kwa sababu ilikuwa ni kazi yao kuwalinda na kuwawajibikia. Hii ina maana kwamba, mwanamke alikuwa anafunzwa kutoka utotoni ni kwa sababu gani alistahili kumheshimu mumewe. Hali hii ni tofauti na jinsia ya kiume iliyokuwa na hiari kuhusu suala hili. Mwanamume kutodharauliwa kumetokana na sifa ambazo jamii ilikuwa imempatia kama vile, kiongozi, shujaa na hakimu bora. Millet (1969) anasema kuwa malezi ndiyo chanzo cha hali dhalilishi na duni ya mwanamke katika jamii. Hii ni kwa sababu mtoto mvulana analelewa kwa namna ya kumdhihirishia sifa za uume; kujikidhia ‘haja’ za kiume. Hali hii inamwandaa na kumtambulisha kuwa uume unahusu matumizi ya nguvu, utundu na umilikaji wa kila kitu. Kwa hivyo, kutokana na sifa hizi, ilibidi mwanamke kunyenyekea kwa kila hali. Kwa msingi huu, limekuwa jambo la kawaida kwa mwanaume kumtawala mwanamke. Katika jamii ya kisasa, mwanamume ataheshimiwa ikiwa anawajibikia familia yake ipasavyo. Aidha, kutokana na madai haya, nsadharia ya Ufeministi wa Kiafrika inanuia kumzindua mwanamke katika kupata ukombozi wake alioupoteza hapo awali. Ili kufanikisha suala hili, ni lazima pawepo usawa ndani ya jamii kiuchumi, kielimu,

kisiasa, kitamaduni, kindoa na kidini. Ni kutokana na hali hii tunaona methali Mf 55 inalazimika kudenguliwa ili ieleweke hasa katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Katika kusisitiza hoja hii, Mohammed (2006) anaeleza kuwa, msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana, kumaanisha ikiwa msomaji hana uwezo wa kusoma na kuelewa kwa undani maana ya methali hii, bila shaka atapoteza maana kamili iliyokusudiwa. Kwa mfano, "*Abashaija tibabagaya"* tafsiri yake wanaume hawastahili kudharauliwa. Kwa hivyo, msomaji anapoisoma methali hii bila kuelewa historia na utamaduni wa jamii ya Wanyankole, atasema wanawake walikuwa wanaonewa na kupendekeza iondolewe katika jamii ya kisasa. Msomaji huyu akisahau, utamaduni ulikuwa umemtengea kila mtu kazi yake kutokana na miundo ya jamii. Aidha, Mohammed (keshatajwa) anaonya kuchukulia maana ya methali hii kijuujuu, kwa sababu kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii, ni vizuri jinsia zote kushirikiana na kuheshimiana ili kuleta maendeleo ndani ya jamii. Kwa hivyo, kulingana na Mohammed, anakubaliana na mwamko mpya, ijapokuwa anaunga mkono heshima kwa mwanamume kuwa ni kitu muhimu katika jamii zote mbili. Kwa msingi huu, muktadha uliathiri maana ya methali hii na kulazimisha idenguliwe ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 56**

**Kinyankole**: *Ibega tiringana na omutwe.*
**Kiswahili:** Bega halilingani na kichwa.

Kimuktadha wa kijadi, mwanamume alikuwa kichwa kumaanisha kiongozi naye mwanamke bega kumaanisha msaidizi wake. Sifa za sehemu hizi, zilizingatiwa kila mtu akifanya kazi zake. Hili lilitokana na sifa ambazo mwanamume alikuwa amepewa ndani ya jamii tofauti na mwanamke. Mwanamke alibaki daima chini ya mwanamume, kwani ilikuwa ni jukumu la mwanamume kuwajibikia boma lake. Methali hii ilionyesha nafasi ya kila jinsia katika jamii. Aidha, ilikuwa ni njia mojawapo ya kuleta

amani katika jamii, kwa sababu kila mtu alijua nafasi yake na majukumu yake. Lakini hata hivyo, hii ilikuwa njia mojawapo ya kumzuia mwanamke kugombea nyadhifa mbalimbali ndani ya jamii. Ni kutokana na hali hii, tunaona Wanaufeministi wa Kiafrika, wanachunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa chanzo cha kumnyima mwanamke haki na utawala wake kwa mujibu wa kunyenyekea. Hali hii imetokana na dai kuwa, mwanamke hakustahili kuwa kiongozi daima pasipo mwanamume, jambo ambalo lilimtweza kimaendeleo. Madai haya yanaungwa mkono na King'ei (2015) anayesema kwamba mila na desturi kama hizi zinazombagua mwanamke zinajitokeza kuwa "silaha ya mwanamume ya kumdunisha" na kumnyanyasa mwanamke. Isitoshe, hata asasi za kiserikali kama vile, sheria zinaendeleza ubaguzi huo wa kijinsia, ambapo mke akitengana na mume wake, anapewa tu haki ya kubaki na mtoto iwapo mtoto huyo ni mchanga ambaye bado anahitaji malezi ya mama. Aidha hii ni mojawapo ya hali ambazo, zimewafanya Wanaufeministi wa Kiafrika kumzindua mwanamke kiuchumi, kielimu, kitamaduni na kisiasa na kuona kuwa jinsia zote zinapata usawa ndani ya jamii.

Kwa hivyo, nadharia hii imempatia mwanamke matumaini ya kujitokeza na kugeuza historia ya kuwa mwanamke hajiwezi. Huu ndio msingi wa utafiti huu kuchanganua maana na matumizi mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa miongoni mwa Wanyankole kiudenguzi.

Mohammed (keshatajwa) anaeleza kuwa msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa kupitia vivuli vya maana. Kwa mfano katika methali hii, *"Ibega tiringana na mutwe"* tafsiri yake "Bega halilingani na kichwa." Ili kuelewa methali hii, ni lazima msomaji atambue maana ya ndani kwa sababu itakuwa vigumu kuelewa namna mwanamume anavyorejelewa kuwa kichwa na vilevile mwanamke kuwa bega. Katika mazingira haya, ndipo Mohammed (2006) anamwonya

msomaji au msikilizaji kuwa na uelewa wa utamaduni wa jamii husika ili kuepukana na kupoteza maana. Kutokana na madai haya, tumeona methali hii imeathirika kimaana katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa na kulazimu udenguzi ufanyike.

**Mf 57**

**Kinyankole:** *Nyineeka kuagamba Omukazi tamugarukamu.*
**Kiswahili:** Mwenye nyumba akiongea mwanamke hamjibu.

Methali hii kimuktadha iliweka bayana kuwa mwanamke katika jamii hii hakuwa na usemi wowote, kwa sababu hakustahili kumjibu mumewe kuhusu jambo lolote. Hii ilimaanisha kuwa, jamii iliamini mwanamke alikuwa hana haja ya kujua kitu chochote nje ya mazingira yake ya nyumbani. Vilevile, kitamaduni mwanamke mwenye maadili alikuwa mnyamavu, na mwenye kujali shughuli zake.

Maoni haya kumhusu mwanamke, yanaungwa mkono na Oqudipe (1987) anayedai kuwa wanawake wamepewa majukumu duni na yanayosawiriwa kihasi kama vile wachawi. Kwa upande mwingine, wanaume husawiriwa kuwa werevu, wenye nguvu, wenye kuaminika na wenye uwezo wa uongozi kwa kuzaliwa na wasiohitaji kujibiwa na mwanamke. Hii ndiyo taswira ya mwanamke wa Kinyankole ambaye alikuwa hana usemi wowote isipokuwa tu kumtumikia mumewe na jamii kwa jumla. Kelly (2003) na Mosha (2013) wanashadidia kwamba kwa kuwa wanawake hawashiriki katika shughuli muhimu kama raia kamili katika jamii, hawawezi kujiendeleza, na hivyo wanabaki kundi duni linalodhalilishwa na kunyanyaswa kwa urahisi.

Mawazo ya wataalam hawa yanajitokeza katika methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole katika nyanja maalum katika jamii hii. Nyanja hizi zilionyesha hali mbalimbali ngumu ambazo mwanamke alipata kupitia ndani ya jamii. Kutokana na hali hizi, Wanaufeministi wa Kiafrika huchunguza hali kama hizi za mwanamke katika jamii zao, na kumsaidia kujikomboa katika kujenga jamii mpya. Kwa hivyo,

mwanamke wa kisasa amejikomboa na kujenga jamii mpya kama vile kiuchumi, kisiasa, kielimu na kitamaduni, jambo ambalo limemwezesha kujimudu kimaisha na kugombea nyadhifa sawa na mwanamume katika jamii moja.

Kwa hiyo, utofauti huu katika miktadha hii miwili ya methali, imeathiri maana na kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kisasa na ya kijadi ya Wanyankole.

**Mf 58**

**Kinyankole**: *Taaha omwasho teba rwango.*
**Kiswahili:** Kwenda nyumbani kwa baba yako si chuki.

Methali hii kimuktadha kijadi ilieleza namna jamii ya Wanyankole ilivyokuwa imejengeka kwa msingi wa mfumo wa kuumeni, pale ambapo mwanamume alikuwa amepewa uongozi na mamlaka ya jamii yote. Vilevile, kimaana jamii hii iliwaruhusu wanaume kuwaoa wanawake wengi ili kupata warithi wa mali zao. Kutokana na kuzaa watoto wengi, ilikuwa ni jukumu la baba kimalezi kuwakusanya watoto wake wote na kuwaleta nyumbani ili kutambua ukoo wao. Mwanamke hakuwa na ukoo, ni mwanamume tu ndiye aliyekuwa na fursa ya kuzaa watoto wengi hata nje ya ndoa na kuwaleta nyumbani. Aidha, kimalezi na kimaadili, ilikuwa ni jambo zuri watoto kufunzwa mambo kutokana na ukoo wa baba kuliko wa mama. Kwa hivyo, baba kama mzazi, ilibidi kuwajibikia malezi na maadili ya watoto wake tofauti na namna mama alivyokuwa anawajibikia.

Ni dhahiri kuwa msimamo huu ungali na mashiko katika jamii ya kisasa kuwa mtoto ni wa mwanamume. Madai haya yanaungwa mkono na Kanu (2014) anayesema kwamba, katika jamii za Kiafrika zinazoongozwa kwa misingi ya mfumo dume, watoto humilikiwa na baba ili kudumisha uhai wa baba katika familia, na kuendeleza ukoo katika kabila kwa ujumla. Hii ni tabia au mila nyingine ya kijamii ambayo inawadhalilisha wanawake na kuwafanya wabaguliwe na wanyanyaswe katika

mahusiano ya ndoa. Ingawa jamii imepitia mabadiliko mengi, bado jukumu kuu la mwanamume ni kuwatambua watoto wake kama utamaduni unavyoshikilia na kuwafundisha utamaduni wake. Kutokana na usawa ambao jinsia zote zimepewa, kazi ya mwanamke ni kushirikiana na mwanamume kuona watoto wanatambua ukoo wao, jambo ambalo lilikuwa mwiko kijadi.

Madai haya yanaungwa mkono na Rorty (keshatajwa) ambaye anafafanua kwamba, udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza, huonekana kama ni usaliti, lakini utokeaji wa ukiushi si ajali bali hukusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano katika methali ya "Kwenda nyumbani kwa babako si chuki" unapoisoma mara ya kwanza unaona inampatia mwanamume mamlaka yote kumhusu mtoto tofauti na mama aliyemzaa. Hii inaonyesha mwanamke alikuwa anasalitiwa kuhusu suala la ndoa kijadi. Kimsingi, siyo hivyo, kwa sababu kimaumbile ni mwanamume ndiye ambaye anambebesha mwanamke mimba. Kwa hivyo, hakuna kosa mtoto kujitambulisha upande wa mwanamume. Kwa msingi huu, methali hii imepata kuathirika kimaana na kusababisha kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kisasa na ile ya kijadi ya Wanyankole.

## 5.2 Maana na Matumizi ya Methali za Kijinsia Kikazi

Huu ni muktadha wa pili ambao ulishughulikia methali za kikazi zilizojitokeza kijinsia kuwahusu wanaume na wanawake katika jamii ya Wanyankole. Katika jamii ya Wanyankole, wanaume walikuwa wamepewa sifa za hadhi ya juu kuliko wanawake. Sifa hizi ni kama vile za uongozi na ushujaa.

Coates (1993) anasema kuwa tofauti za jinsia yaani ubwana wa mwanamume na unyonge wa mwanamke zinaanza siku zao za utotoni. Aidha, Mwachofi (1987) anasisitiza hali hii kutokana na kisasili kimoja ambacho kinashikilia kwamba, zamani

za kuumbwa binadamu, Mungu aligawanya kazi kati ya wake na waume. Mungu aliwashirikisha babu na nyanya zetu katika ugawanyaji huo kwa kuwauliza ni kazi zipi wangependa wenyewe kuzifanya. Hivyo, Mungu alipouliza nani atabeba mimba, atazaa na kulea watoto, atapika na kufanya kazi zote za nyumbani, mke akawa anadakiza na kujibu kwa sauti, "Ni mimi." Mume wakati huo wote alinyamaza. Hakuwa na ulimi mwepesi kama wa mke. Hatimaye Mungu alipouliza, "Nani atakuwa mwindaji?" Mume akajibu kichinichini, "Mimi." Kisasili hiki kinaisha kwa kutaja kwamba wepesi wa ulimi wa mke ndio ulimfanya kuwa na kazi nyingi zaidi ya mume. Mawazo haya yanaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo yanadhihirisha kuwa utamaduni na za Kiafrika ndizo kiini cha kunyanyaswa kwa wanawake wakilinganishwa na wanaume. Historia hii iliendelea kumwathiri mwanamke hadi karne ya 21 ambapo amejitokeza na kuanza kupigania haki zake kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kidini na kindoa, jambo ambalo limesababisha methali kuathirika kimuktadha na kimaana na kulazimu kudenguliwa.

### 5.2.1 Methali za jinsia ya kiume kikazi

Kundi hili limejadili baadhi ya methali za kijinsia ambazo zimeonyesha kijadi namna jinsia ya kiume ilivyostahili kufanya kazi zaidi kuliko ile ya kike. Hili limetokana na namna utamaduni ulivyokuwa umegawanya majukumu yake. Ujinsia katika kazi, uliashiria namna methali za kijinsia za Wanyankole zilivyopambanuliwa kwenye nyanja maalum ndani ya jamii. Hili lilitokana na namna utamaduni ulivyokuwa umempatia mwanamume mamlaka ya kuwa kiongozi katika mambo yote na kwa hivyo ilikuwa ni vyema kufanya kazi kuliko mwanamke. Lakini hata hivyo, katika muktadha wa kisasa, methali hizi zimeathirika kimaana kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii, ambao umeruhusu jinsia zote kufanya kazi na kushirikiana kimajukumu tofauti na msimamo wa kijadi. Wanaufeministi wanaunga mkono jambo la jinsia zote kufanya

kazi kwa pamoja na kujenga jamii mpya. Wanachunguza hali tofauti za mwanamke katika jamii zao zilizomdunisha na kumnyima ukombozi wake. Kwa hivyo, wanaufeminsti wanajaribu kumsaidia mwanamke kufikia usawa ndani ya jamii hii. Ili kufanikisha hili, wamepambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum ndani ya jamii.

**Mf 59**

**Kinyankole:** *Emirimo mingi ekazibira Bigyemano okutobora omukazi.*
**Kiswahili:** Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutoa ubikira wa mwanamke.

Tumetambua kuwa katika jamii ya Wanyankole kimuktadha kijadi, kila jinsia ilikuwa imepewa kazi zake pasipo kusaidiana. Hii inamaanisha kwamba, katika kugawana kazi hizo, mwanamume alikuwa anapewa kazi ngumu kuliko mwanamke, kwa madai ya kwamba mwanamke hakuwa na nguvu kimaumbile. Tofauti na kazi hizo za nje ya nyumba, mwanamume alikuwa na jukumu kuu la kuendeleza kizazi tofauti na jinsia ya kike. Kwa hivyo, methali hii ilikuwa inamkumbusha mwanamume, ingawa alikuwa anakazana kufanya kazi zingine ilikuwa vizuri kupata muda wa kuendeleza kizazi tofauti na mwanamke. Hii ni kwa sababu, jamii ilimheshimu mwanamume aliyekuwa na watoto wengi ikiwemo warithi. Imani kuhusu mwanamke kuwa dhaifu, ilitokana na ubabe-dume ambao ulikuwa umechorwa kwa msingi wa utamaduni. Aidha, imani hii ya mwanamke kuwa dhaifu, inaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa na harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya. Kwa hivyo, hali ambazo jamii ilikuwa imejiwekea kutokana na utamaduni, ilimfanya mwanamke kukata tamaa na kuzoea hali yake duni. Kutokana na hali hii, tunamwona mwanamke wa kisasa amejitokeza kupigania usawa katika uchumi, elimu, siasa, utamaduni, ndoa na dini ndani ya jamii moja na mwanamume. Mwamko huu mpya, umefanya muktadha wa methali hii kuathirika kimaana, katika

jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii hizi.

**Mf 60**

**Kinyankole**: *Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire*.
**Kiswahili:** Mtoto ambaye ana baba yake huepuka majonzi ambayo yangemuua.

Kimuktadha, methali hii imeendelea kuonyesha umuhimu wa mwanamume tofauti na mwanamke ndani ya jamii kuhusu uzalishaji wa mali. Hili liliweka wazi, ilikuwa ni kutokana na jasho la mwanamume ndio watoto wake wangeweza kufurahia maisha ya baadaye. Aidha, katika muktadha wa kisasa, methali hii kimaana na kimatumizi imebadilika kwa sababu jinsia zote zimejimudu kimaisha kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii. Hili limemwezesha mwanamke pia kuwajibikia watoto wake katika uzalishaji wa mali tofauti na jukumu ambalo utamaduni ulikuwa umemtengea. Mwamko huu mpya, unaungwa mkono na wanaufeministi ambao hunuia kumzindua mwanamke kimaendeleo kutokana na udunishaji wa kijadi. Kwa kufanya hivi, mwanamke amepewa nafasi sawa na mwanamume ndani ya jamii moja. Hili limewezekana kwa kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Kwa msingi huu, imelazimu methali hii kudenguliwa kimaana ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 61**

**Kinyankole:** *Omwana bamutinira obushaija bweishe*.
**Kiswahili:** Mtoto huogopwa kutokana na uume wa baba yake.

Kimukatdha, methali hii inakaribiana kimaana na ile ambayo imeishajadiliwa, kwa sababu mtoto kuogopwa katika jamii kulitegemea utajiri ambao baba yake alikuwa amezalisha kama familia. Kimaana, dhana "*Uume*" ilimaanisha sifa na utajiri wa mwanamume. Jinsia ya kike, hawakuruhusiwa kuwa na mali yoyote kwa sababu hao

pia walikuwa wanamilikiwa kama kitu chochote ndani ya familia. Kwa hivyo, jamii ilimtegemea mwanamume kuwa mwenye mali nyingi na wakusifika kuliko mwanamke. Hili limeonyesha kuwa mwanamke hakuwa na hana uwezo juu yake mwenyewe na vitu vilivyomzunguka. Madai haya yanatiliwa mkazo na Izugbara (2005) katika Kibigo (2019) ambaye anabainisha kuwa, kutokana na uume wake (dhakari), mwanaume husawiriwa kuwa na sifa kama vile uwezo, uvumilivu, ushujaa na ujasiri huku mwanamke akichorwa kuwa na sifa kama uoga, kutothubutu mambo na kadhalika. Kwa hivyo, itikadi na utamaduni katika jamii huegemea zaidi kuwajenga wanaume kuwa bora zaidi ya mwanamke.

Mawazo haya yanachukuana na yale ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zinawatweza wanawake kwa madai kuwa hawakuwa na nguvu kama wanaume kufanya kazi zao. Hii ina maana kwamba, mwanamke wa Kiafrika alikuwa amechorwa katika historia ya kutoweza kujifanyia lolote hata kumiliki mali ya umma. Katika muktadha wa kisasa, maana na matumizi ya methali hii imebadilika na kuathirika. Sababu kuu ni kwamba, mwanamke amepewa utawala na ushujaa wake, kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii akisaidiwa na Wanaufeministi wa Kiafrika. Kwa msingi huu, ni bora kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Kwa hivyo, imelazimu methali hii kudenguliwa ili maana, matumizi na muktadha vieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 62**

**Kinyankole:** *Meeme mememe tezaza mwojo.*
**Kiswahili**: Kubembeleza hakuishii kumzaa mtoto wa kiume.

Kimuktadha, jamii ya Wanyankole iliamua kutumia mfano wa mtoto wa kiume kuonyesha umuhimu wa wanaume katika kufanya kazi. Hii inawakumbusha wanaume kwamba, ni lazima wawajibike kuliko wanawake kikazi kama namna utamaduni

unavyoelekeza. Kutokana na mabadiliko mengi ndani ya jamii kama vile kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kidini na kindoa, jinsia zote zimeweza kujitokeza na kushirikiana kikazi tofauti na awamu ya kijadi. Jambo hili limelazimu methali hii kudenguliwa ili ieleweke kimaana na kimuktadha katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 63**

**Kinyankole:** *Eka effire nyineeka ayetondera abaana*.
**Kiswahili:** Boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto wake msamaha.

Kimuktadha, katika jamii ya Wanyankole, neno 'kufa' lilikuwa linaashiria kwamba nyumba hiyo ilikuwa haina uongozi wowote. Lilikuwa ni jambo la aibu sana mwanamume kushindwa majukumu yake na kuanza kuwaomba watoto wake msamaha. Hali hii ilionyesha kuwa mwanamume alikuwa ameshindwa na uongozi wa boma lake. Kwa hivyo, methali hii ilitumika kumuonya kutofika katika hali hii kama mwanamume. Hii inamaanisha kwamba, mwanamume alilazimika kufanya kazi zaidi kuwajibikia boma lake.

Ijapokuwa katika muktadha wa jadi mwanamume alikuwa anatazamwa kama chanzo cha familia kuporomoka, hali hii ni tofauti katika jamii ya kisasa. Hii ni kwa sababu mwanamke amepewa uhuru wa kujikomboa na kuweza kushirikiana na mwanamume katika kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali za jamii. Kwa hivyo, wakishindwa kushirikiana itakuwa si lawama kwa mtu mmoja. Aidha, wanaufeministi wamejitokeza kumuinua na kumzindua mwanamke katika maendeleo ya jamii. Hali hii, imeleta ushirikiano mzuri kati ya mwanamke na mwanamume ndani ya jamii kimaendeleo. Kwa hivyo, methali hii imeathirika kimaana na kimuktadha na kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kijadi na kisasa ya Wanyankole.

**Mf 64**

**Kinyankole:** *Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro.*
**Kiswahili:** Boma ambalo linaelekea kuharibika mwenye boma huamka na kuanza kula kiporo.

Kimuktadha, methali hii haitofautiani sana na hiyo ya mwanamume kuwaomba watoto wake msamaha. Katika methali hii, inaonyesha dalili za boma ambalo linataka kuharibika mwenye nyumba huamka na kuanza kula kiporo. Kwa hivyo, mwanamume hakustahili kufika kiwango hiki cha kula kiporo ikiwa alikuwa amejipanga vizuri kikazi. Aidha, ilikuwa ni jambo la aibu sana, mwanamke kumpatia mumewe kiporo katika jamii ya Wanyankole. Jambo hili lilichukuliwa kama njia moja ya kumdharau mwanamume. Hii ilimaanisha kwamba, jamii ilimtaka mwanamume kufanya kazi kwa bidii kuliko mwanamke. Katika muktadha wa kisasa, jinsia zote zimejiendeleza kimaisha jambo ambalo wanaufeministi huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa zimemnyima uhuru wake wa kujikomboa. Kwa hivyo, wanaufeministi wamejitokeza na kumsaidia mwanamke namna ya kujiendeleza kielimu, kiuchumi kisiasa, kidini, kindoa na kitamaduni. Hali hii imesababisha kuwapo kwa ushirikiano wa mwanamume na mwanamke katika kuleta maendeleo ndani ya jamii. Kwa msingi huu, methali hii ilihitaji kudenguliwa kimaana na kimuktadha ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 65**

**Kinyankole:** *Omwana oine ishe tayekorara enku.*
**Kiswahili:** Mtoto ambaye yuko na baba yake hastahili kubeba kuni.

Kimuktadha, katika jamii ya Wanyankole ilikuwa ni jambo la aibu kubwa, watoto ambao wako na baba kuanza kufanya kazi za rejareja ndani ya jamii kama vile kubebea watu kuni, kuwachotea maji na kulima kwenye mashamba ya wanajamii. Vipengele hivi vyote viliashiria baba alikuwa ameshindwa majukumu yake. Kwa hivyo, methali hii ilitungwa kumkumbusha mwanamume kufanya kazi kwa bidii ili familia yake

iepukane na kazi za aibu. Katika jamii ya kisasa, tunaona muktadha unaathiri maana ya methali hii kwa sababu mwamko mpya ndani ya jamii umeruhusu jinsia zote kufanya kazi sawa jambo ambalo lilikuwa ni mwiko. Kwa hiyo, kutokana na ubadilikaji wa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kitamaduni na kidini, hakuna wa kulaumiwa kuhusu umaskini nyumbani. Ingawa mwanamume amesaidiwa na mwanamke, jamii ingali inamtarajia kufanya kazi kwa bidii kuliko mwanamke. Hali hii imelazimu methali hii kudenguliwa ili maana ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 66**

**Kinyankole:** *Nyineeka atutuka narya obuhoro.*
**Kiswahili:** Mwenye boma anakula kiporo akitoka jasho.

Methali hii kimuktadha imeweka wazi namna utamaduni ulivyokuwa umemtengea mwanamume kazi tofauti na mwanamke. Kutokana na kazi hizi, mwanamume alipaswa kufanya kazi kwa bidii kuliko mwanamke. Hili lilitokana na sifa alizopewa za kuwa shujaa, kiongozi na mwenye mamlaka yote. Aidha, ni kutokana na kufanya kazi hizi ngumu ndipo familia yake ingeishi vizuri. Kwa hivyo, kwenda kinyume na hayo, tunamwona anatoka jasho akiwa anakula kiporo, hii ikiashiria kwamba alikuwa ameshindwa na majukumu yake. Katika jamii ya Wanyankole, ilikuwa ni jambo la aibu mwanamume kula kiporo. Hali hii inachunguzwa na Wanaufeministi wa Kiafrika, ambao huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimewatweza na kuwapatia wanaume mamlaka na utawala wa ushujaa. Kwa hivyo, mwanamume kushindwa majukumu yake, alikuwa ameenda kinyume na matarajio ya jamii yake. Katika jamii ya kisasa, methali hii imepingwa kwa madai kwamba, jamii imepiga hatua kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kidini na kitamaduni, na hivyo jinsia zote zimepata fursa sawa ndani ya jamii tofauti na kijadi. Kwa msingi huu, imelazimu ushirikiano uwepo kati ya jinsia hizi mbili katika kuwajibikia familia zao. Kutokana na mitazamo hii tofauti, tumetambua kuwa muktadha wa methali hii umeathirika kimaana

na kimatumizi na hivyo kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

### 5.2.2 Methali za jinsia ya kike kikazi

Katika kundi hili, tumejadili methali tatu za kijinsia tofauti na kundi la awali lililowahusu wanaume. Hii imeonyesha kuwa kijadi, wanawake hawakutiliwa mkazo sana katika kufanya kazi kwa sababu kitamaduni walichukuliwa kuwa jinsia dhaifu iliyohitaji mwanamume kuisaidia. Kutokana na dai hili, wanaufeministi wanashikilia kuwa wanawake katika jamii nyingi za Kiafrika walikuwa wanapewa kazi hasi ukilinganisha na zile za wanaume. Jambo hili lilichochea kuchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika zilizowanyanyasa na kuwanyima haki zao kwa madai kwamba walikuwa viumbe duni. Ni kutokana na uchunguzi huu tunaona mwanamke anapewa mwamko mpya wa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini ndani ya jamii moja na mwanamume. Maelezo hayo yanajidhihirisha katika methali zifuatazo:

**Mf 67**

**Kinyankole:** *Obwenda kusimwa omukazi akasa oburo ahekire Iba.*
**Kiswahili:** Mwanamke kupenda kushukuriwa alisaga wimbi akimbeba mumewe mgongoni.

Kimuktadha, katika utamaduni wa jamii ya Wanyankole kijadi, wanawake walikuwa wametengewa kazi zao tofauti na za wanaume kama vile kupika, kulima, kuzaa na kulea, kufanya mapenzi na mwanamume na kudumisha usafi nyumbani. Katika jamii ya Wanyankole, wanaume walikuwa wanaruhusiwa kuwaoa wanawake wengi, jambo ambalo lilisababisha kuwapo ushindani ndani ya ndoa, kwa sababu kila mwanamke alikuwa anatafuta njia ya kumfurahisha mwanamume. Kutokana na hali hii, tunamwona mwanamke anaamua kumbeba mumewe mgongoni akisaga wimbi ili aweze kuambiwa asante. Hii ilichukuliwa kama njia mojawapo ya mwanamke

kumwonyesha mumewe kuwa alikuwa anampenda, na kwa upande mwingine ilikuwa ni njia moja ya mwanamke kulinda ndoa yake asipewe talaka. Hali hii ilikuwa ni ya kitumwa kama asemavyo Denoon (1971) kuwa, mwanamke alikuwa na jukumu la kumtunza mumewe, watoto na kupika. Pia, alikuwa na jukumu la kulima na kupanda vyakula vya kutosha kwa ajili ya familia nzima. Alipanda vyakula kama mtama, maharagwe, mahindi, viazi na mihogo. Kwa msingi huu, kazi za wanawake zilikuwa za hadhi ya chini ukizilinganisha na zile za wanaume. Mgawanyo huu wa kazi kijinsia, unaungwa mkono na wanaufeministi ambao huchunguza hali za wanamke katika jamii zao zilizokuwa na harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya.

Katika jamii ya kijadi, wanawake waliishi katika hali ya ufungwa ambayo ilikuwa imesababishwa na miundo ya jamii pamoja na utamaduni ambao hawakuweza kujikomboa. Kwa mfano, mwanamke kufanya kazi nyingi huku akiwa na kazi ya kumbeba mumewe mgongoni pia. Katika jamii ya kisasa, mwanamke amepewa uwezo sawa na mwanamume kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini ndani ya jamii. Jambo hili limesababisha methali hii kuathirika kimaana kutokana na miktadha hii miwili katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole. Mwamko huu umempatia mwanamke uwezo wa kujichagulia mchumba na kufanya kazi za kihadhi tofauti na zamani. Kwa msingi huu, hizi ndizo baadhi ya harakati za kujikomboa na kujenga jamii mpya ambazo wanaufeministi wamekuwa wanapigania wanawake wapewe. Kutokana na madai haya, methali hii imeathirika kimaana na kimuktadha na kusababisha udenguzi kufanyika ili methali hii ieleweke katika jamii hizi mbili za Wanyankole.

**Mf 68**

**Kinyankole:** *Omukazi ne myenda, Omushaija nemirimo.*
**Kiswahili:** Mwanamke ni nguo mwanamume ni kazi.

Katika muktadha wa kijadi, methali hii imeendelea kumdunisha mwanamke katika jamii hii kwa kuonyeshwa namna alivyo pambo tofauti na mwanamume ambaye alitambulika kutokana na kazi alizozifanya. Hii ina maana kwamba, katika jamii ya Wanyankole, mwanamke alikuwa anamtegemea mwanamume kwa kila jambo ikiwemo kimavazi. Aidha, mwanamume alisifika kutokana na namna alivomvalisha mkewe. Kwa hivyo, kazi kuu ya mwanamume ilikuwa kuhakikisha mwanamke alikuwa pambo kimavazi ikiwa yeye ndiye amewajibika. Aidha, mwanamke alikuwa hana uwezo wa kufanya kazi yoyote na kujinunulia mavazi kutokana na utamaduni huu. Hata hivyo, katika muktadha wa leo, mambo ni tofauti, mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume. Fursa hii imeungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo hunuia kumzindua mwanamke kutokana na unyanyasaji wa kijadi na kumpatia uhuru wake.

Hali hii imemsaidia mwanamke kujikomboa na kujinunulia kila kitu kwa hiari yake tofauti na mtazamo wa kijadi. Aidha, hali hii imemsaidia pia kupata uwezo wa kushirikiana na watu wengine katika masuala nyeti ya jamii. Kwa hivyo, methali hii imeathirika kimuktadha na kimaana katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na kusababisha udenguzi ili ieleweke kwa jamii hizi.

Mohammed (2006) anaeleza kuwa, kimaksudi msomaji wa matini fulani anaweza kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana. Kwa sababu maana ya mwanamke kuwa ‘nguo’ na mwanamume kuwa ‘kazi’ ina maana fiche ambayo kina babu walikuwa wanakusudia katika ndoa. Kwa mfano, walikuwa wanamkumbusha mwanamume kuwa, mwanamke kuonekana vizuri ilikuwa ni kazi yake kama kiongozi. Mwanamke naye alikuwa na kazi ya kumtii mumewe na kumfurahisha kwa kila njia ili anunuliwe mavazi apendeze. Kutokana na utamaduni huu, methali hii ilikuwa ni sawa, kwa sababu ndio namna miundo ya jamii ilikuwa imejengeka tofauti na sasa. Kwa hiyo, siyo ukweli

kusema mwanamke alikuwa ameonewa. Hata katika jamii ya kisasa, mwanamume angali na uwezo wa kumnunulia mwanamke nguo ingawa jamii imepiga hatua ya kimaendeleo. Kwa upande mwingine, naye mwanamke anaweza kumnunulia mumewe nguo. Hapa ndipo Mohammed (keshatajwa) anaonya kuhusu kupoteza maana kamili ya methali, ikiwa msomaji hatakuwa na umakini wa kufasiri methali hiyo au mazoea ya utamaduni husika. Kwa msingi huu, methali hii ililazimu kudenguliwa ili ieleweke kimaana katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 69**

**Kinyankole:** *Omukazi ahinga hamwe na Iba taba mugara.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye analima na mumewe si mvivu.

Katika utamaduni wa Wanyankole, mwanamke mvivu hakukubalika tofauti na mwanamume. Kimuktadha, jamii ilitaka mwanamume kuoa mwanamke kutoka katika familia iliyokuwa na bidii katika kila shughuli. Sababu kuu ya kufanya hivi, ilikuwa mwanamke huyo alikuwa wa muhimu katika kuleta maendeleo katika boma lake. Iliaminika kuwa, wanaume wote walikuwa na bidii katika kazi na mwanamke ndiye angemfilisi. Kwa hiyo, kuweza kuthibitisha hili, walimfanya mwanamke kulima na mumewe ili kuona nguvu na bidii zake. Ingawa hiki kilikuwa ni kigezo kikuu wakati wa kijadi, siku hizi wanawake wamejitokeza na kufanya kazi sawa na wanaume na hata kuwashinda. Katika muktadha wa kisasa, jinsia zote zinafanya kazi sawa tofauti na wakati wa kijadi.  Utofauti huu wa mambo, ndio Wanaufeministi wa Kiafrika wanachangamkia kwani wamekuwa wananuia kumwinua mwanamke kikazi na kumpatia ukombozi wake. Kwa hivyo, methali hii imepata kuathirika, kimaana na kimuktadha na kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

### 5.3 Maana ya Methali za Kijinsia Kiuongozi

Jamii ya Wanyankole tangu kijadi, imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni. Hii ina maana kwamba, kazi zote zikiwemo za uongozi zilikuwa za jinsia ya kiume tofauti na za kike. Aidha, katika muktadha wa ndoa, ni mwanamume ndiye aliyekuwa anahusika na masuala nyeti ya jamii tofauti na mwanamke aliyehusika na mambo ya kinyumbani.

Tumusiime (1982) anasema, mwanamume alikuwa anastahili kuongoza familia yake na vyote vilivyomo; mwanamke akiwa mojawapo ya vitu vilivyomilikiwa. Kwa madai haya, unaweza kutambua ni kwa sababu gani methali hizi za uongozi zilitungwa na kuendelezwa kwa njia ya ubabe-dume ndani ya jamii hii. Maoni haya ya Tumusiime yanaendana na yale ya Nadharia ya Ufeministi ambayo huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa ni chanzo cha kumdunisha mwanamke na kumnyima utawala wake. Hii inamaanisha kwamba, mwanamke alikuwa na nafasi duni ndani ya jamii tofauti na mwanamume. Ni kutokana na madai kama haya, tunamwona mwanamke katika jamii ya kisasa amejitokeza na kupigania haki zake kama vile za kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini. Jambo hili limeathiri muktadha na maana ya methali hizi katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole kwa Mtazamo wa Kipragmatiki.

#### 5.3.1 Methali za jinsia ya kiume kiuongozi

Kundi hili limeshughulikia methali tatu za kijinsia zilizohusu wanaume katika jamii ya Wanyankole. Methali hizi zilisaidia kutoa muktadha, maana na matumizi yake. Pia, katika jamii ya Wanyankole kijadi, mwanamume alikuwa amepewa kipaumbele cha uhakimu kwa madai kuwa mwanamke hakuweza jukumu hilo. Hali hii inaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika, ambao huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa zimemtweza katika kila hali tofauti na mwanamume. Hali hizi

tofauti, zimeweza kujitokeza kwa kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum ndani ya jamii.

**Mf 70**

**Kinyankole**: *Omushaija tahinduka omubigambo ahinduka aha kitandi honka.*
**Kiswahili:** Mwanamume hageuki kwenye usemi ila hugeuka kitandani tu.

Katika utamaduni wa Wanyankole kijadi, mwanamume alistahili kuwa kiongozi na hakimu mzuri kuliko mwanamke. Kimuktadha wa kijadi, mwanamume hakustahili kugeuza usemi wake baada ya kutoa hukumu kwa mtu yeyote, kwani hii ilikuwa ishara ya kuonyesha ubobezi katika uongozi wake. Kando na kuwa hakimu mzuri, mwanamume aliweza kusikiliza na kugeuza msimamo wake kuhusu suala la ndoa akiwa na mkewe kitandani tu. Hili lilitokana na kuwa, mwanamume aliyekuwa hana watoto na mno mrithi, alidharauliwa na hakuweza kuwa kiongozi. Kutokana na aibu hii, ilimlazimu kunyenyekea kidogo tofauti na mazoea yake. Shughuli ya kuendeleza kizazi ilikuwa muhimu sana na iliwahusu wazazi wote kushirikiana. Lakini katika muktadha wa kisasa, jinsia zote zimejiendeleza kimaisha na kupewa nafasi sawa ndani ya jamii. Jambo hili limesaidia jinsia zote kushirikiana kuhusu masuala nyeti ya kijamii, ikiwemo mwanamke kugombea nyadhifa tofauti ndani ya jamii, na hata uhakimu ukiwemo. Fursa hii imesaidia kuchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimemdunisha mwanamke na kumnyima utawala wake. Ni kutokana na madai haya, imelazimu methali hii kudenguliwa kwa sababu muktadha umeathiri maana yake katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 71**

**Kinyankole**: *Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja.*
**Kiswahili:** Panapokuwa hakuna wanaume wanawake hutoa hukumu.

Kimuktadha kijadi katika jamii ya Wanyankole, ilikuwa ni jambo la aibu wanawake kutoa hukumu huku wanaume wameketi. Vilevile, kitamaduni ilikuwa ni mwiko mwanamke kufanya kazi hii, kwa sababu ilikuwa ni ishara mwanamume alikuwa ameshindwa. Aidha, Maingi (2005) anadai kuwa mwanaume ndiye aliyeshirikishwa katika utoaaji wa maamuzi muhimu katika jamii huku mwanamke akiwekwa pembeni. Maingi (keshatajwa) anaendelea kudai kuwa mwanamke anasifiwa katika jamii kutokana na mchango wake wa kulea watoto nyumbani pekee. Kwa hiyo, jamii ilikuwa inamwonya mwanamume kutozembea katika majukumu yake. Wanawake kupewa ruhusa ya kutoa hukumu ilikuwa ni ishara kwamba, walikuwa na uwezo sawa na wanaume ila walinyimwa fursa hiyo kutokana na utamaduni. Kutokana na uwezekano huo, wanaufeministi wamezingatia kuwepo kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Wamefanya hivi kwa kuchunguza namna wanavyoweza kumuinua  na kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake kwa kumpatia uhuru wake. Kutokana na madai haya, mwanamke wa kisasa ameweza kujiendeleza kimasomo, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kindoa na kidini na kuonyesha ushirikiano mzuri na uhusiano wake na watu wengine ndani ya jamii tofauti na mtazamo wa kijadi.

Kutokana na mwamko huu mpya ndani ya jamii, wanaudenguzi wamesaidia kutoa maarifa zaidi kuhusu usomaji wa matini. Kwa mfano wanasema, udenguzi ni uhakiki unaojikita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Katika methali hii, *"Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja"* tafsiri yake "Panapokuwa hakuna wanaume wanawake hutoa hukumu." Hii imeonyesha kuwa, katika jamii ya kijadi kulikuwapo uwezekano wa wanawake kuwa mahakimu wazuri kimaana na kimuktadha, ijapokuwa tu hawakupewa fursa kutokana na ubabe–dume uliokuwa unaendeshwa katika jamii

hii. Aidha, katika jamii ya kisasa, mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume tukirejelea methali hii. Hili limedhihirisha kuwa methali hii imeweza kujitosheleza na kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha mmoja. Kwa hivyo, methali hii imeathirika kimaana kutokana na miktadha tofauti ndani ya jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na kusababisha udenguzi.

**Mf 72**

**Kinyankole:** *Omukazi aba orubaju rwomushaija.*
**Kiswahili:** Mwanamke huwa ubavu wa mwanamume.

Kimuktadha wa kijadi, methali hii imeweka wazi kuwa mwanamke alikuwa ametoka ubavuni wa mwanamume kutokana na Biblia. Hii inamaanisha, mwanamke alistahili kunyenyekea katika kila jambo ili asimuudhi mumewe kwa sababu alikuwa anamwakilisha Mungu. Imani hii ilimfanya mwanamke kubaki nyuma katika maendeleo yote ya jamii uongozi ukiwemo. Matembe (2009) anasisitiza kwamba katika familia nyingi ambapo wanaume hunyanyasa wanawake, wanawake hao wakiwaendea viongozi wa dini kwa msaada, huwa wanawakumbusha maneno ya Paulo mtakatifu kwamba wake wajitolee kwa waume kwani ndio viongozi wa familia. Hii ni kwa sababu walitolewa katika ubavu wa mwanamume, kwa maana wao ni sehemu ndogo sana ya mwanamume. Kwa hiyo sharti wamtii na kumnyenyekea mara zote. Anawavamia viongozi wa dini ambao wanaendeleza itikadi kama hizi akisema kwamba hakuna ilipoandikwa katika Bibilia kwamba mwanamume amnyanyase mwanamke. Kwa hali yoyote mwanamume anastahili kumpenda mwanamke kwa kuwa Mungu alipoona kuwa mwanamume hawezi chochote bila wa kumsaidia, akaumba mwanamke ili mwanamume apate mwelekeo. Matembe anawashauri wanaume ambao wako kama Adam ambaye hakuwajibika, akaacha mkewe kushawishiwa na Shetani eti wasipojihadhari, familia zao zitaendelea kuporomoka. Hata hivyo Wanaufeministi wa Kiafrika, wanamuunga mkono Matembe katika jamii ya kisasa kwa kuchunguza

historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zinamnyima uhuru wake kwa msingi wa dini.

Ni kutokana na hali na imani hii ndizo zilizomtweza mwanamke na kumfanya mtumwa. Kwa hivyo, Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitoa mhanga katika jamii ya kisasa, na kumpatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika uchumi, siasa, elimu, utamaduni, ndoa na dini. Jambo hili limeweza kumpatia mwanamke utawala na ushujaa wake alioupoteza wakati wa kijadi. Hili limewezekana kwa sababu wanaume na wanawake wameweza kushirikiana katika kujenga jamii mpya tofauti na mtazamo wa kijadi. Isitoshe mtalaam El- Maawy (2011) amechunguza mausio ya mwanamke wa kisasa na wasiya wa Mwanakupona na kutambua kuwa, ulimwengu umepitia mabadiliko mengi na kuathiri wasiya huu na bila shaka hakuna namna jamii ya Wanyankole ingekosa kuathirika kutokana na mwamko huu mpya ndani ya jamii ya kisasa. Kwa hiyo, methali hii iliathirika kimuktadha na kimaana na kulazimu idenguliwe ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

Aidha, Rorty (1996) anabainisha kuwa udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza, huonekana kama ni usaliti, ijapokuwa utokeaji wa ukiushi huu si ajali bali hukusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Methali hii inapotazamwa kwa mara ya kwanza, inadhihirisha usaliti kwa jinsia ya kike. Usaliti huu unatokana na madai kuwa mwanamke alikuwa ametoka ubavuni mwa mwanamume, na daima ni mwanamume ndiye aliyestahili kumwajibikia. Hata hivyo, Rorty anasema huo si usaliti, isipokuwa ni njia mojawapo ya kumfanya mwanamke kutambua mwanamume alikuwa kiongozi na alifaa kuheshimiwa hata katika jamii ya kisasa. Kwa hivyo, ni bora jinsia zote kushirikiana katika maendeleo ya jamii tofauti na mtazamo wa kijadi, wakati huo mwanamke abaki akijua mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba. Utofauti huu wa mawazo umefanya methali hii kuathirika

kimuktadha na kimaana na hivyo kulazimisha kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

### 5.3.2 Methali za jinsia ya kike kiuongozi

Katika kundi hili, ni methali moja tu ndiyo ambayo imejitokeza. Hii imeweka wazi kwa nini jamii ya Wanyankole ya kijadi haikuweza kuwaruhusu wanawake kuwa viongozi. Hali hii inaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa zimemtweza mwanamke na kumnyima fursa sawa ya kujiendeleza kama ilivyo kwa mwanamume. Kwa hivyo, wanaufeministi wameamua kumsaidia mwanamke kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii kwa kuona namna anavyopata ukombozi wake. Hali hii imemlazimu kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole katika nyanja maalum za jamii, na kudengua methali hii ili kuelewa maana yake katika jamii hizi mbili za Wanyankole.

**Mf 73**

> **Kinyankole**: *Omukazi akanyampira obwato bya ishezaara ati munda yamawe tuzira emitahe.*
> **Kiswahili:** Mwanamke alijambia mtumbwi wa baba mkwe kisha akasema kwetu ni mwiko kunywa pombe.

Katika jamii ya Wanyankole kijadi, kimuktadha wanawake hawakuruhusiwa kufika karibu na mtumbwi wa pombe, au sehemu yoyote ambayo wanaume walikuwa wanakusanyikia. Madai haya yalihusu kuwa ni sehemu muhimu, ambayo ilikuwa inatumiwa kujadili masuala nyeti ya jamii. Kwa hivyo, wanawake hawakuruhusiwa kukaribia sehemu hiyo, kwani walikuwa hawana chochote cha kusema. Aidha, tunamwona mwanamke anajambia mtumbwi wa baba mkwe, na kudanganya kwamba ni mwiko kwao kunywa pombe. Mwanamke kufanya kitendo kama hiki, kilionyesha kuchoka kwake kutokana na kunyimwa fursa ya kujihusisha na masuala nyeti ya jamii. Ni kutokana na hali hii ambapo Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitokeza katika jamii

ya kisasa na kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake. Hili limewezekana kwa kumshirikisha mwanamke kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kitamaduni na kidini ndani ya jamii moja na mwanamume. Jambo hili limemzindua mwanamke katika karne hii ya 21 tofauti na mtazamo wa kijadi. Katika kuelewa hali hii, imelazimu methali hizi kutathiminiwa kikamilifu kijinsia katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa miongoni mwa Wanyankole.

### 5.4 Maana na Matumizi ya Methali za Kijinsia Kitamaduni

Jamii ya Wanyankole ni mojawapo ya jamii nyingi ulimwenguni ambazo zimeweza kuhifadhi mila, desturi na imani zake kupitia utamaduni wa jamii yake. Ni jamii ambayo imetumia fasihi simulizi katika kuelimisha, kuburudisha na kuonya wanajamii wake. Vilevile, jamii hii imeonyesha namna inavyoendeleza kazi zake kwenye mfumo wa kuumeni. Jamii ya Wanyankole ilichukulia suala la ndoa na utamaduni kuwa nguzo kuu katika kuwapo kwake. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa mwanamke kunyanyaswa ndani ya jamii. Wanaufeministi wamesaidia kuchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo ziliwanyima utawala na ushujaa wao. Kufanikisha hili, kumelazimu kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole. Hili litawezesha kuelewa namna ndoa na utamaduni vilivyochangia katika kumkweza mwanamke kupitia historia ya jamii.

#### 5.4.1 Methali za jinsia ya kike kitamaduni

Kundi hili limeweka wazi methali za kijinsia kijadi zilizowahusu wanawake tofauti na wanaume. Pia, katika kundi hili, wanawake ndio waliokuwa wamekwezwa mno na suala la utamaduni kuliko wanaume. Madai haya yanaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao wanakubaliana na suala la utamaduni kuwa chanzo cha jamii nyingi za Kiafrika kumdunisha mwanamke. Kwa hivyo, wamejaribu kwa kila njia kumwinua mwanamke kutokana na hali hiyo. Hili limeweza kufikiwa katika

kumshirikisha mwanamke kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kielimu, kindoa na kidini katika jamii ya kisasa sawa na mwanamume tofauti na mtazamo wa kijadi. Utofauti huu wa mambo, umeathiri miktadha na maana ya methali hizi katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na kulazimu udenguzi ufanyike.

**Mf 74**

**Kinyankole:** *Omukazi oine Iba tarya nkoko.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye ana mume hali nyama ya kuku.

Kimuktadha, mwanamke katika jamii ya Wanyankole kijadi, kitamaduni hakustahili kula baadhi ya vyakula kwa sababu ilikuwa ni mwiko. Kwa mfano, wanawake hawakustahili kula nyama ya kuku na ile ya mbuzi, kwa madai kwamba, iwapo wangekula nyama ya mbuzi wangemea pembe na kidevu. Kutokana na dai hili, wanawake waliamua kupikia waume zao nyama bila wao kula. Sababu nyingine ni kuwa, wanaume walistahili kula vizuri zaidi kutokana na kazi ngumu walizokuwa wanazifanya ndani ya jamii tofauti na kazi za wanawake. Katika muktadha wa kisasa, wanawake wamejiendeleza na kula vyakula vyote kwa hiari yao tofauti na mtazamo wa kale. Mwamko huu mpya kuhusu wanawake, umechangiwa na Nadharia ya Ufeministi ambayo huchunguza hali za mwanamke katika jamii zao zilizokuwa zinamtweza katika daraja zote za maisha. Hali hizi zinajitokeza kwa kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole katika nyanja maalum za jamii. Kwa hivyo, kutokana na muktadha wa methali hii, maana imepata kuathirika na kulazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 75**

**Kinyankole**: *Omufukazi tagaya mboro.*
**Kiswahili:** Mjane hadharau mboro.

Mwanamke katika jamii ya Wanyankole kijadi, kimuktadha alikuwa anarithiwa kama vitu vingine vyovyote ndani ya nyumba. Mumewe alipoaga dunia, ni kaka yake mdogo ndiye aliyepaswa kumrithi. Mjane huyu hakuwa na hiari kupinga uamuzi wa

utamaduni. Kutokana na hali hii, ndiyo sababu methali hii kutungwa kumwonya mwanamke kuhusu kurithiwa. Aidha, kuna uwezekano ilikuwa ni njia mojawapo ya kuleta maadili ndani ya jamii, kwa kujaribu kuepukana na suala la ukahaba la wajane ambao walikuwa wamefiwa na waume zao. Vilevile, hii ilifanyika ili kuepukana na suala la mama wa kambo kuolewa na kutesa watoto ndani ya boma.

Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitokeza kumuinua na kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake kwa kumpatia usawa na mwanamume katika nyadhifa tofauti ndani ya jamii. Hili limewezekana kwa kumshirikisha kiuchumi, kisiasa, kielimu, na kitamaduni sawa na mwanamume. Fursa sawa katika jamii, imemwezesha mwanamke kujichagulia mchumba wa hiari yake, na vilevile mashirika ya taifa na kimataifa yamejitokeza na kumtetea mwanamke. Mashirika haya ni kama vile HCT (HIV Counseling and Testing), WHO (World Health Organisation), VCT (Voluntary Counseling and Testing), UHSBS (Uganda HIV/AIDS SERO-Behavioural Survey), AMREF (African Medical and Research Foundation), AIC (Aids information Centre), TACAIDS (Tanzania Commission for Aids), TASO (The Aids Support Organisation), HBHCT (Home-based HIV Counseling and Testing). Mashirika haya yamehakikisha mambo ya kurithiwa hayapo tena kwa sababu yalikuwa yanaenda kinyume na haki za binadamu.

Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO, 2021) unyanyasaji wa wanawake katika ndoa huwaathiri vibaya sana. Shirika hili linaeleza kwamba 30% ya wanawake duniani wamekabiliwa na unyanyasaji katika mahusiano ya ndoa. Unyanyasaji huu unachochewa na mambo kama vile kiwango cha chini cha elimu, malezi yaliyoshuhudia unyanyasaji, matumizi ya vileo, kutokuwa na ajira /mshahara na kutohamasishwa juu ya uhuru na usawa kijinsia. Ni kwa msingi huu ndipo

tunapendekeza kudenguliwa kwa methali katika Mf 76 ili iafikiane na mahitaji ya jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 76**

**Kinyankole:** *Omukazi oraite eka asiga yacuriza.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye ataharibu boma lake hupiga mbinja.

Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, mwanamke hakustahili kupiga mbinja. Upigaji mbinja ilikuwa ni kazi ya wanaume iliyotumiwa kuashiria shughuli nyingi ndani ya jamii kama vile kuwinda, ufugaji, kuwasiliana, kuburudisha na hata kuhatarisha wanajamii. Hii inamaana kwamba, kila mbinja ilikuwa inaashiria kitu fulani ndani ya jamii. Kwa hivyo, mwanamke kupiga mbinja, ilikuwa ni ishara ya kukosa maadili. Kuna uwezekano mwanamke kutumia mbinja alikuwa anajaribu kupitisha ujumbe fulani kwa jamii kwa sababu kitamaduni hakuruhusiwa kuongea bila ruhusa ya mumewe. Kutokana na kunyimwa haki yake ya kujieleza, alijaribu kutafuta mbinu zozote zile ili asikilizwe. Tunaona Wanaufeministi wa Kiafrika wanavyochunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimemnyima utawala na ushujaa wake. Kutokana na hali hii,, imelazimu kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, methali hii haina mashiko makubwa kwa sababu mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume katika kujieleza kupitia kwa njia ya uchumi, elimu, siasa, dini, utamaduni na ndoa. Huu ndio mwamko mpya ambao wanaufeministi wanataka kila mwanamke apate ili kubadili mtazamo wa kijadi. Kwa msingi huu, methali hii imepata kuathirika kimuktadha na kimaana na kulazimu kudenguliwa.

**Mf 77**

**Kinyankole:** *Abana bahwa omumukazi tibahwa mumushaija.*
**Kiswahili:** Watoto huisha ndani ya mwanamke lakini si kwa mwanamume.

Katika jamii ya Wanyankole kijadi mwanamume alikuwa na suala nyeti la kuendeleza kizazi. Hata hivyo, utamaduni ulimruhusu mwanamume kuoa wanawake wengi kwa sababu kwanza, alikuwa na uwezo wa kuendelea kuzaa hadi uzeeni tofauti na mwanamke ambaye angefika umri fulani asiweze kuendelea kuzaa tena. Pili, kutokana na mali nyingi ambazo wanaume walikuwa nazo, iliwabidi kuzaa watoto wengi ili kuzirithi. Ilikuwa ni vigumu mwanamke kuzaa watoto zaidi ya kumi na watano kabla kizazi hakijaisha. Kwa hivyo, mwanamke alikuwa anaonywa kutolalamika mumewe alipoendelea kuoa wanawake wengi. Katika muktadha wa kisasa, mwanamke amepewa uwezo wa kujiamlia kumhusu mchumba amtakaye, na vilevile idadi ya watoto wa kuzaa. Jambo hili limetokana na usawa ndani ya jamii hii. Mwamko huu mpya ndio Wanaufeministi wa Kiafrika wanauchangamkia kwa kujaribu kumuinua na kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Katika harakati za kumzindua mwanamke, imelazimu kutathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Mitazamo hii tofauti imesababisha udenguzi kufanyika, ili methali hii ieleweke katika jamii ya kisasa na ile ya kijadi ya Wanyankole.

**Mf 78**

**Kinyankole:** *Ozara Omwojo tacwa ruganda.*
**Kiswahili:** Anayemzaa mtoto wa kiume hakomeshi ukoo.

Tumegundua kijadi katika jamii ya Wanyankole, kitamaduni mtoto wa kiume alienziwa mno kuliko wa kike. Ina maaa kwamba, mtoto wa kike aliendeleza ukoo wa mumewe huku wa kiume aliendeleza ukoo wa baba yake. Kwa hivyo, manufaa ya mtoto wa kiume yalikuwa ya hadhi ya juu kuliko yale ya mtoto wa kike. Mwanamke alipoolewa alikuwa anaambiwa methali hii, kukumbushwa ni lazima kumzaa mtoto wa kiume kwa sababu ya kuendeleza ukoo wa mumewe. Aidha, methali hii katika muktadha wa kisasa imepata kubadilika kutokana na mabadiliko mengi ndani ya jamii. Mwanamke

ameweza kujimudu kimaisha, na kuzaa watoto wa jinsia yoyote bila kulazimishwa kuhusu jinsia ya kiume. Tofauti na mtazamo wa kijadi, watoto wote wamepewa fursa sawa ndani ya jamii, jambo ambalo limewafanya wazazi kutambua mtoto wa kike ana manufaa hata kumzidi wa kiume. Madai haya yanaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zinamdunisha mwanamke na kumpatia mwanamume mamlaka yote.

Katika kuchunguza historia hizo, mwanamke amejitokeza na kushirikiana na mwanamume katika kuleta maendeleo ndani ya jamii moja. Hata hivyo, ingawa mwanamke amepewa uhuru wake, mtoto wa kiume angali anatambuliwa kuhusu suala la kuendeleza ukoo wa baba yake kando na kuleta maendeleo ndani ya jamii. Ili kuthibitisha hili, imelazimu kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole, ili kuona namna historia ilivyomwathiri mwanamke na hatimaye kulazimu methali hii kudenguliwa.

Derrida (1981), anahatarisha kupoteza maana kamili katika jamii ya kisasa kuhusu methali hii. Anasema kuwa, udenguzi au ubomozi unahusishwa na usomaji wa kila neno katika matini kwa jicho pekevu. Kwa mfano, tunapotazama hili neno *‘tacweka’* linamaanisha ‘hawezi kukatika’ lakini unaporejelea muktadha na maana ya kijadi, linazungumzia kuendeleza ukoo. Kwa hivyo, mwanajamii wa kisasa inambidi kuelewa muktadha liliyotumika, na maana iliyorejelewa katika kipindi hicho pasipo hivyo, atapotoka. Ili kuepukana na hili, ni lazima methali hii idenguliwe ili maana ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 79**

**Kinyankole:** *Omukazi akaferwa Iba ati zambona.*
**Kiswahili:** Mwanamke alifiwa mumewe akasema zimenikuta.

Kitamaduni, mwanamke alikuwa hastahili kuwajibikia familia yake. Hii ina maana kwamba, katika muktadha wa kijadi ilikuwa ni jukumu la mwanamume kuwajibikia familia. Kwa hivyo, kutokana na kutojua kazi za mumewe, kulimfanya mwanamke kupata shida namna ambavyo angeweza kuendeleza familia yake pasipo mwanamume. Hivyo basi, utamaduni ulimnyima uwezo wa kujihusisha na baadhi ya kazi ambazo zingemsaidia kujimudu kimaisha. Kutokana na hali hii, tunaona Nadharia ya Ufeministi kinachunguza hali duni ambazo mwanamke alipitia wakati wa jadi, na kuona namna anavyoweza kumsaidia mwanamke katika jamii ya kisasa kujikomboa.

Ili kujenga jamii mpya, mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume katika jamii ya kisasa kama kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kidini na kindoa. Fursa hii imemwezesha kujikomboa na kushirikiana na mwanamume katika kuleta maendeleo ndani ya jamii kinyume na kijadi. Kwa hiyo, utofauti huu wa mawazo, umeweza kuathiri muktadha na maana ya methali hii na kulazimisha udenguzi kufanyika ili maana ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

### 5.4.2 Methali za jinsia ya kiume kitamaduni

Katika muktadha huu, tumejadili methali mbili ambazo zilihusu wanaume kitamaduni katika jamii ya Wanyankole. Tofauti na jinsia ya kike, imetambulika kijadi kuwa wanaume walikuwa hawatwezwi mno na utamaduni kama wanawake. Hili linathibitisha kuwa ni wanaume ndio ambao walikuwa wametunga methali hizi kutokana na mfumo wa kuumeni ulioendelezwa na ubabe-dume. Kutokana na hali hii, walijitenga na utamaduni na kuonyesha kwamba, ni mwanamke aliyekuwa anastahili kuheshimu utamaduni pekee yake. Madai haya yanatiliwa mkazo na Wells & Holland (2001) wanaposema, Itikadi za kijamii huongoza fikra kwamba, utawala wa mwanaume umehahalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulisho vya jinsia ya kiume kimaandishi, kimatukio na kimaelezo ya kihistoria

kwa misingi ya jamii husika. Hali hii inaungwa mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika. Aidha, katika kuchunguza historia hiyo iliyomtweza mwanamke, ni lazima kuwapo mwamko mpya ndani ya jamii kama vile: kitamaduni, kielimu, kiuchumi, kisiasa, kindoa na kidini. Pia, lazima mwanamke apate fursa sawa na mwanamume katika nyadhifa zote tofauti ndani ya jamii. Msimamo huu wa wanaufeministi, umesaidia kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 80**

> **Kinyankole:** *Empisi ekagira eti, kumbugana omushaija ashendekyerize ondijo nteraa mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheeka nkaba.*
>
> **Kiswahili:** Fisi alisema kwamba akimkuta mwanamume akimsindikiza mwanamume mwenzake hujificha lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu.

Methali hii ilidhihirisha kwamba, kimuktadha wa kijadi utamaduni ulikuwa umempatia mwanamume uwezo wa kuwajibikia usalama wa nyumba yake na mkewe akiwemo.

Aidha, mwanamke alichukuliwa kuwa kiumbe dhaifu kuhusiana na ulinzi wake mwenyewe pasipo mwanamume. Hapa ndipo sasa mnyama fisi ametumiwa kuashiria hali tofauti za jinsia hizi mbili ndani ya jamii. Mwanamke kuchukuliwa kukosa uwezo wa kujilinda unaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza hali za mwanamke katika jamii za Kiafrika ambazo zilimpatia mwanamke sifa duni za unyonge, uoga, upole, na ukarimu. Hizi ni aina za hali ambazo utamaduni ulikuwa umejiwekea ili kumzuia mwanamke kuwa na usawa na mwanamume katika maendeleo ya jamii. Kwa hiyo, katika jamii ya kisasa, mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume. Kwa kufanya hivi, mwanamke ameonyesha uwezo wake katika nyanja tofauti ndani ya jamii moja na mwanamume. Mitazamo hii tofauti imesababisha

muktadha wa methali hii kuathiri maana na kulazimisha udenguzi kufanyika ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 81**

**Kinyankole:** *Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki.*
**Kiswahili:** Ukoo ambao utaharibika huwazaa wasichana.

Kimuktadha katika jamii ya Wanyankole, ilikuwa ni jambo la mwiko kuwazaa watoto wa kike pekee, kwa sababu jamii hii ilikuwa imejengeka katika mfumo wa kuumeni, ambapo watoto walioenziwa walikuwa wa kiume kwa madai kwamba walikuwa wakiendeleza ukoo wa baba na wala si wa mama. Hali hii kijadi iliwaweka wanawake katika wasiwasi na kuzidi kuwa watumwa kwa waume zao huku wakijaribu kulinda ndoa zao. Aidha, mwanamume ilimlazimu, kuwaoa wanawake wengi kuzuia kuchekwa na wanajamii. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, wanawake wamejitokeza na kupigania haki zao kwa mfano, kiuchumi, kisiasa, kitamaduni, kielimu, kindoa na kidini na kuona kwamba wanapata fursa sawa na wanaume ndani ya jamii. Hili limeweka wazi umuhimu wa mwanamke katika jamii, tofauti na namna jamii ya kijadi ilivyomchukulia kuwa kiumbe duni. Mwamko huu mpya unawafurahisha Wanaufeministi wa Kiafrika ambao hunuia kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Katika kutambua mabadiliko haya mapya, imelazimu kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole.

Aidha, udenguzi unashikilia kwamba, ni uhakiki unaojikita na kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Kwa mfano, katika methali hii "*Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki*" tafsiri yake "Ukoo ambao utaharibika huwazaa watoto wasichana". Kutokana na utamaduni wa kijadi, mtoto wa kiume alikuwa na jukumu la kuendeleza ukoo wa baba yake tofauti na mtoto wa kike. Vilevile, katika jamii ya kisasa ingawa mwanamke

amepata mwamko mpya wa kujimudu kimaisha, bado mtoto wa kiume ana jukumu la kuendeleza ukoo wa baba tofauti na mtoto wa kike. Hii ina maana kwamba, methali hii ingali na ufaafu katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole ingawa muktadha ni tofauti. Kwa hivyo, wanaudenguzi hawakukosea waliposema matini kama chombo kinaweza kujitosheleza na kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Kwa msingi huu, methali hii ililazimu kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

### 5.5 Maana ya Methali za Kijinsia Kiuchumi

Jamii ya Wanyankole kama mojawapo ya jamii nyingi za Kiafrika, imekuwa ikijivunia kipato kutokana na ufugaji wa ng'ombe wao. Ng'ombe hawa walikuwa ni njia mojawapo ya kuendeleza uchumi wao kijadi kama jamii. Wanyankole waliweza kuwauza, kutoa mahari, kupata maziwa na kuuza nyama yenyewe. Isitoshe, kando na uuzaji wa ng'ombe hao, pia jamii hii ilikuwa inalima vyakula vichache kama vile mtama, wimbi, maharagwe na viazi vitamu na kuongezea kwa uchumi wao. Ni vema ieleweke kwamba, uchumi huu pia ulikuwa ni wa kijinsia pale ambapo wanaume walikuwa wafugaji na wanawake wakulima. Utofauti huu wa kikazi, haukuweza kuwaacha Wanaufeministi wa Kiafrika, kukosa kuchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimejengeka kwenye mfumo wa kuumeni, na kumnyima mwanamke fursa ya kujihusisha na masuala nyeti ya jamii. Nadharia hii imeweka wazi kuwa, historia za jamii hii ndio chanzo cha kumwona mwanamke kama mtu duni asiyejiweza kiuchumi. Kwa hiyo, Wanaufeministi wa Kiafrika wamejaribu kumwinua mwanamke kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini ili aweze kugombea nafasi sawa na mwanamume katika jamii. Katika kufanikisha hilo, imelazimu kuchanganua maana mbalimbali za methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na ya kisasa ya Wanyankole kwa Mtazamo wa Kipragmatiki kama ifuatavyo;

### 5.5.1 Methali za jinsia ya kiume kiuchumi

Katika muktadha huu kijadi ni methali mbili za kijinsia zilizowahusu wanaume ndizo zilizojadiliwa. Imefahamika kwamba, wanaume walikuwa wanajihusisha, na uchumi wa kifahari kuliko wanawake. Hili lilitokana na utamaduni uliokuwa unaendeshwa kwa ubabe-dume kuwa mwanamume ni kiongozi kwa kila jambo. Sokolof (1980) anabainisha kuwa, Utamaduni, lugha, Imani na destruri ziliwawezesha wanaumme kuwa watawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilmali zenye thamani katika jamii kama vile, shamba, kazi, pesa na taasis za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa mengi yamebadilika na kumwezesha mwanamke kugombea nyadhifa sawa na mwanamume katika jamii moja tofauti na mtazamo wa kijadi.

Mwamko huu mpya kuhusu mwanamke, ndiyo ushindi ambao Wanaufeministi wa Kiafrika hunuia kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na uhusiano wao na watu wengine. Kutokana na fursa hii sawa, imechochea kuwapo kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa ya Wanyankole.

**Mf 82**

**Kinyankole**: *Kiburwa ente kiburwa Omukazi*.
**Kiswahili:** Akosaye ng’ombe humkosa mke.

Kimuktadha kutokana na uchumi wa jamii hii ambao ulikuwa wa ufugaji wa ng’ombe, ilikuwa ni kosa kubwa mwanamume kukosa ng’ombe. Hii ina maana kwamba mwanamume wa kijadi Mnyankole alikuwa ni lazima awe na ng’ombe kama ishara ya uongozi. Ni kutokana na ng’ombe hawa ndipo aliweza kutoa mahari na kupewa mke. Kwa hivyo, ilimlazimu kufanya kazi kwa bidii kuliko mwanamke. Hii iliweka wazi kuwa, jamii ilimpatia mwanamume kipaumbele katika kuendeleza uchumi wa jamii tofauti na mwanamke. Katika jamii ya kisasa, utofauti huu wa kiuchumi unaungwa

mkono na Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ambayo huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilishikilia kuwa ufugaji ni wa mwanamume tu, kwa sababu alikuwa kiongozi wa nyumba. Katika jamii ya kisasa, tunamwona mwanamke ameinuliwa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni, kindoa na kidini na kufanya kazi pamoja na mwanamume na kuleta maendeleo ndani ya jamii. Usawa huu umemletea utawala na ushujaa wake aliokuwa ameupoteza wakati wa kijadi. Kwa hiyo, methali hii imeathirika kimuktadha na kimaana na kulazimisha udenguzi ufanyike ili ieleweke katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

**Mf 83**

**Kinyankole:** *Okukunda akuha ente otayenda kuofa akuha Omukazi.*
**Kiswahili:** Akupendaye hukupa ng'ombe asiyetaka ufe hukupa mke.

Katika jamii ya Wanyankole kijadi, tofauti na ng'ombe kuwa wa kutolea mahari pia walikuwa wa kuleta udugu na umoja. Aidha, ilikuwa ni jukumu la mwanamume kuendeleza udugu huo wala si mwanamke. Kitamaduni, ni wanaume ndiyo ambao walikuwa wanahusika na masuala ya udugu kwani hao walikuwa viongozi na wala si wanawake. Katika jamii ya kisasa, jinsia zote zimejiendeleza katika kujirundikia mali na kuendeleza udugu pasipo jinsia moja kufanya hivyo. Huu ndio mwamko ambao wanaufeministi wanataka katika kumuinua na kumzindua mwanamke kwa upande wa wanawake na wanajamii wengine. Kwa kufanya hivi, ililazimu kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Kwa hiyo, kutokana na madai haya, imelazimu methali hii kudenguliwa ili ieleweke kimuktadha na kimaana katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 84**

**Kinyankole:** *Omwana wobwengye nahungura ebyaishe.*
**Kiswahili:** Mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake.

Katika jamii ya Wanyankole kijadi, mtoto mwerevu alikuwa ni wa baba na mjinga wa mama. Kwa hivyo, mtoto wa kiume alipendwa kwa sababu alionekana kuwa mwerevu

kuliko wa kike. Pili, alikuwa anaenda kuendeleza ukoo wa baba yake tofauti na mtoto wa kike. Mwisho, alikuwa anaenda kurithi mali ya baba yake tofauti na mtoto wa kike. Hali hii ilimfanya mtoto wa kiume kufunzwa majukumu nyeti ya jamii kama vile ya uchumi tofauti na mtoto wa kike ambaye alifunzwa kazi hasi za nyumbani. Hili lilionyesha kuwa mazingira yote yalikuwa yanampendelea mtoto wa kiume tofauti na wa kike.

Akiunga madai haya, Ndungo (1985) anayeangalia mabadiliko katika mazingira ya mwanamke katika nyakati mbalimbali za kihistoria, anadai kuwa picha ya mwanamke inayojitokeza ni ya kiumbe duni ambacho kimeshurutishwa na mifumo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume. Kutokana na ubaguzi huu, tunaona wanaufeministi wanapinga hali hii katika jamii ya kisasa kwa kuchunguza hali zilizomtweza mwanamke na kumpatia fursa sawa na mwanamume katika nyadhifa zote ndani ya jamii ya kisasa.

Jambo hili limewawezesha kujikomboa na kujenga jamii mpya ambayo jamii ya kijadi haikukusudia. Aidha, katika harakati za kujikomboa, imelazimu kupambanua methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole katika nyanja maalum za jamii. Kwa kufanya hivi, tumeona namna methali tofauti zinavyojitokeza katika nyanja maalum za jamii ya Wanyankole na kuonyesha namna mwanamke anavyodunishwa. Kwa msingi huu, ilibidi methali hii kudenguliwa ili kuonyesha namna muktadha ulivyoathiri maana ya methali hii katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

### 5.5.2 Methali za jinsia ya kike kiuchumi

Katika muktadha huu, ni methali mbili kuhusu uchumi zilizojadiliwa kuwahusu wanawake. Katika kuchunguza methali hizi, imetambulika kuwa wanawake walikuwa wamepewa kazi za hadhi ya chini kijadi ukilinganisha na za wanaume. Pia, wanawake

hawakuruhusiwa kuuza bidhaa baada ya kuvuna kwa madai kwamba hawakujua biashara. Suala hili pia la wanawake kuzuiliwa kuuza lilitokana na kuwa wanaume ndio waliokuwa viongozi na wenye mamlaka kuhusiana na suala hilo. Hili lilimfanya mwanamke kubaki nyuma kimaendeleo kwa sababu hakuweza kushiriki.

Mawazo haya yanasistizwa na Mohammed (1990) anayesema kuwa nafasi na majukumu aliyotwikwa mwanamke hayakumwezesha kujumuika na wenzake ili wazungumze juu ya unyanyasaji huu. Kiuchumi wanawake hawakujiweza na hivyo, wanaume waliutawala uchumi wote wa jamii. Vilevile Bertoncini (1996), katika utafiti wake kuhusu mwanamke katika riwaya ya Kiswahili anaeleza kwamba wanawake wanasawiriwa kama viumbe visivyo na uwezo wa kujitegemea (vamps) au wale wanaoonewa na wanaume (victims).

Wanaufeministi wa Kiafrika wanapinga jambo hili katika muktadha wa kisasa kwa kujaribu kuchunguza namna ya kumuinua na kumzindua mwanamke wa Kiafrika. Wamempatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika nyanja zote za maisha ikiwemo elimu, siasa, biashara, utamaduni, ndoa na dini ili mwanamke aweze kujiinua kimaisha kama mwanamume kikazi. Kwa hivyo, kutokana na usawa huu, methali hizi zimeweza kuathirika kimuktadha na kimaana katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole na kulazimisha kudenguliwa.

**Mf 85**

**Kinyankole:** *Omukazi enyerisa biri aine enfuka*.
**Kiswahili:** Mwanamke anayejilisha kumbe analo jembe.

Imetambulika kuwa, tofauti na jinsia ya kiume, wanawake kijadi walijihusisha pia katika biashara ndogondogo ndani ya jamii kama kulima mazao kwa mfano, mtama, wimbi, mhogo na viazi. Unapolinganisha biashara hizi katika jamii hii, unaona wanaume walikuwa wanaendesha biashara zenye kifahari kuliko wanawake. Kwa

mfano, wanaume walikuwa wanauza ng'ombe na kupata kipato kikubwa kuliko wanawake. Hata hivyo, wanawake walitegemea pesa kidogo na ambazo bado zilichukuliwa tena na wanaume. Utofauti huu wa kiuchumi, ulisababisha mwanamke kubaki nyuma kiuchumi na kimaendeleo. Hata hivyo katika jamii ya kisasa, Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitokeza na kumsaidia mwanamke katika kujihusisha na kazi kubwa ndani ya jamii iikiwemo uchumi, siasa, elimu, utamaduni, ndoa na dini tofauti na zamani. Fursa hii imemsaidia mwanamke kujimudu kimaisha na kujenga jamii mpya kwa kushirikiana na mwanamume. Kwa hivyo sasa, hali hii ililazimu methali hii idenguliwe ili maana na muktadha ueleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 86**

**Kinyankole:** *Omukazi mubi akwita hona.*
**Kiswahili:** Mwanamke mbaya hukudhoofisha kwa kila hali.

Katika jamii ya Wanyankole kimuktadha wa kijadi, mwanamke alikuwa anastahili kumheshimu mumewe na kumsaidia katika kila jambo la nyumbani ikiwemo biashara. Kumaanisha kuwa mwanamke ambaye alikuwa mvivu kikazi, mchafu, mchoyo, asiyejua malezi ya watoto ilikuwa ni ishara kuwa alikuwa ni hasara kubwa katika maendeleo ya jamii. Kwa hivyo, jamii ilitunga methali hii, kumuonya mwanamume na pia mwanamke kuhusu kufanya kazi kwa bidii. Aidha, katika jamii ya kisasa, mambo yamepata kubadilika kwa sababu jinsia zote zinashirikiana katika kuleta maendeleo. Huu ndio mwamko mpya, ambao wanaufeministi wanaunga mkono kwa kumuinua na kumzindua mwanamke kutoka katika minyororo ya kijadi. Hali hii imesababisha haja ya kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Mitazamo hii tofauti imeathiri miktadha na maana ya methali hii na kusababisha kudenguliwa ili ieleweke katika jamii ya kijadi na ile ya kisasa ya Wanyankole.

## 5.6 Hitimisho

Sura hii imeweka bayana namna methali za kijinsia zilivyoathirika kimaana katika nyanja tofauti ndani ya jamii ya Wanyankole. Imebainika kuwa, ni kutokana na kuwapo kwa nyanja hizi tofauti ndani ya jamii, ndiko kulikochangia kuathirika kwa maana za methali hizi kimatumizi na kulazimu kudenguliwa. Katika sura hii, lengo la pili limetumiwa katika kufanikisha uchambuzi wa data. Aidha, imebainika kuwa, suala kuhusu muktadha wa malezi na maadili limejitokeza kuwa na methali nyingi ambazo ziliathirika na kulazimu kudenguliwa ili kuafikiana na jamii ya kisasa. Kwa hiyo, kutokana na uainishaji wa methali hizi, imejitokeza kuwa methali nyingi ziliathirika kimaana na kimatumizi kutokana na nyanja tofauti zilizoathirika, kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii. Mwamko huu ni kama vile kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kitamaduni na kidini. Sura ya sita ya utafiti huu, imetathmini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

# SURA YA SITA

# UAMILIFU WA METHALI ZA KIJINSIA MIONGONI MWA JAMII YA KISASA YA WANYANKOLE

## 6.0 Utangulizi

Katika sura ya tano, tulijadili maana ya methali za kijinsia kimatumizi miongoni mwa Wanyankole. Ilibainika kuwa, ni kutokana na nyanja mbalimbali ndani ya jamii ya kijadi na kisasa ndizo zinasababisha maana na matumizi ya methali hizi kuathirika kimaana. Ni katika sura hii lengo la tatu ambalo linatathimini limetumiwa kutathimini uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole linashughulikiwa. Ili kufanikisha hili, mtafiti aligawanya matokeo ya utafiti wake katika makundi makuu matatu kama ifuatavyo: Kundi la kwanza lilihusu methali za kijinsia ambazo zilipendekezwa kuhifadhiwa katika jamii zote mbili za Wanyankole. Kundi la pili lilihusika na methali ambazo zilipendekezwa kudenguliwa ili kuafikiana na matakwa ya jamii ya kisasa. Na kundi la mwisho lilihusu methali ambazo zilipendekezwa kutupiliwa mbali katika jamii ya kisasa kwa mada kwamba hazifai tena katika jamii inayokua kila uchao.

## 6.1 Methali za Kijinsia za Kuhifadhiwa

Katika kundi hili la kwanza, tumejadili methali za kijinsia za Wanyankole ambazo zilipendekezwa kuhifadhiwa katika jamii zote mbili za Wanyankole kutokana na ufaafu wake.

**Mf 87**

**Kinyankole:** *Taha Omwasho teba rwango.*
**Kiswahili:** Kwenda nyumbani kwa baba yako si chuki.

Katika jamii ya Wanyankole, wanaume wana mazoea ya kupata watoto nje ya ndoa. Kwa hivyo jamii iliona ni jukumu lao la msingi kama baba ya watoto kuhakikisha kwamba watoto wanajua nyumbani kwao. Jambo hili lilimsaidia baba kutambua

kimalezi na kimaadili kuwa watoto wanalelewa katika utamaduni wake. Hii ni tofauti na mwanamke ambaye alikuwa na kazi ya kuzaa na kulea tu watoto. Aidha, katika jamii ya kisasa, jinsia zote zimepewa usawa kiuchumi, kisiasa, kielimu, kitamaduni na kindoa. Jambo hili limewezesha uhusiano mzuri katika malezi na maadili ya watoto tofauti na mtazamo wa kijadi. Vilevile, wanaufeministi wamechochea jinsia zote kushirikiana pamoja tofauti na namna wanawake walivyokuwa wametweza hapo zamani. Kwa msingi huu, methali hii imeonyesha ufaafu wake katika jamii ya kisasa pale ambapo mwanamke na mwanamume wamehusika katika malezi na maadili. Hata hivyo, bado baba ndiye anafaa kufunza watoto mila za ukoo wake kama mtazamo wa kijadi ulivyoshikilia.

Aidha, wanaundenguzi wana mtazamo tofauti kuhusu methali hii. Wao wanashikilia kuwa, udenguzi ni uhakiki unaojikita katika kuzingatia matini kama chombo kinachojitosheleza na kinachoweza kufichua maana mbili kwa kurejelea muktadha. Huu ni ukweli kabisa, kwa sababu katika muktadha wa kijadi lilikuwa ni jukumu la mwanamume kuwatambulisha watoto nyumbani kwao na wala si kwa upande wa mwanamke. Vilevile, katika jamii ya kisasa, ingawa wazazi wote wamepewa fursa sawa ndani ya jamii, bado watoto wanatambulishwa kwa upande wa mwanamume na si wa mwanamke. Kwa hivyo methali hii inasisitiza kuwa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa ana haki kutambulishwa kwa baba mzazi badala ya kutelekezwa au kuachwa alelewe na mama yake tu.

Hii ina maana kwamba, methali hii ilikuwa na maana sawa katika jamii hizi mbili tofauti, lakini katika miktadha tofauti ya namna wanaundenguzi wanavyoshikilia.

**Mf 88**

**Kinyankole:** *Ozara Omwojo tacwa ruganda.*
**Kiswahili:** Anayemzaa mtoto wa kiume hakomeshi ukoo.

Jamii ya kisasa ilipendekeza methali hii pia ihifadhiwe vilivyo kwa sababu ina mashiko katika jamii zote mbili. Kwa mfano katika jamii ya kijadi, mtoto wa kiume aliendeleza ukoo wa baba yake ilhali mtoto wa kike aliendeleza ukoo wa mumewe. Kwa hivyo, kutokana na utamaduni huu, mtoto wa kiume alienziwa kuliko wa kike jambo ambalo lilisababisha ubaguzi kijinsia. Kirindi (1918) anasisitiza kuwa kimila, Wanyankole walipendelea kuzaa watoto wa kiume tu kuliko wa kike. Hii ni kwa sababu mtoto wa kiume angeweza kuendeleza ukoo wa baba yake katika kizazi kingine. Tangu kuzaliwa kwake, mtoto wa kike alitazamwa kama mwenye faida kubwa kwa ukoo mwingine kwa sababu pindi akiolewa na kuzaa watoto aliishia watoto wa kuendeleza ukoo wa mumewe na wala sio wa baba yake. Kwa hivyo, wanawake waliozaa watoto wa kiume walienziwe sana katika jamii.

Kwa hivyo, licha ya jamii ya kisasa kuhimiza jinsia zote kuwa na fursa sawa kuhusu suala la ndoa na urithi, bado suala la kuendeleza ukoo wa baba linabaki kazi ya mtoto wa kiume na si la mtoto wa kike. Kwa mfano, katika kuthibitisha hili ni kuwa, mwanamke anapoolewa huondoka nyumbani kwao na kumfuata mumewe, ilhali mwanamume huoa na kumleta mke nyumbani. Aidha, kutokana na madai haya, hakuna namna mwanamke angepata hadhi ya juu kama mwanamume ndani ya jamii. Jambo hili linaungwa mkono na Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza historia za wanawake katika jamii. Hata hivyo, inatambulika kuwa jamii ya Wanyankole ilikuwa imejengeka katika msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa ubabe-dume. Kwa hivyo, jamii hii ilimtarajia mtoto wa kiume kuwa katika mstari wa mbele katika kuendeleza ukoo, na vilevile kuwa kiongozi wa familia yake anapoa. Kwa msingi huu, hakuna namna jinsia ya kike ingepata uhuru wake kutokana na mazingira kama haya.

Historia na utamaduni ulilazimu mtoto wa kiume kuwa mrithi, katika jamii na haikuweza kubadilishwa hata katika jamii ya kisasa. Kando na mwamko mpya ndani

ya jamii ndani ya jamii, bado mwanamke hajapewa nafasi ya kurithi. Hili limetokana na Wanyankole kushikilia utamaduni wa kumbagua mwanamke kiuchumi. kama Hata hivyo, methali hii iliweka wazi umuhimu wa mtoto wa kiume katika jamii ya kisasa, kama ilivyokuwa wakati wa kijadi kuhusu uendelezaji wa ukoo na urithi. Kwa vile ni njia ya kuhakikisha jamii ya Wanyankole haitoweki ulimwenguni hasa panapokuwa na ndoa baina ya Wanyankole na jamii nyinginezo.

**Mf 89**

**Kinyankole:** *Omukazi taba mugyeni.*
**Kiswahili:** Mwanamke hawi mgeni.

Kimuktadha katika jamii ya kijadi, mwanamke Mnyankole alifunzwa kutoka utotoni namna ya kufanya kazi zake za kijinsia tofauti na zile za kiume. Hii ni kumaanisha kimaumbile alikuwa hana shida kufanya baadhi ya kazi kama vile kupika, kuzaa na kulea, kusafisha nyumbani hata alipoenda ugenini. Aidha, katika jamii ya kisasa, mwanamke angali na jukumu hilo ingawa amepewa fursa sawa na mwanamume katika nyanja tofauti ndani ya jamii. Hali hii inaungwa mkono na Rorty (1996) anayebainisha kuwa udenguzi ni ukiushi wa kaida za matini. Ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza huonekana kama ni usaliti, lakini utokeaji wa ukiushi si ajali bali hukusudia kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Hii ina maana kwamba mwanamke tangu jadi, alikuwa na jukumu hili kutokana na maumbile yake ya kutoweza kufanya kazi ngumu ndani ya jamii kama mwanamume. Kwa hivyo kuendelea kufanya kazi hizo katika jamii ya kisasa, halikuwa jambo la usaliti ila kumkumbusha jukumu lake. Kwa hivyo, ni vizuri methali hii kuhifadhiwa katika jamii kwa sababu mwanamke kimaumbile ana uwezo wa kufanya baadhi ya kazi kumliko mwanamume.

**Mf 90**

**Kinyankole:** *Omukazi tayechwa kizire.*
**Kiswahili:** Mwanamke hajikati kizazi.

Katika jamii ya kijadi ya Wanyankole, ulikuwa mwiko mwanamke kupiga mtoto wake na kumfukuza nyumbani. Hii ni kwa sababu jamii hii ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni, na kuendelezwa kwa ubabe –dume. Aidha, jamii ilimpatia mwanamume uwezo na mamlaka ya kumfukuza nyumbani mtoto aliyeenda kinyume na matarajio ya jamii. Ingawa katika jamii ya kisasa, wazazi wote wamewajibikia watoto wao kutokana na usawa ndani ya jamii, bado mama hana uwezo wa kumfukuza mtoto nyumbani. Uhuru huu ndio Wanaufeministi wa Kiafrika wanaupigania kwa kumzindua mwanamke katika kushiriki masuala nyeti ya jamii. Ingawa mwanamke hawezi kumfukuza mtoto nyumbani, anaweza angalau kujadili na mumewe kuhusu namna ya kumwadhibu mtoto. Kutokana na madai haya, imeonyesha mwanamke angali na umuhimu kumliko mwanamume kuhusu suala la malezi na maadili katika jamii zote mbili za Wanyankole. Kwa msingi huu, ni muhimu kuhifadhi methali hii katika jamii zote mbili za Wanyankole.

**Mf 91**

**Kinyankole**: *Eziwaterwa nyoko tizaba nkoni*.
**Kiswahili:** Viboko ambavyo umepigwa na mama yako si viboko.

Katika muktadha wa kijadi, mama alikuwa amepewa jukumu la malezi na kwa hivyo alikuwa huru kutumia mbinu zozote zile kumwadhibu mtoto pale alipokosa au kwenda kinyume na matarajio ya jamii. Pia iliaminika kuwa, hasira za mama hazingeweza kumdhuru sana mtoto wake ilivyokuwa kwa baba. Ingawa katika jamii ya kisasa, tunaona jinsia zote zimejiendeleza kimaisha pia kuhusu kuwajibikia watoto. Hata hivyo katika jamii ya leo, bado mama anapatiwa jukumu hili kumaanisha ana uwezo kumliko baba kimalezi. Hali hii ndiyo Wanaufeministi wa Kiafrika wanafurahia wanapomwona mwanamke anatambuliwa kutokana na juhudi zake katika jamii ya kisasa. Ntarangwi (2004) anadai kuwa, ukombozi wa mwanamke umetokana na mikondo na harakati za kutetea haki za wanawake ulimwenguni na umejikita katika imani ya usawa wa kijinsia,

kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa hivyo methali Mf 91ingali inathaminiwa ndani ya jamii ya Wanyankole.

**Mf 92**

**Kinyankole:** *Nyineeka kuagamba omukazi tamugarukamu.*
**Kiswahili:** Mwenye nyumba akiongea mwanamke hastahili kumjibu.

Mwanamke Mnyankole kijadi, hakuwa na ruhusa ya kumpinga mumewe kwa njia yoyote kwa vile alikuwa anawajibikia familia yote. Kwa hivyo, ikiwa mwanamume alikuwa anatimiza wajibu wake kifamilia, mwanamke hakuwa na budi kumheshimu. Hali hii ya kutomruhusu mwanamke kuongea inasisitizwa na Liyong (1986) anayesema kuwa ndoa ilikuwa kwa manufaa ya mwanamume wala sio kwa manufaa ya mwanamke. Utamaduni wa Wakikuyu uliegemea kumfanya mwanamume awe shujaa na kumdhalalisha mwanamke. Kwa hivyo, kutokana na hali kama hii, mwanamke hakuweza kumjibu mumewe au kuzungumzia lolote kuhusu maendeleo ya jamii.

Akitafitia hali ya unyanyasaji wa kijinsia nchini Nijeria, Odimegwu (2006) anafafanua aina tano mahususi; unyanyasaji wa kijinsia (kubaka, ukeketaji); unyanyasaji wa kiuchumi (kutomiliki na kunyanganywa mali); unyanyasaji wa kijamii (mila za kibaguzi, ndoa za kulazimishwa); na unyanyasaji wa kiusemi ambao anaurejelea kama wa kisaikolojia au kiakili (matusi, lugha chafu, lawama na vitisho). Odimegwu anaendelea kusisitiza kuhusu dhima ya muktadha katika utafiti wa unyanyasaji wa kijinsia akisema kwamba ni lazima kutambua muktadha mahususi wa kijamii na kiutamaduni ili kuelewa na kupata suluhisho la unyanyasaji huo. Katika utafiti wake alitambua kwamba umaskini, dini na mitazamo hasi ndiyo inayoendeleza hali ya unyanyasaji wa kijinsia nchini Nijeria. Kwa upande mwingine, Dworkin (1976) anaonyesha umuhimu wa mwanamke katika jamii na anapendekeza kukomesha utawala wa wanaume dhidi ya wanawake kwa kubomoa kabisa muundo wa mihimili

ya utamaduni wa jamii kama vile kanisa, sheria kali zinazodhibitiwa na jamii na taswira zote za asasi, mila na desturi ambazo zinamwona mwanamke kuwa mtu ovyo.

Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, inakubalika kuwa kumheshimu mwananaume ni jambo muhimu, haswa ikiwa anawajibikia familia yake vizuri. Kwa hivyo hii methali inafaa ihifadhiwe lakini maana yake inafaa ipanuliwe ili ihimize wanaume wawe na busara katika uongozi wao, la sivyo watapuuzwa na wanawake.

**Mf 93**

> **Kinyankole:** *Emirimo mingi ekazibira Bigyemano okutobora omukazi.*
> **Kiswahili:** Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutomkimu mwanamke katika tendo la ndoa.

Methali hii ilimkumbusha mwanamume kijadi kuwa, ingawa alikuwa na kazi nyingi, alikuwa ni lazima atenge muda wa kuendeleza kizazi. Kwa hivyo, akina babu walikuwa wanamtahadharisha kutosahau jukumu lake, kwa sababu watoto walikuwa muhimu katika kuendeleza kizazi kijacho. Ingawa jamii ya kisasa imepitia mabadiliko mengi, bado mwanamume anakumbushwa jukumu lake kuu kuwa ni kuendeleza kizazi tofauti na mwanamke ambaye jukumu lake kuu ni kuzaa na kulea. Kwa msingi huu, methali hii inafaa kuhifadhiwa katika jamii ya Wanyankole. Hili limeweka wazi kuwa asasi ya ndoa miongoni mwa Waafrika ni muhimu na wanaufeministi wa Kiafrika wanahimiza jinsia zote ziwajibike ili tusije tukapoteza utambulisho wetu kama Waafrika.

**Mf 94**

> **Kinyankole:** *Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire.*
> **Kiswahili:** Mtoto ambaye ana baba yake huepuka majonzi ambayo yangemuua.

Methali hii ilikuwa inamkumbusha baba kufanya kazi kwa bidii ili kuwaepusha watoto wake na shida ambazo wangekumbana nazo katika siku zijazo. Hii ina maana kwamba, ikiwa baba alikosa kufanya kazi kwa nguvu na bidii, familia yake haikuweza kuishi kwa furaha. Aidha, katika jamii ya kisasa, bado mwanamume anaonywa kuhusu

kuwajibikia familia yake kuliko mwanamke. Pamoja na kwamba jinsia zote zimepewa fursa sawa ndani ya jamii, bado mwanamume anahitajika kufanya kazi zaidi kuliko mwanamke. Kwa hivyo, methali hii ingali na umuhimu katika jamii ya Wanyankole na inafaa ihifadhiwe.

## 6.2 Methali za Kinjisia za Kudenguliwa

Katika kundi hili la pili, tumejadili methali za kijinsia ambazo zilipendekezwa kudenguliwa ili kuafikiana na matarajio ya jamii ya kisasa. Aidha, kundi hili limejitokeza likiwa na idadi kubwa ya methali za kijinsia ambazo zilihitaji kudenguliwa. Hili limeonyesha kuwa jamii hii ya Wanyankole, imeathirika kutokana na mabadiliko mengi yanayopatikana ndani ya jamii hii kama inavyofafanulia vifuatavyo:

**Mf 95**

**Kinyankole:** *Omwana mubi ajumisa nyina.*
**Kiswahili:** Mtoto mbaya husababisha mama yake kutukanwa.

Kutokana na methali hii, mama alikuwa na jukumu kuu la kumfunza mtoto maadili na kumlea vizuri. Ikiwa mama alikuwa amezembea katika kazi yake, bila shaka jamii ilikuwa inamhukumu. Jamii iliamini kuwa majukumu ya mama yalikuwa machache na mepesi yakilinganishwa na yale magumu ya mwanamume. Kwa hivyo, yeye kushindwa kumlea mtoto ni ishara ya kutowajibika. Hata hivyo, jamii ya kisasa inapinga methali hii kwa madai kuwa jinsia zote zifanye kazi na kuwajibikia familia kwa pamoja na wala sio kumwachia mama peke yake jukumu la malezi ya watoto. Hii ni kwa sababu katika jamii ya kisasa ya Wanyankole, baba na mama wote wanashirikiana katika kutafuta riziki.

Huu ndio usawa ambao Malenga (2012), anasisitiza ndio ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kitamaduni na kidini zilizomfunga kwa muda mrefu. Ni mwamko

mpya unaoungwa mkono na Wafeministi wa Kiafrika ambao huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimewatweza na kuwanyima nafasi za utawala na kumiliki mali. Kwa hivyo, katika kusisitiza nafasi sawa ya wanawake na wanaume katika suala la malezi, methali hii inafaa iandikwe ifuatavyo: "Mtoto mbaya husababisha mzazi wake kutukanwa."

**Mf 96**

**Kinyankole:** *Enaku yotangambire nyoko tetuba.*
**Kiswahili:** Shida ambayo hujamwambia mama yako haipungui.

Katika muktadha wa jadi, jamii ya Wanyankole ilimwona mama kuwa mzazi ambaye alikuwa na ukaribu sana na mtoto kumliko baba. Kutokana na hali hii, alipewa sifa za kuwa mpole, mkarimu, mwenye upendo, mvumilivu na mnyenyekevu. Aidha, kutokana na sifa hizi alionekana kuwa tayari kumsikiliza mtoto ambaye huenda alikuwa amekumbana na machungu fulani. Licha ya madai kuwa mama alikuwa na sifa hizi, hali hii ilihimizwa na utamaduni. Haya yanathibitishwa na Njiru (1993:33) anayesema:

> "Katika jamii inayozingatia ubabeume, wanawake na wanaume wanajulishwa kukubali nafasi zao, iwe duni au tukufu. Wake kwa waume waitikie hali hii mawazoni mwao. Wanaume wanahimizwa kuwa na ushari, uwazi, uhuru na ushindani, ilihali wanawake hufunzwa kuwa watulivu, wategemezi, wasio na uwazi na watiifu."

Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, tunaona jinsia zote zimepewa fursa sawa katika nyanja tofauti ndani ya jamii na kulazimu hata suala la kuwajibikia watoto liwe la wazazi wote tofauti na mtazamo wa kijadi. Kwa hivyo kutokana na mwamko mpya ndani ya jamii ya Wanyankole, methali katika Mf 96 inabidi idenguliwe na kuandikwa ifuatavyo; "Shida ambayo hujamwambia mzazi haipungui." Kwa njia hii methali hii itabadilishwa kimaana ili wazazi wote baba na mama waone umuhimu wa kuwa karibu na watoto wao wanapokua.

**Mf 97**

**Kinyankole**: *Omwana oine mukaishe tahwa bunaku.*

**Kiswahili**: Mtoto ambaye yuko na mama wa kambo haishiwi huzuni.

Katika muktadha wa kijadi, methali hii imeonyesha kwamba, mama wa kambo alichukuliwa kuwa mtu mbaya kwa madai kuwa hakuwa mama mzazi wa watoto. Katika jamii ya Wanyankole, methali hii ilikuwa inawaonya wanawake kutoacha ndoa zao ila kuwa wavumilivu ili kuwatunza watoto wao. Mwanamke anapoacha ndoa yake, hii ilikuwa sababu nzuri ya mwanamume kumwoa mke mwingine ambaye angewatesa watoto waliochwa. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa mwanamke ana uwezo wa kuyakimu mahitaji yake na ya wanawe iwapo anahisi ndoa inamdhulumu. Isitoshe, japo kuna mama wa kambo wabaya, wapo mama wa kambo wema na pia kuna uwezekano wa kuwepo kwa baba wa kambo wabaya. Kutokana na mabadiliko ya kitamaduni mwanamke ana uhuru wa kujitafutia mchumba mwingine au kuwalea watoto wake kibinafsi pasipo mwanamume kumsaidia. Ni kutokana na mitazamo hii tofauti ambayo imelazimu kutathimini uamilifu wa methali hii ya kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole.

Wanaufeministi wa Kiafrika wanashikilia kuwa mfumo wa kibabe-dume katika jamii za Kiafrika ndio ulihimiza methali ya aina hii ili kuendelea kumtawala mwanamke. Wanachunguza historia za kijadi namna zilivyomtweza mwanamke na kujaribu kumsaidia kupata utawala wake katika jamii ya kisasa. Mwamko huu mpya unachochea ufasiri mbadala wa methali hii Mohammed (keshatajwa), anaeleza kuwa msomaji wa matini fulani anaweza kimakusudi kupoteza maana kabisa kwa vivuli vya maana. Kwa hivyo, katika kuchunguza methali hii kimaana na kimuktadha, Mohammed anajaribu kutahadharisha jamii ya kisasa. Anaitahadharisha kuepukana na kupoteza maana kimakusudi kwa kujumuisha kuwa mama wa kambo wote ni wabaya. Inawezekana hata mtoto akawa ndiye mkosa. Iwapo mtoto atakuwa na huzuni kwa kurekebishwa na

mama wa kambo ni sawa. Ni lazima wachunguze mchango wa mama wa kambo katika jamii hii inayokuwa kila uchao. Kwa msingi huu methali kwenye mf 97 inafaa idenguliwe ili iendane na uhalisia wa jamii ya kisasa. Tukumbuke kuwa siku zote si mapenzi ya mwanamke kuwa mama wa kambo. Aidha, kuna baadhi ya baba wa kambo wabaya kwa watoto wa mwanamke waliyemwoa:

**Mf 98**

**Kinyankole:** *Omukazi mubi tumwihaho Omwana.*
**Kiswahili:** Mwanamke mbaya huzai naye.

Methali hii pia inasisitiza maadili kwa jinsia ya kike katika jamii ya Wanyankole mwanamke alipaswa kuwa muadilifu. Hii ilimaanisha kuwa, ikiwa mwanamke alikuwa na tabia mbaya, watoto wake walifuata nyayo zake, jambo ambalo lilikuwa linahatarisha kizazi cha baadaye kijacho cha jamii hiyo. Ili kuepukana na tatizo kama hili, mwanamume alikuwa na jukumu la kuchunguza mahali ambapo mwanamke alifaa kutoka kabla ya ndoa. Ikiwa familia hiyo ilikuwa ya wachawi, wagomvi, wavivu, wachafu na wagumba, basi mwanamume hangeweza kuoa kutoka familia hiyo. Kwanza kabisa, jinsia zote hazichaguliwi wachumba tena. Na pili, jinsia zote ziko huru kutembeleana kabla ya wazazi kujua. Utofauti huu katika suala la uchumba na ndoa bila shaka umeathiri maana na matumizi ya methali hii. Wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza historia za wanawake, katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimemdunisha mwanamke kwa msingi wa ubabe-dume zinapinga methali kama hii kwani mwanamke ndiye anatakiwa kuwa mwadilifu ilihali mwanamume anaachiwa tu.

Mbali na kutambua boma la mwanamke alipotoka, ubikira ni kipengele ambacho pia kilizingatiwa kabla ya mahari kutolewa. Moris (1962) anadai kuwa, mwanamke wa kale alikuwa anatarajiwa kuwa bikira wakati wa kuolewa. Aidha, ikiwa hakuwa bikira, mama yake na shangazi walilaumiwa kwa kushindwa katika malezi ya binti yao na mara moja harusi ingefutiliwa mbali. Hata hivyo, Msichana alipopata mimba kabla ya

kuolewa, angetupwa bondeni na kuzikwa kule kwa sababu ya kukosa maadili na ilikuwa ishara ya kisirana kwa Wanyankole.

Tofauti na mwanamume, mwanamke alikuwa anatarajiwa kuwa kimya, hakuwa na ruhusa kuongea mbele ya watu hasa wanamume. Aidha, mwanamke alikuwa anaangaliwa kama mnyama baada ya kuolewa kwa kuwa mumewe alimtazama kama 'kitu' kwa sababu ya kulipa mahari ya ng'ombe. Walikuwa wanamfunza mila na desturi za familia hiyo na mwanamke hakuwa na ruhusa kutengana na mumewe hata akimpiga karibu kufa, mwanamke angevumilia kila hali, na kumpa heshima baba mkwe, mama mkwe na wakwe wengine. Aidha, alikuwa anastahili kuhakikisa kwamba kuna kibuyu cha uji kila wakati cha kumpatia mumewe baada ya kutoka kazini.

Tofauti na mwanamume, mwanamke alikuwa na jukuma kuu la kuzaa kama kazi yake. Walikuwa wanamtarajia kuzaa mtoto wa kiume kwanza ambaye alikuwa anaitwa *"Omusika."* Ni kutokana na hali hii ya kuzaa, ndipo tunaona mwanamume ilimbidi kutembelea familia ya msichana kabla ya kuzaa naye, ili kuepukana na kuzaa mrithi aliyekuwa na matatizo. Mwanamke alipofikisha watoto kuzidi wanne, hapo alikuwa anahesabika kama mwanamke ikiwa amezaa watoto wa kiume kwa sababu hii ilikuwa ishara ya kukubalika ndoani. Vilevile wanawake walistahili kuzaa watoto hadi wakati miaka yao haingeweza kuwaruhusu kuendelea kuzaa. Hali hii inalinganishwa na ile methali isemayo *"Abana bahwa omumukazi tibahwa omumushija"* tafsiri yake "Watoto humwisha ndani ya mwanamke lakini si kwa mwanamume." Kwa hiyo kutokana na hali hii, hakuna namna mwanamke Mnyankole angeweza kujiendeleza kimaisha kutokana na mazingira ya udunishaji aliyokuwa anaishi ndani yake.

Kutokana na hali hii, tunaona Wanaufeministi wa Kiafrika, wameweka mikakati yoyote ile ili kumzindua mwanamke katika jamii kwa kumpatia fursa sawa na mwanaumume

katika nyanja zote ndani ya jamii. Vilevile, wanaufeministi wa Kiafrika ambao huchunguza historia za wanawake katika jamii za Kiafrika ambazo zilikuwa zimemdunisha mwanamke kwa msingi wa ubabe-dume zinapinga methali kama hii kwani mwanamke ndiye anatakiwa kuwa mwadilifu ilihali mwanamume anaachiwa tu. Jamii ya kisasa ya Wanyankole inasisitiza kuwa suala la maadili hupaswa kuzingatiwa na jinsia zote ndipo jamii iweze kupata maendeleo endelevu ya kijamii. Kwa msingi huu, methali mf 98 inafaa idenguliwe na kuandikwa "Mchumba mbaya huzai naye." Hii ni kwa sababu baadhi ya wanaume wanatokana na familia zisizo na tabia njema. Kwa hivyo, wanaume wanafaa wajue kuwa wasipokuwa waadilifu huenda watakosa kupata mke wa kuoa. Halikadhalika, Dery (2015) na Maitaria (2019) wanabainisha kwamba desturi ya ulipaji wa mahari imeathiriwa na tabia ya ubinafsi na tamaa ambapo baadhi ya wazazi, hususan wa kiume, wanachukulia suala hili kama njia ya kujinyanyua kiuchumi. Maitaria (keshatajwa) anaonesha kwamba mwenendo huo ambao unaongozwa na tamaa na ubinafsi umewafanya baadhi ya wazazi kuwaangalia binti zao kama "bidhaa ya kunadiwa." Wazazi wenye tamaa na ubinafsi wanalihusisha suala la mahari na pesa, na sifa au utajiri. Utofauti huu katika suala la uchumba na ndoa bila shaka umeathiri maana na matumizi ya methali hii na kubidi ifasiriwe upya ili kuafikiana na matarajio ya jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Katika kutilia mkazo hoja hii, Kaye na wenzake (2005a) walifanya utafiti juu ya unyanyasaji wa wanandoa wajawazito katika wilaya ya Wakiso nchini Uganda. Kwa kutumia mbinu za mijadala ya makundi lengwa na usaili, watafiti walichunguza sababu, mitazamo na athari za unyanysaji wa nyumbani miongoni mwa wanawake wajawazito. Katika utafiti wao waligundua sababu za unyanyasaji huo kama mabadiliko ya kiutamaduni, upotezaji wa ajira, familia kubwa, na kutoelewana kimawasiliano. Hatua zilizopendekezwa kutatua tatizo la unyanyasaji wa wajawazito

ni pamoja na kuwaajiri washauri katika ngazi mbalimbali, utekelezaji wa sheria na uhamasishaji wa wanajamii. Ni kwa msingi huu tunaona msimamo wa Wanaufeministi wa Kiafrika unajitokeza na kuona kwamba mwanamke anapata haki sawa na mwanamume ndani ya jamii. Mintaarafu ya mawazo haya, ilibidi methali hii kufasiriwa upya ili umuhimu wake ueleweke katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 99**

**Kinyankole:** *Omukazi otamanyire ekimutungire eyiba ajikwasa omukono gumwe.*
**Kiswahili:** Mwanamke asiyejua thamani ya mumewe hushika uume wake kwa mkono mmoja.

Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, mwanamume alikuwa na jukumu la kufanya kazi kwa bidii na kuwajibikia familia yake. Hii ni kwa sababu alihitaji kulipa mahari ndipo apate mke. Kwa njia hii, mwanamke alionekana kubahatika kupata mume wa kumkimu. Kwa hivyo, mwanamke alipaswa kuonyesha shukran kwa kumheshimu mumewe. Hata hivyo, Momanyi (1998) na Kimani (2003) wanathibitisha kuwa hali hii inatokana na dhuluma na utegemezi wa mwanamke ulioshinikizwa na asasi za kijamii kama vile ndoa na dini. Momanyi (keshatajwa) anaeleza kuwa dini imetumiwa kuhalalisha ubwana na utwana mbali na kuainisha majukumu ya kijinsia. Anasema kuwa, chini ya kivuli cha dini ya Kiislamu, itikadi na destruri za Waswahili zinabainishwa majukumu yanayomwathiri mwanamke kihasi.

Mambo yamebadilika katika jamii za kisasa na hasa miongoni mwa Wanyankole ambao ni wafuasi wa dini ya Kikristo inayohimiza usawa wa kijinsia. Katika jamii ya leo, jinsia zote zinashiriki katika kuchuma mali katika familia na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, hali hii imeathiri hali ya wanawake kuwategemea wanaume. Kwa hivyo, heshima iliyoendana na hali hii ya utegemezi pia inaelekea kupotea. Hapo jadi, mwanamke alinyimwa uhuru wa kujiendeleza kwa madai kuwa ni kiumbe dhaifu. Hata hivyo Wanaufeministi wa Kiafrika wameonyesha kuwa mwanamke akipewa

nafasi katika jamii anaweza kufanya kazi sawa na mwanamume. Mwamko huu unashikilia kuwapo ushirikiano wa jinsia zote kikazi. Aidha, jinsia zote zinapaswa kuheshimiana kwa vile wanawake kwa wanaume wana nafasi katika maendeleo ya jamii. Kwa msingi huu methali Mf 99 inafaa idenguliwe ili tupate methali ambayo inahimiza jinsia zote kuheshimiana.

**Mf 100**

**Kinyankole:** *Omukazi ayomba azibira omutabani kuragwa.*
**Kiswahili:** Mwanamke mgomvi husababisha mtoto wake wa kiume kutorithishwa.

Methali hii imeweka wazi kuwa katika utamaduni wa Wanyankole mwanamume ndiye alikuwa na uwezo wa kurithisha watoto wake mali. Kwa hivyo, mwanamke alipaswa kuwa na maadili mazuri ili watoto wake wayaige. Mwanamke aliyekuwa mgomvi alichukuliwa kuwa mtovu wa nidhamu na kwa hivyo mumewe angeishia kumtelekeza na wanawe. Kwa kuhofia talaka na hivyo kuhatarisha maslahi ya wanawe, mwanamke alilazimika kumnyenyekea mumewe katika ndoa. Katika muktadha wa leo, methali hii huenda ikadenguliwa kwa sababu mwanamke wa kisasa anaweza kupata kazi nzuri ambayo inamwezesha kupata mali ya kujikimu na hata kurithisha watoto wake bila kumtegemea mwanamume. Mello (1999) anathibitisha kuwa hii leo, wanawake zaidi wanajitokeza kuajiriwa na kufanya kazi ambazo awali zilizodhaniwa kuwa za wanaume. Kwa hivyo, usawa huu wa jinsia kiuchumi ndiyo chanzo cha kufifia kwa maana ya methali hii katika jamii ya Wanyankole inayokua kila uchao.

Kwa hivyo, ingawa methali katika Mf 100 inahimiza jinsia ya kiume kuwarithisha watoto wao, ikumbukwe kuwa wanawake pia wana uwezo huo kiuchumi. Madai haya yanaungwa mkono na Wiliady (2015) ambaye anasema kwamba, ukombozi wa mwanamke unajaribu kuvunja mwiko wa mfumo dume hapa duniani kwa kuanzisha mapambano ya usawa wa kijinsia. Huu ndio msimamo wa Wanaufeministi wa Kiafrika

ambao wanachunguza historia na utamaduni anamojipata mwanamke wa Kiafrika na kujaribu kumzindua ili kuleta usawa katika jinsia zote ndani ya jamii. Aidha, kutokana na mwamko wa kifeministi pamoja na haja ya kumkomboa mwanamke, waandishi wa Kiafrika walianza kuwa na mtazamo tofauti kuhusu usawiri wa mwanamke kwa kumwonesha kama mwenye uwezo na thamani katika jamii (Fonchingong, 2006). Kwa msingi huu, methali hii ilibidi kudenguliwa ili ujumbe wake uafikiane na matarajio ya jamii ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 101**

**Kinyankole:** *Abashaija tibabagaya.*
**Kiswahili:** Wanaume hawadharauliwi.

Katika jamii ya Wanyankole mwanamume hakustahili kudharauliwa na mwanamke kwa njia yoyote ile. Hii ni kwa sababu mwanamume alikuwa kiongozi, na pia alikuwa na jukumu kuu la kuwajibikia familia yake. Kwa hivyo, mwanamke kumkosea heshima lilikuwa ni kosa kubwa kustahili kupewa talaka. Hii pia ilikuwa njia mojawapo ya kuhakikisha nyumbani kunakuwapo amani na heshima. Aidha, hali hii ilitokana na sifa angama za uume kama vile nguvu za mwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, ukakamavu, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo na zinazojitokeza katika desturi za maeneo ya ubabedume kwa jumla (Chafetz na Doyle, 1974; Doyle, 1985).

Kwa hivyo, ufaafu wa methali katika Mf 101 unategemea jitihada ya mwanamume kuhakikisha anawajibikia familia yake akizembea bila shaka mwanamke hataweza kumheshimu. Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika, inaunga mkono suala la jinsia zote kufanya kazi pasipo kubaguana katika jamii. Ushirika huu utaimarisha heshima baina ya wanawake na wanaume na hivyo kuchapuza maendeleo katika jamii za Kiafrika, jamii ya kisasa ya Kinyankole imekumbatia dini ya Kikristo ambayo inatimiza ushirikiano wa kijinsia na kwa hivyo wanandoa wanafaa kuheshimiana na kupendana

kama ndugu na dada. Haya tunayosoma kutoka kwa Barua ya Paulo kwa Waefeso mlango wa 6:10 na kuendelea. Madai haya yanaungwa mkono na Sawe, Makoti na Obuchi (2018) ambao walihakiki suala la uhusiano mwema baina ya wanandoa kama njia ya kudumisha ndoa kwa kurejelea *Utendi wa Ayubu*. Walifafanua kwamba asasi ya ndoa inampa mwanamume nafasi maalumu katika jamii. Wanadai;

> … … dini na tamaduni nyingi za jamii za Kiafrika zimempa mwanamume mamlaka katika ndoa, na maamuzi ya masuala mengi yanayohusiana na ndoa ni jukumu lake (uk.185).

Katika utafiti wao wanasisitiza kwamba imani na mienendo ya kiutamaduni ndiyo msingi wa hadhi, tabia na majukumu ya mwanamume ambayo ni tofauti na ya mwanamke. Hivyo, mume ndiye kichwa cha familia na mke ni msaidizi wake tu. Kwa msingi huu, watalaamu hawa (washatajwa), uhakiki wao ulijikita katika uhusiano mwema, hususan kuafikiana na kuwasiliana kwa njia bora ili kudumisha ndoa kwa kushauri juu ya matumizi ya lugha nzuri katika maongezi ya wanandoa. Kutokana na mawazo ya wataalamu hao, tunaona mwamko mpya ambao Wanaufeministi wa Kiafrika wanaupigia debe kuhusu usawa wa jinsia zote.

**Mf 102**

**Kinyankole:** *Ibega tiringana na mutwe.*
**Kiswahili:** Bega halilingani na kichwa.

Methali hii iliashiria, mwanamume ni kiongozi na mwanamke ni wa kuongozwa. Katika jamii ya Wanyankole, mwanamume alitambulika kuwa kiongozi na mwenye kumiliki kila kitu ndani ya boma. Mwanamke naye alitambuliwa kuwa mfuasi wake katika kila jambo. Kwa hivyo mwanamke hakuwa na usemi wowote kuhusu familia yake na jamii kwa jumla. Hali hii inaungwa mkono na Kibigo (2019) anayesema kuwa utamaduni, itikadi za jamii, mgawanyo wa mamlaka na uwezo wa kijinsia, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu kila mwanajamii humpatia mwanamume nafasi chanya kumliko mwanamke ambaye huwa anadunishwa. Kwa hiyo fursa sawa ambazo

mwanamke amepewa ndani ya jamii, zimemlazimu kubadili mwendo na majukumu ya kijamii kama ilivyo katika Mf 102. Ni muhimu jamii itambue kuwa katika jamii ya kisasa wanawake wana nafasi sawa katika masuala ya uongozi. Kwa hivyo methali hii isichukuliwe kujumuisha kuwa siku zote mwanamke yuko chini ya mwanamume bali tu washirikiane. Hii ni kwa sababu bega na kichwa vyote ni viungo vya mwili ambavyo vinahitajika na mwanadamu.

**Mf 103**

**Kinyankole:** *Omwana bamutinira obushaija bweishe.*

**Kiswahili:** Mtoto huogopwa kutokana na uume wa babake.

Neno 'uume' liliashiria kiasi cha mali ambacho mwanamume alikuwa amejirundikia ndani ya jamii. Katika jamii ya Wanyankole, watoto waliheshimiwa kutokana na utajiri ambao baba yao alikuwa amejirundikia. Kwa hivyo, mwanamume kuheshimika na kupewa cheo ndani ya jamii, kulitegemea mali aliyokuwa nayo. Hali hii ilikuwa ni tofauti na mwanamke ambaye alikuwa hana chochote kwa sababu hata yeye mwenyewe alikuwa anamilikiwa kama kitu kingine chochote na mwanamume katika jamii. Ndungu (1985) akichunguza taswira ya mwanamke katika vipindi mbalimbali vya kihistoria anadai kuwa picha ya mwanamke inayojitokeza ni kiumbe duni ambacho kimeshurutishwa na mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume.

Wollstonecraft (1792) anaeleza kwamba mwanamke anagandamizwa kutokana na mielekeo hasi ya kijamii kwa sababu wanaume na wanawake wanapewa mafunzo na elimu tofauti. Woolf (1929) anafafanua kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika wanawake wanabaguliwa kijamii, kielimu na kiuchumi, na hali hiyo inaendelezwa na itikadi ya kiume kupitia fasihi na historia ya jamii. Mtazamo wa Woolf (keshatajwa) unaendelezwa na Cameron (1992) ambaye anafafanua uhusiano kati ya jinsia na lugha. Cameron (keshatajwa) anaeleza kwamba katika muktadha wa kijinsia, wenye uwezo

(wanaume) hutumia lugha kama chombo cha kubagua, kunyanyasa na kuzima sauti ya walio chini (wanawake). Kisha Beauvoir (1949) anahusisha ugandamizwaji wa wanawake na asasi pamoja na mienendo mbalimbali ya kijamii, kama vile ndoa, utamaduni na dini.

Hata hivyo, hali ni tofauti katika jamii ya kisasa ambapo jinsia zote zina fursa ya kumiliki mali na hivyo kudai heshima. Kutokana na usawa huu wa kiuchumi, methali katika Mf 103 inafaa idenguliwe kimaana ili ihusishe jinsia zote ndipo wake kwa waume washirikishwe katika kuchuma na kulinda mali ya familia. Kwa hivyo methali hii inaweza kuandikwa; "Mtoto huogopwa kutokana na hadhi ya wazazi wake." Hii ni kwa sababu suala la hadhi ya jinsia, katika jamii linatokana na nafasi na uwezo au kuwezeshwa kwao kijamii na wala si suala la maumbile.

**Mf 104**

**Kinyankole:** *Meeme mememe tezaza mwojo.*
**Kiswahili:** Kubembeleza hakuishi kumzaa mtoto wa kiume.

Tunapochunguza methali hii kijadi, tunapata picha kwamba, mwanamume katika jamii ya Wanyankole alikuwa anastahili kufanya kazi kwa bidii tofauti na mwanamke ambaye alikuwa ni msaidizi wake. Kwa hiyo, jamii ilimtumia mtoto wa kiume kuonyesha umuhimu wa kufanya kazi tofauti na yule wa kike. Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume katika nyanja tofauti ndani ya jamii, jambo ambalo limeletea ushirikiano mzuri kati ya jinsia hizi mbili. Ni kutokana na hali hii, tunaona methali hii kimaana inafifia, kwa sababu inafaa ifasiriwe upya ili mtoto wa 'kiume' asichukuliwe kumaanisha mwanamume bali mtoto yeyote yule awe wa kike au wa kiume. Kwa msingi huu, methali mf 104 inafaa ichukuliwe kuwa inahimiza wanandoa na hasa mwanamume ajitahidi kuendeleza kizazi na ila asilegee.

**Mf 105**

**Kinyankole:** *Eka effire nyineeka ayetondera abaana.*
**Kiswahili:** Boma ambalo limekufa mwenye boma huomba watoto wake msamaha.

**Mf 106**

**Kinyankole:** *Eka eyenda kuhwaho nyineeka aimuka narya obuhoro.*
**Kiswahili:** Boma ambalo linaelekea kuharibika mwenye boma huamka na kuanza kula kiporo.

**Mf 107**

**Kinyankole:** *Nyineeka atutuka narya obuhoro.*
**Kiswahili**: Mwenye boma anakula kiporo akitoka jasho.

Kutokana na methali hizi tatu tumetambua kwamba, kuna uhusiano wa karibu. Aidha, katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, wanaume walitarajiwa kufanya kazi kwa bidii na nguvu kuwaliko wanawake. Jambo hili lilitokana na sifa ambazo walipewa na jamii, kama vile shujaa, kiongozi, mfalme na hakimu bora kabisa. Kwa hivyo walitarajiwa kuwajibika ili kuepukana na kupewa uporo na wake zao kama ishara ya kushindwa na majukumu yao. Katika jamii ya Wanyankole, chakula cha uporo ni ishara mbaya sana mwanamume alipopewa kula. Hata hivyo katika jamii ya kisasa, jinsia zote zimepewa fursa sawa kikazi ndani ya jamii. Hii ni kwa sababu katika muktadha wa kisasa jinsia zote zina nafasi ya kufanya kazi na kumiliki mali. Kwa hivyo suala la mwamume kuwa kiongozi pekee halipo tena, kwani mwanamke ana uwezo huo pia. Kwa hivyo methali hizi zinahimiza uwajibikaji wa mzazi wa kiume au viongozi kwa jumla na wala sio kuwa wazembe kwani watadharauliwa na walio chini yao. Hii inakaribiana na mf 105. Hii ni kwa sababu kuomba msamaha ni dalili ya kushuka hadhi. Kwa hivyo wazazi wanafaa kuwa kielelezo kwa watoto wao au viongozi kuwa vielelezo kwa walio chini yao.

**Mf 108**

**Kinyankole***: Omwana oine ishe tayekorara enku.*
**Kiswahili***:* Mtoto ambaye yuko na baba yake hastahili kubeba kuni.

Katika jamii ya Wanyankole ya jadi, lilikuwa ni jambo la aibu kubwa watoto kufanya kazi za hadhi ya chini ndani ya jamii kama vile kuwabebea watu kuni, kuwachotea maji na kuwalimia mashamba ikiwa baba bado angali hai. Kitendo cha mtoto kufanya shughuli hizi zote iliashiria kwamba baba alikuwa ameshindwa majukumu yake. Kwa hivyo, methali hii ilitungwa kumkumbusha mwanamume kufanya kazi kwa bidii ili familia yake iepukane na kazi za aibu katika jamii ya kijadi. Hata hivyo katika jamii ya kisasa, methali hii basi inaweza kudenguliwa ili ijumuishe baba na mama ili kuhimiza wazazi wawajibikie watoto wao. Hii ni kwa sababu katika muktadha wa kisasa jinsia zote zina nafasi ya kufanya kazi na kumiliki mali. Kwa hivyo methali hii inafaa kufasiriwa upya kama "Mtoto ambaye yuko na wazazi hastahili kubebi kuni"

**Mf 109**

**Kinyankole:** *Omukazi ne myenda Omushaija nemirimo.*
**Kiswahili:** Mwanamke ni nguo, mwanamume ni kazi.

Katika jamii ya Wanyankole ya jadi, mwanamume alikuwa anapewa sifa kutokana na namna mkewe alivyokuwa anavaa na kupendeza. Wakati huo, mwanamke jukumu lake lilikuwa ni kumtunza vizuri mumewe ili aendelee kuwajibikia boma lake. Jamii hii ilimuenzi mwanamke ambaye alikuwa anavalishwa vizuri na watoto ambao walikuwa na maadili mazuri. Ingawa mwanamke alikuwa na kazi zake, bado ilimlazimu mwanamume kuwajibika zaidi. Hili lilidhihirisha namna mwanamke katika jamii hii alivyokuwa anatumiwa kama kifaa cha kurembeshwa ili kumvutia mumewe na kumfurahisha kingono. Hali imekuwa tofauti katika jamii ya kisasa, kutokana na fursa ambazo mwanamke amepewa ndani ya jamii kama vile: kuwa mwanasiasa, mfanyabiashara, daktari, rais na mwalimu. Hii imemwezesha mwanamke kujiendeleza na kujipatia mahitaji yake na kwa hivyo hamtegemei tu mwanamume. Kwa vile mwanamke na mwanamume wameweza kushirikiana katika kukimu mahitaji ya familia, ni muhimu methali mf 109 idenguliwe ili ibainishe hali halisi katika jamii ya

kisasa. Jamii ya kisasa ielewe kuwa kazi na 'nguo' hapa ni fumbo kuonyesha ushirikiano kuwa katika tendo la ndoa lazima mwanamke apendeze ndipo amvutie mwamume kuendeleza kikazi.

**Mf 110**

**Kinyankole**: *Omukazi ahinga hamwe na Iba taba mugara.*
**Kiswahili**: Mwanamke ambaye analima na mumewe si mvivu.

Katika jamii ya Wanyankole ya jadi, mwanamke hakustahili kuwa mvivu. Kwa hiyo ili kuona nguvu zake, alilazimika kulima pamoja na mumewe ili kupima uwezo wake. Tangu awali, iliaminika kwamba, mwanamume alikuwa na nguvu kuliko mwanamke na hili lilitokana na utamaduni ambao ulikuwa umejengeka kwenye msingi wa ubabe-udume. Kwa hivyo, hii ndiyo ilikuwa sababu ya kumfanya mwanamke kulima na mwanamume. Lakini katika jamii ya kisasa, mambo mengi yamebadilika ndani ya jamii na nguvu za mwanamke hazipimwi tena kutokana na kulima na mumewe ilihali zinatokana na usawa katika kujihusisha na nyadhifa tofauti ndani ya jamii moja. Kwa hivyo methali hii inafaa ifasiriwe upya. Hii ni kwa kuwa methali hii inahimiza mchango na uwezo sawa walio nao wanandoa katika kuzalisha mali. Kwa hivyo wote waimiliki kwa usawa.

Ingawa mwanamke amepewa fursa sawa na mwanamume katika kufanya kazi, bado jamii inahitaji kulisisitiza jambo hili ili kuepukana na utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume. Beavoir (1949) anasisitiza kuwa, ni kupitia kwa ajira ambapo mwanamke ataweza kujinasua kutokana na hali ya unyanyasaji unaotokana na mila. Hakuna njia nyingine mwafaka ambayo inaweza kumhakikishia uhuru wake maishani isipokuwa hiyo ajira. Pindi tu atakapoacha kuwa mtegemezi na kujitosheleza katika baadhi ya mahitaji, mfumo wa kutegemewa utabadilika na hatakumbana na madhila mengi yanayohitaji kuangaziwa au kuhitaji mtu wa kutegemewa kuleta suluhu la

masaibu yanayomkumba mwanamke duniani. Ni kwa msingi huu ndipo methali hii imeweka wazi umuhimu wa jinsia zote kushirikiana katika kufanya kazi katika nyanja zote za maisha ya jamii.

**Mf 111**

**Kinyankole:** *Omushaija tahinduka omubigambo ahinduka aha kitandi honka.*
**Kiswahili:** Mwanaumme hageuki kwenye usemi ila hugeuka kitandani tu.

Methali hii imeweka wazi kuwa wanaume tu ndio waliopendelewa kuwa viongozi katika jamii ya Wanyankole ya kijadi. Hili lilitokana na mfumo wa kuumeni ambapo utamaduni ulikuwa unachangia katika kuwapatia wanaume sifa za uongozi, ushujaa, na kuwa na msimamo thabiti. Jinsia ya kike ilitengewa kazi ya kupika, kuzaa na kulea. Vilevile, kutokana na uongozi huu, mwanamume alikuwa na usemi wa mwisho kuhusu jambo lolote ndani ya jamii. Aidha, kuhusu mwanamume kugeuka kitandani tu, iliashiria kwamba ilipofika wakati wa kuendeleza kizazi, mwanamume aliweza kulegeza msimamo wake wa uongozi kwa sababu lilikuwa ni suala nyeti la kuwahusu watu wawili; yeye na mkewe tu. Kukosa watoto kwa mwanamume katika jamii hii ni suala la aibu na la kudharauliwa. Kwa hivyo mwanamume alilegeza ushujaa wake kitandani kuhakikisha anapata mtoto. Kwa hivyo methali hii inafaa idenguliwe kuendana na ulimwengu wa kisasa ambapo wanawake na wanaume wanashikilia nyadhifa za uongozi hata katika sekta ya uanasheria na siasa. Kwa hivyo methali hii inaweza kuandikwa “Mja hapaswi kugeuka kwenye usemi ila kitandani.”

**Mf 112**

**Kinyankole**: *Ahu abashaija batari abakazi bachwa emanja.*
**Kiswahili:** Pasipokuwepo wanaume, wanawake hutoa hukumu.

Mwanamume alikumbushwa kuhusu jukumu lake la kutoa hukumu kama kiongozi ndani ya jamii ya kijadi. Ikiwa alizembea, mwanamke alikuwa tayari kufanya kazi hiyo. Mwanamke hakuruhusiwa kutoa hukumu ndani ya jamii kwa sababu ilikuwa ni ishara

ya kumdharau mwanamume. Odimegwu (2006), anaeleza kuwa asasi ya ndoa iliidhinishwa na Mungu mwenyewe ambapo mume alipewa mamlaka juu ya mke wake. Hivyo, baadhi ya waume huangalia hilo kama kisingizio cha kuwatala na kuwadhibiti wake zao. Kadhalika, Odimegwu (keshatajwa) anahusisha madai ya kwamba uhuru ambao Adam alimpa mke wake Eva ulitumiwa vibaya na mke huyo, hadi kukiuka maagizo ya Mungu. Kwa msingi huo, baadhi ya wanaume hudai kwamba mume lazima amdhibiti iwezekanavyo mke wake asije akakosea tena.

Hata hivyo, Bloor na Bloor (2007), wanaonesha kuwa asasi ya dini inaendeleza itikadi na mamlaka ya tabaka tawala, hususan kwa kuwapumbaza wanawake. Kwa msingi huu, jamii ya kisasa imependekeza methali hii kutupiliwa mbali kwa sababu katika jamii ya leo tumewaona wanawake wakifanya kazi sawa na wanaume ikiwemo hata ya uhakimu. Katika masuala ya uongozi kwa mfano nchini Uganda tunao wanawake kama vile Janet Kataha Museveni ambaye ni Waziri Mkuu wa Elimu, HRH Nabagereka Sylvia Naginda, kando na kuwa mke wa Mfalme Kabaka wa Buganda ameanzisha mashirika mengi ambayo yanamwezesha mtoto wa kike kujifunza kazi za aina mbalimbali kuweza kujimudu kimaisha. Meaza Ashenafi ni mwanamke wa kwanza kuwa Jaji Mkuu nchini Ethiopia; kuna mwanariadha mashuhuri nchini Kenya kwa jina Joan Chelimo, na mwisho tuna Fatuma Ndagiza ambaye ni kiongozi wa masuala ya Umoja na Maridhiano, Usawa wa kijinsia na Uongozi Mwema nchini Rwanda. Mwamko huu mpya ndio Wanaufeministi wa Kiafrika wanachangamkia, wanapomwona mwanamke anainuliwa katika jamii na kuwa mtu mashuhuri hata kumliko mwanamume. Kuna uwezekano wa methali hii kufasiriwa upya, na kuonyesha umuhimu wa jinsia zote kujihusisha na uongozi katika jamii ya kisasa tofauti na wakati wa kijadi.

**Mf 113**

**Kinyankole**: *Omukazi aba orubaju rwiba.*

**Kiswahili**: Mwanamke huwa ubavu wa mumewe.

Katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, mwanamke alikuwa anakumbushwa kuwa kuwapo kwake kulitegemea kuwapo kwa mwanamume. Hii ina maana kwamba, mwanamke alistahili kumtumkia mwanamume daima kwa sababu alitoka ubavuni mwake na hangethubutu kuwa kiongozi. Arthur (1969) anadai kwamba changamoto zinazowakumba wanawake haziwakumbi wanaume. Kwa mfano, ubakaji, uoaji wa wake wengi bila ya mke wa kwanza kujulishwa, uolewaji wa wajane, urithi wa wanawake, kuwateka nyara wanawake, wasichana kuolewa wangali watoto,wanawake kuwa kama wafanya kazi wa kazi za nyumbani na kuwafurahisha wanaume kingono hata ikiwa si kwa hiari yao. Tunamwona mwanamke huyu hakuwa tofauti na hali inayojitokeza katika Utendi wa Mwanakupona (1990). Mwanakupona binti yake, anamwambia kufuata yoyote anayoagizwa na mumewe na kumtii mara zote. Kwa hivyo suala la hadhi ya mwanamke kumnyenyekea mwanamume, haliko tu katika jamii ya Wanyankole pekee, bali pia hata katika jamii nyinginezo kwingineko.

Aidha, mawazo haya ya Mwanakupona yanapingwa na jamii ya kisasa kwa madai kuwa, mengi ya haya yamebadilika na kwa hivyo ni sharti mwanamke na mwanamume wapendane, waheshimiane na kusaidiana. Hii ni kwa sababu mwanamke ni msaidizi wake na wala si mtumwa wake. Madai haya yanaungwa mkono na Bibilia takatifu kutoka kitabu cha Waefeso mlango wa 5: 25 kuendelea mbele kinasisitiza mwanamume na mwanamke kupendana na kusaidiana kwa sababu ni mwili mmoja. Aidha, hali hii ikizingatiwa italeta umoja na ushirikiano katika maendeleo ya jamii ya Wanyankole. Kwa msingi huu, methali hii inafaa ifasiriwe upya na kuwa “Mwanamke huwa mkono wa kulia wa mumewe” na si ubavu wake tena.

**Mf 114**

**Kinyankole:** *Omukazi enyerisa biri aine enfuka.*
**Kiswahili:** Mwanamke anayejilisha kumbe ana jembe.

Katika muktadha wa kijadi, kila jinsia ilikuwa na kazi yake maalum ya kufanya ili kuendeleza uchumi wa jamii. Mwanamume alikuwa mfugaji, naye mwanamke alikuwa mkulima. Utofauti wa kazi hizi uliweka bayana ujinsia katika majukumu haya mawili.

Kwanza kabisa, mwanamke alikuwa anafanya kazi nzito ya kulima, ilhali mwanamume alikuwa anafanya kazi ya kufuga ng'ombe ambayo haikuhitaji kutumia nguvu. Zaidi ya hayo, chakula ambacho mwanamke alikuwa anapanda, ni mwanamume ndiye ambaye alikuwa na mamlaka kukihusu kifedha. Ingawa hali ilikuwa hivyo kijadi, ilionyesha kuwa kulikuwepo na umoja na ushirikiano katika kuzalisha mali ya jamii ingawa ilikuwa ya kijinsia. Aidha, katika jamii ya kisasa mengi yamebadilika ndani ya jamii, na kila jinsia kupewa usawa katika daraja tofauti zinazopatikana ndani ya jamii. Hali imeonyesha kuwa, katika jamii ya kisasa jinsia zote ziko huru kufanya kazi yoyote na kujimudu kimaisha bila kubaguana. Hatimaye uzalishaji wa mali umeongezeka na ushirikiano mzuri kujitokeza. Kwa hivyo methali hii inafaa kufasiriwa upya kuwa "Wazazi wanaojilisha kumbe wana jembe."

Akisisitiza umuhimu wa mwanamke kuwa na uwezo kiuchumi, Coser (1963) anasema kuwa mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Kwa ujumla katika jamii nyingi ulimwenguni, nyenzo zote za kuzalisha mali zinatawaliwa na wanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Hali hii huwakumba wanawake kwa sababu tangu zamani wanawake wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi. Kwa hivyo Coser (keshatajwa) anapendekeza kuwa mwanamke apewe uhuru wa kiuchumi ili aepuke unyanyasaji na dhuluma. Kutokana na msimamo huo, jamii nyingi za kisasa ya Wanyankole ikiwemo zimehamasishwa na zimeanza kuwa na mtazamo chanya wa kuwapatia wanawake fursa

sawa ya kujiendeleza kiuchumi kupitia uundaji wa vyama vya wanawake. Aidha, Mutungi (2009) na Evans (2010) wanasisitiza umuhimu wa wanawake kujitoa mhanga na kupigania usawa ndani ya jamii. Wanasema kwamba wanawake wanahitaji kuungana na kushirikiana ili kujenga nguvu za pamoja katika kujitetea dhidi ya unyanyasaji unaosababishwa na mamlaka ya kiume kupitia mfumo wa kuumeni. Ni kutokana na hali hii ndipo tunaona baadhi ya methali za kijinsia zinahitaji kufasiriwa upya kama hizi zifuatazo:

**Mf 115**

**Kinyankole:** *Omukazi mubi akwita hona.*
**Kiswahili:** Mwanamke mbaya hukudhoofisha kwa kila hali.

Suala kuu la ndoa katika jamii ya Wanyankole, lilikuwa mwanamke kumtii mumewe na kuweza kumsaidia katika kuleta maendeleo ndani ya jamii. Hii ni kwa sababu jamii iliamini kwamba, jinsia hizi mbili zikiwa zenye bidii zingeweza kuzalisha mali ndani ya jamii na kuishi kwa furaha. Kwa msingi huu, iwapo mwanamke ambaye alikuwa ameolewa alikuwa mvivu, mchawi, mgomvi au mgumba, basi hiyo ilikuwa ni ishara kwamba familia hiyo haingeweza kujiendeleza kwa furaha. Ili kuepukana na hali hii, mwanamume alikuwa anasaidiwa na wazazi wake kutafuta mwanamke kutoka kwenye ukoo wa maadili. Lakini katika jamii ya kisasa, kuna mwamko mpya ambao umelazimu kila jinsia kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ndani ya jamii bila kubaguana. Hili limetokana na usawa, ambao umepewa jinsia zote mbili ndani ya jamii. Aidha, suala la maadili kati ya jinsia zote mbili ni muhimu katika jamii ya kisasa. Hii ni kwa sababu, ikiwa jinsia zote hazitaweza kuheshimiana na kushirikiana itakuwa ni vigumu kuleta maendeleo ndani ya jamii. Kwa hivyo methali hii inabidi kudenguliwa, kwa sababu si mwanamke tu ambaye anaweza kudhoofisha mwanamume, bali mwanamume pia anaweza kufanya hivyo. Kwa hivyo methali hii inafaa kufasiriwa, ili kuonyesha umuhimu wa jinsia zote kushirikiana katika kuzalisha mali ya jamii.

**Mf 116**

**Kinyankole:** *Kiburwa ente kiburwa Omukazi.*
**Kiswahili:** Akosaye ng'ombe humkosa mke.

Jamii ya Wanyankole ya jadi ilienzi sana ufugaji wa ng'ombe kuliko kazi nyingine yoyote. Jukumu hili la ufugaji, lilikuwa linaendeshwa na wanaume ilhali wanawake walikuwa na jukumu la kulima mashamba. Utajiri wa Mnyankole ulikadiriwa kwa msingi wa idadi ya ng'ombe aliomiliki kuliko kitu kingine. Katika muktadha wa ndoa, mwanamume alihitajika kutoa ng'ombe kama mahari ili kuoa mke. Kwa hivyo methali katika Mf 116 inapaswa iandikwe upya kama "Akosaye mahari humkosa mke." Hii ni kwa sababu jamii imepiga hatua kimaendeleo na si ng'ombe tu ambao wanaweza kutolewa kama mahari, pesa zinaweza pia kutumiwa. Licha ya kuwa mahari hayasistizwi sana katika ndoa za kisasa, methali hii ilihimiza mwanamume kugharamika ili apate mali ndipo aoe. Kwa hivyo, methali hii inafaa ifasiriwe upya ndipo maana yake chanya iimarishwe katika jamii ya kisasa.

**Mf 117**

**Kinyankole**: *Okukunda akuha ente otayenda kwofa akuha omukazi.*
**Kiswahili:** Anayekupenda hukupatia ng'ombe na asiyetaka ufe hukupatia mke.

Katika jamii ya Wanyankole wa jadi, ng'ombe walithaminiwa kama njia mojawapo ya kuleta udugu. Kwa hivyo, ng'ombe walikuwa wanatumiwa katika jamii kuendeleza shughuli nyingi za kiuchumi ndoa ikiwa ni mojawapo. Tofauti na jamii ya kijadi, jamii ya kisasa ina vitu vingi ambavyo inaweza kutumiwa kuleta undugu mbali na ng'ombe. Kwa mfano mtu anaweza kupewa shamba, gari, nyumba, kama ishara ya upendo. Mabadiliko haya yanaonyesha kuwa jamii hii imepiga hatua, kiuchumi, kielimu na kitamaduni na kuona mambo tofauti. Hata hivyo wanawake wamepewa fursa sawa na wanaume, katika kuchangia maendeleo ya jamii na tunaona wanaweza kuchangia

katika kuleta undugu ndani ya jamii. Kwa hivyo, methali Mf 117 inahitaji kufasiriwa upya kuwa, Anayekupenda hukupatia chochote na asiyetaka ufe hukupatia mke."

**Mf 118**

**Kinyankole**: *Omwana wobwengye nahungura ebyaishe.*
**Kiswahili:** Mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake.

Jamii ya Wanyankole ya kijadi, ilichukulia kuwa mtoto wa kiume ndiye ambaye kuwa na busara, hekima na sifa za uongozi tofauti na mtoto wa kike. Hili lilisababishwa na jamii ya Wanyankole iliyokuwa imejengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa ubabe-dume. Katika jamii hii, mtoto wa kiume alikuwa anapewa hadhi ya juu kuliko mtoto wa kike. Kwa hivyo, ilikuwa ni bora baba kumsaidia mtoto wake wa kiume kuwa na sifa ambazo alizitarajia wakati wa kumrithisha, na vilevile kuendeleza uchumi wa jamii kwa sababu mwishowe yeye ndiye angerithi mali hiyo. Engels (1975) anasisitiza kuwa chanzo cha historia ya kunyonywa na kukandamizwa kwa mwanamke wakati jamii ya binadamu iligawanyika katika matabaka mbalimbali. Jamii ilipobadilika na kuwa ya kitabaka, ilianzisha urithi upande wa kuumeni. Kutokana na haya, umilikaji wa mali ulimwendea mwanamume ukiwemo pia ukiritimba wa nyenzo za uzalishaji mali. Hali hii ilimpa mwanamke uwezo mdogo kiuchumi akilinganishwa na mwanamume. Kwa hivyo, akawa mtumwa kwa mwanamume ambaye alimdunisha mwanamke kwa kuwa na uwezo mdogo kiuchumi. Nafasi ya mwanamke iliendelea kuwa nyuma kutokana na tofauti za kikazi. Kazi nyingi za hadhi kama vile uongozi zilitengewa wanaume huku jamii ikifunzwa kuamini kuwa mahala panapomfaa mwanamke ni nyumbani.

Mawazo ya Engels yanaafiki hasa jamii ya jadi ya Wanyankole ambapo, mwanamke alikandamizwa kwa madai kuwa ni kiumbe duni asiyeweza kujihusisha na mambo ya uchumi na uongozi ndani ya jamii. Lakini katika muktadha wa kisasa, methali hii inafaa ifasiriwe upya ili kuzihusisha jinsia zote. Hii ni kwa sababu jamii imepitia mabadiliko

mengi, na kuwapa usawa wa kielimu na kiuchumi wote bila kubaguliwa. Kutokana na usawa huu, tumeweza kumwona mtoto wa kike akifaulu maishani sawa na mtoto wa kiume. Kando na hilo watoto wa kike wameweza kujihusisha, na masuala nyeti ya uchumi vizuri na kubidi kurithishwa na wazazi wao sawa na mtoto wa kiume. Hili limethibitisha kuwa mtoto wa kike amepewa ushujaa na ukombozi wake katika kujiendeleza kimaisha, Ni kutokana na utofauti huu wa kimawazo, methali hii inapendekezwa kufasiriwa upya kuwa; "Mtoto mwerevu hurithi mali ya wazazi wake."

### 6.3 Methali za Kinjisia za Kutupiliwa Mbali

Kutokana na uchanganuzi wa data, hili ndilo kundi la tatu na la mwisho ambalo lilishughulikia methali zilizopendekezwa kutupiliwa mbali katika jamii ya kisasa ya Kinyankole kwa madai ya kuwa hazina ufaafu tena.

**Mf 119**

> **Kinyankole:** *Empisi ekagira eti, kumbugana omushaija ashendekyerize ondijo nteraa mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheeka nkaba.*
>
> **Kiswahili:** Fisi alisema kwamba akimkuta mwanamume akimsindikiza mwanamume mwenzake hujificha, lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu.

Katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, ilikuwa ni kazi ya mwanamume kumlinda mwanamke kwa sababu alichukuliwa kuwa mwenye uwezo na nguvu. Isitoshe, mwanamke alijua jukumu hilo la kumlinda lilikuwa ni la mwanamume, na hivyo hangeweza kuthubutu kulifanya. Aidha, mwanamke kumsindikiza mwenzake, ilikuwa ni ishara ya kutekeleza jukumu la mwanamume. Lakini katika jamii ya kisasa, methali hii ilifaa itupiliwe mbali kwa sababu kuna baadhi ya wanawake ambao kimaumbile ni wenye nguvu kuliko hata wanaume wenyewe. Kwa hivyo, inakuwa vigumu kueleza ufaafu wa methali hii katika muktadha wa leo, ikiwa wanawake wameweza kufanya kazi zinazohitaji nguvu kama wanaume katika nyanja tofauti ndani ya jamii. Aidha,

wengine wana uwezo wa kujilinda vizuri hata kuliko wanaume. Kutokana na madai haya, methali hii inaonekana kutokuwa na mashiko katika jamii ya kisasa kwa sababu sifa zote ambazo zilikuwa zinamrejelea mwanamume, sasa zinapatikana pia kwa mwanamke. Kwa hivyo, methali hii inakosa mashiko katika jamii ya kisasa.

**Mf 120**

**Kinyankole**: *Omufukazi tagaya mboro.*
**Kiswahili:** Mjane hadharau mboro.

Mwanamke katika jamii ya Wanyankole kijadi, kimuktadha alikuwa anarithiwa kama vitu vingine vyovyote ndani ya nyumba. Mumewe alipoaga dunia ni mdogo wake wa kiume ndiye aliyemrithi na hakuwa na hiari kupinga uamuzi wa utamaduni. Kutokana na hali hii, ndiyo sababu methali hii kutungwa kumwonya mwanamke kuhusu kurithiwa. Lakini katika jamii ya kisasa, methali hii imekashifiwa vibaya sana kwa sababu ilimwonyesha mwanamke kuwa kiumbe dhaifu na asiyejiweza kimwili kwani alikuwa anaamuliwa na jamii la kufanyiwa.

Katika kusisitiza hoja hii, Mulokozi (1982) katika nakala yake 'Protest and Resistance in Kiswahili poetry 1660-1885' amezungumzia maswala mengi ikiwemo taswira ya mwanamke. Ameona kuwa ushairi wa Kiswahili uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mfumo wa Kimwinyi ambao ulithamini sana anasa, mapambo na kumchukulia mwanamke kama chombo au kitu cha kudondosha hamu ya mwanaume kimapenzi. Hivyo, ushairi ulifuata mwelekeo huo kwa kumsawiri mwanamke kuwa ni kiumbe duni ambaye anatumiwa kama chombo cha kuburudisha na kutimiza haja ya mapenzi ya mwanamume. Kutokana na hali hii, mwanamke wa kisasa amepewa fursa sawa na mwanamume katika nyanja tofauti ndani ya jamii moja. Jambo hili limesababisha mwamko mpya wa kiuchumi, elimu, kitamaduni na siasa na kumwona mwanamke anavyojaribu kujikomboa kutoka unyanyasaji huu na jinsi anavyopigania haki yake

sawa na kuleta maendeleo katika jamii. Mwamko huu mpya ndio furaha ya Wanaufeministi wa Kiafrika ambao wamejitahidi kumzindua mwanamke kutokana na utamaduni uliomdunisha kwa kumpatia usawa na mwanamume katika nyanja zote ndani ya jamii.

Kwa msingi huu, fursa ya usawa ambayo mwanamke amepewa ndani ya jamii ya kisasa imemwezesha mwanamke kujichagulia mchumba kwa hiari yake. Zaidi ya hayo, mashirika ya taifa na kimataifa yamejitokeza na kumtetea mwanamke kama vile HCT (HIV Counseling and Testing), WHO (The World Health Organisation), VCT (Voluntary Counseling and Testing), UHSBS (Uganda HIV/AIDS SERO-Behavioural Survey), AMREF (African Medical and Research Foundation), AIC (Aids information Centre), TACAIDS (Tanzania Commission for Aids), TASO (The Aids Support Organisation), HBHCT (Home-based HIV Counseling and Testing). Mashirika haya yamehakikisha kupigwa marufuku kwa mambo ya kurithiwa kwa sababu yalikuwa yanaenda kinyume na haki za binadamu. Kutokana na utetezi huu, ni wazi kuwa mwanamke katika jamii ya kisasa amepewa uhuru wake. Aidha, kutokana na madai haya, ni bora methali Mf 120 itupiliwe katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

Buckley (1997) anaonyesha athari za mila ambazo zinamwathiri mwanamke kwa kuchunguza kazi ya fasihi katika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu mila ya kurithi mjane. Anadai kuwa mila hii ni njia ya kuambukiza UKIMWI katika jamii fulani nchini Kenya. Mawazo haya yanaungwa mkono na Owino (1998) anayedai kuwa hata kama mila hii ilikuwa na manufaa wakati uliopita, katika nyakati hizi inachangia maambukizi ya UKIMWI. Jamii ya Wanyankole ni kati ya jamii ambazo zilienzi mila hii hadi mwaka wa 1982 walipogundua ya kuwa UKIMWI ungewamaliza ikiwa hawangeachana na mila hii. Ni kwa msingi huu ndipo tunapendekeza kutupiliwa

mbali kwa methali hii kwa sababu haina mashiko tena katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 121**

**Kinyankole***: Omukazi murungi niwe anyamisiriza Iba.*
**Kiswahili:** Mwanamke mzuri ndiye humbembeleza mumewe kulala.

Methali hii imeweka bayana namna mwanamke wa Kinyankole kijadi alivyokuwa anachukuliwa kuwa kifaa cha kumhudumia mwanamume. Jamii ya Wanyankole ilitegemea mwanamke kuwa amelelewa vizuri na mwenye maadili. Kwa hivyo, kwenda kinyume na haya, ilichukuliwa kuwa ukosefu wa nidhamu. Katika jamii hii, mwanamke alikuwa na jukumu kuu la kumtunza mumewe kwa njia nzuri kwa sababu alikuwa anamwajibikia. Madai haya yanaungwa mkono na mtalaam Oduyoye (1998) anayesema:

> "Katika jamii za Kiafrika, wanawake wanachukuliwa kama watu wa hadhi ya chini. Wanachukuliwa na kutumiwa na wanaume kama mali ya kibinafsi. Wanadhulumiwa na kubekuliwa na kutumikishwa."

Kutokana na mawazo haya, jamii ya kisasa imeipinga methali hii kwa madai kuwa imepitwa na wakati. Hii ni kwa sababu jamii hii imepitia mabadiliko mengi, na kupatia jinsia zote usawa katika shughuli tofauti ndani ya jamii. Kumaanisha muda ambao mwanamke, alikuwa ametengewa kijadi kumbembeleza mumewe kulala sasa anautumia kufanya kazi zingine za umma. Mabadiliko haya yanabidi kila jinsia, kufanya kazi kwa bidii na kuheshimiana ili kuzalisha mali ya jamii na isitoshe ulimwengu umebadilika. Huu ndio mwamko mpya ambao wanaufeministi, wanautetea ili kila mwanamke kuweza kujimudu kimaisha na si kumtegemea mwanamume. Kutokana na madai haya, methali hii ilibidi kutupiliwa mbali kwa kukosa ufaafu ndani ya jamii.

**Mf 122**

**Kinyankole:** *Omukazi oine Iba tarya nkoko.*
**Kiswahili:** Mwanamke ambaye ana mume hali nyama ya kuku.

Katika methali hii, tumetambua jinsi ambavyo katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, mwanamke hakuruhusiwa kula baadhi ya vyakula ambavyo vilichukuliwa kuwa ilikuwa ni mwiko kitamaduni. Kwa mfano, katika jamii ya Wanyankole, mwanamke hakuruhusiwa kula nyama ya kuku wala nyama ya mbuzi kwa madai kwamba angeota pembe na ndevu. Pia, iliaminika ni wanaume tu ndio ambao walistahili kula vyakula hivi, kwa sababu walikuwa wanafanya kazi nzito kuliko wanawake kama vile kuwinda, kujenga, kulinda usalama na kuwafuga ng'ombe. Kutokana na mtazamo huu, jamii ya kisasa imeonelea ni bora methali hii kuondolewa katika jamii ya kisasa kwani haina mashiko tena. Hili limetokana na jinsia zote kupewa fursa sawa ndani ya jamii na kumlazimisha mwanamke kula vyakula sawa na mwanamume. Aidha, vyakula ambavyo jamii ya kijadi ilikuwa inamkataza mwanamke kula, ndivyo madaktari wanahimiza jinsia zote kula kiafya. Kwa hivyo methali hii imeonyesha haina ufaafu katika jamii ya kisasa, kwa sababu mwanamke amejikomboa na kupata uhuru wake tofauti na mtazamo wa kijadi.

**Mf: 123**

> **Kinyankole:** *Abana bahwa omumukazi tibahwa mumushaija.*
> **Kiswahili:** Watoto huisha ndani ya mwanamke lakini si kwa mwanamume.

Methali hii inaashiria namna ambavyo wakati wa kale, mwanamke wa Kinyankole alivyostahili kuzaa hadi watoto walipokwisha tumboni. Ili kuepukana na ugomvi katika jamii kuhusu mwanamume kuwaoa wanawake wengi, waliamua kutunga methali hii kumwonyesha mwanamke ni kwa sababu gani mwanamume alikuwa na uwezo zaidi wa kuendelea kuzaa kumliko. Kwanza kabisa, mwanamke hakuweza kuzaa zaidi ya watoto kumi na watano kabla kizazi hakijakwisha. Sababu ya pili, wanaume walikuwa na mali nyingi na waliwahitaji watoto wa kurithi. Kutokana na sababu hizi, mwanamume alilazimika kuwaoa wanawake wengi ili kuendeleza kikazi chake.

Akiyaunga mkono madai haya, Momanyi (1998) anasema kuwa dini imetumiwa kuhalalisha ubwana na utwana mbali na kuainisha majukumu ya mwanamume. Chini ya kivuli cha dini ya Kiislamu, itikadi na desturi za Waswahili zinaweza kuainishwa hasa zile zinazomwathiri mwanamke. Hoja ya uislamu imeathiri vilevile jamii ya Wanyankole, kwani mwanaume anaruhusiwa kuwaoa wake wengi kwa msingi wa dini. Iwapo ana mali nyingi, mwanamume huona kuwa lazima azae watoto wengi ili warithi mali yake.

Hata hivyo, katika jamii ya kisasa, suala la kuzaa watoto wengi limefifia kwa sababu ya ugumu wa maisha ambao umesababishwa na uhaba wa ardhi, uchumi kuwa ghali na sera za serikali ambazo hazimjali mwananchi. Kutokana na madai haya, methali hii inakosa ufaafu katika jamii ya kisasa ya Wanyankole.

**Mf 124**

**Kinyankole:** *Obwenda kusimwa Omukazi akasa oburo aheekire Iba.*
**Kiswahili:** Kupenda kushukuriwa mwanamke alisaga wimbi akimbeba mumewe mgongoni.

Katika jamii ya jadi ya Wanyankole, mwanamke alikuwa ametengewa kazi zake maalum tofauti na zile za mwanamume. Hali hii ilimlazimu kufanya kazi kwa bidii bila kumtegemea mumewe. Aidha, iligunduliwa wanaume katika jamii hii, waliruhusiwa kuwaoa wanawake wengi kama sifa moja ya kuheshimika ndani ya jamii. Hali hii ilisababisha ushindani ndani ya jamii huku kila mwanamke akitafuta njia ya kumfurahisha mumewe. Kwa hivyo mwanamke aliishia kumbeba mumewe mgongoni akiwa anasaga wimbi.

Wataalam mbalimbali wakiwemo, Ferguson (2002) na Ifachelobi (2014) wanadhihirisha utumwa huu wa mwanamke. Ferguson (keshatajwa) anasema kuwa mfumo dume kwa kawaida unalazimisha sauti za wanawake kuzimika, kama njia ya kuwaweka chini/ pembezoni ili wasishiriki katika masuala ya jamii. Anaeleza kwamba

mila na desturi za kijamii zinawahimiza wanawake kuwa kimya. Hivyo, kimya kinaendeleza mamlaka na utawala wa kiume kwa kuhakikisha unyonge/utiifu wa mwanamke. Ifachelobi (2014) anaeleza kwamba mfumo dume unampa mwanamume mamlaka ya kudidimiza uhuru na hata ‘kuzima’ sauti ya mwanamke katika jamii. Nao Denham-Vanghan na Edmond (2010) wanaeleza kwamba kimya kinaweza kutumiwa katika kudhihirisha hisi nzito za heshima na woga katika utangamano. Hali hii ilionyesha namna mwanamke alivyokuwa anachukuliwa kama kifaa na mtumwa ndani ya ndoa yake.

Hata hivyo, jamii ya kisasa inapinga methali hii, na kupendekeza itupiliwe mbali kwa sababu mwanamke wa kisasa amepewa fursa sawa na mwanamume katika nyanja mbalimbali ndani ya jamii. Aidha, heshima na ushirikiano, vinasisitizwa kwa kila jinsia katika utekelazaji wa kazi. Hata hivyo, wakati wa kumbeba mwanamume mgongoni haupo tena, kwa sababu jinsia zote zinashughulika kupata kipato cha kila siku. Kwa hivyo Wanaufeministi wa Kiafrika wanapinga tamaduni kama ya uke wenza ambao unamdhulumu mwanamke na kumkweza mwanamume. Ni kutokana na msimamo huu ndipo Wanaufeministi wa Kiafrika wanahimiza wanawake kupigania haki zao kupitia machapisho ya kifasihi zikiwemo methali (Richard na wenzake, 2007). Kwa msingi huu, methali hii inafaa kutupiliwa mbali katika jamii ya kisasa kwa vile wanandoa wanafaa kupendana na kuheshimiana.

**Mf 125**

> **Kinyankole:** *Omukazi akanyampira obwato bya ishezaara ati munda yamawe tuzira emitahe.*
> **Kiswahili:** Mwanamke alijambia mtumbwi wa baba mkwe kisha akasema kwetu ni mwiko kunywa pombe.

Tangu jadi, mwanamke alikuwa na sehemu yake maalum ambayo ilikuwa ni jikoni. Hakufaa kuhudhuria au kujumuika katika mikutano ya wanaume, kwani ilikuwa ni

ishara ya utovu wa nidhamu. Kutokana na utaratibu huu, mwanamke aliyekosa kutii, alijikuta katika matatizo na ndipo sasa tunamwona mwanamke huyu akijambia mtumbwi wa baba mkwe. Isitoshe, methali hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kuwazuia wanawake kujihusisha na masuala nyeti ya kijamii. Hali hii ilionyesha baadhi ya wanawake walivyoandaliwa na kuikubali hali yao duni, van Dijik (1986) na Bourdieu (1991) wanaeleza kwamba miendo ya kijamii inawaandaa watu kukubali au kuangalia unyonge wao kama ukweli wa kimaisha au hali yao ya kawaida. Aidha, Wamitila (2002) anakiri kuwa katika jamii nyingi za jadi, mwanamke huchukuliwa kama mali ya mwanamume anayestahili kumtii mwanamume. Asipofanya hivi, huwa anaangaliwa kama ameharibika kimaadili na kukiuka mienendo ya jamii yake.

Hali ni tofauti katika jamii za kisasa ndiposa, methali hii ilipendekezwa kutupiliwa mbali kwa sababu mwanamke wa kisasa amepewa nafasi sawa na mwanamume na ameweze kujihusisha na masuala nyeti ya jamii, uchumi na siasa. Aidha, ameweza kuhudhuria mikutano mikubwa ya taifa na mataifa tofauti na mtazamo wa kijadi. Kwa msingi huu, methali hii haina mashiko katika jamii ambayo inakua kila uchao.

**Mf 126**

**Kinyankole:** *Omukazi akaferwa Iba ati zambona.*
**Kiswahili:** Mwanamke alifiwa mumewe na kusema zimenikuta.

Mwanamke katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, alikuwa haruhusiwi kuwajibikia familia, hii ilikuwa ni kazi ya mwanamume. Hali hii ilitokana na jamii hii ambayo ilikuwa imejengeka kwenye msingi wa mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa ubabe-dume. Kutokana na hali hii, mwanamke hakuweza kujisimamia wakati mwanamume alipoaga dunia. Aidha, ni kutokana na imani kama hii, tunaona mwanamke alikuwa anarithiwa na ndugu ya mumewe. Hata hivyo jamii ya kisasa, inapinga imani hizi kwa kumpatia mwanamke fursa sawa na mwanamume katika

nyanja tofauti ndani ya jamii. Jambo hili limemwezesha mwanamke kujimudu kimaisha na hata kuweza kuwajibikia familia yake kando na kuwa na mwanamume. Aidha, mwanamke wa kisasa, ana uwezo wa kujiamulia mchumba bila kulazimishwa na utamaduni.

Kwa mujibu wa TGNP (2001), katika bara la Afrika hususani Afrika kusini, wanawake wamewekwa katika kundi la wanyonge na kuachwa nyuma kiasi kwamba bado hawajaifaidi hali ya usawa kama waliokuwa nao wanaume katika kupata huduma mbalimbali za kijamii. Hali hii imepelekea kuchunguza ufaafu wa methali hizi za kijinsia katika jamii ya kisasa ya Wanyankole ili kuwaelemisha wanawake wa Afrika kokote kujua athari zinazowakumba katika maendeleo na namna wanaweza kujaribu kujikomboa. Kwa madai haya, methali Mf 126 haina umuhimu katika jamii ya kisasa na inafaa kutupiliwa mbali.

**Mf 127**

**Kinyankole:** *Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki.*
**Kiswahili:** Ukoo ambao utaisha huwazaa wasichana.

Jamii ya Wanyankole ya kijadi ilikuwa imejengwa katika msingi wa mfumo wa kuumeni. Kwa hivyo, mtoto wa kike hakuwa na nafasi katika jamii hii ukimlinganisha na yule wa kiume. Jamii hii ilimwona mtoto wa kike kuwa hasara kwa familia, kwa madai kuwa alikuwa anaenda kuendeleza ukoo wa jamii nyingine na siyo wao. Kwa upande mwingine, mtoto wa kiume alikuwa wa manufaa kwa sababu aliendeleza ukoo wa baba yake. Kutokana na mawazo haya, kulisababisha majukumu kugawanywa pia kijinsia. Lakini katika muktadha wa kisasa, methali hii itabidi kutupiliwa mbali kwa madai kwamba jamii imepitia mabadiliko mengi na kusababisha jinsia zote za watoto kuwa sawa. Aidha, usawa wa elimu na uchumi umelazimisha jinsia zote kuona mambo tofauti na mtazamo wa kijadi. Kwanza kabisa idadi ya watoto itategemea uwezo wa

wazazi, kumaanisha ikiwa idadi ambayo imezaliwa ni jinsia moja basi itakuwa hivyo. Hali hii inaonyesha kuwa, wazazi wamekubali kuwa jinsia zote za watoto zina manufaa sawa tofauti na mtazamo wa kijadi. Kutokana na kukubali hali hii, imeonyesha kuwa methali hii haina mashiko tena katika jamii hii inayokua kila uchao.

Omari (2008) amechunguza namna mtoto wa kiume na wa kike wanavyochorwa na kushirikishwa katika nyimbo za watoto za Tanzania. Anahitimisha kuwa nyimbo hizo zimemsawiri mwanamke kuwa hana sauti mbele ya mumewe, mzalishaji mali na kiungo muhimu cha malezi ya familia. Mwanamume kwa upande mwingine anaonekana kuwa ndiye mwenye kumiliki mali katika familia, mwenye sauti na mamlaka makubwa katika familia.

Mungonya (1958) anaendelea kusisisitiza hoja hii, kwa kuonyesha jinsi mahakama ya ufalme ilivyotekeleza wajibu wa kuelimisha jamii ya Wanyankole kuhusu maisha na maadili mema. Mbali na kuwa na serikali iliyokuwa utawalani, mahakama ya ufalme ilitekeleza jukumu la utamaduni na elimu rasmi ndani ya ufalme. Tofauti na jinsia ya kike, wavulana kutoka katika familia mashuhuri na ukoo kutoka katika jamii yote walipelekwa mahakamani kujifunza utamaduni pamoja na utawala wa umma. Vijana wa kiume walifunzwa kupigana vita, kupigana miereka, itikadi na itifaki, historia ya kuwinda, nyimbo, uhariri wa mashujaa waliopo na waliokufa zamani. Hali hii ilitokana na kuwa, jamii hii ilikuwa imejengeka kwenye mfumo wa kuumeni na kuendelezwa kwa msingi wa ubabe-dume pale ambapo mtoto wa kike hakuwa na nafasi katika jamii hii. Kwa hiyo, ikiwa mwanamume alikuwa amewazaa watoto wa kike pekee aliambiwa methali hiyo, kuonyesha alikuwa ameua ukoo wake.

Ukweli ni kwamba, katika jamii ya kisasa, methali hii haina mashiko tena, kwa sababu jinsia zote zimepewa fursa sawa katika uchumi, elimu, utamaduni, na siasa. Kwa mfano

kuhusu suala la ulinzi, wanawake pia siku hizi ni Askari polisi na jeshi, kwa hivyo kile mwanamume anafanya pia mwanamke anaweza kukifanya. Aidha, ni kutokana na mwamko huu mpya, ambapo Wanaufeministi wa Kiafrika wanapenda kumwona mwanamke anapata usawa na mwanamume kwa kuvunja minyororo ya utamaduni ya udunishaji. Katika kusisitiza hoja hii ya kutupilia mbali methali hii, tunawaona Mutungi (2009) na Servranckx (2009) wanaeleza kwamba mfumo dume umekabiliwa na itikadi kali za kimapinduzi pamoja na harakati imara za kifeministi, kiasi kwamba mfumo huo umeanza kubadilika na kuonekana dhaifu, hususan katika muktadha wa fasihi au sanaa kwa ujumla. Kwa kuwa mamlaka na itikadi huendelezwa na/(au) kupingwa kupitia kilongo (van Dijk, 1995; Wodak na Meyer, 2001; Lazar, 2007), hadhi za mwanamke na mwanamume zinabainika katika lugha ambayo kila mmoja wao anatumia katika utangamano na mahusiano yao mazuri, tofauti na mtazamo wa kijadi ambao jamii ilishikilia kuwaenzi watoto wa kiume tofauti na wale wa kike.

**Mf 128**

> **Kinyankole:** Enkoni eteire mukabaro ku'ogibona ogirenzya orugo.
> **Kiswahili:** Fimbo iliyotumiwa kumpiga mke mwenza, ukiipata unaitupa nje ya zizi.

Katika jamii ya Wanyankole ya kijadi, wanawake walitarajiwa kuwa watiifu kwa waume wao. Kwa hivyo, mwanamke aliyeenda kinyume na matarajio ya jamii alikuwa anachukuliwa hatua kali ya kupigwa viboko au hata kupewa talaka. Aidha, mke mwenza alipoona kiboko ambacho kilikuwa kimetumiwa kumpiga mwenzake, aliingiwa hofu na uoga na kukitupa mbali. Tofauti na jamii ya kisasa, mwanamke hapigwi tena kutokana na mwamko mpya wa usawa ndani ya jamii. Wanaufeministi wa Kiafrika wamejitokeza kwa kupinga vikali desturi za kumdhalilisha mwanamke katika jamii za Kiafrika. Uke wenza ulikuwa ni njia moja ya kuendeleza utawala wa mwanamume katika jamii nyingi za kijadi barani Afrika.

Hali ni tofauti katika jamii ya kisasa kwa vile mwanamke ana uwezo wa kuyakimu mahitaji yake na kwa hivyo si lazima avumilie uke wenza iwapo hafurahishwi na ndoa hiyo. Kulingana na Wanaufeministi, mtu hawezi kuwa na uhusiano mzuri wa kimapenzi akiwa hana nguvu katika uhusiano huo au akiwa anaangaliwa kama mali ya mtu mwingine (Margaret, 2004). Wanasisitiza kuwa mapenzi ya kisasa yanadai ushirikiano kati ya mwanamke na mwanamume katika ugawanyaji wa madaraka katika jamii.

Kwa hivyo, methali katika Mf 128 inafaa itupiliwe mbali kwa vile inaelekea kupoteza maana katika jamii ya kisasa ambapo dhuluma za kijinsia zinapingwa na watetezi wa haki za kibinadamu. Baadhi ya mashirika ya utetezi wa wanawake nchini Uganda na kwingineko ni kama vile Centre for Rights Education and Awareness (CREAW), Women's Human Rights Defenders Uganda (WHRDN-U), Association for Women's Rights in Development (AWID), Women Democracy Network(WDN), National Union of Women with Disabilities of Uganda (NUWODU). Kuwepo kwa mashirika haya, kumethibitisha kuwa jamii imepata mwamko mpya na methali hii haina ufaafu katika jamii hii tena.

### 6.4 Hitimisho

Sura ya sita ilihusu uhakiki wa methali za kijinsia kimaana miongoni mwa Wanyankole. Aidha, sura hii imetokana na uainishaji uliofanyika kuhusu methali 42. Methali hizi ziligawanywa katika makundi matatu yaani: Kundi la kwanza limehusu methali za kijinsia (08), ambazo zilipendekezwa kuhifadhiwa kutokana na umuhimu wake katika jamii zote mbili za Wanyankole; kundi la pili limehusu methali za kijinsia (24) zilizopendekezwa kufasiriwa upya ili kuafikiana na matarajio ya jamii ya kisasa inayokua kila uchao na hatimaye kundi la tatu limehusu methali za kijinsia (10), ambazo zilipendekezwa kuondolewa kabisa katika jamii ya kisasa kwa sababu hazina

ufaafu kwa msingi huu, tumebainisha kuwa, jamii ya Wanyankole imepata kuathirika kutokana na mwamko huu mpya ndani ya jamii, na kusababisha idadi kubwa ya methali hizi kufasiriwa upya kimaana ili kuafikiana na matarajio ya jamii inayokua kila uchao. Hata hivyo methali nane zilizohifadhiwa, zimeonyesha kuwa jamii ya kijadi ingali na mashiko makubwa katika jamii ya kisasa kuhusu uendelezaji wa utamaduni wake.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Utangulizi

Sura ya sita ilishughulikia ufaafu wa methali za kijinsia katika jamii ya kisasa. Katika sura hii, tumetoa muhtasari, matokeo, mchango na hatimaye mapendekezo ya utafiti huu.

## 7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii imegawanywa katika sura saba. Utafiti ulichunguza, uhakiki wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole: Mtazamo wa Kipragmatiki. Sura ya kwanza ilitupa msingi wa masuala yote yaliyoibuliwa katika utafiti huu kama vile: misingi ya utafiti, usuli wa suala la utafiti, jamii ya Wanyankole, ndoa na familia katika jamii ya Wanyankole, nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii ya Wanyankole, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu ya kuchagua mada, upeo wa utafiti na mwisho ni umuhimu wa utafiti. Masuala haya yalijadiliwa kwa kuzingatia mada ya utafiti.

Katika sura ya pili, tulipitia maandishi na matini mbalimbali yanayohusiana na malengo ya utafiti. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Nadharia ya Udenguzi. Tuliigawa kazi hii katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ilihusu yalioandikwa kuhusu lugha na jinsia. Sehemu ya pili ilihusu yale yaliyoandikwa kuhusu hadhi ya mwanamke na mwanamume ikiwemo kigezo kikuu cha methali za kijinsia.

Sura ya tatu imejadili mbinu za utafiti ambazo ni: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, vifaa vya kukusanya data za utafiti, na pia ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Tulikusanya data kutoka nyanjani

zilizohusu methali za kijinsia. Data iliyohakikiwa imeonyeshwa katika kurasa za viambatisho.

Katika sura ya nne, tuliangazia matumizi ya methali za kijinsia kimuktadha miongoni mwa Wanyankole. Kwa mfano, miktadha tofauti ndani ya jamii ya Wanyankole ni kama vile uchumi, uongozi, utamaduni, dini, elimu, ndoa, kazi, malezi na maadili. Katika kufanikisha zoezi hili, tulichunguza ni kwa namna gani miktadha hii tofauti ilivyojitokeza ndani ya jamii. Sura ya tano ilihusu uhakiki wa methali za kijinsia kimaana katika jamii ya Wanyankole. Kwa kufanya hivi, methali hizi zilichunguzwa namna zilivyoathirika kimaana kutokana na nyanja mbalimbali zilizopatikani ndani ya jamii ya Wanyankole. Hatimaye, sura ya sita iliweka bayana ufaafu wa methali za kijinsia katika jamii ya kisasa. Sura hii imetusaidia kuelewa methali hizi, kwa kuzigawanya katika makundi matatu yaani; kundi la kwanza limehusu methali zilizopendekezwa kuhifadhiwa katika jamii zote mbili za Wanyankole kwa madai zingali bado na umuhimu; kundi la pili limehusu methali zilizopendekezwa kudenguliwa ili kuafikiana na matarajio ya jamii ya kisasa, na mwisho ni kundi ambalo limehusu methali zilizohitaji kutupiliwa mbali katika jamii ya kisasa kwani hazina ufaafu tena.

Kwa muhtasari, uhakiki wa methali hizi kwa kutumia kipengele cha udenguzi kwa Mtazamo wa Kipragmatiki umeweka bayana kwamba, methali hizi za kijinsia zimekuwa na mashiko makubwa katika jamii zote mbili kutokana na nyanja mbalimbali ambazo zilipatikana ndani ya jamii hii. Aidha, nyanja hizi zimesaidia kuonyesha, namna maana mbalimbali inavyoweza kujitokeza katika methali hizi kimatumizi.

Hata hivyo, baada ya methali hizi kudenguliwa, iliweka wazi kuwa methali hizi zilikuwa na umuhimu katika jamii ya Wanyankole kwa sababu zilikuwa zinaleta umoja, ushirikiano, amani na maendeleo katika jamii.

## 7.2 Matokeo ya Utafiti

Katika sehemu hii matokeo ya utafiti yamegawika katika sehemu kuu tatu, ambapo kila lengo limeangaziwa kwa mujibu wa matokeo yake. Katika utafiti huu kulikuwa na malengo matatu kama inavyojidhihirisha.

### 7.2.1 Matokeo kuhusu kupambanua methali za kijinsia ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii

Katika lengo la kwanza, matokeo ya utafiti yalijikita katika methali za kijinsia ambazo zilipatikana ndani ya jamii ya Wanyankole. Ilifahamika, methali hizi zilikuwa zinatungwa kwa mfumo wa kuumeni, kwani ni jamii ambayo ilikuwa imempatia mwanamume hadhi ya juu kuliko mwanamke. Aidha, methali hizi zilitungwa wakati jamii ya Wanyankole ilipokuwa na ardhi ya kutosha, idadi ya wanajamii ilikuwa ndogo ukilinganisha na ya kisasa, vyakula vilikuwepo kwa wingi, na ng'ombe wa kurithisha watoto walikuwepo kwa wingi pia, tofauti na jamii ya kisasa ambayo imejiendeleza kiuchumi, kielimu, kisiasa, kitamaduni, kidini na kindoa na kusababisha uhaba wa amali hizi.

Uhaba wa amali hizi na kuwapo usawa katika jinsia zote, umechangia mengi kubadilika ndani ya jamii ya Wanyankole wa kisasa. Kutokana na msingi huu, methali hizi zilichukua mkondo wa kumwona mwanamume kama mtu aliyekuwa anajipenda na kujitakia mazuri kuliko mwanamke katika jamii. Hili limeweza kuthibitishwa kutokana na nyanja mbalimbali, zilizopatikana ndani ya jamii kama vile; uongozi, uchumi, ndoa, dini, elimu na utamduni ambapo mwanamume alikuwa amepewa kipaumbele kihadhi

kuliko mwanamke. Kwa mfano katika nyanja ya ndoa na kazi, mwanamume alionekana kupewa kazi za kihadhi kuliko mwanamke. Kwa mfano alikuwa ni kiongozi, hakimu, mlinzi wa usalama, shujaa kutokana na vita alivyoshinda na kazi za kuwinda. Hii ilikuwa ni tofauti na jinsia ya kike ambayo ilikuwa na kazi ya kuzaa na kulea, kupika, kulima, kudumisha usafi na kumfurahisha mwanamume kingono. Aidha, ni kutokana na ukosefu wa usawa katika mgawanyo wa kazi, ambao umechangia methali hizi kupambanuliwa katika jamii ya Wanyankole kwenye nyanja maalum za jamii, ili kutambua iwapo mwanamume wa kisasa angali anapewa hadhi hiyo ya kijadi au la katika jami hii inayokua kila uchao.

### 7.2.2 Matokeo kuhusu uhakiki wa maana na matumizi mbalimbali ya methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole

Kuhusu lengo la pili tulibainisha kwamba kadiri ulimwengu unavyoendelea kukua, ndivyo fasihi inavyoendelea kukua kwa kasi hiyohiyo, na vilevile ndivyo jamii zinavyopata mwamko mpya kutokana na ulimwengu unaokua kwa kasi kiuchumi, kisiasa, kielimu, kindoa, kidini na kitamaduni. Mengi yamebadilika ndani ya jamii ya Wanyankole na kulazimisha baadhi ya methali hizi kufasiriwa upya kimaana na kimatumizi katika nyanja mbalimbali ndani ya jamii hii. Hili limetokana na jamii ya kisasa kuongezeka kiidadi, ardhi, ng'ombe na vyakula kupungua na jinsia zote zimeweza kupata fursa sawa ndani ya jamii, jambo ambalo limeleta mwamko mpya ndani ya jamii ya Wanyankole. Aidha, kutokana na hali hii imelazimu methali hizi kuchanganuliwa upya kimaana, kimatumizi na kimuktadha ili kuthibitisha ikiwa methali hizi kimaana zingali na mtazamo wa kijadi au la kutokana na jamii ya kisasa inayokua kila uchao.

### 7.2.3 Matokeo kuhusu tathmini ya uamilifu wa methali za kijinsia katika jamii ya Wanyankole

Katika lengo la tatu, tumetambua mwamko mpya ndani ya jamii hii umesababishwa na jamii ya kisasa ambayo imepata fursa sawa katika kila nyanja ndani ya jamii. Jambo hili, limeiwezesha jamii ya kisasa kujimudu kimaisha tofauti na jamii ya kijadi ambayo ilikuwa imemtweza mwanamke kwa kila hali. Aidha, ni vizuri kutambua hizi ni jamii mbili tofauti, ambazo mitazamo yake kuhusu maisha ni tofauti kutokana na mabadiliko mengi yanayopatikana ndani ya jamii na ulimwengu kwa jumla. Kwa hivyo, kuiwezesha jamii kuendelea kujivunia utamaduni wao kupitia kigezo cha methali, imelazimu kutathimini uamilifu wa methali hizi za kijinsia katika jamii ya kijadi na kisasa miongoni mwa Wanyankole. Hili likishafanyika, tutaweza kubainisha ufaafu wa methali hizi za kijinsia katika jamii ya kisasa inayokua kila uchao.

Kutokana na utafiti huu, imegunduliwa kuwa jamii hizi mbili tofauti, zimekubaliana kuhusu baadhi ya methali hizi kuhifadhiwa, kudenguliwa, na hatimaye zingine kuondolewa kabisa kwenye jamii kwa sababu hazina umuhimu tena katika jamii ya kisasa ambayo imepata mwamko mpya. Aidha, wamezingatia kuwa ni muhimu kuhifadhi na kudengua baadhi ya methali hizi kwa minajili ya vizazi vya leo na vijavyo. Kwa kufanya hivi, wamekinufaisha kizazi hiki na hivyo kufaidika kutokana na kipengele hiki cha fasihi simulizi katika jamii hizi mbili tofauti za Wanyankole.

### 7.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umechambua namna mwanamume alivyochukua majukumu na nafasi muhimu katika jamii na kumwachia mwanamke majukumu hasi na nafasi duni. Jambo hili ni wazi hasa pale mwanamume anapotambuliwa kama kiongozi, hakimu na mlinzi na anayetegemewa katika ushauri wa jamii. Kwa msingi huu, utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa sababu utasaidia katika kuboresha ugawaji wa mali za jamii kwa usawa

na kimajukumu katika jamii ya Wanyankole na jamii nyinginezo ambazo zinaendeleza ujinsia katika shughuli za kila siku.

Utafiti huu kitaalumu, utachangia katika kuwezesha vigezo vingine vya fasihi ambavyo havijaweza kutumiwa katika utafiti huu kutumika kama vile vitandawili, nyimbo, ushairi, ngano, vivugo ili kuonyesha namna kipengele cha ujinsia kinavyoweza kujitokeza katika jamii tofauti bila hata kutumia methali za kijinsia. Aidha, tutakuwa tunaendeleza kipengele cha fasihi simulizi kama kipera cha fasihi, na kuona mchango wake katika kuelimisha jamii ya Wanyankole, kuhusu namna methali za kijinsia zilivyopata kubadilika katika awamu hizi mbili tofauti na kusababisha mwamko mpya. Hata hivyo mwamko huu mpya katika jamii ya Wanyankole, utawezesha jamii zingine duniani kubadili mtazamo wao kumhusu mwanamke kwa kupitia kipera cha methali au tanzu nyingine za fasihi simulizi. Kwa msingi huu, mchango wa kutumia vigezo vingine vya fasihi simulizi vitawezesha utanzu huu kutumika kwa upana kuhusiana na masuala tofauti ndani ya jamii, jambo ambalo litafanya taaluma ya Kiswahili kueleweka na kutumika zaidi ulimwenguni.

Pia, utafiti huu utachangia katika kuelewa namna nadharia za fasihi zinavyoweza kutumika katika kazi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu, utafiti huu umetumia nadharia mbili ikiwemo Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na ile ya Udenguzi katika kuangazia suala la ujinsia katika methali za Wanyankole. Aidha, utafiti huu utatoa changamoto kwa wanafasihi, kuweza kutumia nadharia nyingine katika kuhakiki suala la ujinsia katika taaluma mbalimbali za Kiswahili. Nadharia hizi zimekuwa za manufaa zaidi katika kuweka wazi namna ujinsia unavyojitokeza katika jamii ya Wanyankole. Kwanza kabisa, Nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika imeweka bayana jinsi mwanamke katika jamii hii, alivyokuwa amedunishwa kutokana na mfumo wa kuumeni ulioendelezwa kwa ubabe-dume pamoja na utamaduni uliomchora mwanamke kuwa

mtu dhaifu na duni. Aidha, Nadharia ya Udenguzi ilisaidia kudengua au kubomoa methali hizo, kimaana zaidi na kimatumizi katika kurejelea nyanja mbalimbali ndani ya jamii. Kwa hiyo, kutokana na nadharia hizi, jamii za Waswahili na nyinginezo ulimwenguni zinaweza kutumia nadharia hizi au nyingine katika kujibu masuala nyeti ndani ya jamii zao kando na suala la methali za kijinsia.

Mwisho, utafiti huu utatoa mchango wa kitaaluma kwa kuonyesha jamii yenye mwamko mpya kuhusu mwanamke wa kisasa, tofauti na yule ambaye jamii ya kijadi ilikuwa inamtazama. Mwanamke wa kisasa ameweza kugombea nafasi sawa na mwanamume katika jamii, na kufanya kazi bora kuliko mwanamume, tofauti na namna utamaduni ulivyokuwa umemdunisha. Utafiti huu utawezesha jamii nyingi kumtazama mwanamke kama kiumbe mwenye uwezo sawa na mwanamume. Kwa hivyo, fursa ambazo jinsia ya kike imepewa katika karne hii, ni mojawapo ya kuonyesha usawa na maendeleo katika jamii nyingi za Kiafrika. Tumeshuhudia namna wanawake wamekuwa marais, walimu, wabunge, walimu, madaktari, wanamuziki, wajenzi, mahakimu, madereva, wakulima na hata wafanyabiashara mashuhuri tofauti na jamii ya kijadi. Ni kutokana na mwamko huu tunaona wanaufeministi wanachangamkia juhudi za mwanamke katika karne 21.

**7.4 Hitimisho**

Sehemu hii imegawika katika sehemu tatu ambazo ni: matokeo, mchango na mapendekezo ya ufafiti. Sehemu ya matokeo ya utafiti imepambanua matokeo ya utafiti kwa kuzingatia kila lengo la utafiti. Katika sehemu ya mchango wa utafiti nimeangazia mchango wa kitaaluma ambao unatokana na matokeo ya utafiti huu. Sehemu ya mapendekezo inafafanua kile tafiti za siku za usoni zinaweza kuchunguza hasa kutokana na mahitimisho ya utafiti huu.

## 7.5 Mapendekezo ya Utafiti

Katika utafiti huu tumeonyesha namna methali za kijinsia zilivyokuwa zinatumika katika jamii ya Wanyankole katika shughuli tofauti zilizopatikana ndani ya jamii. Kigezo kikuu kilikuwa kuona namna, maana na matumizi ya methali hizi inavyojitokeza katika nyanja tofauti kama vile uchumi, siasa, elimu, dini, ndoa, kazi, na utamaduni. Kwa msingi huu, methali hizi zilihakikiwa kipragmatiki kwa kuzingatia muktadha wa jamii ya Wanyankole ya jadi na ya kisasa. Aidha, kutokana na msingi huu, tunapata mapendekezo yafuatayo ya utafiti wetu.

Kwanza, utafiti huu umejikita katika kushughulikia methali za kijinsia ndani ya jamii ya Wanyankole. Kwa hivyo, itakuwa bora ikiwa tafiti nyingine za usoni zitaweza kutumia vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile vitendawili, nyimbo, hadithi, ushairi, ngano na mafumbo kuonyesha namna ujinsia unavyoweza kujitokeza katika jamii zingine za Kiafrika tofauti na ile ya Wanyankole.

Pili ni muhimu kuelewa, tofauti ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika na Udenguzi zilizotumika katika kufasiri upya methali za kijinsia za Wanyankole, tafiti za usoni zinaweza kutumia nadharia zingine za fasihi kufasiri upya kipengele cha ujinsia katika vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile nyimbo, ngano, ushairi na vitendawili.

Hitimisho ni kwamba, kuna baadhi ya methali za kijinsia ambazo zingali na ufaafu katika jamii ya kisasa ya Wanyankole na kwa hivyo ni vyema zikihifadhiwa kwa madhumuni ya jamii ya kisasa na ile ijayo. Imebainika kuwa, methali nyingi za Wanyankole ziliathirika kutokana na mfumo wa kuumeni ambao uliendeleza ubabe-dume katika nyanja zote za jamii na kumwona mwanamke kuwa kiumbe duni. Ni kwa msingi huu, baadhi ya methali hizi zilipata kuathirika kimuktadha, kimaana na kimatumizi na kubidi kudenguliwa ili ziweze kukubalika katika jamii ya kisasa. Ni

kutokana na kudenguliwa huku tunaona baadhi ya methali zinaathirika na kuondolewa kabisa katika jamii zote mbili za Wanyankole.

## MAREJELEO

Akivaga, S. K., & Odaga, A. (1982). *Oral literature: A school certificate course*. Heinemann Kenya, Books.

Alex, N. (1990). *Fasihi Simulizi*. Maandalizi ya K.C.S.E: Nairobi- Kenya.

Alexander, S. (1987). *Efumu Omurunyankole Rukiga, Omuhanda*. Mbarara: Gokumanya Publishers.

Alster, B. (1993). *Proverbs from Ancient Mesopotamia*: The History and Social Implications.

Arthur, R. (1969). African Literature V: Novels of Disillusion. *Journal of Commonwealth Literature*, *6*, 250-255.

Babbie, E. (1992). The Practice of Social Research . Belmont, CA: Wadsworth *Journal of MultiDisciplinary Evaluation*, *4*(7), 112-314.

Bamgbose, O. (2006). "Customary Law Practices: The Position Under the Nigerian Legal System". Katika F. Munaaba (Mh.). *Women's Rights and Violence: Global Challenges.* Kampala: Department of Women and Gender Studies, Makerere University.kur.86-113.

Beauvoir, S. D. (1949). 1989. The second sex. *Trans. HM PARSHLEY. New York, Vintage Books*.

Bernard, J. (1972). *The Sex Game*. New York: Antheneum

Bertoncini- Zubkova, Elena (ed.). (1996). *Vamps and Victims. Women in Modern Swahili Literature*. Koln: Koppe

Bloor, M., & Bloor, T. (2007). *The Practice of Critical Discourse Analysis: An Introduction.* London: Hodder Arnold.

Bobbie, E. (1999). *The Basics of Social Research.* London: Wardsworth Publishing

Bourdieu, P. (1991). *Language and Symbolic Power*. Cambridge: Policy Press.

Cameron, D. (1992). *Feminism and Linguistics Theory*. London: Palgrave Macmillan.

Carter, D. (2006). *The Pocket Essential: Literary Theory. Herts:* Cox &Wyman Ltd.

Chafetz, J., & Doyle, J.A, (1974). *Masculine / Feminine or Human?* Itasca, IL: Peacock Publishers

Chomba, E. (2005). *Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Kikuyu*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Cisternino, M. (1987). *The proverbs of Kigezi and Ankole*. Kampala: Fountain Publisher.

Coates, J. (1993). *Women, Men and Language: A Sociolinquistic Account of Sex Difference in Language*. London: Longman Group.

Coates, J. (2004). *Women, men and language*. London: Pearson/Longman.

Coser, L. (1963). *Sociology through literature: an introductory reader*. Englewood Cliffs: Prentice Hall

Denham-Vangham, J., & Edmond, V. (2010). The Value of Silence, *Gestalt Journal of Austalia and Newzealand*, Juz. 6(2):5-19.

Denoon, D. (1971). *History of Nkore in Western Uganda to 1896*. Oxford: Cleredon Press.

Derrida, J. (1981). *Deconstruction Theory: Gerd Zacher Encounter* Rotterdam: The Netherlands pubishers.

Dery, I. (2015). BridePrice and Domestic Violence: Empirical Perspective from Nandom District in the North Western Region of Ghana". *Journal of Development and Sustainability*, Juz, 4 (3):258-271.

Eagleton, M., & Mufin, R.C. (1991). *Feminine Literary Criticism*. London: Longmann Group Limited. Educational Publishers.

Eagly, A.H. (2009). The *His* and *Hers* of Prosocial Behaviour: An Examination of the Social Psychology of Gender. *American Psychologist*, Juz 64: 644-658

Edward, J. (1985). *Language, Society and Identity*: Oxford Basil and Blackwell

Eisenchlas, S. A. (2013). Gender roles and expectations: Any changes online?. *Sage Open*, *3*(4), 2158244013506446.

El-Maawy, A. (2011). *Jawabu la Mwanakupona. Mausio ya Mke wa Kisasa na Wasiya wa Mwana Kupona*. Dar es Salaam: Taasis ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Engels, F. (1975). *The Origin of the Family Private Property and the State.* New York: Pathfinders Press Inc.

Evans, P. (2010). *The Verbally Abusive Man*: Can He Change? Massachusetts: Adams Media

Ferguson, K. (2002). "Silence-A Poliyics." *Contemporary Political Theory,* Juz. 1:1-17

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.

Fisher, J. (1958). Social influence on the choice of a lingustuistic variant. In D. Hymes (ed) (1964). *Language in culture and society* New York: Harper and Row.

Fonchingong, C.C. (2006). Unbending Gender Narratives in African Literature". *Journal of Women's Studies.* Juz. 8 (1):135-147.

Friedan, B. (1963). *The feminine mystique.* New York: Norton.

Geoff, R. (2007). *Taking the Proverbial*. New York: Oxford, University press.

Graddol and Swann. (1989). *Renewing Gender*. Kampala: Fountain Publishers.

Greville, C. (1982). *Gender*: Published in Great Britain.

Hass, M. (1974). *Men's and Women's Speech in Koosati in Language*. 20.pg. 147-149

Holmes, J. (1992). Women's talk in public contexts. *Discourse & Society*, *3*(2), 131-150.

Ifachelobi, J.E. (2014). Feminism: Silence and Voicelessness as Tools of Patriachy in Chimanda Adiches's 'Purple Hibiscus..*African Research Review,*-Juz. 8(4):30-48.

Irib, World Service. (2014). *Matatizo ya Wanawake katika Ulimwengu wa Magharibi.* Katika http://www.kiswahili.irib.ir/38823

Iribemwangi, P., & Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers Ltd

Izugbara, C. O. (2005). Hypothesis on the origin of hegemonic masculinity. *Sexuality in Africa Magazine*, *2*(1), 13-14.

Jeniffer, (1975). The dictionary of feminist theory. In *The dictionary of feminist theory*. Edinburgh University Press.

Joon, Y. (1992). *Methali kama falsafa ya Maisha: Uhakiki- Linganishi wa Methali za Kikorea na za Kiswahili*. Nairobi Press.

Joro, V. (2016). *Gender and Domestic Violence: Narrative Analysis of Social Construction of Gender in Uganda.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Jyvaskyla, Helsinki.

Kanu, I. A. (2014). Kinship in African Philisophy and the Issue of Development. *Internal Journal of Humanities, Social Sciences and Education, Juz. 1(9): 1-6*

Kaye, D. K., Mirembe, F., A. M., Bantebya, G., & Johansson, A. (2005b). "The Implication of Bride Price on Domestic Violence and Resproductive Health in Wakiso District, Uganda." *African Health Sciences,* Juz. 5 (4): 300-303.

Kelly, K. A. (2003). *Domestic Vilence and the Politics of Privacy*. Londo: Cornell Univwersity Press.

Kibigo, M. (2019). Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo ya Waisukha Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Kisemantiki. *(*Tasnifu ya Uzamifu ambayo imewasilishwa kwa *East African Journal of Swahili Studies,* 4(1), 2019

Kimani, C. (2003). "Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Kinge'ei, G.K. (2015). *Mwongozo wa "Mama ee"* ( Mwachofi.1987). Nairobi: East African Educational Publishers.

Kipury, N. (1983). Oral literature of the Masaai. Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd.

Kirindi, P.G.N. (2008). *History and Culture of the Kingdom of Ankole* Kampala: Fountain Publishers

Klein, P. (1971): "Men's and Women's Language." *The American Catholic Sociological Review* 5:218-23.

Kramer, C. (1974). "Perceptions of Male and Female Speech". *Language and Speech*. 20:151-618.622

Lakoff, R. (1975). *Language and Woman's Place*. New York: Harper Colophon Books.

Larsen, M.M. (2016). "Theoretical and Empirical Perspectives on Intimate Partner Violence". Health Inequities Related to Intimate Partner Violence Against Women, Social Disparities in Health and Health Care. Zurich: Springer Internatonal Publishing. DOI 10.1007/978-3-319-29565-7-2 Inapatikana katika https://www.google.com/search?client=Larsen%2C+M.+M.+%282016%29%E2%80%9CTheoretical+and+Empirical+Perspectives+on+Intimate+Prtner+Violence%E2%80%9D. Ilisomwa tarehe Septemba 2019.

Lazar. M.M. (2007). Feminist Critical Discourse Analysis: Articulating a Feminist Discourse Praxis". *Critical Discourse Analysis Sudies*, Juz. 4 (2): 141-164.

Litosseliti, L. (2008). *Sex and Gender, 2nd Edition*. Oxford: Blackwell PublisherLtd.

Lubuuka, Y. (2010). "*Usawiri wa mwanamke katika Methali za Wanyankole*." Uganda: Tasnifu MA. Islamic University (Haijachapishwa).

Madumulla, J. (1981). *Proverbs and Sayings*: *Theory and Practice*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Maganga, J. (2000). *Functions of Proverbs among the Abhakwaya People with focus on Proverbs of Ordinary Advice*. *B.A (With Education) degree dissertation.* Dar es Salaam: Department of Literature. University of Dar es Salaam (unpublished).

Maingi, R. (2005). "The Kenyan Constitutional Reforms Process" A Case Study on the Work of PIDA Kenya in Securing Womens Right' *Feminist Africa* 63,66.

Maitaria. J.N. (2019). "Methali za Kiswahili kama Wenzo wa Kunainisha Falsafa ya Kiafrika kuhusu Familia". Katika A.S. Ponera na Z.A.Badru (Wah.) *Koja La Taaluma za Insia.* Dar es Salaam: Karljamer Publishers. Kur. 435-458.

Malenga, M. (2012). *Matumizi ya lugha katika Fasihi Simulizi*. Mwanza: Inland Press.

Maltz, D.N., & Borker, R.A. (1982). "A Cultural Approach to Male-Female Miscommunication"in Gumperz, J.J. (ed). *Language and Social Identity.* Cambridge Univwesity Press.

Margret, L. (2004). *Sociology, Understanding a Diverse Society,* USA: Wads Worth\ Thomson Learning, Belmont, CA 94002-3098

Matembe, M. (2009). *Woman in the eyes of God Reclaiming a lost Identity.* New Life Publishers Kampala-Uganda.

Mello, R.A. (1999). Narrating Gender. Children's Response to Gender Roles Despicted in Orally told Folktales and Other Traditional Stories. P.h.D Dissertation. Lesley College.

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa Wa Isimu, Fonetiki, Fonolojia Na Mfolojia Ya Kiswahili,* Nairobi –Kenya: Longhorn publishers

Miller, J. (1976). *Towards a new psychology of women*. Boston: Beacon Press.

Millet, K. (1969). From sexual politics: Theory of sexual politics. *Feminist theory: A reader*, 218-219.

Millet, K. (1979). *Sexual Politics*. New York: Garden City.

Mnenuka, A. (2001). Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Feva: Tanzania

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (1998). Usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili kama ilivyobainika katika Ushairi wa Kiswahili, Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Momanyi, C. (2000). Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Fasihi ya Kiswahili, Dar es Salaam: Department of Literature.

Morris, H. (1914). *History of Nkore* EALB. Kampala: Fountain Publishers.

Mosha, E.S. (2013). *Discourse Analysis of Gender- based Violence in Contemporary Kiswahili Fiction: A Case of Selected Novels of the Past Three Decades (1975-2004) and Young Tanzania' Intepretations. Tasnifu ya Uzamili* (Haijachapishwa). University of Waikato, New Zealand.

Mugo, E. (1982). *Kikuyu People. Brief outline of Their Customs &Traditions*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mugonya, C. (1961). *The Proverbs of Kigezi and Ankole*. Uganda: Gokumanya Publishers.

Mugonya, Z. (1958). *A History of Ankole.* Kampala: Fountain Publishers

Mulokozi, M. (1982). Protest and Resistance in Swahili Poetry 1660-1885. katika *Kiswahili* 45 (1), 25-24.

Murfin, R. C. (1991). Feminist Criticism and The Scarlet Letter. In *Nathaniel Hawthorne* (pp. 275-303). Macmillan Education UK.

Muthengeki, S.B., Kule, S., & Naeemah, A. (2012). "An Exploratory Study of Bride Price and Domestic Violence in Bundibugyo District, Uganda." A Research Report by Centre for Human Rights Avancement (Uganda). South African Medical Research Council- Gender and Health Research Unit. Ilifadhiliwa na International Centre for Research on Women (ICRW). Inapatikana katika https:www.google.com/url?g=http://196.21.144,194/gender>bridepricedomesticviolence.pdf. Ilisomwa tarehe 8 Januari 2020

Mutungi, B. (2009). Wahusika Wanume kama Kielelezo cha Udume katika Tamthilia za Chacha Nyaigoti- Chacha. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Makerere, Kampala.

Mwachofi, A.K. (1987). *Mama ee.* Nairobi: East African Educational Publishers

Mwamzandi, L. (2013). "Riwaya teule za karne ya ishirini na moja na udurusu Wa nadharia za fasihi". *Swahili Forum* 20:48-66.

Nandwa and Bukenya, A. L. (1992) Gender and Ideology: The Cultural Context Paper presented at AWORD Seminar.

Ndalu, A., & Kingei, K. G. (1999). *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd

Ndulute, C. (1987). *Notes on African Proverbs. Diffusion Morpholpgy & Transmutation* (unpublished article).

Ndungo, C. (1985). Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ngugi, F. (1975). *The Changing Image of Women over Three Crucial Historical Phases.* Nairobi: Kenya Literature Bureau

Njogu, K., & Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.

Ntaragwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi,* Augustana College: Rock Island.

Odimegwu, C.O. (2006). Epidimiology of Gender –based Violence in Nigeria". Katika F. Munaaba (Mh.) *Violence: Global Challenges*. Department of Women and Gender Studies, Makerere University, kur. 68-85

Oduyoye, M. A. (1998). Women, culture and Theology: A foreword. *Women, Culture and Theological Education*, 31-7.

Okpewho, I. (1992). *African oral literature: Backgrounds, character, and continuity* (Vol. 710). Indiana University Press.

Omari, S. (2008). Fasihi simulizi na jinsia. Katika *Kiswahili Juzuu* (71), Dar es Salaam: TUKI.

Oqudipe, L. (1987). *The Female Writter and Her Commitment.* London. Routledge.

Reik, T. (1945). "Psychology of Question Intonation and sex Roles" Katika *Psychological Bulletin* Vol, 33 No.3 1979 610-61

Richard na wenzake, (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Sai Industries Ltd.

Rorty, R. (1996). *Deconstruction and circumvention*. The University of Chicago Press

Rwegoshora, H. M. (2006). A guideline to social science research. *Mkuki and Nyota, Dar es Salaam. Tanzania*.

Sawe, A., Makoti, V. na Obuchi,, S.M. (2018). Uhusiano Mwema kati ya Mke na Mume kama njia ya Kudumisha Ndoa: Mifano kutoka *Utendi wa Ayubu.*

Schmitz, T.A. (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: An Introduction* Maiden: Blackwell Publishing

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na Jamii.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Servanckx, P. (2009). *Deconstruction Partriarchal Society through Literature: Angela Cartet and the 'Demythologising Business'.* Tasnifu ya Umahiri. (Haijachapishwa). Ghent University, Ghent, Belgium.

Sokoloff, N. (1980). *Between Money and Love*. New York: Praeger.

Steady, F.C. (1981). *The Black Women Cross-Culturally*. Cambridge: Schenkam Publication

TGNP (2001). *Usawiri wa Mwanamke katika Nyimbo za Kizazi Kipya.* Bara la Afrika Kusini mwa Afrika.

Trudgil, P. (1972). Sex, covert prestige and linguistic change in the urban British English of Norwich, in *Language in Society*. Page 179-195.

TUKI (1990). *Kamusi Sanifu Ya Isimu Na Lugha,* TUKI Daresalaam.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Oxford University Press.

Tumusiime, J. (1982). *Entanda Yomugambi Worunyankole Rukiga.* Kampala: Fountain Publishers.

Uchendu, E. (2005). Forthcoming Masculinities and Nigeria Youths. *Nordic Journal of African Studies*

Urlich, H.L. & Cosell, T.B. (2009). *Handbook of Gender Roles.* New York: Nova Sciences Publishers Inc

van Dijk, T.A. (1986). *Racism in the Press.* London: Arnold.

van Dijk, T.A. (1995). "Aims of Critical Discourse Analysis". *Japanese Discourse,*

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake,* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003b). Kazi ya Fasihi: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. (2008). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus publication.

Wamitila, K.W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Kenya: Longhorn publishers Ltd

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia:* Nairobi: Focus Publications Limited.

Wanjiku, K., & Akinyi, N. (1993). *Celebrating Womens's resistance. A case study Of Women Groups Movement in Kenya.* Nairobi: Africa Women Perspective.

Wells-Wilbon, R., & Holland, S. (2001). *Social learning theory and the Influence of male role models on African American children in PROJECT 2000.*

White, M. (1987). *Introduction of Cultural Linguistics of Men and Women.* British Library cataloguinig I publication.

Williady, H. (2013). Mabadiliko kutoksa U-Aristole kwenda Ujadi wa Kiafrika. Tasnifu ya Uzamili katika Fasihi Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa)

Wodak, R., & Meyer, M. (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis*. London: SAGE.

Wollstonecraft, M. (1792). *A vindication of the Rights of Woman*. Boston: Peter Edes.

Woolf, V. (1929). *A Room of One's Own and Three Guineas.* New York: Harcourt

Zakaria, M. Z. (1989). *Methali za Kiswahili*. Kenya: Longhorn Publishers Limited

# VIAMBATISHO

Baadhi ya Data kuhusu Mwanamke katika Methali za Kijinsia.

## Kiambatisho 1: Mwanamke katika Methali za Kijinsia

| KINYANKOLE | | KISWAHILI |
|---|---|---|
| 1. | *Omukazi otamanyire ekimutungire eyiba agikwatisa omukono gumwe* | Mwanamke asiyejua linalomtunza hushika uume wa mumewe kwa mkono mmoja |
| 2. | *Omukazi ayomba azibira omutabani kuragwa* | Mwanamke mgomvi huzuia mtoto wake wa kiume kurithishwa |
| 3. | *Omwana mubi ajumisa nyina* | Mtoto mbaya husababisha mama yake yake kutukanwa |
| 4. | *Omukazi taba Mugyenyi* | Mwanamke hawi mgeni |
| 5. | *Omukazi oine Iba tarya nkonko* | Mwanamke ambaye ana mume hali nyama ya kuku |
| 6. | *Ozara Omwojo tacwa ruganda* | Anayemzaa mtoto wa kiume hakomeshi ukoo |
| 7. | *Omwana oine mukaishe tahwa bunaku* | Mtoto ambaye ana mama wa kambo haishiwi na huzuni |
| 8. | *Omufukazi tagaya mboro* | Mjane hadharau mboro |
| 9. | *Omukazi akanyampira aha bwato bwa ishezaara, ati enda ya maawe tuzira emitaha* | Mwanamke alijambia kwenye mtumbwi wa baba mkwe na kusema ni mwiko kwetu kunywa pombe |
| 10. | *Obwenda kusima omukazi akasa oburo aheekire Iba* | Kupenda kushukuriwa mwanamke alisaga wimbi huku amembeba mumewe mgongoni |
| 11. | *Enaku yotagambire nyoko tetuba* | Tatizo ambalo hujamwambia mama yako halipungui. |
| 12. | *Abana bahwa omumukazi tibahwa mu mushaija* | Watoto huisha mwanamke tumboni ila si mwanamume |
| 13. | *Omukazi tayecwa kizire* | Mwanamke hajikati kizazi |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | *Eziwaterwa nyoko tiziba nkoni* | Viboko ambavyo umepigwa na mama yako si viboko |
| 15. | *Omukazi oraite eka asiga yacuriza* | Mwanamke ambaye ataharibu boma lake hupiga mbinja. |
| 16 | *Omukazi mubi tumwihaho omwana* | Mwanamke mbaya huzai naye |
| 17 | *Omukazi mubi akwita hona* | Mwanamke mbaya hukudhoofisha kwa kila hali |
| 18 | *Omukazi akaferwa Iba ati zambona* | Mwanamke alifiwa mumewe akasema zimenikuta |
| 19 | *Omukazi murungi niwe anyamisiriza Iba* | Mwanamke mzuri ni yule anayembembeleza mumewe kulala |
| 20 | *Omukazi enyerisa biri aine enfuka* | Mwanamke anayejilisha kumbe ana jembe |
| 21 | *Omukazi aba orubaju rwiba* | Mwanamke huwa ubavu wa mumewe |
| 22 | *Omukazi ahinga hamwe na Iba taba mugara* | Mwanamke ambaye analima na mumewe hawi mvivu |
| 23 | *Omukazi ne myende Omushaija nemirimo* | Mwanamke ni nguo, mwanamume ni kazi |
| 24 | *Enkoni eteire mukabaro ku'ogibona ogirenzya orugo* | Fimbo iliyotumiwa kumpiga mke mwenza, ukiipata unaitupa nje ya zizi |

**Kiambatisho 2: Mwanamume katika methali za Kijinsia**

Baadhi ya Data kuhusu Mwanamke katika Methali za Kijinsia

| KINYANKOLE | | KISWAHILI |
|---|---|---|
| 1. | *Omwana bamutinira obushija bwa Ishe* | Mtoto huogopwa kutokana na uume wa baba yake |
| 2. | *Omwana oine Ishe tayekorera nku* | Mtoto ambaye ana baba yake habebi kuni |
| 3. | *Taaha omwasho teba rwango* | Kwenda nyumbani kwa baba yako si chuki |
| 4. | *Emirimo mingyi ekazibira Bigyemano kutobora omukazi* | Kazi nyingi zilimzuia Bigyemano kutoa bikra ya mwanamke |
| 5. | *Ahu bashaija batari abakazi bacwa emanja* | Pasipokuwapo wanaume wanawake hutoa hukumu |
| 6. | *Empisi ekagira eti kumbugana omushaija ashendekyerize ondiijo nteera mpunga, nkimbugana omukazi ashendekyerize ondiijo nsheka nkaba* | Fisi alisema kwamba akimkuta mwanamume akimsindikiza mwanamume mwenzake hujificha, lakini akimkuta mwanamke akimsindikiza mwanamke mwenzake hucheka na kuvunjika mbavu. |
| 7. | *Meeme meeme tezaza mwojo* | Kubembeleza hakuishi kumzaa mtoto wa kiume |
| 8, | *Abashaija tibabagaya* | Wanaume hawadharauliwi |
| 9. | *Nyineeka atutuka narya obuhoro* | Mwenye boma hutokwa jasho akila kiporo |
| 10. | *Omwana wobwengye nahangura ebyaishe* | Mtoto mwerevu hurithi mali ya baba yake |
| 11. | *Omushaija tahinduka omubigambo ahinnduka ahakitanda kyonka* | Mwanamume habadiliki katika usemi wake ila katika kitanda tu |
| 12 | *Ibega tiringana na omutwe* | Bega halilingani na kichwa |
| 13 | *Nyineeka kuagaba omukazi tamugarukamu* | Mwenya nyumba akiongea mwanamke hamjibu |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | *Omwana oine Ishe akira enaku ezakumwitsire* | Mtoto ambaye ana baba yake huepukana na majonzi ambayo yangemuua |
| 15 | *Eka effire nyineeka ayetondera abana* | Boma ambalo limekufa mwenye boma huwaomba watoto msamaha |
| 16 | *Oruganda rurachwekye ruzara abaishiki* | Ukoo ambao utaharibika huwazaa wasichana |
| 17 | *Kiburwa ente kiburwa omukazi* | Akosaye ng'ombe humkosa mke |
| 18 | *Okukunda akuha ente atayenda kuofa akuha omukazi* | Akupendaye hukupa ng'ombe asiyetaka ufe hukupa mke |

**Kiambatisho 3: Maswali ya Mahojiano Kwa Wasailiwa Kumi na Wawili (12)**

Kinyankole: *Sebo/Nyabo ngambira enfumu zo bushaija nabukazi nizimanyishakyi omubanyakole.*
Kiswahili: Bwana/Bibi eleza dhana ya methali ya kijinsia katika jamii ya Wanyankole.

Kinyankole: *Sebo/Nyabo ngambira obukomoko bwa Wanyankole.*
Kiswahili: Bwana/Bibi, nieleze asili ya jamii ya Wanyankole.

Kinyankole: *Sebo/Nyabo gamba ahabwenkyi omwana womwishikyi akaba atakuzwa nko womwojo ombanyankole.*
Kiswahili: Bwana/ Bibi eleza ni kwa sababu gani mtoto wa kike alikuwa analelewa tofauti na wa kiume katika jamii ya Wanyankole.

Kinyankole: *Sebo/ Nyabo Enfumu zikaba zine mugashokyi omumagara ga Banyankole?*
Kiswahili: Bwana/ Bibi je, methali za kijinsia zilikuwa na umuhimu gani katika maisha ya jamii ya Wanyankole?

Kinyankole: *Sebo/ Nyabo Omukutekateka kwawe, nojira ezi enfumu zikaba zina obwinganisa omumuka ga Banyankole ninga? Hayo enshonga zawe*
Kiswahili: Bwana/ Bibi kutokana na kuelewa kwako, je methali hizi za kijinsia zilikuwa na usawa ndani ya jamii ya Wanyankole? Toa sababu zako.

Kinyankole: S*ebo/ Nyabo gamba enfumu zitarizimwe nazimwe ezine akakwate aha bashaija na bakazi kandi ohereze na makuru gaazo.*
Kiswahili: Bwana/ Bibi Taja methali za kijinsia zilizomhusu mwanamume na mwanamke kisha utoe maana zake.

Kinyankoe: *Sebo/Nyabo Enfumu ezi nogiira ngu zikaaba zikoresibwa kutungura abakazi ninga kubabandika omukyanga, hereza enshonga?*
Kiswahili: Bwana/ Bibi je, unafikiria methali hizi za kijinsia zilikuwa zinatumiwa kumjenga mwanamke au kumdunisha? Toa sababu zako

Kinyankole: *Sebo/ Nyabo Omukurugirira omukwetegyereza kwawe enfumu zobushaija na obukazi omubwire obu zikyine omugasho ahantuura ya Banyankole?*
Kiswahili: Bwana/Bibi kutokana na kuelewa kwako je, hizi methali za kijinsia zingali na umuhimu katika jamii ya kisasa ya Wanyankole? Toa sababu zako.

Kinyankole: *Sebo/ Nyabo Enfumu ezi zikanyiga zita abaturaine kurujiraa aha emirimo yibabire nibakola omukyanga?*
Kiswahili: Bwana/ Bibi je methali hizi za kijinsia ziliathiri namna gani majukumu tofauti yaliyopatikana ndani ya jamii hii?

Kinyankole: *Sebo/ Nyabo Enfumu ezi ziyambire zita ahankulakulana ye ntura ya Banyankole?*
Kiswahili: Bwana / Bibi je, methali hizi zimechangia namna gani katika maendeleo ya jamii ya Wanyankole?

Kinyankole: *Omukwetegyereza kwawe, nojira ni bantu kyi abahandikyire efumu za Banyankole, kandi ahabwenkyi?*
Kiswahili: Bwana/ Bibi je, kwa maoni yako unafikiria ni jinsia gani ilitunga methali hizi za kijinsia za Wanyankole? Na kwa sababu gani?

Haya ni baadhi ya maswali ambayo mtafiti alitumia kuwahoji wasailiwa wake, na kuweza kuona ikiwa kweli waliweza kulijibu suala lake la utafiti ambalo lilikuwa ni, kuhakiki methali za kijinsia katika jamii jamii ya Wanyankole kwa Mtazamo wa Kipragmatiki. Kwa hivyo, kutokana na namna walivyojibu maswali haya, yalimwezesha mtafiti kuweza kupata data ya kutosha katika utafiti wake jambo ambalo limesaidia katika kufanikisha utafiti huu.